

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Sita – Tarehe 9 Aprili, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Chuo Kikuu Mzumbe kwa mwaka ulioisha tarehe 30 Juni, 2017 (*The Annual Report and Audited Accounts of Mzumbe University for the year ended 30th June, 2017*).

MWENYEKITI: Katibu!

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Swali letu la kwanza leo linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo hapa kwa niaba.

MWENYEKITI: Wewe unatoka Busega?

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Hapana, ila hili ni la kitaifa.

MWENYEKITI: Aaa, sawa, kwa niaba.

Na. 43

Kauli Mbiu ya Kuvutia Wawekezaji Nchini

MHE. RASHID A. SHANGAZI (K.n.y. MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI) aliuliza:-

Kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ni pamoja na kuongeza uwekezaji kwa kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa vikwazo vinavyoathiri dhana hiyo vinaondolewa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Jimbo la Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Dira ya Taifa ya mwaka 2025 ni kuifanya Tanzania kuwa Taifa lenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Ili kutimiza dhamira hiyo tunatekeleza mipango mitatu ya maendeleo ya miaka mitano mitano ambayo imeainisha vipaumbele vya Taifa kuelekea uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Kwa sasa Serikali inatekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa kipindi cha 2016/2017 hadi kufikia mwaka 2020/2021 ambao kipaumbele chake ni ujenzi wa uchumi wa viwanda. Mkakati wa Serikali ni kuhakikisha vikwazo vinavyoathiri uwekezaji na biashara nchini vinaondolewa kwa kuweka miundombinu muhimu na mazingira ya kisera, kisheria, kanuni na kiutendaji ambao ni wezeshi kwa ajili ya kuendesha shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha miundombinu wezeshi kama vile ujenzi wa reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari, umeme na maji hatua ambayo inapunguza gharama za uendeshaji wa biashara na uwekezaji na kuleta wepesi katika uwekezaji na biashara. Aidha, Serikali imeimarisha upatikanaji wa ardhi ambapo Mamlaka za Upangaji Miji zimeelekezwa kuzingatia utengaji wa asilimia 10 ya kila aneo la Mpango Kabambe wa Mji kwa ajili ya uwekezaji wa biashara na viwanda. Vilevile Serikali inaendelea kuendeleza Maeneo Maalum ya Uwekezaji au *Special Economic Zones* ili kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya uzalishaji yenye miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeendelea kuhakikisha uwepo wa mazingira bora ya uwekezaji kwa kutekeleza programu za kuboresha mazingira ya uwekezaji na hii ni pamoja na mpango wa kuboresha mfumo wa

udhibiti wa mazingira ya biashara nchini au *Blueprint*. Serikali inaendelea kuimarisha ushirikiano na majadiliano na Sekta binafsi kupitia Baraza la Biashara la Taifa (*TNBC*) pamoja na mikutano ya wadau wa Sekta mbalimbali kwa ngazi za Kitaifa, Mikoa na Wilaya ambapo changamoto zinazobainishwa zinapatiwa ufumbuzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Nimemwona mwenye swali Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ya Uwekezaji kwa majibu mazuri na ya kina. Pamoja na majibu haya nina maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza; kwa kuwa Watanzania wana hamu kubwa sana ya kuingia kwenye uchumi wa viwanda kama ambavyo kauli ya Mheshimiwa Rais ambayo siku zote amekuwa akiisema na kwa kuwa Wizara hii iko chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nini kauli ya Serikali ya kuleta mabadiliko ya haraka na ghafla yaani *radical change* yatakayowezesha kutekeleza mapendekezo ya *Blueprint* ambayo amezungumza hapa na mikakati mingine ya kuharakisha uwekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wako baadhi ya wawekezaji wa ndani na nje ambao wamekuwa wakizunguka ofisi baada ya ofisi nyingine wakitafuta vibali mbalimbali vya uwekezaji, kitu ambacho kimekuwa kikichafua sana nchi hii kwa sababu wanaposhindwa kupata vibali hivi kwa muda wanahama kwenda nchi zingine na hii inakuwa haileti dalili njema kwa nchi yetu. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kipindi hiki cha Bunge la Bajeti awaite wawekezaji wote ambao wana kero mbalimbali, akutane nao pamoja na Mawaziri wengine wote ili kuhakikisha kwamba matatizo yao yanatatuliwa mara moja? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Angella Kairuki.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chegeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kuhusiana na tunatoa kauli gani ya kuleta mabadiliko ya haraka au kama alivyoeleza mwenyewe *radical change*, nipende kusema kwamba ni kweli ili tuhakikishe kwamba tunapata faida ya uwekezaji na biashara nchini, ni lazima mabadiliko ya kina yaweze kufanyika. Tayari kama nilivyoeleza kwenye majibu ya msingi Serikali imeanza kuchukua hatua kupitia maboresho mbalimbali na kama alivyoeleza mwenyewe mpango mzuri wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, tumeandaa pia mpango jumuishi kwa ajili ya utekelezaji wa mpango kazi huu wa kuboresha mazingira ya biashara. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango huu utatekelezwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mpango kazi huo jumuishi tumeleza kabisa ni masuala gani ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi na Wizara ipi pamoja na taasisi zipi za kisekta na tutaendelea kuwafuatilia pia kwa mujibu wa *road map* ya utekelezaji wa mpango huo kwa namna tulivyojipangia. Pia tutaleta mpango huo kazi tutakapokuwa tayari ili na Waheshimiwa Wabunge waweze kuuona na kuweza kufuatilia na kuweza kujua ni hatua gani tumefikia katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili kama nitakuwa tayari kufanya kikao katika kipindi hiki cha Bunge kuwaita wawekezaji wote wenye kero mbalimbali. Kwanza nipende kusema ni ushauri mzuri, lakini la pili tayari tumeanza, nimejigawia vipaumbele, moja tumeanza na mikoa mbalimbali na tunaendelea kufanya hivyo kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa.

Pili, kwa kushirikiana na Mawaziri mbalimbali wa kisekta tutaendelea kufanya vikao mbalimbali vya kisekta kwa wawekezaji na wafanyabiashara ili kuhakikisha kwamba tunatatua kero zao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Mbunge ni shuhuda tulipoenda Rungwe kupitia kampuni ile ya Rungwe *Avocado* pamoja na bwana Robert Clowes ambaye tulienda kuangalia na kutatua mgogoro ule kwenye sekta ile ya kilimo cha maparachichi.

Nimshukuru sana kwa ushirikiano ambao aliutoa kipindi hicho na naamini mgogoro ule sasa utafika sehemu nzuri na utaweza kumalizika. Pia nimhakikishie na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote na naomba pia ushirikiano wao wa dhati, endapo kuna mgogoro maalum kwa mwekezaji ambaye anamfahamu au katika Jimbo lake analoliongoza au mkoa wake, basi wasisite kunipa taarifa kwa sababu nimeteuliwa kwa kazi hiyo maalum na niko tayari kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, pamoja na mikoa, pamoja na sekta mbalimbali, ili kuweza kuhakikisha kwamba taswira yetu kama nchi katika uwekezaji tunaendelea kuikuza, wiki ijayo kuanzia tarehe 17 nitakuwa na kikao na wawekezaji wote wa kichina na tutaendelea kufanya hivyo na wawekezaji wa Uturuki, wa Marekani, Uingereza na nchi zingine kwa mujibu wa viwango vile vya nchi 10 zinazoongoza katika kuvutia mitaji nchini kwetu, lakini tutahakikisha pia na nchi zingine tutazingatia. Kwa hiyo nimshukuru Mheshimiwa Mbunge, lakini nitaomba ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge wa dhati. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Muda umekwenda Waheshimiwa, tunaendelea swali linalofuata, Mheshimiwa Justin Joseph Monko.

Na. 44

Hitaji la Vituo vya Afya Tarafa ya Mtinko – Singida Kaskazini

MHE. JUSTIN J. MONKO aliuliza:-

Tarafa ya Mtinko Jimbo la Singida Kaskazini yenye Kata sita haina kituo cha afya cha Serikali:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kukamilisha jengo la kituo cha afya katika Kata ya Makuro lililojengwa na wananchi ili wananchi waweze kupata huduma za rufaa kutoka katika Zahanati zilizopo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha za majengo ya ziada katika kituo cha afya Kata ya Makuro ili kutoa huduma bora kwa wananchi?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justin Joseph Monko Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Mtinko yenye Kata sita ina zahanati tisa na haina kituo cha afya. Hata hivyo, wananchi wa Tarafa hiyo hupata huduma za afya za rufaa kwenye hospitali teule ya Wilaya ya *St. Carols Council Designated Hospital*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ya Singida imepokea jumla ya shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya na kukarabati vituo vya afya viwili yaani kituo cha afya cha Msange na kito cha afya cha Mgori ili kuweza kutoa huduma za upasuaji kwa mama na mtoto. Serikali itaendelea kujenga na kukamilisha maboma ya vituo vya kutolea huduma za afya kwa awamu kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyowezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha afya cha Makuro kimejengwa kwa nguvu za wananchi na mpaka sasa jengo

la wagonjwa wa nje lipo katika hatua za ujenzi kwenye ukuta. Nazielekeza halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma na vituo vya kutolea huduma kwenye maeneo yao ya kiutawala. Serikali itaendelea kukamilisha maboma na kujenga kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Monko.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa maswali ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Awali ya yote kwanza napenda niishukuru sana Serikali kwa fedha ambazo imetupatia sisi kwa ujenzi kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri. Hata hivyo, hospitali teule ya Wilaya ya Mtinko ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameisema tangu ilipopandishwa hadhi mwaka jana haijapangiwa Madaktari wala Wauguzi wa kufanya kazi na kuongeza huduma katika hospitali hiyo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuwasiliana pia na Wizara ya Afya ili kuhakikisha kwamba hospitali hiyo inapata Wauguzi na Madaktari wa kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anajua tofauti ya kituo cha afya na hospitali ya Wilaya na wananchi wale ambao ni zaidi ya wananchi 80,000 hawana kituo chochote cha afya na wamejenga jengo hilo kwa zaidi ya miaka nane na halmashauri yetu imeshindwa kutenga fedha za kukamilisha jengo hilo. Je, Wizara iko tayari kutenga fedha ya kukamilisha jengo hilo la kituo cha afya cha Makuro na kutenga fedha kwa ajili ya majengo mengine ili kituo cha afya cha Makuro kiweze kuanza kufanya kazi kwa Tarafa ya Mtinko. Ahsante?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwanza naomba nimpongeze

Mheshimiwa Mbunge Monko kwa kuendelea kuwasimamia wananchi wa Jimbo lake la Singida Kaskazini. Sasa naomba nimjibu swali lake la kwanza na la pili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza anazungumzia habari ya kupata Wauguzi na Madaktari. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumelipokea jambo hili, katika wale Wauguzi na Madaktari ambao tumewaomba kibali maalum Ofisi ya Utumishi wakipatikana, basi tutaangalia pia eneo hili ili wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili anazungumza habari ya kutenga fedha ya kukamilisha boma hili ambalo limejengwa kwa nguvu za wananchi. Namkaribisha Mheshimiwa Mbunge ofisini kwetu tuzungumze, tuone kitakachowezekana, lengo na makusudi ni kwamba jambo hili likamilike na nguvu za wananchi ziweze kuungwa mkono, zisipotee bure ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Dihimba yenye vijiji zaidi ya 30 haina kituo cha afya hata kimoja na Kata ya Mangopachanne tayari wameshaanza ujenzi wa kituo cha afya. Je, Serikali iko tayari kuwaunga mkono katika kukamilisha kituo cha afya katika Kata ya Mangopachanne?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu kwa kifupi mtawaunga mkono.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi ipo tayari sana kuunga mkono wananchi hawa. Tuendeleo kuwasiliana, tutatafuta fedha, zikipatikana tupeleke kukamilisha maboma yote na sio kule kwa Mheshimiwa Hawa Ghasia peke yake ila ni nchi nzima kwa

Majimbo mbalimbali kukamilisha maboma yaliyojengwa na nguvu za wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Flatei.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Jimbo la Mbulu Vijijini lina kituo kimoja tu cha afya, je wananchi wa Maretadu wamejenga sana kituo cha afya cha Maretadu, je, Mheshimiwa Waziriy uko tayari kutusaidia fedha ya kumalizia kituo cha afya Maretadu?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nimemwona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri yote ya kwanza. Namfahamu Mheshimiwa Flatei Massay na katika Jimbo lake kulikuwa na changamoto kubwa sana ya afya na ndio maana katika kelele zake nyingi sana kwa kuwaombea wananchi wake tulimpelekea hospitali ya Wilaya na kituo cha afya cha Dongobeshi. Hata hivyo, tunalichukua ombi hilo tatalifanyia kazi kwa sababu lengo letu na mkakati wetu wananchi wote wapate huduma ya afya, kwa hiyo jambo hili tatalichukua, tutaangalia jinsi gani ya kulifanyia kazi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gashaza.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa ipo zahanati ya Kijiji cha Kigarama ambayo jengo la *OPD* limejengwa kwa nguvu ya wananchi mpaka kukamilika, lakini zahanati hiyo takribani miaka miwili haijaweza kufanya kazi kwa sababu hakuna nyumba ya watumishi na choo hakijakamilika. Upo uwezekano wa kupata nyumba ya kupanga kwenye *center* hiyo ya karibu ambapo ni rahisi Mganga kuweza kuhudumia akitokea hapo.

Je, Wizara iko tayari kutoa kibali ili zahanati hiyo iweze kufunguliwa kuondoa adha ya akinamama wanaokwenda kujifungua kutembea umbali mrefu zaidi ya kilomita 30 wakati tayari wameshatoa mchango kwa ajili ya ujenzi wa zahanati hiyo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, mko tayari kutoa kibali?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa kauli yako naomba nimwagize Mganga Mkuu wetu wa Mkoa wa Kagera aende akafanye ufuatiliaji wa zahanati hiyo, kama imekamiliwa kweli lazima wahakikishe nguvu za wananchi ambao lengo lao wapate huduma kuhakikisha kwamba wanaipata. Kwa hiyo namwagiza Mganga wetu Mkuu wa Mkoa wetu wa Kagera aende akafanye kazi ili na Mheshimiwa Mbunge apate kibali na wananchi wapate huduma.

MWENYEKITII: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 45

Unyanyasaji Unaofanywa na Mkuu wa Wilaya ya Ikungi

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. JESCA D. KISHOA)
aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Mkuu wa Wilaya ya Ikingu amekuwa akijichukulia sheria mkononi na kuwanyanyasa wananchi wa Kata za Ighombwe, Iglansoni na maeneo ya Wilaya ya Ikingi.

Je, Serikali inaweza kutoa majibu ni mamlaka yapi aliyonayo Mkuu huyo wa Wilaya ya kuwanyanyasa na kuamrisha mali za wananchi kuchomwa moto au kuporwa

na Serikali bila utaratibu wowote wa kisheria kwa kisingizio kuwa wanaishi maeneo yasiyoidhinishwa kwa makazi?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Igombwe, Iglasoni na maeneo ya Wilaya ya Ikungi zinapakana na hifadhi ya Msitu wa Minyughe yenye ukubwa wa hekta 264,600. Kwa nyakati tofauti shughuli za kibinadamu kwenye vijiji vinavyozunguka msitu huu zilianza kuhatarisha mazingira ya hifadhi hasa baada ya wananchi kadhaa kuhamia eneo la hifadhi na kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kupitia vikao vya kisheria vya Baraza la Madiwani liliazimia kuulinda msitu huu na kuwaondoa wavamizi, hivyo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ambayo ndiyo yenye mamlaka aliyopewa na Sheria ya Tawala za Mikoa ya *Regional Administrative Act* ya mwaka 2002, chini ya Kifungu cha 15 kutoa amri halali, iliwataka wananchi hao kuondoka katika maeneo ya Hifadhi ya Msitu wa Minyughe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuwaondoa wavamizi lilifanyika kwa awamu mbili, yaani Mei na Oktoba, 2017 ambapo watu 119 waliondolewa kwenye hifadhi hiyo pamoja na ng'ombe 2,243, mbuzi 455 na kondoo 169. Zoezi hili lilishirikisha Askari wa Jeshi la Polisi waliofanya kazi yao kwa weledi wa hali ya juu kwa sababu hakuna raia aliyejeruhiwa wala kupoteza mali zake. Ni dhahiri uwepo wa Askari Polisi ambao ni wasimamizi wa sheria uliwezesha operesheni hiyo

kufanyika salama na hakuna kielelezo wala ushahidi kwamba haki zao za msingi zilivunjwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Muuliza swali, Mheshimiwa Joseph Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na hayo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, wananchi wanajenga katika maeneo mbalimbali ambayo Serikali inasema hayaruhusiwi kwa sababu ya uhaba wa ardhi lakini wakati huohuo maeneo hayo yana viongozi na baada ya kujenga wanapelekewa maji, umeme na kadhalika. Nataka kujua, Serikali inawachukulia hatua gani watendaji au viongozi wa maeneo kama hayo ambao wanawaacha wananchi wanajenga wakishakamilisha ndiyo wanaingia kwenda kuwaondoa na kwa sababu hiyo kuharibu mali zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, suala la kuchukua madaraka vibaya kwa baadhi ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa bado linaendelea nchini. Natambua juhudi za Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jafo na Waziri Mheshimiwa George Mkuchika na hatua mbalimbali ambazo baadhi ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wamechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna wilaya nyingine kwa mfano Wilaya ya Hai, Mkuu wa Wilaya bado anaendelea na vitendo vya kuwakamata hovyoo wawekezaji, wananchi na kushinikiza baadhi ya wanasiasa kwa kutumia vikosi vya askari wahame kwenye vyama vyao, hata Mkuu wa Mkoa wa Iringa...

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Tulikuwa naye kwenye kikao juzi hapa tukamwambia ajirekebishe, akatoka akaenda ku-*tweet* kwamba sasa atakwenda *speed* kilometa 120 badala

ya 80 alizokuwa anaenda nazo, sasa hii ni *insubordination* kwa Serikali. Baada ya matamko yote ya Mawaziri, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ambao bado wanaendelea ku-*insubordinate* Serikali ni hatua zipi ambazo Serikali imepanga kuchukua? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Jafo, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mjumbe wa Kamati yangu ya TAMISEMI, kaka yangu Mheshimiwa Selasini kwa maswali yake mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumeshatoa maelekezo mbalimbali; jambo la kwanza watu wasivamie maeneo ambayo siyo halali kwa ujenzi, lakini jambo la pili tumetoa maelekezo kwa viongozi wetu kwa sababu wao tumewapa dhamana wahakikishe wanasimamia maeneo hayo. Kitendo cha wananchi hata kujenga sehemu isiyoruhusiwa halafu tunawaangalia mwisho wa siku kuja kuwabomolea sio jambo sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maelekezo hayo tumeshayatoa. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo katika baadhi ya vijiji na kuna Kamati Maalum inaongozwa na ndugu yangu Mheshimiwa Lukuvi inafanya kazi hiyohiyo lakini na maelekezo mengine ya Kiserikali tunayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili la kwamba baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanaendelea kufanya mambo ambayo siyo sawasawa, ni kweli Mheshimiwa Mbunge unafahamu kwamba tulipotoka hali ilikuwa ni mbaya sana. Tulikuwa na idadi kubwa sana ya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya hali kadhalika Wakurugenzi wa Halmashauri, hasahasa Wakuu wa Wilaya walikuwa wakifanya mambo sivyo lakini kazi kubwa iliendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ndani tunafanya tathmini hali imebadilika sana lakini katika tabia za binadamu tuna *case by case* ambazo tunazishughulikia na hata mambo unayozungumzia hivi sasa mengine yako katika utaratibu wa kushughulikiwa. Kwa hiyo, tuvute subira siyo kila kitu ni kutangaza *publically* lakini kuna mambo kama Serikali tunayafanyia kazi kwa sababu lengo letu ni utii wa sheria bila shuruti uweze kufanyika lakini kufuata utaratibu, sheria na kanuni kwa viongozi na wananchi wote. Ahsante.

MWENYEKITI: Sawa. Mheshimiwa Mlinga na Mheshimiwa Devotha Minja. Tunaanza na Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ukiacha Wakuu wa Wilaya ambao wanafanya vibaya wako Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wanaofanya vizuri. Kwa mfano, kwa Wakuu wa Mikoa yupo Salum Hapi wa Iringa amekuwa mbunifu kupita kiasi, Ndugu Alexander Mnyeti, Ndugu Mrisho Gambo na Ndugu Paul Makonda... (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, uliza swali Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu ni hili, je, Wizara ina mkakati gani wa kuwaandalia motisha ama tuzo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya hawa ambao wanafanya kazi vizuri?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), mtawatambua je hao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama nilivyosema hapo awali mwanzo tulikuwa na matatizo mengi sana, sasa hivi matatizo haya kwa kweli kwa kiwango kikubwa yamefungua sana. Ni kweli nikiri wazi kwamba kuna Wakuu wa Mikoa hivi sasa wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, tulianzisha programu ya ujenzi wa viwanda, katika kila mkoa viwanda 100, matarajio yetu ni kupata viwanda 2,600 lakini tumepata viwanda 4,877 ni *outstanding performance*, lakini kazi hii imesimamiwa na Wakuu wa Mikoa.

Kwa hiyo, agenda ya kuwapa *appreciation* baadhi ya Wakuu wa Mikoa tumeshaanza kuifanya katika vikao vyetu na juzi-juzi baadhi ya Wakuu wa Mikoa tumeshawakabidhi vyeti vyao kwa jinsi walivyoshiriki katika kuhakikish mambo ya Serikali yanaenda vizuri. Kwa hiyo, hilo tutaendelea kulifanyia kazi, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Devotha Minja.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Si Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya tu ambao hawafanyi vizuri, wapo pia ma-*RPC* ambao hawafanyi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *RPC* anapotangaza kwamba wananchi wakiandamana atawapiga hadi wachakazwe, hivi kazi ya msingi ya Jeshi la Polisi kwa wananchi wanaolipa kodi ili walipwe mishahara, ni kuchakaza wananchi? (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana swali la dada yangu Mheshimiwa Devotha Minja. Nadhani kitu kikubwa kama Taifa, jambo la kwanza tuweke ushirikiano katika kila eneo. Nadhani vyombo vingine vinaongozwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni hasa katika suala zima la mambo ya ndani na sitaki kuviingilia. Kwa hiyo, imani yangu ni kwamba wananchi wote tutafuata utaratibu wa utii wa sheria bila shuruti kwa ajili ya kuepuka migongano mingine ambayo inawezekana siyo ya lazima kwa afya ya Taifa letu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, linaelekezwa kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 46

Mkakati wa Kudhibiti Wanafunzi wa Kike Wasipate Mimba

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na ongezeko la wasichana wanaokatishwa shule kwa sababu ya mimba?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na ongezeko la wasichana wanaokatishwa shule kwa sababu za mimba, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 78. Katika marekebisho hayo ya mwaka 2016, mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya kumpa mimba mwanafunzi wa shule ya msingi au sekondari atahukumiwa kifungo cha miaka 30 jela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa sheria hiyo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kudhibiti ongezeko la mimba kwa wanafunzi, kama vile ujenzi wa mabweni, hosteli na shule katika maeneo ambayo wanafunzi wanalazimika kutembea umbali mrefu. Aidha, huduma za ushauri na unasihi hutolewa kwa wanafunzi

ambapo mwongozo wa ushauri na unasihi umeandaliwa. Vilevile mafunzo mbalimbali juu ya stadi za maisha, elimu na afya na uzazi hutolewa kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti mimba kwa wanafunzi, ili kuhakikisha kuwa, wanafunzi wote wanakamilisha mzunguko wa elimu bila kikwazo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Asha Abdullah.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa majibu niliyopatiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la watoto wetu wanaoendelea kupata mimba bado limeshika kasi. Ni juzi tu tumepata habari kwamba kuna mwalimu amewafanya wake zake watoto wa *primary* karibu 10. Wako wanaopata mimba kwa kubakwa, wako wanaopata mimba kwa kushawishiwa na wako wanaopata mimba kwa bahati mbaya yoyote ambayo inatokezea lakini huwa siyo dhamira, dhamira hasa ni watu hawa wapate haki ya kielimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni zito sana...

MWENYEKITI: Swali sasa.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Sheria Na. 5 imetoa adhabu ya miaka 30 kwa yule mharibifu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abdullah, nipe maswali.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, nataka niulize Serikali ni lini hasa itakaa chini itizame upya kadhia hii inayowakuta watoto wa wanyonge, wafanyakazi na wakulima, wasichana ambao wanakosa haki yao kielimu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, lini Serikali itatafuta mbinu mbadala ya kuwasaidia watoto hawa ambao

wanakosa haki yao ya kimsingi? Hili jambo linauma sana, lazima Serikali itazame upya. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Olenasha, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu kwenye swali la msingi, Serikali inachukua hatua kadhaa kuhakikisha inadhhibiti tatizo hili. Kubwa ambalo limezungumziwa ni mabadiliko ya sheria ambapo imekuwa ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kumpa mimba mwanafunzi wa shule ya msingi au sekondari. Tunachoomba na Waheshimiwa Wabunge ni mabalozi wazuri katika hili, Serikali ina dhamira ya kuhakikisha kwamba wale wote wanaokutwa na makosa haya wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sharia na kama tulivyosema tumeweka kifungo cha miaka 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi kinachotokea ni kwamba ushirikiano kutoka kwa wazazi wa wanafunzi ambao wameathirika unakuwa siyo mkubwa. Pindi tutakapopata ushirikiano na ushahidi ukiwepo, Serikali itaendelea kuchukua hatua kuhakikisha kwamba wale wahusika wote wanachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili tunachukua hatua zipi kuhakikisha kwamba wale wanafunzi wanaoathirika wanaendelea na safari ya masomo? Napenda kuliirifu Bunge lako Tukufu kwamba mwanafunzi kupata mimba haimaanishi kwamba ndiyo mwisho wa safari yake ya masomo. Serikali imeweka taratibu kadha wa kadha ili kuhakikisha wanafunzi wale bado wanapata fursa nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa hiyo ipo katika maeneo matatu makubwa; moja Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ina utaratibu wa kutoa elimu nje ya mfumo rasmi. Napenda

kutoa taarifa kwamba kwa mwaka jana kuna wanafunzi 10,000 ambao wamehitimu kidato cha nne kupitia utaratibu wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na 6,000 ni wasichana. Tunaamini kwamba baadhi yao ni wanafunzi wale ambao walikatisha masomo kwa sababu ya mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na *UNICEF* tunaendesha Mradi wa Elimu Changamani kwa wanafunzi ambao wameshindwa kuendelea na shule kwa sababu ya kupata ujauzito. Pia, Serikali imeendelea kuimarisha elimu ya ufundi, kwa hiyo, wanafunzi ambao hawajaweza kwenda sekondari au ambao wameshindwa kuendelea kwa sababu ya kupata ujauzito kuna fursa vilevile ya kupata elimu ya ufundi na tumeendelea kuimarisha na elimu hiyo sasa hivi ni bora.

Kwa hiyo, tunachosema kimsingi, hata kama mwanafunzi amepata ujauzito sio mwisho wa safari yake ya masomo kuna fursa nyingine na kuna wengi ambao wamenufaika. Nina hakika hata baadhi ya Wabunge kwenye Bunge hili wamenufaika na mipango hii ya Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Fatma Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatozo la mimba utotoni pia linawahusu sana watoto wenye ulemavu walio nje ya shule na ambao wako ndani ya shule. Je, Serikali inawanusuru vipi hawa watoto wenye ulemavu na mimba za utotoni?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Olenasha, Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu niliyotoa kuhusu watoto wa kike wanaokatishwa safari ya masomo kutokana na mimba, vilevile yanaweza yakatumika kwa ajili ya watoto walemavu kwa sababu tunachosema Wizara yetu na Serikali kwa ujumla inahakikisha kwamba hakuna mtoto yoyote wa Kitanzania atakayekosa elimu kwa sababu yoyote ile. Sisi tunachotaka ni ushirikiano kutoka kwa wazazi kwa sababu tayari Serikali ina mipango ya kuhakikisha kwamba yeyote yule anapata elimu bila kujali changamoto yoyote imempata katika safari yake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati ya Serikali ya kuweza kutoa adhabu kali na sheria ya kifungo cha miaka 30 kwa wale ambao wanawapa mimba wanafunzi lakini inaonekana bado wanafunzi wanapata mimba na idadi inaongezeka. Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada kwa baadhi ya madereva wa bodaboda wanaowachukua wanafunzi wetu ambapo wamekuwa wakilalamika kwamba wanatendewa vitendo visivyo za kutoa elimu ya kutosha kwa madereva hao wanaowachukua wanafunzi kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine?

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masoud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu langu nilitoa katika majibu yangu ya swali la msingi kwamba Serikali inachukua hatua kadha wa kadha. Moja ni kuzuia na tunazuia kwa njia mbili na kubwa kupitia kitu tunachoita *deterrence*; kwa kuwaadhibu wale wanaofanya makosa ili wengine wasije wakafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto ambayo watoto wanapata wakiwa wanaelekea shuleni, Serikali imeendelea kujenga shule karibu na wananchi lakini vilevile kwenye maeneo ambayo shule ziko mbali tumejenga mabweni. Vilevile tunatoa elimu kwa umma na wanafunzi kwa kupitia huduma za unasihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachotaka tu kusema ni kwamba Serikali inajua hili ni tatizo kubwa lakini hatujakaa kimya tumeendelea kufanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba hayatokei. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kutokana na takwimu tulizonazo tatizo haliongezeki limepungua.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali olinalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum na bado linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 47

Kuzikarabati Shule za Sekondari Rugambwa na Bukoba

MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU aliuliza:-

Miundombinu ya Shule ya Sekondari Rugambwa ilijengwa mwaka 1964 na Sekondari ya Bukoba imejengwa mwaka 1939, hivyo imechakaa sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati shule hizo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Olenasha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza fursa na kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa ni bora, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule na vyuo nchini. Hii ni pamoja na utekelezaji wa mpango wa ukarabati wa shule zote kongwe 88 na sekondari nchini ambapo hadi sasa shule 48 zipo katika hatua mbalimbali za ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari ya Bukoba ni moja kati ya shule zinazoendelea na ukarabati ambapo tayari kiasi cha Sh.1,481,701,194 kimetolewa. Aidha, Shule ya Sekondari Rugambwa ipo katika mpango wa ukarabati awamu ya pili ambao utafanyika katika mwaka huu unaoisha 2018/2019. Tathmini ya kupata gharama halisi za ukarabati (*conditional survey*) ilishafanyika chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa, hivyo ukarabati unatarajiwa kuanza tarehe 15 Aprili, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika shule na vyuo nchini kadiri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mushashu.

MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Bukoba Sekondari ina umri wa miaka 80, Rugambwa Sekondari ina umri wa miaka 55 lakini pamoja na uzee shule zote zilipitiwa na tetemeko na Bukoba Sekondari ikaja vilevile ikaezuliwa na kimbunga. Kwa niaba ya Mkoa wa Kagera na wanafunzi wanaosoma katika shule hizo, naipongeza sana Serikali kwa

kutoa Sh.1,481,000,000 kwa ajili ya kukarabati Bukoba Sekondari na kuahidi kukarabati Rugambwa mwaka huu kuanzia mwezi huu wa Aprili. Kwa kuwa Rugambwa wakati wa tetemeko nyumba za walimu na zenyewe zilianguka na nyingine zikaathirika sana, hadi leo Mkuu wa Shule hana mahali pa kuishi, je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea nyumba za kuishi walimu wa Shule ya Sekondari Rugambwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, shule zote mbili, Bukoba Sekondari na Rugambwa zinahitaji kumbi za mikutano. Bukoba Sekondari haina ukumbi kabisa, Rugambwa ukumbi wake ni mdogo sana unachukua watoto 300 wakati wako wanafunzi karibu 700/800. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea kumbi za mikutano ili wanafunzi wapate mahali pa kufanyia mitihani na kufanyia mikutano?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kwa dhati kabisa na kwa furaha kubwa nipokee shukrani na pongezi za Mheshimiwa Mbunge kwa kazi ambayo Serikali imefanya katika shule zake. Lazima niseme kwamba Mheshimiwa Mushashu ni moja kati ya Wabunge makini sana katika Sekta ya Elimu na tumeendelea kufarijika na uzoefu wake mkubwa kama Mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maswali yake, kwanza kuhusiana na nyumba za Walimu katika Shule ya Rugambwa, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunavyozungumza tayari Serikali inafikiria kujenga nyumba nane za Walimu katika shule ya Rugambwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kumbi za mikutano katika shule zote mbili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na

miundombinu katika shule zake kadiri uwezo wa fedha utakavyoruhusu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Joyce Sokombi.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi hii. Tatizo lililopo Bukoba ni sawa na tatizo lililopo katika Mkoa wa Mara hasa Jimbo la Bunda Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunda Vijijini tuna Shule za Sekondari 12...

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naweka hoja vizuri ili swali lieleweke. Ili mtoto awe na usikivu mzuri darasani, mazingira ya shule zile ni mabaya sana, maboma hayajamaliziwa, kwa hiyo, ili mtoto awe na usikivu darasani ni vizuri kuwe na miundombinu mizuri na mazingira mazuri.

Je, ni lini Serikali itahakikisha inajenga na kuzimalizia zile Shule za Sekondari katika Jimbo la Bunda Vijijini? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule zetu na ndiyo maana Serikali imeendelea kutenga fedha kwa mabilioni kuhakikisha kwamba tunaondoa changamoto ya miundombinu katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu katika mwezi wa Januari ilitoa shilingi bilioni 56 kwa shule tofauti 500 nchi nzima. Lengo lake ni kuendelea kupunguza changamoto za miundombinu katika shule hizo. Hata Mkoa wa Mara na Bunda anapotoka Mheshimiwa Mbunge nao wamefaidika

na mpango ule wa ujenzi kupitia mradi wa kulipa kulingana na matokeo (EP4R).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ya TAMISEMI hivi karibuni imetoa fedha kwa ajili ya kumaliza maboma nchi nzima. Naomba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri yake kupata taarifa sahihi kwa sababu fedha hizo zimeenda nchi nzima. Kama bado kuna upungufu ni nia ya Serikali kuendelea kukabiliana na changamoto hizo kadiri uwezo wa fedha utakavyoruhusu. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mary Chatanda.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa kunipa nafasi. Naipongeza Serikali kwa kutupatia fedha *Korogwe Girls* za ukarabati wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana katika ukarabati ule bwani moja la Thabita limeshindikana kabisa kukarabatiwa kutokana na ubovu wa bwani lile.

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutupatia fedha ili tuweze kujenga jengo hilo kutokana na watoto 120 kwenda kutawanywa kwenye mabweni mengine? (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mary Chatanda pale Wizarani kwangu ameshatengewa kiti kwa sababu kila wakati amekuwa akija Wizarani kufuatilia changamoto za miundombinu kwa ajili ya shule zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu siyo mara ya kwanza kuleta changamoto hii, Wizara yangu imejipanga kuondoa hiyo kero moja kwa moja ili watoto wetu waweze kusoma katika mazingira mazuri. (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Antony Calist, Mbunge wa Moshi Vijijini na linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Na. 48

**Kupima Mashamba Yaliyotaifishwa Wakati wa
Azimio la Arusha**

MHE. ANTONY C. KOMU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya mara kwa mara ya kuyapima upya mashamba yaliyotaifishwa wakati wa Azimio la Arusha ambayo hivi sasa yamebadilishwa matumizi na kujengwa Shule, Zahanati, Hospitali, Makazi na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA
MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Antony Calist Komu, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna mashamba kadhaa nchini yaliyotaifishwa wakati wa Azimio la Arusha. Baadhi ya mashamba hayo yaligawiwa kwa mashirika na taasisi za Umma kwa ajili ya kuyaendeleza hususan kwa kilimo cha kahawa na mkonge.

Hata hivyo, baadhi ya mashamba hayo yamebadilishiwa matumizi na yamekuwa yakitumiwa na wananchi kwa matumizi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ikiwemo makazi, shule, zahanati, hospitali na kadhalika. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini, imeendelea kuyakagua, kuyaandalia mipango ya matumizi ya ardhi na kupima upya baadhi ya mashamba hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mashamba ambayo Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri imeyaandalia mpano wa matumizi ya ardhi ni pamoja na *Kihuhwi Estate, Sagulas Estate, Lewa Estate, Bombwera Estate, Geiglitz Azimio, Kilapula* pamoja na Kibaranga yote ya Mkoa wa Tanga. Mashamba mengine ni *New Msovero Farm, Mvumi Farms/Estate* Kilosa pamoja na *Luipa Estate* yaliyopo Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi jukumu la kuandaa mipango ya matumizi ya mashamba hayo ni la Halmashauri husika yalipo mashamba hayo. Hivyo, ninaagiza Halmashauri zote nchini kuendelea kukagua mashamba yaliyotaifishwa wakati wa Azimio la Arusha ili yaandaliwe mipango ya matumizi ya ardhi na kupimwa.

Aidha, natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatenga bajeti kwa ajili ya kupanga na kupima mashamba husika ili yaweze kutumika kwa tija kulingana na mahitaji halisi ya sasa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Komu.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna hiyo haja ya kupima upya hayo mashamba yaliyotaifishwa na kwamba jukumu hilo lipo kwenye Halmashauri, lakini kama inavyofahamika, sasa hivi Halmashauri nyingi nchini zina hali mbaya sana ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini.

Je, Serikali iko tayari kutoa fedha kwa namna ya upendeleo, kama tutatenga fedha kwenye Halmashauri kwa ajili ya kuharakisha huo upimaji? Kwa sababu tatizo kule ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Katika hayo mashamba yaliyotaifishwa, yapo mashamba ambayo yamegawanywa kabisa kwa ujumla na matumizi

yakabadilika, kwa hiyo, wamiliki ni wapya kabisa. Sasa kila wakijaribu kuomba kupimiwa upya inakuwa ni tatizo kwa sababu zile hati za awali hazijafutwa. Mfano hai ni shamba moja kule Uru lililokuwa chini ya Chama cha Msingi Uru Kati, shamba linaloitwa Kosata. Mfano Shule ya Sekondari ya Uru Seminari imeshaomba kwa zaidi ya miaka kumi kupimiwa lakini hati ile haijafutwa.

Je, Serikali itafuta lini hizo hati za mashamba ya aina hiyo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anauliza kama Wizara ni lini itaweza kusaidia Halmashauri ambazo pengine zipo duni kiuchumi kwa ajili ya kuweza kuongeza kasi ya upimaji. Naomba niseme, jana wakati najibu swali moja hapa nadhani la Mheshimiwa Joyce, nilitoa kwa ufafanuzi mkubwa sana kwamba pamoja na kwamba mamlaka za upangaji miji ni Halmashauri zenyewe, lakini wizara imeweka juhudi kubwa kuhakikisha kwamba inazipa *support* kubwa ya kuwawezesha kuweza kupima maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi kubwa ya kwanza ambayo tulifanya ni kuweka vifaa vya upimaji katika kanda zote na vifaa vile vinatolewa bure katika Halmashauri na inasaidia katika kupima kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tulitoa pesa, shilingi bilioni 6.4 na nimesema jana, katika Halmashauri 25 ambazo tunawasaidia kwa ajili ya upimaji, wamechukua zile pesa ili kuweza kuongeza kasi ya upimaji. Kwa hiyo, Halmashauri yake kama nayo ni mhitaji, nadhani tutaangalia uwezekano kwa kipindi kinachokuja tuweze kuona ni jinsi gani tutawawezesha ili waweze kupima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe Halmashauri zote wanatakiwa kutenga bajeti kwenye bajeti zao kwa ajili ya kuongeza kasi ya upimaji kwenye maeneo yao ili kupunguza migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ameongelea suala la shamba lile la ushirika ambalo kuna maeneo yamegawiwa kwa taasisi nyingine kwa mfano Jimbo Katoliki la Moshi wamepewa eneo hilo, Uru Seminari ambayo ameisema wamepewa eneo hilo lakini hawajaweza kumilikishwa kwa sababu nyaraka zinasemekana kwenye kile Chama cha Ushirika zimepotea. Mwezi Februari mwaka 2019 wametoa taarifa rasmi Polisi kuonyesha kwamba zimepotea. Sasa huwezi kumilikisha mtu mwingine wakati ile hati nyingine iliyokuwepo bado haijafutwa na haijaweza kupatikana kiasi cha kuweza kuwapa hati wale wengine. Kwa hiyo, kinachofanyika sasa baada ya ule utaratibu wa kisheria kukamilika, basi na hawa wengine ambao wamepewa maeneo yale katika lile shamba lililokuwa awali lililobadilishiwa matumizi, nao watapata. Pia kwa sehemu kubwa inaweza ikafanyika kwenye zoezi la urasimishaji kwa sababu tayari kuna maeneo mengi yameshajengwa hospitali, shule na makazi. Kwa hiyo, hilo litafanyika kulingana na taratibu za kisheria mara taarifa zilizopelekwa Polisi zitakapokuwa zimefikia hatima yake. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tupo nyuma sana ya muda. Naendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, Mbunge wa Viti Maalum kwa Wizara hiyo hiyo ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Na. 49

Uhaba wa Ardhi ya Kilimo kwa Wananchi wa Handeni

MHE. SONIA J. MAGOGO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Handeni ambao wanakosa ardhi ya kuendesha

shughuli zao za kilimo kwa sababu ya kumilikiwa na wachache?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa mashamba uliofanyika katika kipindi cha 2018/2019 Wilayani Handeni ulibaini kuwepo kwa mashamba manne makubwa yenye hekta 7,279.26 ambayo hayajaendelezwa ipasavyo na hivyo kupelekea baadhi ya mashamba hayo kuvamiwa na wananchi. Serikali inaendelea na utaratibu wa ufutaji wa miliki za mashamba hayo yaliyokiuka masharti ya uendelezaji ambapo wamiliki wanne wameshatumiwa ilani zao ubatilisho. *(Makoff)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya miliki hizo kubatilishwa, ardhi husika itaandaliwa mipango ya matumizi ikiwemo ya kilimo na ufugaji na kugawia kwa wananchi wenye uhaba wa ardhi. Aidha, mipango hiyo itazingatia utengaji wa ardhi ya akiba *(land bank)* kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa wananchi kutumia ardhi yao kwa tija kwani ardhi haiongezeki wakati idadi ya watu, mifugo na shughuli za uzalishaji zinahitaji ardhi zinaongezeka. Vilevile, viongozi wa Vijiji na Kata waache tabia ya kuwagawia ardhi kwa mtindo wa kuwakodisha wananchi kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha taratibu na sheria za nchi yetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sonia.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya

nyongeza. Wilaya ya Handeni ni Wilaya kubwa sana lakini kwa bahati mbaya hawana Baraza la Ardhi kiasi kwamba yanapotokea matatizo yanayohusu ardhi inawabidi wananchi kusafiri mpaka Wilaya ya Korogwe:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi hawa Baraza la Ardhi? *(Makofi)*

Swali la pili; kumekuwa na migogoro ya muda mrefu katika Vijiji vya Sezakofi Kata ya Ndolo, Wilaya ya Handeni na Kata ya Kwagunda Wilaya ya Korogwe:-

Je, Mheshimiwa Waziri ni lini atakwenda kuwaona wananchi hawa ili kusikiliza kero zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Mabula.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza Mheshimiwa Sonia ameuliza ni lini tutaweka Baraza la Ardhi katika Wilaya ya Handeni, kwa sababu sasa hivi wanakwenda Korogwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimfahamishe kwamba ni dhamira njema ya Serikali kuhakikisha kwamba inakuwa na Mabaraza ya Ardhi katika kila Wilaya. Mpaka sasa tuliyonayo kisheria ni mabaraza 97 ambapo 53 yanafanya kazi na 44 hajaweza kuanza kufanya kazi. Tatizo kubwa lililopo katika uanzishwaji wa mabaraza, jambo la kwanza ni ile rasilimali watu wa kuweza kuhudumia mabaraza hayo lakini pia na maeneo au majengo kwa ajili ya kufanyia shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, pia tunapeleka baraza pale ambapo pengine pana mashauri mengi kiasi kwamba panahitaji nguvu ya ziada. Ni hivi karibuni tu

tumeongeza mabaraza mengine likiwemo la Mbulu na maeneo mengine kwa sababu tu tayari tulishapata nafasi ya ofisi katika eneo lile na sisi jukumu letu kama Wizara ni kupeleka watumishi pamoja na samani za ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaangalia tawimu zilizo kwa Handeni kama kweli ni nyingi kiasi cha kutaka kuwa na baraza, basi nitawaomba uongozi wa pale watuandalie eneo ambalo litakuwa ni ofisi linalokidhi vigezo vya kuwa Baraza la Wilaya. Vinginevyo nitawaomba waendeleo kutumia Baraza la Korogwe kwa sababu lipo karibu na bado hawana mashauri mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ameuliza ni lini nitakwenda katika eneo la Handeni kwenye Kata ya Sasako na Kwagunda kwa ajili ya kutatua migogoro. Naomba nimthibitishie tu kwamba ni dhamira njema ya Wizara kuhakikisha kwamba tunafika maeneo yote yenye migogoro lakini kabla hatujafika, uongozi uliopo katika maeneo yale unafanya kazi nzuri sana ya kuweza kutatua migogoro. Pale ambapo inashindikana na uongozi uliopo pale, basi Wizara ipo tayari kufika. Kwa kesi yake huyu, basi tutaangalia uwezekano wa kuweza kwenda kutatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mbunge wa eneo lile, Mheshimiwa Mboni, amekuwa akiulizia pamoja na jirani yake Mheshimiwa Kigoda, nikawaambia tutafika pale. Nilikuwepo mwaka 2016 lakini nitatafuta muda tena kama bado kuna kero, tutaenda kuzitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mboni Mhita.

MHE. MBONI M. MHITA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona...

MWENYEKITI: Aah, samahani. Subiri kidogo Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA

MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nataka kutoa nyongeza nimfahamishe Mheshimiwa Sonia kwamba takwimu zinaonyesha kwamba mashauri mengi ya ardhi yalikuwa yanatoka Wilaya ya Lushoto ndani ya Mkoa wa Tanga. Kwa hiyo, Serikali hivi sasa imefanya jitihada ya kuongeza

Baraza jipya la Lushoto ili kupunguza *load* ya mashauri ndani ya Mkoa wa Tanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa tumeanzisha baraza, ukiacha Korogwe ambao walikuwa wanahudumia mpaka Lushoto, sasa Lushoto wanajitegemea. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo maana yake hata Handeni sasa mtapata huduma nafuu zaidi kwa sababu nusu ya matatizo ya kero ya ardhi ya Tanga sasa yamepatiwa ufumbuzi kwa kumpeleka Mwenyekiti mpya Wilaya ya Lushoto. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mboni.

MHE. MBONI M. MHITA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Naomba nitumie fursa hii kwanza kuipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua kubwa ambayo Wizara imekuwa ikiendelea kufanya hasa katika zoezi zima la kutoa *notice* kwa wakulima wakubwa wenye kuhodhi maeneo makubwa. Nami ni shahidi kabisa kwa Jimbo la Handeni Vijijini, zoezi hili limekuwa linaendelea kwa kasi na limepelekea wananchi wa Jimbo la Handeni sasa kujikita sana kwenye kilimo cha muhogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe tu ushuhuda hasa kwenye Kata ya Kabuku na Mkata sasa hivi zoezi hilo linaendelea na Halmashauri imekuwa ikipambana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitumie fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri, kasi hii iweze kuendelea kwa sababu Handeni, hususan Jimbo la Handeni Vijijini tuna maeneo makubwa sana japokuwa mpaka sasa kwa kusema

kweli nitoe tu ushuhuda kwamba hakuna *conflict* ya maeneo. Wananchi wameendelea kujitoa sana na kilimo cha muhogo na mpaka sasa hivi ni mashahidi kwamba Handeni tunaongoza kwenye kilimo cha muhogo na tunapata viwanda ambacho Serikali kupitia Balozi wetu wa nchini China wametuletea kiwanda cha mihogo ambacho tunategemea hivi karibuni kitaanza kujengwa.

MWENYEKITI: Haya ahsante.

MHE. MBONI M. MHITA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu; naomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kutuambia zoezi hili litaendelea mpaka lini kwa sababu wananchi wa Jimbo la Handeni wanaendelea kuwa na chachu kubwa sana ya kuweza kupata. Nashukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mboni Mhita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze na nimshukuru kwa kupongeza Serikali, lakini niseme tu kwamba zoezi hilo aliloliluliza nadhani sio kwa Handeni peke yake, zoezi hili linatakiwa kufanyika nchi nzima. Zoezi hili linatakiwa kufanywa na halmashauri husika zenyewe, wao ndio wenye maeneo, ndio wanajua nani kaendeleza, nani hajaendeleza. Kwa hiyo nitoe rai kwa halmashauri zote; jukumu lenu ni kuhakikisha mnafanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye mashamba ya wawekezaji ambao hawajaweza kuyaendeleza. Wakituletea taarifa Mheshimiwa Waziri atamshauri Mheshimiwa Rais kuyafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunapokea kutoka kwao, Wizara sio inayoanzisha ufutwaji wa mashamba au ukaguzi unafanywa na halmashauri husika. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, jukumu hili ni la halmashauri,

naomba walitekeleze na sisi kama Wizara tuko tayari kuwasaidia kumshauri Mheshimiwa Rais.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nsanzugwanko.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina swali dogo la nyongeza; tatizo la Baraza la Ardhi kwa Mkoa wa Kigoma ni tatizo sugu na mashauri mengi ya ardhi katika Mkoa wa Kigoma yapo katika Wilaya ya Kasulu, wameshafanya utafiti wa kuanzisha baraza pale lakini huu ni mwaka na nusu sasa. Je, ni lini wanatuanzishia Baraza la Ardhi Kasulu ili kupunguza matatizo ya ardhi na watu wasiende Kigoma na wengine kutoka Kibondo kwenda Kigoma?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri mwenyewe, lini bwana? Mheshimiwa Naibu Waziri, lini?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mabaraza mapya ambayo yameanzishwa nadhani na Kasulu limo kama kumbukumbu zangu ziko vizuri. Kwa hiyo nasema tutafika tuweze kuona eneo ambalo limeandaliwa kwa ajili ya baraza kwa sababu katika yale yaliyoongezeka nadhani na Kasulu imo. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Na. 50

Kuenzi Wanariadha Walioliletea Taifa Heshima

MHE. ESTER A. MAHAWA aliuliza:-

Mkoa wa Manyara, hususani Wilaya ya Mbulu, umewahi kutoa wanariadha mahiri ambao waliililetea Taifa

heshima kubwa, lakini cha kushangaza wanariadha hao wametelekezwa:-

(a) Je, ni lini Serikali sasa itaandaa utaratibu wa kuwaenzi wanariadha hao?

(b) Je, ni lini sasa Serikali itajenga uwanja kwa ajili ya riadha katika Mkoa wa Manyara ili kuwahamasisha wanariadha wapya?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, picha anayoichora Mheshimiwa Mbunge ya wanamichezo kutothaminiwa haiendani na hali halisi upande wa wanamichezo nchini waliofanya vizuri na kujituma ipasavyo. Naomba nitoe mifano kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanariadha Filbert Bayi aliyevunja rekodi ya dunia ya mbio za mita 1,500 huko New Zealand mwaka 1974 ni Katibu Mkuu wa Kamati ya Olimpiki ya Tanzania na mmiliki wa Shule za Filbert Bayi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Suleiman Nyambui, mshindi wa medali ya shaba Mashindano ya *All African Games* mwaka 1978 na medali ya fedha ya Michezo ya Olimpiki 1980 kwa mbio za mita 5,000 sasa ni Kocha wa Riadha wa Taifa wa Brunei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Juma Ikangaa, mshindi wa kwanza wa mbio ndefu za *marathon* Jijini New York mwaka 1988 na mshindi wa pili mara tatu mfululizo wa *marathon* Jijini Boston mwaka 1988 – 1990 ni Mjumbe wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na mratibu wa mashindano ya riadha kwa wanawake (*ladies first*) yanayodhaminiwa na Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japan (*JICA*) pamoja na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Samson Ramadhani, mshindi wa *marathon* medali ya dhahabu Australia mwaka 2006 ni Afisa wa Jeshi;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gidamis Shahanga, mshindi wa medali ya dhahabu mbio za *marathon* nchini Canada mwaka 1978, Uholanzi 1984, Nairobi 1988 na Vienna, Austria 1990 ni Mwenyekiti Mstaafu wa Halmashauri ya Katesh Manyara; na wengine wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanamichezo, wakiwepo wanariadha waliolitea Taifa hili sifa na heshima kubwa wanatoka sehemu mbalimbali za Tanzania. Wizara imeanza mchakato wa kuanzisha makumbusho maalum Uwanja wa Taifa ambapo picha za wanamichezo wote waliolitea Taifa letu heshima katika vipindi mbalimbali zitawekwa.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Asilimia 90 ya wanariadha wanatokea Mkoa wa Manyara, lakini pia wapo wengi na taarifa iliyosomwa hapo na Naibu Waziri ni kuanzia miaka ya tisini kurudi nyuma, wapo wengi, akina John Yuda Msuri, Fabian Joseph, Andrew Sambu Sipe; wote hawa rekodi zao hazijavunjwa mpaka sasa kwa kuwa walikuwa wameshiriki mbio mbalimbali za kimataifa. Swali langu la msingi lilisema; ni lini utaratibu wa kuwaenzi wanariadha hawa utafanyiwa kazi sasa? Muda mfupi uliopita tulizungumza habari hapa na Waziri wa TAMISEMI alijibu suala la Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanaofanya vizuri kuwa *recognized* na kupewa vyeti, habari gani kwa ajili ya wanariadha hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, amejibu hapa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba picha zao zitawekwa kwenye jumba la makumbusho, je, hiyo inatosha? Wapo wanariadha wengi ambao hali zao za kimaisha ni duni, naomba kujua wanafanyiwa lini mchakato wa kutambuliwa juhudi zao. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kuweza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa ni mfuatiliaji mzuri sana wa masuala ya michezo. Nikianza na swali lake la kwanza, ni kweli kwamba sisi kama Wizara tunatambua kwamba wapo wanariadha wengi sana ambao wanatoka kwenye Mkoa wa Manyara kama ambavyo yeye mwenyewe amewataja, lakini sisi kama Serikali hatuwezi kuangalia tu mkoa mmoja, ni wanariadha wengi ambao wanatoka maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi kwamba sisi kama Serikali tunao mpango wa kuanzisha makumbusho rasmi kwa ajili ya kuweka kumbukumbu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua sasa hivi sisi kama Wizara tunayo ile kampeni yetu ya uzalendo ambayo kila mwaka tumekuwa tukiifanya na kitu ambacho tunafanya ni kuweza kuwaenzi watu mbalimbali ambao wameliletea heshima kubwa Taifa hili. Mwaka jana nakumbuka tulianza kwa wanamuziki lakini mwaka huu tutajipanga kuangalia namna gani ambavyo tunaweza tukawaenzi wanariadha wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante wanamichezo. Mheshimiwa Massare.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niulize swali la wanariadha

ambao nao Mkoa wa Singida ni miongoni mwa mikoa ambayo ilikuwa inafanya vizuri sana katika riadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimbo ninalotoka mimi kulikuwa na wanariadha miaka ya nyuma, lakini hata mimi mwenyewe nilikuwa mwanariadha. Kwa kuwa ili wanariadha na vijana ambao wapo shuleni waweze kupata hamasa ya michezo ni pamoja na vyombo vya habari ikiwemo *TBC* kusikika katika maeneo mbalimbali. Je, ni lini sasa Serikali itafanya *TBC* isikike katika eneo la Itigi ambapo haisikiki kabisa?

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Shonza.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie fursa hii kuweza kumpongeza Mheshimiwa Massare kwa sababu swali lake la usikivu wa *TBC* amekuwa akiuliza karibu kila Bunge, lakini niseme kwamba ni suala la kibajeti na kwa kuwa hili ni Bunge la Bajeti kwa mwaka huu tutaangalia namna gani ambavyo tutaboresha usikivu katika eneo lake la Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Anna Gidarya.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Natambua juhudi kubwa anayofanya Naibu Waziri. Michezo ni sekta muhimu, lakini pamoja na hivyo, vyo vyetu vikuu havina vipaumbele vya miundombinu ya viwanja. Mfano mzuri ni mwaka jana, tulikuwa na mashindano ya vyo vikuu vya Afrika Mashariki, tulikuwa na michezo...

MWENYEKITI: Uliza swali tu Mheshimiwa.

MHE. ANNA J. GIDARYA: ...kulikuwa na michezo kumi na tisa, Tanzania tulishiriki michezo tisa tu jambo ambalo

limesababisha nchi yetu kukosa vikombe vingi. Je, ni lini sasa Serikali itaboresha miundombinu na kuipa michezo kipaumbele katika vyuo vyetu?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuweza kumpongeza Mheshimiwa Anna kwa sababu kwanza ni mwanamichezo mahiri, lakini vilevile ni Kiongozi wa CHANETA Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye swali lake la msingi, ametaka kujua kwamba ni lini sasa Serikali itaweza kuboresha viwanja vya michezo, hususan kwenye vyuo vikuu. Nikiri kwamba ni kweli mwaka jana tulikuwa tuna mashindano na yeye mwenyewe pia alishiriki, pamoja na kwamba tuna uhaba wa viwanja vya michezo, lakini kama ambavyo tumekuwa tukisema kwamba Sera yetu ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 inasisitiza kwamba suala la michezo sio suala la Serikali peke yake, ni suala la Serikali lakini vilevile tuweze kushirikiana pamoja na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuweza kuwaambia na kuwaomba Wabunge wote kuiga mfano wa Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu kwa namna ambavyo amefanya maboresho ya kiwanja kule Lindi. Kwa hiyo suala hili la michezo sio suala la kuiachia Serikali peke yake, tuendeleo kushirikiana pamoja na Serikali na sisi kama Wizara tuko tayari kuendelea kutoa utaalam pamoja na mafunzo mbalimbali namna gani ya kuweza kuboresha hivyo viwanja.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata, linauliza na Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala na linaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Zedi.

Na. 51

**Wachimbaji Wadogo Wadogo Kutokuwa na
Maeneo Msalala**

MHE. SELEMANI J. ZEDI (K.n.y. MHE. EZEKIEL M. MAIGE)
aliuliza:-

Wananchi wa Msalala wengi wao ni wachimbaji wadogo, lakini hawana maeneo ya kufanyia kazi, maeneo mengi ya kufanyia kazi yana leseni za wachimbaji wakubwa na hawazifanyii kazi:-

(a) Je, kuna leseni ngapi za utafiti wa madini zilizotolewa kwa maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala?

(b) Je, ni maeneo gani Serikali inadhamiria kuyatoa kwa wachimbaji wadogo wa Msalala?

(c) Je, kwa kuanzia, Serikali inaweza kuwaruhusu wananchi wafanye uchimbaji mdogo kwenye maeneo ya reef 2, Kijiji cha Kakola namba Tisa, Kata ya Bulyanhulu, Bushimangila na Msabi Kata ya Mega na Lwabakanga na Nyangalata Kata za Lunguya na Bulyanhulu?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ya Hamashauri ya Wilaya ya Msalala kuna jumla ya leseni hai 78 za utafutaji madini na leseni za uchimbaji mdogo 53

zilizokwishatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Msalala, Serikali imetenga eneo la Nyangalata lililopo katika Kata ya Lunguya lenye ukubwa wa kilometa za mraba 10.74 kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Hata hivyo, Serikali imedhamiria kutenga maeneo mengi zaidi katika Halmashauri ya Msalala, maeneo hayo ni Kata ya Segese maeneo mawili yenye ukubwa wa kilometa za mraba 19.67 na 9.84; Kata ya Mega lenye ukubwa wa kilometa za mraba 4.93; na Kata ya Kalole lenye ukubwa wa hekta 360.13.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haiwezi kuruhusu wachimbaji wadogo kufanya shughuli za uchimbaji katika maeneo ya *Reef 2*, Lwabakanga na Namba Tisa katika Kijiji cha Kakola, Kata Bulyanhulu kwa kuwa yamo ndani ya leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini (*special mining license*) Na. 44/99 inayomilikiwa na Kampuni ya Bulyanhulu *Gold Mine*. Aidha, maeneo ya Bushimangila na Masabi yaliyopo katika Kata ya Mega yamo ndani ya maeneo yaliyooombewa leseni ya uchimbaji mdogo (*primary mining license*). Hivyo, natoa wito kwa wananchi wa Halmashauri ya Msalala kuchangamkia fursa katika maeneo yaliyotengwa na kupewa leseni ya uchimbaji mdogo ya Nyangalata.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Zedi.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nichukue fursa hii kuipongeza Wizara ya Madini kwa uamuzi wake wa kuyagawa au kutoa leseni za wachimbaji wadogo kwenye maeneo ambayo awali yalikuwa yana leseni za utafiti za wachimbaji wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu ni kwamba kwa kuwa maeneo haya ambayo yalikuwa na leseni za utafiti za wachimbaji wakubwa yameshafanyiwa utafiti na Serikali ina taarifa za utafiti zinazoonesha wapi kuna madini, yako kiasi gani, yako umbali gani na kadhalika. Je, ili kuwasaidia

wachimbaji wadogowadogo waliopewa maeneo haya wasichimbe kwa kubahatisha na hatimaye kuingia hasara, Serikali iko tayari ku-*share*, kuwapatia wachimbaji hawa hizo taarifa za utafiti wa haya maeneo ili wachimbaji wadogo wawe wanachimba kwa uhakika wakijua hapa kuna madini na kuondokana na hali iliyopo sasa hivi ambapo wanachimba kwa kubahatisha na hatimaye wanapata hasara?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu, Wizara ya Madini, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selemani Zedi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kampuni kubwa na za kati ambazo zinamiliki maeneo ambayo ni ya utafiti sisi sasa hivi kama Serikali tumeamua kuyarudisha, kwa yale maeneo ambayo yalikuwa hayafanyiwi kazi, tumewarudishia wachimbaji wadogo waweze kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amehoji kwa nini tusiwape *data* zile wachimbaji wadogo kwa ajili ya kuzitumia kwa maana ya kuchimba bila kubahatisha. Ni kwamba *Geological Survey of Tanzania (GST)* ambayo iko chini ya Wizara yetu ina ripoti nyingi za maeneo mbalimbali ya uchimbaji. Tunawaomba wale ambao walikuwa tayari wameshaanza kufanya utafiti watupe zile *data* walizozipata katika maeneo waliyofanyia utafiti. Kwa kweli *data* tunazo, kwa wachimbaji wanaotaka kupata *geological data* au *report* kutoka *GST* waje wafuate taratibu na watapewa *data* hizo na waweze kuchimba bila kubahatisha waweze kujipatia tija katika uchimbaji.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hussein Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wachimbaji wa Msalala kero zao

zinafanana kabisa na kero ya Wilaya ya Nyang'hwale; nataka kujua ni lini Serikali itatoa leseni kwa wachimbaji wadogo wa maeneo ya Bululu, Ifugandi, Kasubuya, Isonda, Nyamalapa, Lyulu, Lubando na Iyenze ili hao wachimbaji waweze kupata hizo leseni na kuchimba ili waweze kuwa na uhakika wa uchimbaji wao na waweze kupata mikopo kutoka benki waweze kuchimba kisasa?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Stanslaus Nyong'o.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyong'za la Mheshimiwa Amar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumetenga maeneo mengi na tumetenga maeneo makubwa, zaidi ya maeneo matano katika maeneo hayo.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyozungumza katika majibu ya swali la msingi, nimewaomba wananchi wa maeneo hayo wachangamkie hii fursa, waje waombe tuwagawie maeneo haya. Mpaka sasa hivi tuna maombi mengi ambayo tayari yamekwishatolewa na sisi sasa hivi tuko katika mchakato wa kuwagawia wachimbaji wadogo na ni maeneo ambayo ni mazuri, yana *reserve* ya kutosha na wataweza kuchimba kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo bado tunaendelea kuweka mchakato mzuri wa kuweza kufanya *resource estimation* katika maeneo mbalimbali ya uchimbaji ili tupate uhakika wa *reserve* na benki ziweze kuwaamini hawa kutokana na *data* ambazo tunaweza kuzitoa katika *geological reports* zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa fursa au kuwaeleza wananchi wa maeneo haya kwamba, wachangamkie fursa tuweze kuwagawia maeneo ya uchimbaji.

MWENYEKITI: Ahsante. Bado tuko Wizara hiyo hiyo ya Madini, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi.

Na. 52

Serikali Kuwaunga Mkono Wachimbaji Wadogo wa Busiri – Biharamulo

MHE. OSCAR R. MUKASA aliuliza:-

Wananchi wa Kijiji cha Busiri, Wilayani Biharamulo ni miongoni mwa Watanzania ambao wanaendesha maisha kwa shughuli za uchimbaji mdogo kama ilivyo kwa wenzao wengi na kwingineko nchini. Uchimbaji mdogo wa Busiri unahitaji kuungwa mkono na Serikali kimkakati:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaunga mkono wachimbaji wadogo wa Busiri na ni upi?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuwatembelea wananchi wa Kijiji cha Busiri ili kuwaelewesha ni namna gani itaanza utekelezaji wa mpango huo wa kuwaunga mkono wachimbaji hao?

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali ina mikakati mingi ya kuwaunga mkono wachimbaji wadogo nchini wakiwemo wachimbaji wa Kijiji cha Busiri, Wilaya ya Biharamulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mkakati wa kuwasadia wachimbaji wadogo nchini kupitia Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) limenunua mtambo mkubwa wa

kusaidia kufanya utafiti wa kina kwa kuchoronga miamba kwa bei nafuu ili kubaini mashapo zaidi na hivyo kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini inakamilisha uandaaji wa kitabu cha madini yapatikanayo Tanzania, toleo la nne, ambacho kinaonesha uwepo wa madini katika mikoa, wilaya, vijiji, hivyo kusaidia wananchi na wachimbaji wadogo ikiwemo wa Kijiji cha Busiri kutambua madini yaliyopo katika maeneo yao na matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (*SMMRP*), inakamilisha kujenga vituo vya umahiri katika Wilaya za Bukoba, Bariadi, Songea, Handeni, Musoma, Mpanda na Chunya ili kuwawezesha wachimbaji wadogo kujifunza kwa vitendo. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara kwa wachimbaji wadogo ili wanufaike zaidi na kazi ya uchimbaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mukasa.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti ilishafanya utafiti Wilayani Biharamulo ikiwemo eneo la Busiri na ripoti ipo; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema *STAMICO* imenunua mtambo utakaosaidia wachimbaji kuongeza uzalishaji, je, Serikali iko tayari sasa kupeleka mtambo huo sambamba na kwenda na Waziri ili tukaweke mipango vizuri pale ili tuanze shughuli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Waziri amesema Vituo vya Umahiri vinaanzishwa na kwenye Mkoa wa Kagera ni mmojawapo lakini bahati mbaya siyo Biharamuro ambapo ndiko *reserved* kubwa ya madini ya dhahabu ipo. Je, Serikali

inaweza ikatuambia ni kwa nini Kituo hicho cha Umahiri hakikuwekwa Biharamulo? Kwa sababu kuweka kiwanda cha korosho Bukoba au kiwanda cha kupaki senene Mtwara ni jambo ambalo linaweza lisiwe na tija.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Madini.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na *STAMICO* tuko tayari kabisa kupeleka mtambo huo katika maeneo hayo kwa ajili ya utafiti. Waletе maombi na sisi tupo tayari kupeleka mtambo huo kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa amehoji kwa nini Kituo cha Umahiri tumekiweka sehemu nyingine na wala si Biharamuro. Kwa kweli kituo hicho tumekiweka katika Mji wa Bukoba na kitaendesha mafunzo yake katika Mji wa Bukoba kwa sababu tumeangalia sehemu ambayo ni *center*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera ni mkubwa, tuna uchimbaji mwingine mfano wa *tin* kutoka Kyerwa, dhahabu kutoka Biharamuro na maeneo mengine. Kwa hiyo, pale ni *center* ambapo wachimbaji watakutana na ni rahisi kufika Bukoba. Kama ilivyokuwa katika huduma zingine za kimkoa kutoka wilaya mbalimbali wanakusanyika pale Bukoba. Kwa hiyo, tuliamua hivyo kwa sababu pale ni *center*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nimhakikishie tu Mheshimiwa Oscar kwamba tupo pamoja na yeye na tutakwenda na tutashirikiana naye na tufanya kazi pamoja kuwasaidia wapigakura wake. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha na pia tumepitiliza sana. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni wa Waheshimiwa wa Bunge. Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Mwita Waitara, Naibu

Waziri Ofisi ya Raisi (TAMISEMI) ambao ni viongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kutoka Mkoa wa Mtwara wakiongozwa na Mwenyekiti wa CWT Mtwara Ndugu Zahabu Christopher. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Doto Biteko, Waziri wa Madini wakiongozwa na Ndugu Elias Wadutya. Wageni wa Mheshimiwa Doto karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Angellah Kairuki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) ambaye ni Waziri Mkuu wa Serikali ya Wanafunzi Chuo cha Madini Dodoma, Ndugu Kalori Magije. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Ally Keissy ambaye ni Katibu Mwenezi wa CCM, Wilaya ya Karagwe kutoka Mkoani Kagera, Ndugu Joshua Mushenyera. *(Makofi)*

Wageni 63 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Obadia Chitalya. Wanamaombi karibuni sana endeeleni kuiombea nchi yetu na Bunge. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni Wanakwaya wa Morovian wakiongozwa na Mchungaji Isaac Siame. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambae ni rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Novatus Igosha. Bwana Igosha karibu. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Mary Chatanda kutoka Korogwe Mkoani Tanga wakiongozwa na Balozi wa Shina wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Ndugu Ramadhani Hamisi. Korongwe karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Rashid Shangazi kutoka Jimboni kwake Mlalo, Mkoani Tanga wakiongozwa na Ndugu Seif Shaaban Khamisi. Karibuni. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Aida Khenani ambaye ni ndugu yake kutoka Mkoani Rukwa, Ndugu Jackline Tung'ombe. Ndugu Tung'ombe Jackline karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Yassin Yassi. Ndugu Yassin karibu sana. *(Makofi)*

Tuna taarifa ya mabadiliko ya uongozi wa Chama cha CUF humu Bungeni ambayo imesainiwa na Mheshimiwa Rukia Ahmed, niwatangazie kwamba Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk atakuwa Mwenyekiti wa Wabunge hao; Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed atakuwa ni Katibu wao; Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo atakuwa ni Mweka Hazina na Ndugu Kiza Hussein Mayeye atakuwa Mnadhimu wa Bunge wa CUF humu Bungeni. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Msiniingize katika hayo malumbano yenu, sitaki. *(Makofi)*

Tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa imani ya Kikrito, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada anawatangazia Wabunge wote kuhudhuria Ibada katika *Chapel* ya Pius Msekwa leo Jumanne tarehe 9 Aprili, 2019 mara tu baada ya shughuli za Bunge kusitishwa mchana huu.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyonayo, nisime tu leo ratiba yetu imebanana kweli kweli, nawaomba sana hata wale ambao mpo kwenye orodha ya kuchangia kwenye orodha ya vyama vyenu hatutaweza kuwapeba wote, tutachukuwa wawili labda mmoja kwa sababu Serikali itaanza kujibu baadhi ya hoja zenu kwa sababu jioni Mheshimiwa Waziri Mkuu atahitimisha hoja yake lakini pia tutaingia kwenye kupitisha mafungu yanayoombewa pesa yaliyo katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Ofisi ya Waziri Mkuu

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia sasa hivi nitajitahidi ili nimalize shughuli hizi by saa 7.00. Naanza na Mheshimiwa Selemani Bungara atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Amar na Mheshimiwa Kubenea ajiandae.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kilwa Kusini kwa kuongea nao kwa muda mfupi baada ya sintofahamu ya chama chetu ya muda mrefu na hatimaye mgogoro umemalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Jaji kwa kutumia hekima kuomaliza mgogoro kwa njia ya kisayansi. Sasa chama ni kimoja na Wabunge wa CUF ni Wabunge wa CUF hakuna lile swali la CUF gani, sasa hivi CUF ni moja. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Jaji aliyehukumu kesi hii. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachangia hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 15 umezungumzia hali ya kisiasa na Mheshimiwa Waziri Mkuu amejisifu kwamba hali ya kisiasa ni nzuri na kulikuwa na chaguzi za marudio na CCM imeshinda kata 230, CHADEMA kata moja, CUF hakuna kitu. Mimi siamini kwamba ushindi huu wa kata 230 na CHADEMA kushinda kata moja kwamba uchaguzi huu ulikuwa huru na wa haki. Siamini kabisa na hali ya kisiasa katika nchi yetu ni mbaya mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano katika Wilaya yangu ya Kilwa tulingombea kata tatu na CCM zote wakashinda. Hata hivyo, Polisi waliojaa katika uchaguzi huo wa kata tatu utasema kuna vita ya Vietnam na Marekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchaguzi huo *Janjaweed* wa CCM waliwateka watu watatu. Tarehe 27 walimteka kijana mmoja anaitwa Abdulrahman Bungara, wakampiga, ni mwanachama wa *CUF*, wakamnyang'anya saa na hela. Tarehe 29 hao hao watu wa CCM wakampiga kijana mmoja jina lake Shaban Mkongo wakamnyanganya fedha. Tarehe 2 siku ya uchaguzi walimteka Juma Ngondae, wakampiga na wakamfikisha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wote tulifungua mafaili ya kesi lakini mpaka leo hajakamatwa mtu hata mmoja. Waliokuwa wanafanya matukio hayo wanajulikana na gari waliyokuwa wakitumia kuwateka watu hao inajulikana na gari hiyo ni ya Mbunge mmoja ambaye yupo humu humu ndani. Tumefungua kesi lakini mpaka leo hawajakamatwa lakini mwenye gari tunamjua ni ya aliyekuwa Mbunge wa *CUF* sasa hivi yupo CCM, gari yake tunaijuwa ndiyo iliyotumika kuteka watu wote hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zikaja kata zingine tatu, wagombea wetu wakarudisha fomu na ndiyo niliyowapeleka kurudisha fomu. Siku ya siku wakasema fomu za *CUF* zote hazikurudishwa na wagombea wa CCM wamepita bila kupigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapojisifu wewe Waziri Mkuu kwamba tulipita, upitishaji wenyewe wa kunyang'anya, hakuna siasa safi na uongozi bora katika nchi hii. Tunaamini kabisa kwa Tume hii ya Uchaguzi 2020 tegemeeni kutakuwa na vita kubwa sana kati ya wananchi na watu wa Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Uchaguzi Mdogo ndiyo mnachukua Jeshi zima, mnapeleka Kilwa Kivinje Jeshi zima,

Kilwa Kivinje mnaleta Jeshi zima, je, Uchaguzi Mkuu mna Jeshi ninyi la kusambaza Tanzania nzima, jeshi hilo mnalo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa sana CCM inashindaje? Nyavu za watu mnachoma moto, watu mnawateka, mnawapoteza, korosho zao hamuwalipi vizuri, wakulima mnawauzi, wafanyakazi mishahara hamuwapi, wavuvi...

MWENYEKITI: Wewe na mimi ndiyo nakumaliza hapo hapo, ahsante kwa mchango wako, tunaendelea.

WABUNGE FULANI: Aaaaaa.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Hata bila kengele?

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Sasa ikiwa kwamba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selemani, muda wako umeisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa ulikuwa bado.

MWENYEKITI: Hapana, tulia Mheshimiwa. Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/2018 ambayo sasa tunaelekea kuandaa bajeti mpya unakuta katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Serikali ilikusanya takribani shilingi trilioni 17 na matumizi yalikuwa shilingi trilioni 18, hii ni kwa mujibu wa kitabu hiki. Kama mapato yalikuwa shilingi trilioni 17.9 matumizi yakawa shilingi trilioni 18.7 maana yake ni kwamba nakisi ya bajeti yetu ilikuwa inakaribia shilingi trilioni 1 na hiyo ama ipatikane kutokana na mikopo ama misaada kutoka nje, matokeo yake bajeti imeshindwa kutekelezwa. Ukisoma

bajeti yote, mishahara na matumizi mengine ya Serikali karibu fedha zote zilizokusanywa zimetumika katika matumizi ya mishahara na matumizi mengine ya madeni ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isiyofikia malengo ya makusanyo yake haiwezi kutekeleza bajeti yake kikamilifu. shilingi trilioni 6 ambazo zilitengwa kwa ajili ya maendeleo hizi zote maana yake hazipo katika makusanyo ya Serikali, zenyewe ni lazima zipatikane ama kutokana na mikopo ama kutokana na misaada kutoka nje. Misaada sasa imekuwa shida kutokana na mahusiano yetu kuwa siyo mazuri na nchi wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye bajeti, kwa mfano, uvuvi, makadirio yalikuwa shilingi bilioni 7.1, fedha za ndani shilingi bilioni 3, fedha za nje shilingi bilioni 4, zilizotoka shilingi bilioni 4 maana yake pengine Serikali haikutoa hata shilingi katika uvuvi. Matokeo yake Serikali imeenda ku-*deal* na wanaoitwa wavuvi haramu, uvuvi watu hawawezi tena. Hatukuweza kutoa mafunzo tumeishia kulipa mishahara, matokeo watu wanalipwa mishahara, wanakaa ofisini wanasoma magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye kilimo, makadirio ni shilingi bilioni 98.1, zilizotoka ni shilingi bilioni 41.2 sawasawa na asilimia 42 *plus*. Sasa kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili. Kwenye kilimo ndiko kwenye miwa, kwenye sukari; kwenye kilimo ndiko kwenye chakula, Serikali inashindwa kuwekeza kwenye kilimo, tunategemea wahisani, halafu matokeo yake tunasema tumetekeleza bajeti yetu, tunakaa hapa tunajisifu, tunasema mwakani kusiwe na uchaguzi, tunatumia shilingi milioni 800 Dola za Marekani kuagiza chakula nje, karibu shilingi trilioni 1.8.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mwenyekiti taarifa.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo,...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kubenea, subiri kidogo. Taarifa Mheshimiwa Ulega.

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Kubenea, kwa faida yake na kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge wengine kutokana na kauli aliyoisema kuwa Serikali haiwekezi na hivyo kupelekea wataalam katika Wizara kama vile ya Uvuvi, wanakaa wanasoma magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa kuwa katika Wizara ambazo Serikali imetenda vyema, hata kupelekea kuvuka malengo katika utekelezaji wa kazi, ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika mwaka wa 2018/2019 ambao sasa tupo katika robo ya mwisho. Idara Kuu ya Mifugo imetengewa kukusanya pesa za maduhuli ya Serikali takriban shilingi bilioni 18. Mpaka hivi sasa tunavyozungumza, tumeshakusanya shilingi bilioni 26. Maana yake ni kwamba tuko zaidi ya asilimia 140. Idara kuu ya Uvuvi ilipangiwa kukusanya shilingi bilioni 16, mpaka sasa hivi tumeshakusanya zaidi ya shilingi bilioni 24. Maana yake tuko zaidi ya asilimia 110. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Mbunge anaposema kuwa watu wamekaa wanasoma magazeti, ni kwa sababu sio mfuatiliaji wa haya mambo. Nampa nafasi afuatilie zaidi ili aweze kuona mchango chanya unaotokana na Idara kubwa hizi mbili kwa mapato ya Taifa letu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu. Anaposema maduhuli, maana yake ni kodi, maana yake ni faini. Haya siyo makusanyo yanayotokana na fedha za kodi, ni faini. Ndiyo maana Ziwa Victoria Tanzania inamiliki zaidi ya asilimia 50 ya Ziwa Victoria; Uganda wanamiliki asilimia 33; na Kenya wanamiliki asilimia 6. Tokea Serikalli ya Awamu ya Tano iingie

madarakani, viwanda saba vipya vimefunguliwa Uganda na Watanzania, kwa sababu ya urasimu uliopo kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi; kwa sababu ya kuweka sheria za operesheni hizo za wavuvi. Watu wamekimbia nchi wameenda kuwekeza Uganda kwa sababu ya faini hizo za shilingi bilioni 20 anazodai hapo Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapozungumza, hii niliyosoma, shilingi bilioni tatu ni ya Wizara yenyewe, kwamba fedha iliyopelekwa ni shilingi bilioni tatu, siyo ya kwangu mimi. Sasa anapozungumza kwamba wamekusanya, kukusanya maduhuli, maduhuli sijui anaelewa maana ya maduhuli? Maduhuli siyo kodi ya kila siku ya Serikali, ni vyanzo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona niachane naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndiyo uti wa mgongo. Pembejeo zote zinazopatikana kwenye kilimo...

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agness, taarifa.

T A A R I F A

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mwongaji, pale aliposema kwamba Tanzania hatuna mahusiano mazuri na nchi wahisani. Labda kama hana kumbukumbu nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majuzi *Chancellor Merkel*, Rais wa Ujerumani, aliipongeza Tanzania kwa kuwa na mahusiano mazuri na nchi nyingine na kwamba uchumi wetu umekua sana. Pia nampa taarifa kwamba juzi tumefungua Ubalazi mpya...

MWENYEKITI: Imetosha, taarifa ni moja tu bwana.

MHE. AGNESS M. MARWA: ...Cuba ambao yeye anapaswa kuji...

MWENYEKITI: Hapana taarifa ni moja tu.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kubenea, taarifa moja tu ile ya kwanza.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi hiyo taarifa wala sina sababu nayo kuipokea kwa sababu mimi nimepokea taarifa ya Serikali yenyewe, Mheshimiwa Waziri ameeleza ndani ya bajeti kwamba mahusiano yao siyo mazuri na wahisani, kwa hiyo, wahisani hawatoi hela vizuri. Hata hii inathibitisha.

MWENYEKITI: Kwenye ripoti gani hiyo wewe Mheshimiwa?

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ni...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kubenea, hebu nisaidie na mimi ili *record* ikae vizuri. Kwenye taarifa ipi?

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mradi wa Mheshimiwa Zitto Kabwe, alikuwa na mradi kule Kigoma, ambao...

MWENYEKITI: Hapana. Mheshimiwa Kubenea, hapa tuna hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe niambie tu katika andiko.

MHE. SAED A. KUBENEA: Nimeiondoa, nichangie.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Haya.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimemsikia Mheshimiwa Rais anasema kwamba viwanda vyote ambavyo vimebinafishwa na Serikali na wale ambao walipewa kazi ya kubinafisha viwanda hivyo ambao walibinafishiwa viwanda hivyo, hawakuviendeleza wavirejeshe Serikalini. Mheshimiwa Rais akaomba radhi kwa niaba yake binafsi na kwa niaba ya watangulizi wake kwa mambo ambayo yalifanyika katika nchi katika uuzaji na ubinafishaji wa mali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amesahau jambo moja kubwa sana ambalo limefanyika katika nchi hii. Nyumba za Serikali zilizouzwa Rais hajasema zirejeshwe, tunaomba nyumba zote za Serikali zilizouzwa kiholela na kienyeji, zirejeshwe mikononi mwa Umma. Nyumba hizi waliouziwa...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Muda ndiyo huo Mheshimiwa. Muda wako umekwisha Mheshimiwa Kubenea. Hata nimekulindia na ule wa taarifa, umekwisha. Ahsante.

Mheshimiwa Hussein Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza kabisa, niweze kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kunipa afya njema na kuweza kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuipongeza kwanza hotuba ya Waziri Mkuu, imesheheni mambo mazuri. Serikali yetu imefanya kazi vizuri, labda tu kabla sijaingia kwenye kuchangia, wachangiaji wawili waliotangulia, wamesema maneno mengi lakini hakuna hata neno moja la maana kwa sababu hotuba ya Waziri Mkuu imeonyesha mafanikio ya nchi hii. Cha ajabu wao kazi yao ni kuponda kila jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukawa una macho lakini huoni, unaweza ukawa una masikio lakini husikii. Cha ajabu ni kwamba hawa watani zetu wa jadi walisema mzigo mzito mpe Mnyamwezi na Mnyamwezi ameubeba mzigo huo na amefanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo amefanya. Nadhani pia wanazidi kumkufuru Mungu kwa sababu hakuna mwanadamu aliyekamilika, lazima mwanadamu awe na upungufu. Kilichotakiwa ni kueleza mafanikio ya Serikali, lakini pia kuishauri maeneo ambayo yana upungufu kidogo. Kwa hiyo, ndugu zetu hao kazi yao ni kulalamika na wanasema 2020 tutakuwa na jeshi gani la kuweza kumudu uchaguzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawahakikishieni kwamba uchaguzi wa 2020 asilimia kubwa ni CCM. Wananchi wanashuhudia Serikali ya CCM ni kazi ipi ambayo inafanywa nitazungumza kazi nzuri ambazo zimefanywa kwa kipindi cha miaka minne. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeweza kuanzisha elimu ya msingi bila malipo hadi sekondari. Hayo ni mafanikio mazuri na wananchi ni mashuhuda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu kidogo katika elimu ya bure. Tunaishauri Serikali ijaribu kuiangalia huo upungufu kwa sababu wimbi la wanafunzi kuandikishwa na kuingia mashuleni limekuwa kubwa. Pamekuwa na upungufu kidogo wa madarasa, madawati, Walimu na vyoo. Huu ndiyo ushauri tunatakiwa tuishauri Serikali ijaribu kuangalia na kuboresha maeneo kama hayo. Siyo kukaa mnalalamika kwamba Serikali haijafanya lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajaribu kuzungumzia kwenye upande wa afya. Serikali imeweza kupunguza gharama za wagonjwa kuwapeleka nje, imeweza kuboresha Hospitali zake za Rufaa, tumeweza kujenga shule, kujenga Hospitali nyingi za Wilaya na Vituo vya Afya. Leo hii tumeweza ku-save pesa nyingi za kuwapeleka wagonjwa wetu nje. Hiyo ni kazi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tujaribu tu kuangalia upungufu kidogo uliopo. Mfano, katika Wilaya yangu ya Nyang'hwale, vifaa vipo lakini tumepungukiwa kama vile *x-ray*. Hatuna *x-ray*. Naiomba Serikali iweze basi kutuletea *x-ray* katika Kituo chetu cha Afya pale Kaluma. Huu ni upungufu lakini kazi kubwa imefanywa, dawa zipo za kutosha, majengo mazuri yapo na madaktari wapo pamoja na kwamba hawatoshelizi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijaribu kuzungumzia upande wa madini. Upande wa madini naipongeza Serikali imeweza kuweka utaratibu mzuri kuwasaidia wachimbaji kuondoa kero zao. Bado naiomba Serikali, kuna upotevu mkubwa sana ambao unapoteza mapato ya Serikali kwa kuchelewa kuwapa maeneo ya wachimbaji wetu kutoa leseni na kuweza kuwatambua. Kwa sababu wachimbaji walioko wengi sana katika Wilaya ya Nyang'hwale hawajarasimishwa na hawana leseni. Kwa hiyo, upotevu ni mkubwa na Serikali wala haiwatambui. Naiomba Serikali sasa iweze kuwatambua hao wachimbaji wadogo kwa kuwapatia leseni ili waweze kutambulika na waweze kuikusanyia Serikali mapato mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nyang'wale, Serikali imefanya kazi nzuri sana, lakini kuna upungufu kidogo. Tuna mradi wetu mkubwa wa maji ambapo mradi ule umetengewa takribani shilingi bilioni 15.5, lakini mradi huo leo una zaidi ya miaka minne haujakamilika. Wakandarasi wako kazini wanailalamikia Serikali yao kwamba inawacheleweshea malipo. Nataka nijue, ni kweli Serikali inachelewesha malipo ama Makandarasi ni matapeli? Naomba nipate majibu wakati Waziri atakapokuja kufanya majumuisho hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mapambano dhidi ya Ukimwi, nilikuwa nataka nitoe ushauri. Serikali inatoa fedha nyingi sana kupambana na suala hili la Ukimwi. Suala hili tujaribu kuliangalia. Nataka nitoe ushauri, nitakuja kuchangia zaidi kule mbele. Kuna masuala ambayo yanasababisha kuongezeka. Pamoja na kwamba tunapambana, lakini bado

kuna maeneo ambayo yanatakiwa yafanyiwe kazi. Mfano, kuna magulio maeneo mbalimbali hapa nchini. Magulio haya yanaanza saa 10.00 jioni na yanakwenda...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wetu ndiyo huo.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie machache kwenye mjadala ulio mezani asubuhi ya leo. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya nzuri siku ya leo, lakini niendeleo kumwomba anilinde kunipa afya njema mpaka siku nitakayopiga kura ya bajeti ili nami kwa mara ya kwanza niweze kuwatendea haki wananchi kwa kupiga kura ya ndiyo kwenye bajeti hii. *(Makoff)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze sana Serikali kwa namna ambavyo imemwaga miradi mingi Majimboni kwetu katika kuboresha huduma za jamii. Imeweka fedha nyingi sana kwenye miradi ya afya na huduma za afya kwa kweli zimeboreka kwa kiasi kikubwa. *(Makoff)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kabla ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani, ulikuwa ni utaratibu wa kawaida wamama wanapoenda kujifungua, kubeba vifaa vya kujifungulia, kubeba mabeseni na vitu vya namna hiyo, jambo ambalo kwa sasa limekuwa ni historia. Wamama wanakwenda kujifungua, wanapata huduma zote hospitalini na hawachajiwi. Jambo hili limekuwa ni la kihistoria na wananchi wa Temeke wanaishukuru sana Serikali ya Awamu

ya Tano kwa namna ambavyo imejikita katika kuboresha huduma za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kwenye huduma za afya, lakini pili, kwenye uboreshaji wa miundombinu. Nikitolea mfano tu wa huko huko Jimboni kwangu Temeke, kuna ujenzi mkubwa wa miundombinu, achilia mbali daraja la juu (*flyover*) ambalo limerahisisha sasa foleni zilizokuwa zikiwakabili watu wakati wakwenda *Airport*, lakini barabara nyingine zinazoungana na zenyewe pia zinaendelea kujengwa. Wakandarasi wako *site* wanaboresha miundombinu. Tunaipongeza sana Serikali kwa jambo hili lakini Waziri Mkuu na Ofisi yake kwa namna ambavyo wanakuja kusimamia na kuhakikisha kwamba ujenzi na matumizi ya fedha hizi za Serikali unakuwa ni wenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze sana Tume ya Uchaguzi kwa namna ambavyo wamekuwa wanafanya kazi zao vizuri. Tume ya Uchaguzi inafanya kazi zake vizuri na mfano mkubwa ni kwenye chaguzi hizi chache ambazo zimepita hivi karibuni ambavyo wamezisimamia vizuri. Sisi Wandengereko huwa tuna usemi wetu tunasema, “maiti ya Kimakonde haikosi mchawi.” Ni kwa maana pamoja na kazi nzuri mnayoifanya, bado wapo watu ambao wataendelea kuwakosoa. Wanaowakosoa kwa kusema kwamba Tume ya Uchaguzi inapendelea, ni hao hao ambao nanyi mliwahi kuwatangaza na leo ni Wabunge huku. Kwa hiyo, hayo...

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Tusikie taarifa.

TAARIFA

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji anayezungumza, mimi binafsi amenishtua kidogo aliposema maiti ya Mmakonde haikosi mchawi.

Nataka ufafanuzi, atufafanulie tafsiri yake ni nini hapo? Ahsante.

MWENYEKITI: Hilo ni swali, mtaeleza huko nje. Endelea Mheshimiwa.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sasa ombi langu kwa Tume ya Uchaguzi, nilikuwa nataka sasa iende mbali zaidi. kwa kuwa imefanikiwa katika usimamizi wa taratibu za uchaguzi, iende mbali kuhakikisha kwamba utekelezaji wa mambo ambayo viongozi waliochaguliwa unaendelezwa hata baada ya wao kumaliza muda wake. Kwa mfano, tunapopata viongozi mahiri kama Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ambaye anaanzisha vitu vingi vikubwa, tena vyenye tija kwa Taifa ambavyo vingine vitakuwa bado havijakamilika wakati muda wa miaka 10 unakwisha, ni vizuri Tume ya Uchaguzi ikaandaa mfumo ambapo atakayekuja sasa madarakani naye asianze na vitu vipya, aendeleze yaliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia kuweka Makao Makuu Dodoma. Mpango huu ni endelevu, nyumba na Ofisi za Serikali zinaendelea kujengwa, zipo zitakazokamilika na zipo ambazo zitakuwa hazijakamilika mpaka Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli anaondoka madarakani. Sasa tusipoweka mfumo mzuri kwamba anayekuja naye aendeleo mle mle, maana yake anaweza akaja mwingine akaanzisha vitu vipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tumeweka sheria ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu, lakini sheria zinabadilika, maana yake afadhali lingekuwa ni jambo la kikatiba, utaratibu wake kidogo ni mgumu, lakini sheria zinaweza zikaja *amendments* zikabadilisha tukarudi tena Dar es Salaam. Jambo hili litakuwa ni hasara kubwa kwa Taifa. Sasa ni vizuri mambo haya yakawekewa utaratibu mzuri.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtolea, taarifa.

T A A R I F A

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mtolea kwa ushauri ambao ametoa kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwamba angependa sana kuwe na utaratibu ambao utawafanya viongozi ambao amesema mahiri baadaye na wao vitu ambavyo wamevianzisha ili viendeleo. Akumbuke kwamba hata waliomtangulia Mheshimiwa Dkt. Magufuli viko walivyovianzisha naye aliviacha. Kwa mfano, miradi ya gesi ambayo Serikali ya nchi hii ilizunguka nchi nzima kuwaambia Watanzania kwamba sasa gesi ikishapatikana tutakuwa hatuna tena tatizo la umeme katika Taifa hili...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakajoka!

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: ...lakini ameacha na sasa hivi tuna mradi wa *Stiegler's Gorge* unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipuuze hiyo taarifa kama ambavyo nampuuza na yeye mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachozungumza ni kwamba, tunahitaji mambo ya msingi, mambo makubwa ambayo yameanzishwa hivi sasa ambayo kila Mtanzania anayaona na anakubali kwamba yana tija kwa kizazi hiki na kizazi kijacho yaweze kuendelezwa. Yasiishie pale ambapo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli atamaliza muda wake. Kama tunashindwa kumwongezea muda yeye aendeleo, basi tuwe na mfumo ambayo Ofisi kwa maana ya Rais kama taasisi itaendeleza yale ambayo aliyaanzisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu si muda wa sisi kwenda mbele na kurudi nyuma tena, tumeshapiga *mark time* kwa muda mrefu. Sasa hivi tumepata mtu ambaye ametuonesha njia, ni vizuri tukaenda nae. Watu kama Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hawazaliwi kila wakati, akipita huyu, inaweza kupita miaka 50 au miaka 100 tusipate mtu mwenye maono ya namna hii. Kwa hiyo ni vizuri tukaona kwamba, haya maono yake... (*Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kadutu, dakika tano.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtemi Chenge nakushukuru kwa kunipa hizo dakika tano niweze kusema machache, japo nilikuwa na mlolongo mrefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mwaka jana nilipiga kelele juu ya Maziri kutofika Jimboni Ulyankulu, lakini leo napenda kuwashukuru Mawaziri karibu watano, sita, wamefika Jimboni Ulyankulu nawashukuru sana wamekuja kunitutia moyo kwa kazi zetu hizi za maendeleo, lakini nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa usimamizi wa shughuli za Serikali lakini kubwa zaidi ni lile la kuwa karibu sana na timu yetu ya Taifa. Kupitia yeye na Serikali niipongeze *TTF* ambayo nami ni sehemu yake. Tutaendelea kujipanga kuhakikisha timu yetu inafanya vizuri na niwaalike Waheshimiwa Wabunge mwezi Juni twende Misri kwenda kushangilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo kwa haraka haraka ni suala la umeme, ile spidi ya umeme vijiji inaelekea imepungua kabisa. Sasa niwaombe wenzetu wa Nishati wajaribu kuihuisha tena, kazi hizi za umeme zinaleta maendeleo makubwa sana kwenye vijiji vyetu, basi haraka uwepo na utekelezaji maana yake yawezekana Mawaziri wakasema, wakiondoka huku nyuma watendaji wakawa si watu wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mzuri wa uchimbaji bwawa pale kwenye Kijiji ya Ichemba, niombe sana Wizara inayohusika kumekuwepo na upembuzi, lakini toka wameondoka hatujui kinachoendea

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la barabara, kwa nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Kwandikwa, jirani yangu huyu, anapita kila wakati kuzikagua hizi barabara, Jimbo la Ulyankulu lina barabara kama tatu. Barabara ya Tabora Mjini kuja Ulyankulu; halafu barabara ya kutoka Kahama kwenda Ulyankulu mpaka Kaliua. Barabara hizi zinatusaidia kwa matatizo mbalimbali, jiografia ya jimbo la Ulyankulu si rafiki, nitatoa mfano, Kaliua tunajenga Hospitali ya Wilaya, tunajenga ofisi mbalimbali lakini wananchi wa jimbo la Ulyankulu hawapati huduma kule, wanapata Kahama pamoja na Tabora Mjini. Kwa hiyo, tunaposema maeneo ya utawala, najua hilo tumeshamwelewa Mheshimwa Rais, lakini najua mbele ya safari litakuja kukubalika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uchaguzi kwenye kata tatu bado nitaendelea kulisemea. Inakuwaje hawa watu wametupigia kura na Mheshimiwa Rais, lakini Serikali imewazuia kupiga kura kwa ajili ya Madiwani, jambo hili sidhani kama lina majibu yaliyonyooka na Serikali inapindisha pindisha. Hebu Serikali ije na ufumbuzi wa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Afya pamoja na TAMISEMI kwa kutupatia shilingi milioni mia nne, tumeweza kutengeneza kituo vizuri cha pale Ulyankulu. Lakini imetuhamasisha na sisi kama wananchi kujenga vituo viwili vya afya vingine kwa nguvu zetu. Bahati nzuri Wilaya ya Kaliua ni Wilaya inayoongoza kwa mapato ya ndani kwenye Mkoa wetu wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tumeweza kujenga shule za sekondari na shule za msingi, sasa tuombe tu Serikali iharakishe hasa kwenye shule ya msingi vile vikwazo vikwazo vya ubora na nini, watusaidie kuvipunguza ili watoto waweze kuendelea na masomo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kuendelea na mambo mengi, nisingependa kengele inikute. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kadutu.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa ujumla katika utekelezaji wa majukumu yake katika kipindi hiki cha miaka mitatu yanaridhisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unajikita katika kifungu 8.7, ukurasa 41 wa kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu, kuhusu huduma za uchumi; suala la migogoro ya ardhi kati ya wananchi na hifadhi/mapori tengefu. Katika Wilaya ya Malinyi/Morogoro wakazi wa vijiji karibu 18 vinavyopakana na Pori Tengefu la Kilombero wana mgogoro mkubwa wa marekebisho ya mipaka bado sio rafiki kwa wananchi. Sehemu kubwa ya mashamba yao yanayotumika kwa kilimo/ufugaji yamechukuliwa na *buffer zone* ya Pori Tengefu la Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa ni waathirika wa mabadiliko ya Sheria ya Wanyamapori ya 2009 ambapo sasa mashamba yao hayo ambayo walikuwa wakiyatumia hapo kabla ya 2009 yamenyang'amywa hivyo kusababisha kuwa na uhaba wa mashamba kwa shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali warejee tena upya zoezi la kurekebisha mipaka ya Pori Tengefu la Kilombero ili kupunguza upana wa *buffer zone* kwa kuyaachia mashamba hayo yarudishwe kaika ardhi ya vijiji kwa faida ya maendeleo na ustawi ya wakazi wa Wilaya ya Malinyi, karibu watu 92,000 wameathirika na mgogoro huu wa mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri walio chini ya ofisi yake kwa utendaji wao uliotukuka. Pia nipongeze hotuba yake nzuri na bora yenye dhamira ya kuifanya nchi hii ijitegemee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 42 ameonesha nia na dhamira ya Serikali ya kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo ya nchi yetu. Ipo dhamira ya Serikali ya kuunganisha mikoa yote kwa kiwango cha lami. Mkoa wa Singida unaungana na Mkoa wa Mbeya kwa njia ya barabara. Barabara hii imejengwa toka Mkoa wa Mbeya, Serikali ilionesha nia ya kuanza kujenga kutokea Mkoa wa Singida kutoka Mkiwa Itigi hadi Moranga kilometa 56.9 na mkandarasi alipatikana ambaye ni *SIMOHYDRO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuwa anafungua barabara ya Manyoni – Chaya kilometa 89 tarehe 25 Julai, 2017 alibaini mchakato wa zabuni ulikuwa na harufu mbaya na akatoa maelekezo yaliyosababisha barabara hii kutokujengwa au kuanza kujengwa hadi hivi leo. Je, ni lini sasa Serikali itaona ni vyema kuwatendea vyema wananchi wa jimbo langu kwa kuanza kujenga barabara hii.

Naomba sasa mwaka huu basi Serikali ianze ujenzi wa barabara hii ambayo ni muhimu sana katika kuunganisha Mkoa wetu wa Singida na Mkoa wa Mbeya. Barabara hii ndiyo pekee iliyobaki ya kuunganisha mkoa na mkoa ambayo ni ndefu kuliko zote Tanzania kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii tena kuipongeza Serikali na pia nimpongeze kipekee Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa utendaji wake na juhudi nyingi katika ujenzi wa miundombinu ya reli ya kisasa na ununuzi wa ndege na hata vivuko katika maziwa yetu.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kuhusu Sekta ya Kilimo; kwa kuwa mwaka huu Kanda ya Kaskazini hasa Mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro inakabiliwa na ukame kufuatia mvua za masika kutonyesha, nashauri Serikali iandae bajeti ya kutosha na kuweka utaratibu wa kuwaletea wananchi chakula cha bei nafuu toka mikoa yenye chakula cha kutosha mwaka huu.

Pili ni kuhusu Sekta ya Mifugo na Uvuvi; nashauri Serikali iwekeze katika uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo na uanzishwaji wa masoko ya ndani ya uhakika. Pia nashauri Serikali ipange bei elekezi kwenye bidhaa za mifugo na ipange bei ya kishindani kwa kulinganisha na bei ya bidhaa husika katika masoko ya nchi jirani kama vile Kenya. Vile vile nashauri bei ya nyama ya mbuzi, kondoo na ng'ombe kwa kilo ipangwe na Serikali na mifugo minadani iuzwe kwa kupimwa kwenye mizani na bei ya mifugo kwa mnyama hai (*live weight*) ipangwe na Serikali kama ilivyo kwa mazao ya kilimo (mazao ya biashara).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni Sekta ya Utalii; nashauri Serikali ipanue wigo wa biashara ya utalii kwa kuunganisha utangazaji wa vivutio vya utalii nchini ili pamoja na wanyamapori ambao ndio kivutio kikuu, pia tutangaze utalii katika misitu yetu ya asilia (*Nature reserves*) sambamba na utalii wa utamaduni (*cultural tourism*). Pia nashauri *channel* yetu ya utalii itangaze kwa lugha mbalimbali za mataifa yanayopenda utalii. Sambamba na hilo tuombe *airtime space* kwenye channel za Serikali za mataifa yanayopenda utalii na vivutio tulivyonavyo. Baadhi ya *Channels* hizo ni pamoja na *PBS* ya Marekani (*Public Broadcasting Service*), *BBC*, *DW* na *National Geographic Society*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, utitiri wa kodi uunganishwe ili kuwa na kituo kimoja (*one stop center*) na kodi moja jumuishi ili kuondolea wawekezaji na wateja usumbufu na urasimu usio wa lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Sekta ya Ardhi; nashauri Serikali iongeze bajeti na rasilimali fedha, vifaa na wataalam

wa kutosha hadi ngazi ya Halmashauri za Wilaya nchini ili kuongeza kasi ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi ya nchi yetu kulingana na Sera na Mpango wa Taifa wa Ardhi 2013 – 2033.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano ni Sekta ya Barabara; katika kufungua barabara zenye kufungua fursa za kiuchumi kwa wananchi, naomba Serikali itoe kipaumbele mwaka huu wa fedha kumalizia kipande cha barabara chenye urefu wa kilomita 41 zilizobaki kwenye barabara ya Sanya Juu hadi Kimwanga kuzunguka Mlima Kilimanjaro. Pia barabara ya Siha/Sanya juu – Longido (kilomita 56) ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, kuhusu Kazi, Ajira na Vijana; nashauri Serikali mgawo wa 10% ya mapato ya ndani ya Halmashauri zetu za Wilaya ambapo akinamama na vijana hupewa mikopo isiyo na riba kwa uwiano wa 4% kwa kila kundi na watu wenye ulemavu 2%. Nashauri watu wenye ulemavu wasikopeshwe hiyo 2% wanazogaiwa bali wapewe kama msaada (*seed fund*) wa kuwawezesha kuanzisha miradi ya kujikimu kimaisha. Kwa kuwa watu wenye ulemavu huwategemea ndugu na jamaa na watu wenye mapenzi mema kuwazungushia mitaji yao, mara nyingi kasi ya miradi huwa ndogo na pia uwezo wa kurejesha mikopo yao kwa wakati kuwa hafifu. Hivyo basi nashauri iwe sehemu ya *social welfare* na uwajibikaji (*CSR*) wa Serikali yetu kuwapa watu wenye ulemavu hiyo 2% kama msaada na siyo mikopo ya kurudishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira za moja kwa moja katika Utumishi wa Umma; nashauri Serikali iongeze bajeti ya kutoa ajira za moja kwa moja ili kuondoa upungufu mkubwa wa watumishi wa kada mbalimbali unaozikabili Halmashauri za Wilaya zetu na sekta mbalimbali za Serikali. Kwa kutoa ajira za moja kwa moja Serikali itaondoa changamoto kubwa iliyopo ya kuwa na utitiri wa watumishi wanaokaimu nafasi mbalimbali na kwa muda mrefu. Jambo hili linaathiri utendaji (*performance*) katika Halmashauri ya Wilaya yangu ya Longido ambapo zaidi ya 50% ya Watendaji wa Vijiji (*VEDS*) ni watumishi wanaokaimu nafasi hizo na kwa miaka mingi.

Pia kwenye idara za halmashauri tuna upungufu mkubwa na lundo la watumishi wanaokaimu nafasi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naomba kutamka kuwa naunga mkono hoja! Ahsante.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya 33, ukurasa wa 15 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge amezungumzia kuhusu marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa na utekelezaji wake ambao umeanza. Hata hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu haijzungumzia hatua iliyofikiwa katika kuandaa kanuni kufuatia marekebisho hayo ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni nyeti na tete, kwa kuwa wakati Muswada wa marekebisho ya sheria hiyo ulipotoka, Msajili wa Vyama vya Siasa aliwasilisha pia rasimu ya kanuni kabla hata ya sheria kutungwa. Baada ya kubaini kasoro hiyo, rasimu hiyo ilichukuliwa na Msajili. Hata hivyo, rasimu ya Kanuni hiyo ilionesha kwamba masharti mengi yaliyo kinyume na Katiba ya Nchi na ziada ya mambo yaliyokuwa katika Muswada na sheria yanakusudiwa kupenyezwa kupitia kanuni. Katika muktadha huo Waziri mwenye dhamana pamoja na Ofisi ya Msajili hawapaswi kujifungia na kuandaa rasimu, bali mchakato mzima wa marekebisho ya kanuni zinazohusu Sheria ya Vyama vya Siasa unapaswa kuwa shirikishi na vyama vya siasa viitwe kwa ajili ya majadiliano kuhusu suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya 36, ukurasa wa 17, Serikali imeeleza kuwa imekamilisha maandalizi ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Hii ni katika hotuba ya tarehe 4 Aprili, 2019 wakati ambapo tarehe 1 na 2 Aprili, 2019 nimeshiriki mkutano baina ya Wizara ya TAMISEMI na Vyama vya Siasa ambapo wadau tulitoa maoni ya marekebisho kwenye vifungu na vipengele vingi vya rasimu ya kanuni zilizowasilishwa. Aidha, tarehe 3 Aprili, 2019 Wizara ya TAMISEMI, ilikutana na Asasi za Kiraia na wadau wengine

kwa ajili ya kupokea maoni yao katika kikao ambacho kiliisha jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira hayo inawezekanaje tarehe 4 Aprili, 2019 isemwe Bungeni kuwa maandalizi ya kanuni za uchaguzi huo yamekamilika? Hotuba hii ya Waziri Mkuu sio ushahidi wa kwamba vikao vya wadau vimeitwa kwa kujikosha wakati ambapo tayari Serikali imeshafanya maandalizi ya kanuni za uchaguzi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inajitokeza pia katika aya ya 37 ambapo Waziri Mkuu ameeleza kuwa kanuni za uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura zimeandaliwa na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali Na. 792 na 793 ya tarehe 28 Desemba, 2018. Kanuni hizo ziliandaliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*) na kutangazwa bila kwanza wadau kupewa rasimu na kutoa maoni. Mwezi Machi, 2019 ndipo *NEC* ilikutana na vyama kupata maoni wakati tayari kanuni zilishatangazwa. Waziri Mkuu awasiliane na *NEC* kutoa majibu Bungeni ni lini marekebisho ya kanuni hizo yatafanyika kabla zoezi la uboreshaji haujafanyika nchi nzima. Aidha, naomba kupewa nakala ya Kanuni iliyotangazwa 28 Disemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Aya ya 92, ukurasa wa 44 wa hotuba ya Waziri Mkuu, Serikali imezungumzia kuhusu kuondoa msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Naunga mkono upanuzi wa barabara ya Kimara Mwisho – Kiluvya kilometa 19.2 kutoka njia mbili kuwa nane na ni vyema kiwango cha fedha katika bajeti kikaongezwa na kutolewa kwa wakati ili ujenzi ukamilike mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na ujenzi huo kuendelea, bado nasisitiza haja ya Serikali kuwalipa fidia wananchi waliobomolewa kupisha ujenzi wa barabara hiyo. Ombi hili la wananchi niliwasilisha mbele ya Rais tarehe 19, Desemba, 2018, wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa barabara hiyo. Rais alikataa ombi hilo kwa maelezo kwamba kesi ilishaamuliwa na Mahakama Kuu. Naomba Waziri Mkuu na Mawaziri wengine wenye dhamana wamkumbushe Rais

kuwa kesi anayoirejea wananchi waliohusika ni wa Kimara pekee waliofungua kesi haikuhusu eneo lote linalohusika na ujenzi hivi sasa na haihusu *substantive grounds* bali wananchi walishindwa kwa *technicalities*.

Mheshimiwa Spika, baadaye wananchi wa Mbezi walifungua kesi nyingine mwaka 2005 kupitia shauri Na. 80 katika Mahakama Kuu, Kitengo cha Ardhi na hukumu ilitolewa tarehe 31 Mei, 2013 ambapo wananchi walishinda. Pamoja na mambo mengine, mahakama ilitamka kuwa *the Highway Ordinance Cap 167, Government Notice No. 161* ya tarehe 5 Mei, 1967 ambayo hutumiwa na *TANROADS* kutwaa ardhi za wananchi bila fidia ni batili kwa kutofautiana na vifungu vya 15 na 16 vya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Rais alisema kuwa upana wa barabara wa toka mwaka 1932 uliingizwa kwenye Sheria ya Barabara mwaka 2007. Hata hivyo, ukipitia Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 haina kifungu kinachotaja upana wa Barabara ya Morogoro. Upana unaolalamikiwa sasa uko kwenye Kanuni ya Barabara za mwaka 2009 ambazo zinakinzana na Sheria ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 na sheria nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hayo, naomba Rais abadili uamuzi na kuwezesha wananchi hao kulipwa fidia. Kama Serikali haiwezi kulipa fidia kamili basi ifuate misingi ya haki na kuwalipa wananchi hao *ex gratia* kwa kuzingatia kuwa Serikali yenyewe ndiyo iliyoweka wananchi katika maeneo hayo toka wakati wa operesheni ya vijiji ambapo sasa imewaondoa bila ya kuwalipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine naamini Serikali imeona faida ya barabara za mlisho/mizunguko/pete katika kupunguza foleni kupitia Barabara ya Mbezi – Goba, Temboni – Msingwa – Msigani – Malamba Mawili mpaka Kinyerezi. Kwa umuhimu huohuo, naomba Serikali itenge fedha kwa barabara za Mbezi – Mpiji Magohe, Kibamba – kibwegere, Malamba Mawili – Kwembe na zingine zilizoko kwenye mpango wa barabara za mlisho (*feeder*),

mzunguko (*ring*) ambazo zitaishia barabara ya Morogoro inayojengwa zikiunganisha Wilaya ya Ubungo na Wilaya za Kinondoni na Ilala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya 115 ya hotuba ya Waziri, ukurasa wa 55 ameeleza kwamba hadi Februari, 2019 upatikanaji wa maji safi na salama katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine yanayohudumiwa na DAWASA imefikia asilimia 85. Kiwango cha asilimia 85 hakina ukweli ukilinganisha na hali halisi ya matatizo ya maji ilivyo. Hivyo, katika majumuisho Mheshimiwa Waziri Mkuu aeleze ni vigezo gani vimetumika kupata takwimu hizo kwa kulinganisha baina ya idadi ya kaya na watu katika Jiji la Dar es Salaam na hali halisi ya upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano wa Jimbo la Kibamba lenye kata sita ili Ofisi ya Waziri Mkuu ishirikiane na Wizara ya Maji na DAWASA kutoa majibu ya takwimu halisi na kuchukua hatua za kuongeza kwa haraka kiwango cha upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, katika Kata ya Goba, Mitaa ya Matosa Goba, Tegeta A na Kulungwa, maji hayatoki na uwekaji wa mabomba ya maji unakwenda kwa kusuasua. Hata katika maeneo ambayo wananchi walijitolea kuchimba mitaro na mabomba kuwepo, lakini maji hayatoki. Kwa hali hiyo upatikanaji wa maji Kata ya Goba hauwezi kuwa umefikia asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Kata ya Msigani, Mitaa ya Malamba Mawili, Kwa Yusufu na mitaa mingine mambomba ya maji hayatoi maji kwa kuwa hayajaunganishwa na bomba lenye maji kwa madai kuwa hakuna vifaa. Mradi uko chini ya kampuni ya India ambayo nayo imeipa kazi kampuni ya kutoka China. Kampuni hizi mbili zinatupiana mpira kuhusu ukamilishaji wa kazi. Aidha, baadhi ya vifaa vinasubiriwa mpaka vitoke India, hali inayofanya mashimo yaliyochimba kuweka mabomba mengine kuanza kujaa mchanga/ udongo. Hivyo, kata hii nayo haijafikiwa kwa asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Kata ya Mbezi Luis, Mtaa wa Makabe, mabomba ya inchi nane yamechimbwa ardhini toka 2017, lakini maji hayatoki na kuwa mtandao na mabomba kwenda barabara za ndani kwenda kuwafikiwa wananchi. Pia kuna ujenzi wa tanki ambao umesimama kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mtaa wa Msakuzi hakuna mtandao wa mabomba. Mtaa wa Luis wameunganishwa walioko kwenye mita 50 kwa mkopo lakini maji hayatoki katika bomba kubwa. Pia maeneo manne katika mtaa huo hayajauunganishwa na Bomba Kuu. Kata hiyo nayo maji hayatoki kwa asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Kata ya Kwembe, Mtaa wa King'azi B wanamaliza kufunga vizimba lakini maji hayatoki hata kwa walio pembezoni ya bomba. Hali iko hivyo maeneo mengi ya Mtaa wa Mji Mpya. Hivyo, kata hii nayo haina maji kwa asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Kata ya Kibamba Mitaa ya Hondogo, Kibwegere na mingine hakuna maji. Kibwegere walihidiwa toka 2016 kupelekewa bomba la inchi nane mpaka Daraja la Mpiji Magohe toka 2016 lakini kazi hiyo haijafanyika. Hivyo, napo haiwezi kuwa asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, Kata ya Saranga, Mtaa wa Saranga mabomba ndiyo kwanza yanatandazwa kwa kusuasua. Mtaa wa Kimara B, maji yakitoka ni mara moja kwa mwezi. Kwa ufupi kwa wastani huo haiwezekani Jimbo la Kibamba kama sehemu ya Dar es Salaam kuwa imefikiwa kwa asilimia 85. Hatua gani zitachukuliwa ili kufikia lengo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu pia inapaswa kumshauri Rais kuweka kipaumbele maalum kwenye maendeleo ya vijana na kuongeza fursa za ajira kwa vijana. Tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana lisipodhibitiwa kwa haraka litaleta madhara makubwa kwa nchi. Katika aya ya 138, ukurasa wa 65, programu ya kuendeleza vijana

imewezesha vikundi 755 tu ambavyo vimepatiwa shilingi bilioni 4.2 pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020 kiwango cha fedha katika mfuko wa maendeleo ya vijana kinapaswa kuongezwa. Katika kutumia mfuko huo, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu itoe mikopo pia kwa vikundi vya vijana katika Jimbo la Kibamba. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali inatarajia kuwezesha vijana kupata mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa vijana 46,950. Mpango huo wa mafunzo utekelezwe. Pia katika Jimbo la Kibamba na Ofisi ya Mbunge na Manispaa ya Ubungo tuko tayari kutoa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ya fursa za ajira, kiwango cha kutengeneza fursa hizo hakilingani na kiwango cha nguvu kazi ya vijana kinachoingia kwenye soko la ajira kwa mwaka. Aidha, kitendo cha jumla ya ajira 221,807 kuwa zimezalishwa kufikia Februari, 2019 huku ajira kwa sekta binafsi zikiwa 75,393, sawa na asilimia 34, kinadhihirisha kwamba programu ya kutengeneza ajira siyo endelevu. Mkakati endelevu wa kuibua fursa za ajira kwa vijana hauwezi kutegemea zaidi utekelezaji wa miradi ya Umma bali kutoa fursa kwa sekta binafsi hutengeneza ajira kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika hotuba yote ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hakuna mahali ambapo amezungumzia kuhusu Baraza la Vijana la Taifa kama nyenzo ya kuwaunganisha vijana kuanzia ngazi ya chini mpaka ya Taifa katika masuala ya maendeleo ya vijana. Sheria ya Baraza la Vijana ilipitishwa mwaka 2015, lakini mpaka sasa miaka mitatu imepita bila baraza kuundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kisingizio kilikuwa kutokamilika kwa kanuni jambo ambalo haliwezi kuwa sababu tena kwa kuwa kanuni zilishachapishwa kwenye gazeti la Serikali. Hivyo, katika majumuisho Serikali ieleze mchakato na ratiba ya kukamilisha uundwaji wa Baraza la Vijana katika ngazi zote zilizojatwa katika sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, kanuni zimeweka utaratibu wa Asasi za Kiraia na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayolenga vijana kuwasilisha maombi ya kufanya kazi kwa baraza. Haya ni mashirika ambayo yamepitia mchakato wa makubaliano (*compliance*) kwa sheria nyingine zinazotawala mashirika yasiyo ya kiserikali. Kwa uwezo mdogo wa taasisi za vijana, kutakiwa kulipa gharama za usajili/kujandikisha kwa mamlaka zaidi ya moja ni mzigo mkubwa. Hivyo ni vyema kanuni zirekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu ina wajibu, pamoja na mambo mengine wa kushughulikia masuala ya Bunge na Wabunge kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge. Katika masuala hayo ni pamoja na ujenzi wa Ofisi za Wabunge. Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge zito maelezo Bungeni ni kwanini Ofisi za Wabunge hazijengwi katika Majimbo mbalimbali ambayo hayana Ofisi za Wabunge mpaka sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Wabunge kupewa Ofisi kwenye majengo ya Wakuu wa Wilaya, kimefanya Wabunge kutokuwa kwa huru juu ya matumizi ya Ofisi hizo. Pia kupewa nafasi ndogo ya chumba kimoja ya Mbunge na Watendaji wake wote na hivyo kukosekana faragha ya kuwahudumia wananchi. Aidha, wapo Wakuu wa Wilaya ambao wamewanyang'anya Wabunge Ofisi kwa maelezo kwamba zinahitajika na Watendaji wengine walio chini ya Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jimbo la Kibamba, lipo katika Wilaya mpya ya Ubungo ambapo kumekuwa na mchakato wa kutenga viwanja/maeneo kwa ajili ya Makao Makuu ya Halmashauri na Mkuu wa Wilaya. Baadhi ya viwanja hivyo vimepatikana kutoka ardhi iliyokuwa chini ya *National Housing Corporation (NHC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka kadhaa, nimeomba Ofisi ya Waziri Mkuu iratibu mambo nyingine kuwezesha kiwanja/eneo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mbunge. Hata hivyo, mpaka sasa sijapatiwa majibu stahili.

Hivyo katika majumuisho, Ofisi ya Waziri Mkuu inipe majibu, ni eneo gani hasa limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mbunge? Hata kama hakuna fedha za ujenzi kwa sasa, kiwanja kipatikane wakati huu kabla ardhi iliyo wazi haijaendelezwa kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kutaka pia uratibu ufanyike kuwezesha kutengwa kwa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama jirani na panapojengwa Makao Makuu mapya ya Wilaya ya Ubungo.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mungu, mwingi wa rehema na wakati wote nitaendelea kuwashukuru wazazi na wapigakura wangu wa Jiji la Tanga kwa kuniwezesha kuwa Mbunge wao. Nitaendelea kuwawakilisha katika kufikisha kero zao katika Bunge letu ili ziweze kufanyiwa kazi na kuwapelekea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya vijana; vijana wote ndio *engine* ya maendeleo na nguvu kazi katika sekta zote iwe ajira, michezo, kilimo, uvuvi, viwanda na kadhalika, mfano, vijana wana nguvu ya kusukuma mbele shughuli za kiuchumi. Ajira viwandani wanaajiriwa viwanda kwa kuwa wana nguvu ya kuendesha mashine kubeba na kutengeza mashine na kupakiwa bidhaa na kupeleka maeneo mbalimbali ya nchi. Hivyo nadiriki kusema vijana Taifa la leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zamani wanafunzi walikosa nafasi kuendelea na masomo kidato cha kwanza na kidato cha tano na sita, walikuwa wanajiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na waliweza kupata mafunzo ya ufundi umeme, uashi, seremala na vifaa vya kielektroniki kama *computer*, magari na kadhalika. Baada ya kufuzu mafunzo yao, waliweza kujajiri na kuweza kupata kipato cha kujikimu kimaisha. Nashauri vijana walioondolewa masharti magumu kujiunga na JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walemavu, nichukue fursa hii kumpongeza agizo la Serikali na pia kusisitiza kuwa

utaratibu wa kutenga 10% ya mapato ya Halmashauri zote nchini kwa magawanyo zifuatao 2% watu wenye ulemavu, 4% vijana, 4% akina mama. Nashauri mgawanyo huu usimamiwe kikamilifu na fedha zitolewe kwa wakati ili kufikia malengo tuliojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kiuchumi ukurasa II, pato la Taifa lilikuwa kwa 6.7 mwaka 2018 badala ya 6.2 mwaka 2017 ukiangalia wananchi watanania mitaani wamechoka wako hpi bi taaban mzunguko wa fedha ni mdogo, benki hazikopeshi, masharti ya mikopo ni magumu sana, hali inayopelekea wananchi kukopa katika *VICOPA*, *BRAC*, *SEDA*, *Poverty Africa*, *FINCA* na kadhalika ambazo zinatoza riba kubwa sana kiasi kupelekea wakopaji kunyang'anywa vyombo vyao, nyumba zao kupigwa mnada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya shilingi kuporomoka; thamani ya shilingi ya Tanzania kila kukicha imekuwa ikiporomoka/kushuka kwa thamani (*inflation*), lakini tunaambiwa uchumi unakua, naomba ufafanuzi katika hili kwa faida ya Watanzania. Mfano, mwaka 2018 *USD* moja ilikuwa sawasawa na shilingi 2226 mpaka mwaka 2019 *USD* moja ni sawasawa na Sh.2400. Mwaka 2018 *pound* moja ilikuwa sawasawa na shilingi mpaka mwaka 2019 *pound* moja ni sawasawa na shilingi.... Mwaka 2018 shilingi moja ya Kenya ilikuwa sawasawa na shilingi 20 mpaka mwaka 2019, shilingi moja ya Kenya sawasawa na shilingi 220. Mwaka 2018 *S/Rand* moja ilikuwa sawasawa na shilingi...mpaka mwaka 2019 *S/Rand* moja ni sawasawa na shilingi Katika hali hii ambapo shilingi ya Tanzania inashuka uchumi unakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei, ulipungua kwa wastani 4.0%, mwaka 2018 hadi 3.0 mwaka 2019 mwezi Januari. Sasa nataka nipate ufafanuzi kwa kuwa naona ipo tofauti katika taarifa kwa mfano ufuatao:-

(i) Mwaka 2018 Juni – Sukari kilo moja ilikuwa shilingi 2,100 lakini mwaka 2019 sukari kilo moja ni shilingi 2,500;

- (ii) Mwaka 2018 Juni –Maharage kilo moja yalikuwa Sh.1,700, lakini mwaka 2019, maharage kilo moja ni Sh.2,400;
- (iii) Mwaka 2018 Juni –Tambi zilikuwa kilo moja Sh.1,800, mpaka mwaka 2019, tambi kilo moja ni Sh.2,500;
- (iv) Mwaka 2018 Juni – mafuta yalikuwa lita moja ni Sh.1,100, mpaka kufikia 2019, mafuta lita moja Sh.2,000; na
- (v) Mwaka 2018, *petrol* lita moja ilikuwa Sh.1,600, lakini mpaka kufikia mwaka 2019, *petrol* lita moja ni Sh.2,206.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hii hapo juu mfumuko wa bei Tanzania umeshuka au umezidi? Waziri atoe ufafanuzi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu na sintofahamu kwa wazazi, Katika sekta ya elimu kuna sintofahamu hasa baada ya Serikali kutangaza elimu bure darasa la kwanza hadi kidato cha nne. Wazazi wanaelewa kuwa bure ni *free no charge*, hivyo hawalipii maji, umeme, mlinzi, uji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaeleza kwa kila mwezi inatoa fedha katika sekta ya elimu Sh.... kwa mwezi, wananchi wanajua fedha za Serikali ni nyingi na zipo. Hali imepelekea umeme na maji kukatwa shuleni (mkumbuke Mheshimiwa Rais aliwaambia *TANESCO*, penye deni la umeme kata na pia ulinzi hakuna na vifaa shuleni vimeanza kuibwa. Ushauri, naomba Serikali itolee ufafanuzi elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Jamii *NSSF, LAPF, LPF, PSPF, PPF* na wafanyakazi. Mifuko hii inakusanya mapato kupitia makato yanayokatwa katika kipato cha watumishi mbalimbali Serikalini na sekta binafsi na Mfuko mmoja *PSSF* lakini bado kuna tatizo pale wastaafu wanapodai mafao yao baada ya kustaafu kuna usumbufu mkubwa sana. Kama tunavyojua ukustaafu mategemeo ni akiba yako (mafao ya kustaafu). Hivyo nashauri na kuomba Waziri aeleze usumbufu huu chanzo chake nini na usumbufu huu utakwisha lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo utaratibu umefanyika wa kuwaongezea *pension* waliokuwa watumishi wa Serikali toka Sh.50,000 hadi Sh.100,000 lakini kwa waliokuwa watumishi wa Mashirika ya Umma (SU), bado watumishi wa SU wanaendelea kulipwa *pension* ya Sh.50,000 kwa malimbikizo ya malipo baada ya miezi mitatu (3). Tukumbuke wastaafu ni watu wenye umri mkubwa na wana shida na matatizo mengi. Ushauri wangu ni kwamba, waliokuwa watumishi (SU) waongezewe na wao toka Sh.50,000 hadi Sh.100,000 na walipwe kila mwezi bila malimbikizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kisiasa nchini ni ngumu na demokrasia inahitaji kuboreshwa na kuimarishwa. Kitendo cha kuzuia mikutano ya hadhara na maandamano kumepelekea msimko wa kisiasa na uelewa wa siasa kwa wananchi kurudi nyuma au kupunguza hamu na ladha ya siasa hadi kupelekea baadhi ya wanasiasa kupotea katika ramani ya siasa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomzuia mwanasiasa asifanye mikutano ya hadhara, asifanye maandamano, ni sawa na kumzuia mkulima asiende shambani, mvuvi asiende baharini, mchezaji asiende uwanjani au mfanyakazi asiende ofisi, kwa kuwa mwanasiasa ofisi yake ni jukwaa la mikutano au mkutano. Ushauri ni kwamba, naiomba Serikali katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu hali hii ingeangaliwa upya.

MHE. MWANTUM DAU HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakulima vijijini wanapata tabu sana kuhangaika kulima chakula chao, matokeo yake hawafanikiwi kutokana na wanyama kuingia mashambani wakavuruga mazao hayo, jambo ambalo linawarudisha nyuma kuendelea na harakati zao za maendeleo. Napenda kuishauri Serikali kuwa, wafugaji wanaofanya vitendo hivi wachukuliwe hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za jamii kama elimu; Serikali inatekeleza kikamilifu mafanikio ya elimu licha ya juhudi za Serikali wanazozifanya, kuna watu wachache wanarejesha nyuma Serikali yetu hasa uvujaji wa mitihani

nchini. Kuna sehemu mitihani ilichelewa kufanywa, nishukuru Serikali yangu kwa jitihada zake, mithani imeendelea kufanywa, lakini napenda kuishauri Serikali suala hili waliangalie kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira na vijana; nguvu kazi za vijana ni muhimu sana kuwezesha nchini, asilimia yao wanayopata wanaifanyia kazi kubwa lakini changamoto zao katika kazi zao ni kwamba hawana soko madhubuti la kuuza vitu vyao. Sasa basi, naomba Serikali Tukufu ilione suala hili na iwapatie soko la uhakika ili waondokane na tatizo hili . Sasa nimpongeze Waziri Mkuu na watendaji wake kwa jitihada nasema asanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuweza kuchangia hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafao ya wafanyakazi wa iliyokuwa *Kilombero Sugar Company* ambayo mwaka 1999 ilibinafsishwa kwa mwekezaji wa Illovo. Wafanyakazi zaidi ya 3,000 ambao walifanya kazi kwa weledi mkubwa walishastaafishwa mwaka 1999 – 2000. Kampuni ya *Kilombero Sugar* ilipobinafsishwa mpaka sasa wanapigwa danadana kuhusu mafao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge nilishafanya jitihada za kuwaleta wawakilishi wa wazee hawa mpaka kwa Waziri Jenista Mhagama, lakini mpaka leo bado hawajapatiwa ufumbuzi wa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilileta mara kadhaa swali la msingi hapa Bungeni, lakini cha kustaajabisha swali hili limekuwa haliletwi kabisa kwenye *order paper*, jambo ambalo linatupa wasiwasi kwamba, Serikali haina majibu ya swali lao kwamba ni ni lini watu hawa maskini watalipwa mafao yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli alipofanya ziara kwenye uzinduzi wa barabara ya Kidatu – Kilombero, nilimwomba atusaidie ili wafanyakazi hawa ambao wengi wao wameshakuwa watu wazima sana na wengine wameshatangulia mbele za haki, bila kulipwa stahiki zao kitu ambacho kwa kweli kinawafanya waishi kwenye maisha duni sana huku wengine wakiwa hawana hata uwezo wa kuhudumia familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa kabisa, Mheshimiwa Rais ambaye aliwapa moyo sana wananchi hawa kwa kuwaambia kuwa atahakikisha wanapata stahiki zao na atazungumza na Mawaziri husika lakini mpaka leo wananchi hawa bado hawajapata majibu yoyote na hawajui leo yao wala kesho yao. Namwomba sana Waziri akija kwenye majumuisho ya hoja yake, atupe majibu; Je, ni lini hasa waliokuwa wafanyakazi 3,000 wa *Kilombero Sugar Company* watalipwa mafao yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa Serikali waliopunguzwa na baadaye kurudishwa kwenye zoezi la vyeti feki; kuna idadi kubwa sana ya watumishi katika Wilaya ya Kilosa ambao walipunguzwa kwenye zoezi la vyeti feki, lakini baadaye wakaonekana wanastahili kuendelea na kazi lakini mpaka sasa hawajalipwa pesa zao walizokuwa wanastahili, kupokea kipindi walipokuwa Watendaji wa Vijiji, Walimu, Watumishi wa Afya, Madereva na kadhalika. Nakumbuka Waziri wa Utumishi alisema, watu wote waliosimamishwa kimakosa watalipwa stahiki zao, ningependa kujua, je, watumishi hawa wa Serikali watalipwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya *TARURA* ni ndogo sana, lakini pia *TARURA* wanafanya kazi yao ya kutengeneza barabara za ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kwa kusuasua sana, kwa mfano, barabara ya Ruaha Mbuyuni – Malolo – Kibakwe ambayo ni muhimu sana kwa wakulima wetu na kwa umuhimu huo pia, barabara hii inaunganisha Mikoa ya Morogoro – Iringa na Dodoma. Tuliomba ipandishwe

hadhi ili ihudumiwe na *TANROAD* lakini mpaka sasa barabara hii inaharibika sana na kuna kipindi haipitiki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya muhimu ya Ulaya – Madizini – Malolo – Kibakwe pia ni muhimu sana inayounganisha Mkoa ya Morogoro – Iringa na Dodoma, lakini imekuwa haipitiki hasa kipindi kama hiki cha masika, naomba sana waifikirie ili iweze kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kususua sana kwa zoezi la uunganishwaji wa nishati ya umeme kwenye Jimbo la Mikumi, ningependa kujua; je, ni lini Serikali itaweka umeme kenye barabara kuu ya Tanzania – Zambia hasa maeneo ya kona za Msimba, Ng’apa na kadhalika ambapo panaunganisha na maeneo ya Ruaha Darajani lakini umeme unapita juu na kushindwa kuunganishwa umeme kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeshauliza mara kadhaa hapa Bungeni kuhusu jimbo letu lenye sifa kubwa ya utalii, lakini maeneo mengi ni ya giza. Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi yake ya kuwaunganishia umeme wananchi wa Kata za Vidunda, Ulelingombe, Malolo, Wedo – Kisanga, Zombo, Ulaya, Mhenda, Tindiga, Mbamba, Kiduhi, Tambukareli, Kikwalaza, Munisagala, Dodoma Isanga, Udung’u Mgogozi, Chabi, Kielezo, Gezaulole, Dinima na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mikumi tumekuwa na matatizo makubwa sana ya mawasiliano ya simu. Mfano, barabara ya *TANZAM* (Tanzania – Zambia), pale maeneo ya Msimba, Iyovi na Ng’apa kumekuwa kuna ajali nyingi sana na sehemu hii ina kona kali nyingi sana na ajali nyingi sana zimekuwa zinatokea, lakini jambo baya kabisa ni kuwa, maeneo haya kuanzia Msimba mpaka Ruaha Mbuyuni hakuna mawasiliano yoyote yale ya simu na hakuna umeme kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali ilitupie jicho la huruma eneo hili ambapo wasafiri wengi sana wa

ndani ya nchi na wengi wa nje ya nchi wanapata matatizo mbalimbali lakini hawawezi kuwasiliana na wenzao na kusubiri kudra za Mwenyezi Mungu tu. Pia, katika Jimbo la Mikumi kwenye Kata za Vidunda, Malolo, Tindiga, Kisanga, Kilangali, Ulelingombe, mabwerebwere na eneo la muhimu kabisa la katikati ya Hifadhi ya Mikumi ambalo ni muhimu sana kwa watalii na linaongeza sana pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa tuta la Mto Miyombo/Bwawa la Kidete; nashukuru sana Ofisi hii ya Waziri Mkuu kwa kuwa mara nyingi wamekuwa wakitusaidia pale tunapopata maafa ya mafuriko kwenye Wilaya yetu ya Kilosa na Jimbo la Mikumi. Kubwa ni kupasuka kwa kuta za Bwawa la Kidete ambalo Serikali kila siku imekuwa ikituahidi kuwa, imetenga pesa kwa ajili ya kujenga bwawa hili muhimu la Kidete kuzuia mafuriko hayo. Pia, kingo za Mto Miyombo zimezidiwa na wingi wa maji na mvua inapozidi, maji hufurika kwa wananchi na kuleta maafa. Naomba majibu ya Serikali, ni lini itajenga Bwawa la Kidete na lini itajenga tuta la Mto Miyombo?

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipongeze hotuba nzuri ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa. Pia, nina mambo ambayo nataka kuishauri Serikali ambayo mengine ni kero kwa wananchi na yanahitaji kufanyiwa kazi ipasavyo na maoni mengine ni kuishauri Serikali ili kuweza kupiga hatua mbele katika kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya; Serikali imejitahidi kujenga hospitali, vituo vya afya na zahanati, maoni yangu nashauri Serikali iweke vifaa tiba katika vituo vya afya na hospitali ili kuweza kuondoa msongamano katika hospitali za rufaa. Katika Hospitali ya Rufaa Temeke, Dar es Salaam ina uchache wa wodi za wagonjwa na majengo mengi ni chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijenge wodi za zamani maghorofa, ili kuweza kukidhi mahitaji ya idadi kubwa ya wagonjwa kwa sababu hospitali hii ya Temeke, hupokea

wagonjwa kutoka wilaya za jirani za Mkoa wa Pwani kama vile Wilaya ya Mkuranga, pia Wilaya ya Kigamboni. Serikali iwapatie hospitali ya rufaa Temeke mashine ya kufulia mashuka ya wagonjwa, maana kwa sasa yanapelekwa katika hospitali ya Taifa Muhimbili kwa ajili ya kufuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika hospitali za rufaa mfano Muhimbili, Mloganzila, Serikali ijenge maeneo maalum ambayo yatatumiwa na ndugu wa wagonjwa wakati wagonjwa wao wanasubiri, siyo wagonjwa wote wanandugu au jamaa katika Mkoa wa Dar es Salaam. Huduma ya kuhifadhi maiti iwe bure, maana mara nyingi tunaona inawakwaza wafiwa kwa kushindwa kulipia maiti zao na hatimaye Serikali inapewa lawama kuwa haina huruma na wananchi, ukizingatia wakati wa uhai wake marehemu alikuwa anachangia pato la Taifa kwa kulipa kodi kupitia huduma mbalimbali alizokuwa anazifanya, kama vile kununua mahitaji yake ya kila siku, kuna kodi za Serikali inachukua. Huduma hii ya kuhifadhi maiti iwe bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ije na sheria ya kuongeza muda wa likizo ya uzazi kwa akinamama wanaojifungua watoto chini ya miezi tisa (njiti) na kwa akinamama waliojaliwa kujifungua watoto zaidi ya mmoja ili kuweza kuwapa muda wa kuwalea watoto wao, maana miezi mitatu wakati mwingine ni michache mno, ukilinganisha na mwanamke aliyejifungua mtoto mmoja na ambaye ametimiza miezi tisa tumboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa biashara na viwanda, nashauri Serikali itoe muda maalum *grace period* angalau wa miezi mitatu, kisha ndipo waanze kumkadiria mtu ambaye anataka kuanza kufanya biashara na siyo mfumo unaotumika sasa wa kulipa mapato kabla ya mwananchi kuanza biashara yake. Hili si jambo zuri kabisa. Kuna asilimia 15 ambayo wenye viwanda vinavyotumia sukari ya viwandani huilipa waingizapo sukari hiyo nchini, lakini wafanyabiashara hao wanaidai Serikali fedha nyingi sana na wamefanya taratibu zote zinazohitajika ili waweze kujereshewa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwalipe wenye viwanda hivyo ambavyo wanadai ili fedha hizo ziweze kuwasaidia kuendesha viwanda vyao, maana suala la kutolipwa kwa wakati kunaathiri uzalishaji katika viwanda vyao. Ni muhimu kwa kuelekea uchumi wa viwanda, kuwalipa kwa wakati na siyo kidogo kidogo kama ifuatavyo Serikali sasa hivi, walipe kwa mkupuo kama wao walivyokuwa wanalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga nchi yetu ni muhimu Serikali itatue changamoto zote ambazo zipo ndani ya uwezo wake ili kuweza kufikia lengo la kuondoa umaskini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote walio kwenye ofisi yake pamoja na ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu; mafunzo kwa wanawake wajasiriamali. Tunashukuru kwa vitambulisho. Kipekee tunaomba wawezeshwe kielimu na hasa kwenye utunzaji wa fedha ili wakuze *vicoba* vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. GETRUDE P. RWAKATALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake kwa hotuba nzuri. Barabara ya Kidatu – Ifakara ujenzi wake unasuasua kwa nini? Tunaomba Waziri Mkuu aingilie kati. Tunaomba Wizara ya Ujenzi iingilie kati.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ukurasa wa 25 wa hotuba, unatoa takwimu za miradi mipya ya uwekezaji mpaka Februari 2019 kuwa 145. Ningetaka kujua ni mingapi mpaka sasa imeanza kujengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea na baadhi ya wawekezaji ambao wamelalamikia mlolongo wa vikwazo au taratibu ambazo si rafiki kwa wawekezaji wanaokuja na mitaji yao. Kupata kibali au leseni inachukuliwa muda mrefu. Nashauri Serikali ipitie upya taratibu na hatua zilizopo ili tuvutie zaidi wawekezaji waje Tanzania badala ya kwenda kwa nchi za jirani. Kwa mfano, tunaweza tukaamua uwekezaji wa kujenga kiwanda, mlolongo wote wa hatua za kuchukuliwa zikamilike ndani ya Taasisi moja (*one center*) na kila hatua ipewe muda maalum (*that is time factor*) na uwepo ufuatiliaji wa kila hatua ili kujua sababu za mkwamo na hatua za kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa viwanda vinavyochakata mazao ya wakulima na wafugaji vipewe kipaumbele kwani hivi vitainua uchumi wa wananchi na kutoa ajira. Yupo Mwekezaji wa kujenga kiwanda cha kuchakata matunda ya maparachichi kinachotarajiwa kujengwa Wilayani Wanging'ombe (*OLIVADO CO*) amekuwa anazungushwa karibu amekata tamaa, nataka kujua ni lini atapewa leseni ili ajenge kiwanda hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na tatizo la soko la matunda ya parachichi kwa muda mrefu na baada ya mwekezaji huyu kuja tumehamasisha wananchi wetu kulima zao hili la parachichi, naomba sana Serikali itumie nguvu iliyokuwa nayo ili kiwanda hiki kijengwe mapema.

MHE. ALLY S. UGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba hii kwa maandishi. Kwanza naipongeza Serikali yangu ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri ya kuhudumia wananchi wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Makamu wetu wa Rais mama yetu Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu kwa kazi nzuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kazi nzuri anayoifanya. Jimbo langu la Kibiti lina jumla ya Kata 16, Vijiji 58, Vitongoji 272, Shule za Msingi 74, Sekondari 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya, katika Jimbo langu la Kibiti kuna upungufu mkubwa wa watumishi wa kada hii ya afya kama 320 waliopo ni 120. Tunaomba Serikali yetu sikivu ituangalie kwa jicho la huruma. Pili kuna maeneo ya baadhi za kata zina wingi wa watu, lakini hadi leo hakuna vituo vya afya. Kata hizo ni kama Bungu, Ruaruke, Jaribu Mpakanina Mlanzi. Sambamba na hilo kituo cha afya Kibiti kinafanya kazi kubwa kuhudumia wananchi wa kata zaidi ya moja, naomba tufanyiwe ukarabati mkubwa ili kiweze kutoa huduma yenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Wilaya ya Kibiti haina gari la chanjo na wagonjwa, ina upungufu mkubwa wa magari, naomba Serikali yetu ituangalie kwa jicho la huruma. Wilayani Kibiti kuna baadhi za kata zipo *Delta* kwenye Bahari ya Hindi Visiwani kama Kata ya Mbuchi, Kiongoroni, Msala, Maparoni, Salale sawa na kata tano, vijiji 17, vitongoji 42, vipo *Delta*. Naomba watumishi wa maeneo haya Serikali iwaangalie kwa jicho la kipekee kutokana na kufanya kazi kwenye mazingira magumu, kama kupewa motisha na kutofanya kazi kwa muda mrefu kwenye kituo kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo hatuna kabisa mafriji ya kuwekea chanjo, boti kwa ajili ya kusafirisha pindi mama mjamzito atakapopata rufaa, upungufu mkubwa wa nyumba za watumishi. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibiti, tunamshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kutusaidia vituo vya afya viwili, ambavyo tunavifanyia ukarabati mkubwa na ujenzi wa hospitali ya Wilaya ambavyo vyote ujenzi wake unaendelea kwa kasi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu, moja ya Ilani ya Uchaguzi ya 2015 ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ni elimu bila malipo (elimu bure). Kwenye Jimbo langu la Kibiti mwitikio wake ni mkubwa sana. Lakini kila panapo mafanikio hapakosi kuwa na changamoto kama vile upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa, nyumba za Walimu, vyoo bora vya kujisitiri Walimu na wanafunzi, upungufu wa Walimu na Walimu

kukaa sehemu moja kwa muda mrefu mpaka Walimu sasa wanakuwa kama wanakijiji na baadhi ya Walimu kudai madai yao ya uhamisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo badhi ya shule kwenye visiwa jumla yake ni 17 ambazo Walimu wake mahitaji yao muhimu kama huduma za kibenki inawalazimu waje Kibiti. Naomba Serikali yangu sikivu ituangalie, hawa wapewe hata posho ya kujikimu kwa mazingira magumu kama motisha. Naomba kushukuru kwa kupata pesa za ujenzi wa mabweni, madarasa machache, pikipiki kwa ajili ya Maafisa Waratibu Elimu Kata na pesa za *EPFR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji; hadi leo Kibiti hakuna hata mradi mmoja wa maji ambao unatekelezwa licha la kuchimba visima jumla 12 na kupata maji. Naomba Serikali yangu sikivu tuanze kujenga miundombinu ili zana ya kumtua mama ndoo kichwani iendani na kauli ya hapa kazi tu. Tuna miradi Kibiti takriban mitano inahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara; nashukuru Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa kuunda chombo ambacho kinasimamia shughuli za kurekebisha miundombinu yetu katika majimbo yetu *TARURA*. Chombo hiki kinafanya kazi nzuri, kwa hiyo kuna kila sababu ya kuongezewa uwezo wa kifedha na watumishi ili waweze kuwahudumia wananchi kwa ufanisi. Changamoto kubwa kwenye Jimbo langu la Kibiti, moja kuchonga barabara za mitaa za Kibiti, Bungu, Jaribu Mpakani, Nyamisati, pamoja na kujenga mifereji yake barabara ya Muhoro Mbuchi, iangaliwe kwa jicho la huruma kupata tuta la kifusi ili iweze kutoa huduma kipindi chote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kumalizia barabara ya kwenda Makao Makuu ya Wilaya, kilomita mbili zilizobakia kwani ujenzi wa Ofisi hii unakwenda kwa kasi kubwa. Wananchi wa maeneo ya *DELTA* wanapata shida kubwa kipindi wakiwa wanasafiri, tunaomba ujenzi wa magati katika bandari zetu ndogondogo kama Kiomboni, Mfisini, Mchinga, Salale, Simbaulanga, Ruma, Jafa, Mbwera, Kechuru, Maparoni, kujengewa barabara ya lami kutoka

Bungu hadi Nyamisati kwani ujenzi wa gati karibu na unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme; naomba Kibiti ituangalie kwa jicho la huruma katika maeneo ya *DELTA* visiwani, hadi leo hakuna hata kisiwa kimoja kimepata umeme wa aina yoyote kama Kata ya Salali, Msala, Mparoni, Klongoroni, Mbuchi na Vitongoji vyake vyote. Hata kwenye maeneo haya ya nchi kavu kama kama Makima, Zimbwini, Mbumba, Msoro, Nyamwimbe, Manguri na maeneo mengine, tunashukuru kwa kupata Meneja wa *TANESCO*, kwa hiyo tunaomba sasa tujengewe Ofisi ya *TANESCO* kwenye Wilaya yetu ya Kibiti.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji dhidi ya kazi/ajira; pamoja na jitihada za Serikali kuifanya *TIC* kuwa chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, bado kuna jitihada inapaswa zitazamwe katika suala zima la *welfare* ya wafanyakazi katika maeneo yaliyowekezwa. Wafanyakazi hawalipwi ipasavyo, hakuna *social security*, hakuna utaratibu wa bima za afya, kimsingi ustawi wa wafanyakazi katika sekta binafsi ni eneo linalopaswa kutazamwa kwa ukaribu na wenzetu wa kazi na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa umma wakati wa uhakiki wa watumishi, wako ambao kimakosa waliondolewa kwenye mfumo na baadaye walirejeshwa. Hata hivyo hawajalipwa malimbikizo yao ambayo kimsingi mamlaka husika zimeshayathibitisha, isipokuwa ni Hazina kufanya malipo. Suala hili hakika linashusha morali ya watumishi, nashauri na kupendekeza Hazina walipe malimbikizo hayo kwa kuwa ni makosa ya kibinadamu ambayo yamerekebisha ni muafaka sasa wa kulipa malimbikizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme; Mafinga kutokana na viwanda vingi Mji wa Mafinga nimeshauri mara kadhaa nishati (*TANESCO*) watazame kwa macho mawili pawepo na Wilaya ya ki-*TANESCO* ya Mafinga maana pia Mufindi kama Wilaya ina Viwanda vingi vya Chai, Karatasi Mgololo, hivyo

uhitaji wa umeme ni mkubwa sana kutokana na mazao ya misitu. Nashauri kuwa uwekezaji tunaovutia uendane na upatikanaji wa umeme wa viwandani maana kadri uzalishaji unavyoongezeka ndivyo na ajira na mapato zaidi.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuonesha kuwa uchumi unakuwa kwa 6.7 mwaka 2018 kutoka 6.2 kwa mwaka 2017, katika kukuza ajira na uboreshaji wa miundombinu na pia imefanikiwa kupunguza mfumuko wa bei katika jamii. Bidhaa na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi bado hazina uhalisia na maisha ya wananchi ambapo bado maisha ni magumu na ajira bado Serikali imeshindwa kutatua kero hii ambayo ndiyo hoja kuu na changamoto kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya vijana na akinamama wajasiriamali wadogo bado ni magumu katika halmashauri zetu, japo Serikali imejikita katika kuwapa mikopo katika makundi haya, lakini bado marejesho katika vikundi hivi yameshindikana. Kwa hali iliyopo asa sioni kwamba mikopo hii inawasaidia moja kwa moja akinamama kwa sababu urejeshwaji wa mikopo hii kwao bila kuwasimamia, mafunzo, kuwatafutia masoko, miundombinu mibovu imepelekea vikundi hivi kushindwa kufanya biashara na ukosefu wa vifungashio ambavyo ni bora. Matatizo haya ya kimazingira na masoko ni kero kwa wajasiriamali, hivyo Serikali ije na mkakati thabiti kuokoa makundi haya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho vya wajasiriamali wadogo 670,000. Serikali hii pamoja na kuwatambua na kuwaondolea usumbufu wa maeneo ya biashara kupitia Serikali za Mitaa, bado kuna tatizo kwa sababu wajasiriamali wametoa Sh.20,000 lakini mpaka sasa hatuoni kwamba Serikali hii ina nia ya dhati kusaidia kundi hili kwa sababu kundi hili wanalipa kodi, ushuru na huku Serikali iko kimya. Je, ni lini watalimaliza hili kwa wakati?

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na

Waheshimiwa Mawaziri na watendaji wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri na hasa usimamizi wa Serikali na miradi mikubwa ya maendeleo. Hata hivyo ninayo mambo yafuatayo kama ushauri:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundi, kwa kuwa Serikali imejikita katika uchumi wa viwanda ni lazima irejeshe elimu ya ufundi ya mafundi sadifu (*technicians*), sasa hivi Serikali inajikita kuandaa mafundi mchundo (*artizans*) kutoka VETA. Mfumo huu wa elimu unaacha ombwe kati ya mfumo wa utendaji kazi za ufundi, Mhandisi mmoja kutoka vyuo vikuu, Mafundi Sadifu 25 kutoka vyuo vya ufundi na Mafundi Mchundo 15 kutoka VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waajiri sekta binafsi wanalipa tozo ya SDL ya 4.5% iliyolengwa kupelekwa VETA kuongeza ujuzi wa wafanyakazi, lakini fedha hizo hazipelekwi zote, sehemu kubwa inapelekwa vyuo vya elimu ya juu kwa wanafunzi, siyo wafanyakazi, waajiri wanaona kuwa hii si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waajiri wanaamini kuwa lilikuwa kosa la kiufundi kuiweka VETA chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, VETA ilistahili kuwa chini ya Wizara ya Kazi na Ajira, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu VETA ililenga kuongeza ujuzi wa wafanyakazi.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kutumia wasaa huu kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu kwa Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri wetu Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa juhudi zake chanya katika mchakato mzima wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka mitano. Waziri wetu Mkuu huyu amekuwa akitekeleza majukumu yake kwa ufanisi na unyenyekevu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu utajikita katika sehemu mbili; bandari kwa masaa ya mchakato wa uagizaji mafuta na usambazaji wake na suala zima la biashara ya magari, hasa *bonded warehouse*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 kilianzishwa chombo kilichokuwa kinaitwa *Petroleum Importer Coordinator (PIC)* ambapo chombo hiki baadaye kilivunjwa na kuanzishwa *PBPA* Wizarani ikiwa na majukumu ya kusimamia uagizaji wa mafuta na ku-*discharge* mafuta kwa wasambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo shida katika Taifa letu, shida hii lazima kama Taifa Bunge letu litimize wajibu wake kuishauri Serikali kwa maslahi ya nchi. Serikali yetu ina umiliki wa asilimia 50 katika Kampuni ya *Tipper* lakini vita inayoikumba kampuni hii utashangaa. Inawezekanaje tunaagiza mafuta nje ya nchi, yakifika Dar es Salaam kila *importer* anapelekewa mafuta moja kwa moja kwenye *deposit* yake wakati tunayo *Tipper*, chombo ambacho kina *capacity* kuhifadhi mafuta yote ya nchi hii na yaliyopo kwenye *transit*? *Tipper* wanapigwa vita eti wanaiba mafuta, sisi tumerogwa na nani? Serikali tuna hisa *fifty percent Tipper* ina maana Serikali tunaiba mafuta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaiba mafuta *against* nani? Tunawaamini zaidi *importers* wakiwemo *Engen, Oryx, Oilcom, Lake Oil* kuliko chombo hiki cha umma ambacho tukiweza kuwa na *one* au *single terminal receiving* matanki ya *Tipper* yana uwezo wa kuhifadhi mafuta lita milioni 220, sawa na *capacity* ya kupakua meli tatu kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tipper* ambayo ni sehemu ya Serikali ikipewa jukumu la kusambaza mafuta yote ya *Oil Marketing Companies (OMC)* wanaweza kusambaza mafuta ndani ya siku tatu baada ya ku-*deliver* na jambo hili linaweza kufanyika ndani ya siku sita tu kwenye *depots*. Ni muda muafaka sasa Tanzania kuepuka ujanja na wizi unaofanywa

na wafanyabiashara wa mafuta kwa kupiga vita *single terminal receiving*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *single terminal receiving* ya mafuta ndiyo mfumo pekee unaotumika duniani kote. Hata mafuta ya *transit* wanunuzi wa nje ya nchi watachukulia mafuta kutoka *Tipper* na hivyo kuliingizia Taifa mapato na pia kuisaidia *TRA* kukusanya mapato yake kutoka eneo moja tofauti na *practice* ya sasa ya kufuatilia mapato kutoka kwa *OMC* moja moja kutoka *depots* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *damage charges* tunazolingia kwa meli kuwa katika foleni, *OMC* wanalipia wastani wa dola 25,000. Dola 25,000 *USD* kwa siku, sasa unajuliza kama hakuna ujanja kwa nini tunafisha *efficiency* kwa chombo ambacho Serikali tunaweza ku-*monitor* uingiaji wa mafuta na usambazaji na kuliingizia Taifa ajira.

Mheshimiwa Waziri Mkuu najua yeye ni mzalendo na mtu wa haki, weka historia katika nchi hii kwa kuhakikisha kuanzia leo mafuta yote yanayoagizwa nchini yanamezwa na *Tipper* na waagizaji wote wapeleke kwenye *deposits* zao toka *Tipper*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za kuwa na *single receiving terminal* ni hizi; moja, hapatakuwa na *damage* sababu meli zitaweza kumwaga mafuta kwa wakati. Mbili, ili kuepuka wizi au *diversion* ya mafuta mabomba ya mafuta kati ya *SBM* na *Tipper* itenganishwe; na tatu, tutaongeza wigo wa *Transit Cargo Consignment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu na Serikali wajue kwamba wafanyabiashara wanapoteza wastani wa shilingi milioni 330 kwa gharama za *demurrage* kwa wastani wa siku @25,000 *USD* kila meli inapokuja kupakua mafuta, wastani wa *call* za *vessel* za mafuta ni 24 kwa mwaka, hivyo wastani huu unapelekea kupoteza pesa karibu 19,776,970,608 kila mwaka zinapotea sawa na wastani wa milioni 824,040,422 kwa kila *shipment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili ni kazi yake kuishauri Serikali, ni wakati muafaka katika majumuisho ya hotuba ya Waziri Mkuu Serikali sasa wakubali kufanya mabadiliko ya haraka kwa maslahi mapana ya nchi yetu kwa kuifanya *Tipperi*we mpokeaji na msambazaji wa mafuta yote ya nchi kutoka kwa *petroleum traders*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa sasa kwa upakuaji wa mafuta bandarini una kasoro kubwa na unatia walakini wa ukweli wa idadi halisi ya mafuta yanayoingizwa nchini kwa mfano kwa idadi ya *terminal* 18 – saa kati ya 36-54 zinapotea kutokana na kuhamisha umwagaji kutoka *terminal* moja kwenda nyingine. Taifa letu tuna shida moja tunalalamika sana, tunatengeneza vitu vizuri lakini hatutaki kutekeleza wakati mwingine kwa viongozi wetu kupotoshwa kwa makusudi au kwa kutokujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tipper*ni chombo ambacho Serikali yetu ina umiliki, ukifanya *analysis* ya kimapato nje ya gawio, Serikali imepata *revenue* karibu asilimia 68 kutoka *Tipper* moja kwa moja, Serikali tunapata *revenue* ya *almost* 70% kutoka *Tipper* na *orxy* mbili anachukua asilimia 30% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ushauri huu, naiomba Serikali yangu sikivu ya CCM kuanza mara moja matumizi ya *single terminal receiving*. Naunga mkono hoja

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza jitihada za Mheshimiwa Waziri Mkuu za kufua zao la chikichi na kuongeza zao la chikichi katika mazao ya kimkakati nchini. Zao la chikichi litabadilisha uchumi wa Mkoa wa Kigoma na kunufaisha wakulima wa zao hili, lakini pia kufufua zao hili itasaidia kupunguza uingizwaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi na badala yake kuchochea uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata mafuta ya kula (*palm oil*) ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la chikichi linahitaji uwekezaji wa miaka mitatu tu lakini mkulima akianza kuvuna anaweza kuvuna kwa zaidi ya miaka nane. Zao la chikichi

linaweza kuzalisha bidhaa ya mafuta ya kula (*palm oil*), sabuni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani lakini mashudu ya zao la chikichi yanaweza kutumika kwa ajili ya chakula cha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu ataendelea kushukuriwa na Wanakigoma kwa kuchochea maendeleo kwa kuhakikisha zao la chikichi linakuwa na tija. Aidha, tunaomba zoezi la upatikanaji wa mbegu za zao la chikichi litiliwe/liongezewe mkazo ili wakulima wapate mbegu za kutosha na mbegu zenye ubora. Mbegu za chikichi zinauzwa shilingi elfu sita kwa mbegu, gharama hii ni kubwa, tunaomba Serikali iweze kuangalia namna ya kurahisisha na kupunguza gharama za upatikanaji wa mbegu za chikichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma inathamini sana jitihada za Serikali katika kampeni hii muhimu ya kufufua zao la chikichi. Wabunge na wadau mbalimbali tutaendelea kuunga mkono jitihada hizi za Serikali yetu makini.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa juhudi kubwa sana za kuwaletea wananchi maendeleo. Nawapongeza viongozi wetu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu/Bunge kwa utendaji wa kazi ulio bora katika kuongeza juhudi za kuwatumikia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, masuala ya Muungano; naipongeza Serikali yangu kupitia kikao chake cha Baraza la Mawaziri kuridhia kuondosha kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) kwa kiwango cha asilimia sifuri kwa umeme unaouzwa kwa Shirika la Umeme la Zanzibar (*ZECO*) kutoka Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) sambamba na kufuta malimbikizo ya deni la *VAT* la shilingi bilioni 22.9 kwa Shirika la umeme (*ZECO*).

Mheshimiwa Spika, ulinzi na usalama; navipongeza vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa wanayofanya

kuhakikisha nchi yetu iko salama na ulinzi wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, miundombinu; Serikali imefanya juhudi kubwa katika kuimarisha sekta hii kama viwanja vya ndege, barabara, reli na hasa reli ya mwendokasi, naipongeza Serikali pia. Nashauri kuongeza uwekezaji katika eneo la bahari kwa meli za abiria, mizigo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iendelee na juhudi za kuweka mazingira wezeshi zaidi kwa wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi ili sekta ya uwekezaji izidi kuimarika ili kuongeza pato la Taifa, kuinua uchumi na kuongeza ajira kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawatakia utekelezaji mwema wa majukumu ya kazi zenu.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Magufuli katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya kuwaletea wananchi maendeleo kwa kasi na ufanisi mkubwa. Awamu hii tumeona miradi mikubwa inayofanywa kwa fedha zetu za ndani na kwa muda mfupi. Naamini uthubutu wa Mheshimiwa wetu, Watanzania tukiacha kufanya kazi kwa mazoea, tukiungana na mwendo kasi wa Rais wetu, muda mfupi ujao Tanzania itakuwa ya kupigiwa mfano kwa mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuamua kukifanya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kihinga Mkoani Kigoma kuwa Kituo cha Utafiti wa Mbegu Bora za Chikichi. Ushauri wangu kwa Serikali, kupitia kituo chetu hiki kuangaliwe uwezekano wa kufanya utafiti kwa zao la tende kwa Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la tende Dodoma, kwa mitende iliyopo inazaa vizuri sana na tende kiafya zina lishe nzuri. Hivyo, ni chakula kizuri kinacholiwa Tanzania kutoka nchi za Kiarabu. Kiufupi mitende Dodoma inazaa vizuri kuliko hata huko nchi za Kiarabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiujumla utafiti wa mazao mbalimbali unahitajika ili kuondokana na kilimo cha mazoea tulichokirithi kwa wazee wetu ili mazao yetu yawe bora na kuweza kuuza nje ya nchi na kutuingizia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa hatua za makusudi za kunyanyua mchezo wa soka katika nchi yetu na tumeshuhudia timu zikifanya vizuri ndani na nje ya nchi, pamoja na mchezo wa ngumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na soka, pia tuna michezo mingi ambayo ikiangaliwa ipasavyo na kupewa msukumo nayo inaweza ikaitangaza nchi yetu na kuletea faida kubwa. Hivyo ni vyema Serikali kupitia Wizara ya Michezo kukaa na vilabu vya michezo mbalimbali kuona mipango yao ili kuweza kuandaa mikakati ya kunyanyua michezo hiyo, mfano, *netball*, riadha, *basketball*, *volleyball* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwaka 2020. Sambamba na hilo, nashauri upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa vya Mtanzania, kwani vijana wengi waliotimiza umri wa miaka 18 bado wanahangaikia vitambulisho. Hivyo hawajapatiwa na bila ya kitambulisho huwezo kuandikishwa kwenye Daftari la Wapigakura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kubwa kwa Serikali kwa juhudi kubwa inayofanya ya usimamizi wa mapato na matumizi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe

Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ubunifu wa kutoa vitambulisho vya wajasilimali wenye mitaji midogo. Hili litasaidia kuwatambua na kukuza mitaji yao. Hili ni jambo jema sana kwa Watanzania. Inakadiriwa vitambulisho 670,000 tayari vimetolewa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iongoze vizuri katika utoaji wa vitambulisho, sababu kuna wajanja wataanza kujifanya kuwa ni wajasilimali wadogo wadogo ili kukwepa kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchumi inaonekana ni nzuri, hii inatokana na Serikali kusimamia vizuri shughuli za kiuchumi. Kwa mfano, ongezeko la viwanda nchini, kuimarisha ujenzi wa barabara, umeme, maji, Vituo vya Afya na elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iendeele kutoa elimu kwa Watanzania kuwa, uchumi wa nchi yetu unajengwa na Watanzania wenyewe. Kwa hiyo, kila mtu ana wajibu wa kufanya kazi kwa bidii katika nafasi yake kama ni mkulima alime sana, kama ni mfanyabiashara afanye biashara sana, kama ni mfanyakazi wa kuajiriwa afanye kazi kwa bidii na uaminifu kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Serikali kwa kusimamia vizuri suala la kupunguza mfumko wa bei kutoka 4.0 (2018) hadi 3.0 Januari, 2019. Hii ni hali nzuri kwa Watanzania. Serikali imesimamia vizuri hasa katika hali ya upatikanaji wa chakula ili kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata chakula cha kutosha na kupunguza njaa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba kwa kuwa asilimia kubwa ya Watanzania wanategema kilimo, naomba Serikali iimarisha viwanda vya pembejeo hasa viwanda vya mbolea ili wakulima wanunue kwa bei ndogo na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na mazao ya biashara, kwa mfano, njegere, njugu, mbaazi, ufuta, maharage, alizeti na njugu. Haya ni mazao ambayo yanawasaidia sana wakulima

wadogo wadogo kupata fedha kiurahisi na inasaidia sana kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ya kizalendo anayoifanya katika nchi yetu. Mchango wangu utajikita katika maeneo matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni afya. Jimbo la Mufindi Kaskazini lina Tarafa nne, lakini kwa masikitiko makubwa tuna kituo kimoja kinachofanya kazi cha Ifwagi. Nakupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutupatia shilingi milioni 400 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Ifwagi na sasa kiko katika hatua za mwisho, lakini Tarafa tatu zilizobaki hazina Kituo cha Afya. Naomba nichukue nafasi hii kuiomba Serikali itusaidie kupata Kituo cha Afya kimoja kwa kila Tarafa nasi wananchi tuko tayari kusaidia katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni miundombinu ya barabara. Kumekuwa na tatizo kubwa la miundombinu katika Jimbo la Mufindi Kaskazini. Barabara hazipitiki kabisa; Barabara ya Mtili – Ifwagi – Mdeburo – Ihenu – Mpanga – Tazara – Mrimba. Barabara ya Tambaranyimbo – Uyele – Ikwaha - Kwa Twanga haipitiki kabisa na *TARURA* ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana kupitia Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI aingilie kati barabara ya Kinyanambo A – Isalavenu –Igombavanu, Sadani – Madibira - Rugisa ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM toka mwaka 2000/2005, 2005/2010, 2010/2015, 2015/2020 lakini hajajengwa hata kilometa moja ya lami. Ni vyema sasa Serikali ikasema ili tuweze kuwaambia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kuhusu miundombinu ya maji. Ni vyema sasa Serikali ikakubaliana

na Wabunge kwa kuingiza tozo ya shilingi 50 ambayo sisi tuna uhakika ikiongezwa itapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la maji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa uongozi wake mahiri katika kuzisimamia rasilimali za nchi yetu ili ziweze kuwanufaisha wananchi wa nchi hii bila kujali tofauti ya itikadi, dini, kabila, rangi na mipaka ya kikanda. Ama kwa hakika kwa namna Serikali ya Awamu ya Tano inavyotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ni Serikali ya kupigiwa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kielelezo inayotekelezwa nchini ni kielelezo tosha cha kuonesha dhamira ya Rais ya kuona Tanzania mpya, Tanzania ya uchumi wa kati na Tanzania ya viwanda. Miradi kama reli ya *SGR*, umeme wa maporomoko ya Rufiji, ununuzi wa ndege, ujenzi wa viwanja vya ndege, ujenzi wa barabara za juu Jijini Dar es Salaam, ujenzi wa Hospitali za Wilaya na vituo vya afya, ni mifano michache ya Tanzania mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitambulisho vya wajasiriamali, naomba visigawiwe kwa idadi sawa kwa kila Wilaya. Ziko Wilaya ambazo zina wajasiriamali wachache, Wakuu wa Wilaya wanalazimika kuwakopesha watu ambao hawana uwezo wa kupata hata hiyo Sh.20,000 na kuwa kero kwa wananchi wanyonge kwani Mkuu wa Wilaya analazimika kumaliza hivyo vitambulisho vya wajasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria au kanuni za uendeshaji ni bora zikafanyiwa mapitio kwani zingine tayari zimepitwa na wakati. Mfano kwenye zile Halmashauri zinazoongozwa na upinzani, Diwani akikiuka kanuni fulani, Mwenyekiti ana madaraka ya kumtoa nje au adhabu nyingine lakini inapotokea Mwenyekiti amevunja kanuni,

kanuni au sharia hizo hazisemi chochote. Kwa namna hii baadhi ya Wenyeviti wanajifanya Mungu watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya wazee ni jambo muhimu sana. Ni muda mrefu sasa suala hili limekuwa likisemwa bila utekelezaji. Katika Wizara ya Afya hasa hospitali zetu nyingi, kuna vibao vyenye maneno kama “mpishe mzee” lakini ni mzee gani huyu tunayemzungumzia? Hivyo, umefika wakati sasa sheria hii ikaletwa hapa Bungeni ili hawa wazee wakatambuliwa na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale ni ya zamani sana ina umri wa miaka 43 lakini haina jengo hata moja la kuitambulisha Wilaya hiyo. Mfano, haina jengo la Mkuu wa Wilaya; jengo la Mahakama ya Wilaya; jengo la Polisi Wilaya na jengo la Hospitali ya Wilaya. Taasisi zote hizo nilizozitaja, zinatumia majengo ya iliyokuwa Tarafa ya Liwale Mjini ndiyo walirithi majengo hayo na kwa kuwa ni ya Tarafa yanashindwa kukizi mahitaji ya ofisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ilani ya CCM ya 2015-2010 barabara za Nachingwea - Liwale na Nangurukuru - Liwale zimeelezwa kuwa ni miongoni mwa barabara zitakazofanyiwa upembuzi na usanifu wa kina. Hivyo, naomba kwa bajeti hii jambo hili litekelezwe. Sambamba na hili, Mikoa ya Morogoro na Lindi bado haijaunganishwa kwa barabara za kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya maliasili kuhusu kifuta machozi kwa waathirika wa majanga yanayotokana na wanyamapori kama vile kuliwa mazao yao au kujeruhiwa nashauri ifanyiwe marekebisho. Bora sasa waathirika wakapewa fidia badala ya kile kinachoitwa kifuta machozi ambacho hakitolewi kwa wakati, sheria hii imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuongeza kasi ya ulipaji wa madeni kwenye taasisi zake. Zipo taasisi zinazoshindwa kujiendesha kwa kukosa mitaji, kwani fedha zao nyingi ziko Serikali Kuu (Hazina). Yako Mashirika na taasisi

zinazoidai Hazina fedha nyingi kiasi cha Mashirika hayo kushindwa kujiendesha. Pia, taasisi zingine zingefutiwa madeni yaliyopitwa na wakati na hayalipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo inaajiri wananchi wengi sana. Kwa hiyo, Serikali inatakiwa kuipa kipaumbele sana. Hapa mkazo mkubwa uwe kwenye utafutaji wa masoko na uwekezaji katika uchakataji wa mazao ya kilimo. Wakulima wengi hivi sasa wanashindwa kuchagua wajikite na mazao gani kwani bei za mazao zimekuwa zikibadilika mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, mwaka huu korosho zikishuka wakulima wanahamia kwenye ufuta. Mwaka unaofuata ufuta ukishuka, wakulima wanahamia kwenye mbaazi na mbaazi zikishuka wanahamia kwenye alizeti. Hivyo, nashauri Serikali ijikite kwenye kuimarisha masoko. Hii ndiyo changamoto kubwa sasa kwenye kilimo kuliko hata changamoto za pembejeo.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Halmashauri za Miji Midogo; za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji kuna kanuni za uendeshaji ambazo zinapelekea kuwepo kwa vikao vingi sana kwa mwaka. Kamati ni nyingi mno na malipo ni ya mara kwa mara kwa kila Diwani na zaidi kwa Wenyeviti/Mameya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wawakilishi hawa ni wengi sana, hivyo ipo haja ya kuangalia kama Kongwa unahitaji Madiwani 30 waliopo *plus* miji miwili midogo ya Kongwa na Kibaigwa ina Wenyeviti wa Mitaa 30 pia. Kwa Mkoa wa Dodoma kwa mfano, Halmashauri ni Kondoa Vijijini; Kondoa Mji; Chemba; Bahi; Dodoma Jiji; Chamwino; Mpwapwa; Kongwa; Mpwapwa Mji Mdogo; Kibaigwa Mji Mdogo; Kongwa Mji Mdogo, jumla ni 10. Kama wawakilishi ni 30 tu kwa kila Halmashauri kwa kikao kimoja cha Madiwani hao $30 \times 10 = 300$ na kila mmoja hulipwa shilingi 240,000 kwa kikao, jumla ya kikao kimoja tu ni shilingi 72,000,000 (hii ni *minimum*). Wajumbe wa Bodi za Afya kila Wilaya ni $100 \times 240,000 = 24,000,000$. Madiwani wajumbe wa Kamati za Fedha

na Mipango wanakaa mara 12 kwa mwaka, kwa vikao vya Kamati hiyo tu na hao hao ni wajumbe wa Kamati nyingine kwa hiyo wanalipwa *each* siyo chini ya mara ishirini kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ni kwamba vikao vipunguzwe kwa idadi na malipo yapungue. Patolewe mwongozo maana malipo haya ni kwa fedha za ndani za Halmashauri. Kipaumbele kinakuwa ni vikao vya Madiwani, fedha za maendeleo zinakosekana.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kuishukuru Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Magufuli kwa uimara wake katika kuendesha vyema nchi jambo ambalo limewezesha kuleta matokeo mengi mazuri. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Watendaji wake wote kwa kuweza kuitengeneza na kuiwakilisha hotuba hii kwa ufasaha wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo, kwanza ni kuhusu ziara za viongozi wa Serikal. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa viongozi wote wa Serikali namna wanavyofanya ziara katika nchi yetu. Hili ni jambo zuri ambalo linaamsha ari kwa sehemu zinazotembelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika jambo hili ni kwamba naomba ziara za viongozi wa taasisi za Muungano ziendelee kwa pande zote za Muungano. Kwa kuwa ziara hizi pamoja na mambo mengine zinaimarisha Muungano ni vyema zikatiliwa mkazo kwa kuwekewa mpango maalum wenye msisitizo wa kutembelea sehemu hizi za Muungano ili kuimarisha na kuchochea maendeleo katika Jamhuri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nizungumzie uwekezaji. Naipongeza Serikali yetu kwa juhudi kubwa inayochukua

katika kutilia mkazo uwekezaji katika nchi yetu. Uwekezaji ni miongoni mwa vyanzo vikubwa vya uchumi katika nchi. Aidha, uwekezaji unachochea upatikanaji wa ajira kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kuendelea kuweka mazingira mazuri ambayo yatawavutia wawekezaji wa ndani na wa nje kwa kuweka miundombinu rafiki itakayorahisha uwekezaji. Aidha, Serikali iweke mazingira bora yatakayoondoa urasimu wa upatikanaji ruhusa ya uwekezaji kwa wageni na wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MAKAME MASHAKA FOUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwako kwa kazi nzuri ya kuliongoza Bunge Tukufu. Pia namshukuru Mungu kunijalia afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Joseph Magufuli pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa Majaliwa kwa kazi nzuri ya kujenga Tanzania kufikia uchumi wa kati ifikapo 2015. Mwenye macho haambiwi tazama, jitihada za Awamu ya Tano tunazona, Ilani ya CCM imeweza kutekeleza kama ujenzi wa bandari, ununuzi wa ndege, ujenzi wa madaraja na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu zaidi ni kuhusu uwekezaji sehemu ya uvuvi. Tunayo maeneo makubwa ya uvuvi wa maji baridi na bahari. Kwenye bahari yetu tunao samaki wengi ila tuna upungufu wa vyombo vya uvuvi wa kisasa pamoja na utaalum. Pia tuna upungufu wa viwanda vya kusindika na kuchakata mazao yatokanayo na uvuvi. Naomba Serikali yangu kufanya jitihada za kuwekeza vizuri kwenye eneo hili ili kupunguza tatizo la upungufu wa ajira kwa vijana na kuliingizia pato Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kufungua vyuo vya uvuvi hasa maeneo ya pwani ili vijana wetu wapate taaluma ya mazao yatokanayo na uvuvi pamoja na kuhifadhi

mazingira ya bahari. Yako baadhi ya mazao ya baharini yako hatarini kutoweka kama kovu, kamba na wengine wengi. Hivyo, tuweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha tunalinda mazao haya muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu. Natoa shukrani kwa Serikali kwa ujenzi wa daraja la Mto Momba linalounganisha Mikoa miwili y Songwe na Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo, tunaomba sasa barabara ya kutoka Kilyamatundu hadi Kasansa, barabara inayounganisha Mikoa mitatu ya Rukwa, Songwe na Katavi. Barabara hiyo sasa itengewe fedha kwa ajili ya usanifu ili hatimaye ijengwe kwa kiwango cha lami kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutengewa pesa kwa ajili ya kumalizia maboma ya majengo ya madarasa na nyumba za walimu. Katika Jimbo la Kwela lililopo Sumbawanga DC upande wa elimu tunayo maboma 259. Zahanati tunayo maboma 32 ambayo yamejengwa na wananchi yanahitaji fedha za kumalizia. Vituo vya afya vilivyoanzishwa na wananchi saba (7) vinahitaji fedha ili vimaliziwe vianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna upungufu wa watumishi. Upande wa afya tuna upungufu wa watumishi 667 katika Halmashauri ya Sumbawanga DC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali itoe mgao wa miradi ya maendeleo na watumishi kwa uwiano ulio sawa bila kuwa na upendeleo. Baadhi ya Mawaziri wanapendelea maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Ntendo - Muze, tunaomba ijengwe kwa kiwango cha lami. Tunashukuru Serikali katika bajeti ya mwaka 2018/2019 ilitengewa fedha na kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami kilomita 2. Kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, tunaomba kilomita ziongezeke walau ziwe kilomita 5 ili kuwatendea haki wananchi kwani barabara hii ina umuhimu mkubwa sana kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa gari katika Kituo cha Afya Milepa. Kituo hiki ni kwa muda mrefu Serikali iliahidi kukipatia gari lakini hadi leo hakijapatiwa. Matokeo yake kimekuwa kikipoteza akina mama wajawazito wengi baada ya kukosa gari la kuwasafirisha kuwapeleka katika hospitali za rufaa kwa ujuzi ulio juu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu, wakati wa Kampeni za Uchaguzi za mwaka 2015 alitoa ahadi ya kujenga barabara ya Mtowisa – Ng’ongo - Kristu Mfalme kwa kiwango cha changarawe. Tunaomba ahadi hiyo itekelezwe ili kumpa heshima mama yetu na kuondoa shida wanayopata wananchi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji bado ni tatizo kubwa katika nchi yetu hususan Jimbo langu la Kwela, nikianza na Serikali kutucheleweshea kibali cha kutangaza mradi wa maji wa Vijiji kumi unaoitwa *MUZE GROUP*. Tunaomba kibali hicho kitolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kushindwa kulipa fedha kwa wakandarasi mfano Mradi wa Maji Ikozi. Naomba Serikali iwalipe wakandarasi hawa ili wasaidie upatikanaji wa maji kwa wananchi wangu.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika mahali hapa nami kuchangia hoja hii muhimu iliyopo mbele yetu. Vilevile nichukue fursa hii

kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa utendaji kazi mzuri katika kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu inatuonyesha mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2019/2020. Hotuba hii inakwenda kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kama ilivyoanishwa hasa katika kuleta maendeleo kwa wananchi na kukamilisha miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite katika kuchangia hotuba hii kwa kuanza na kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi ikiongozwa na Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Mafuguli, kwa kazi nzuri zilizofanywa na zinazoendelea kutekelezwa. Mapendekezo ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2019/2020 yamezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/2020 ambao ni wa nne katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka ya kutekeleza Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021. Dhima ya Mpango huo ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu wa Taifa hili. Aidha, mpango huu unatekelezwa sanjari na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 – 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi za Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka wa 2015 na zile alizozitoa katika hotuba yake ya kuzindua Bunge hili mwezi Novemba, 2015. Naipongeza Serikali kwa kuendelea kuona vipaumbele vya Mpango wa mwaka 2019/2020 ni kuendelea kuimarisha msingi wa uchumi wa viwanda, kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, kuendelea kuboresha mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji na kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya mwaka 2019/2020, Serikali

imeendelea kutekeleza Mradi wa Umeme wa Maji wa Mto Rufiji (*Stiegler's Gorge*). Ni jambo kubwa sana na la kupongezwa na si kubezwa kwani tumeshuhudia baadhi ya wapinga maendeleo wakija na hoja mbalimbali za kupinga mpango huu. Aidha, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa miundombinu ya reli ya kisasa (*SGR*), barabara pamoja na kukuza sekta ya anga. Utekelezaji wa miradi hiyo ya miundombinu wezeshi ya kiuchumi una lengo la kufungamanisha ukuaji wa sekta hizo na sekta nyingine hususan za biashara, kilimo na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwisha tangulia kusema hapo awali kwa kuipongeza Serikali katika miradi yake mbalimbali ya miundombinu na mingineyo, lakini kumekuwa na changamoto mbalimbali katika miradi hii ambazo mara zote Serikali imezichukulia kama fursa katika kuzitatua. Mradi wa ujenzi wa barabara njia nne (4) ambao kwa hivi sasa unaendelea ni mradi utakaoleta mapinduzi makubwa sana ila napenda kuishauri Serikali mradi huu ujengwe na kufika hadi Ruvu na kuendelea mpaka Mizani Vigwaza. Kwa kufanya hivyo kutasaidia sana kuleta mafanikio makubwa kwa eneo husika ambalo litaongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Mamlaka za Mji lakini kwa muda mrefu imekosa Mkurugenzi. Naomba katika mwaka huu wa fedha basi Serikali yangu sikivu iweze kutatua changamoto hii kwani kukosekana kwa Mkurugenzi kunazorotesha baadhi ya shughuli za Mamlaka hasa katika kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuishukuru Serikali kwa kutupatia fedha kiasi cha Sh.2,745,425,524 kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Halmashauri. Jengo hili liko katika hatua za mwisho kumalizika. Jengo hili litasaidia sana kupunguza changamoto iliyokuwa inatukabili ya kufuata huduma mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa kutoa mchango wake kiasi cha Sh.1,500,000 aliyotupatia

kuchangia ujenzi wa uzio wa Kituo chetu cha Afya Mlandizi. Tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuwa na dhamira ya kujenga uchumi wa viwanda sambasamba na kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya umeme wa kutosha na wa uhakika na nafuu. Kwa kutambua hilo, Serikali yetu inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya uzalishaji wa umeme yenye lengo la kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi ya uchumi wa kati unaochochewa na ukuaji wa viwanda ifikapo mwaka 2025, hizi ni hatua nzuri na zenye mlengo chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hatua kubwa ya uwekaji saina mkataba wa ujenzi wa Mradi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme wa MW 2,100 kati ya Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) na Kampuni ya *JV Arab Contractors & Elsewedy Electric* ya Misri ni hatua nzuri na ya kimaendeleo. Mradi huo unaotarajiwa kukamilika 2021/2022 utawezesha ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuhakikisha upatikanaji wa umeme tena wa bei nafuu na hivyo kukamilisha kivitendo dhana nzima ya mabadiliko na kipaumbele cha kuifanya Tanzania ya viwanda, kwani nishati ya umeme ndio chachu ya kuvutia uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu katika sekta hii ya nishati hadi kufikia mwishoni wa Februari, 2019 uwezo wa jumla wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini umeongezeka kutoka MW 1,205 mwaka 2015 hadi kufikia MW 1,614 mwaka 2019. Ongezeko hilo limepelekea kuwa na umeme wa ziada wa wastani wa zaidi ya MW 300 ambao utatuwezesha sasa nchi kama nchi kuwa na uhakika wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya Serikali ya kutekeleza kwa mafanikio makubwa Mpango wa Usambazaji wa Umeme Vijijini umekuwa wa mafanikio makubwa sana hasa kwa sisi tunaotoka maeneo ya vijijini kwani kwetu tatizo la ukosefu wa umeme lilikuwa ni changamoto kubwa sana. Kwa ujumla katika mwaka 2018/2019, vijiji 1,782

vimeunganishwa na umeme. Aidha, tangu kuanza kwa usambazaji wa umeme vijijini, tayari vijiji 5,746 vimeunganishwa umeme kati ya vijiji 12,268 vilivyopo nchini, sawa na takribani asilimia 47 ya vijiji vyote. Nalisema hili pasipo shaka yoyote kwani katika vijiji hivyo pia vipo vya Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia na kunipa afya nikaweza kuchangia hotuba hii muhimu sasa ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa utendaji wake mzuri sana uliotukuka na uliojaa uzalendo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu hii ninayoitoa Bungeni hapa na pia nitachangia kwa maandishi nitachangia kuhusu hoja moja tu ya uwekezaji ndani ya nchi yangu ya Tanzania. Nimpongeze Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kufanya miradi ya maendeleo ya nchi yetu, anamalizia viporo vya tangu Awamu ya Kwanza mpaka sasa Awamu ya Tano. Mungu ambariki sana Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi kwa Rais, nirudie kumpongeza kwa kuona umuhimu wa uwekezaji Tanzania. Nasema hivi kwa sababu Mheshimiwa Rais ameamua kuiunda Wizara ya Uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, lengo lake likiwa ni kuimarisha uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira yetu ya Maendeleo inataka ifikapo mwaka 2025 Tanzania iwe imeshafika kuwa nchi ya uchumi wa kati (*middle income country*). Nchi haitaweza kufikia nchi ya uchumi wa kati bila ya kuwa na viwanda vya kutosha. Rais wetu amechukua hatua nzuri sana

kumteua Waziri anayesimamia Uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ambako vilevile tuna Kituo cha Uwekezaji (Tanzania *investment Centre*) ili kuratibu vizuri juhudi zote za uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili alilolifanya katika mikakati yake ya kuboresha uwekezaji ni pale alipomtaka kwamba mwaka 2019 kuwa ni mwaka wa uwekezaji Tanzania. Alitoa tamko hili mbele ya Mabalizi wote wa nchi za nje wanaowakilisha nchi zao hapa Tanzania. Tamko hili la Rais ni la Kitaifa na ni la Kimataifa. Mheshimiwa Rais kutoa tamko hili la kuitambua mwaka 2019 kuwa mwaka wa uwekezaji amewatuma Mabalizi wa nchi za nje kualika nchi zao kuja kuwekeza nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia uwekezaji nchini nikisema yafuatayo. Tanzania tunalima pamba kwenye Mikoa mikuu minne ambayo ni Simiyu; Shinyanga; Mwanza na Geita. Simiyu peke yake inaongoza kwa kulima pamba zaidi ya 40% ya pamba yote inayolimwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiangalie Tanzania kwenye kilimo cha pamba ndani ya Afrika na ulimwenguni. Tanzania kwa kulima pamba inashika nafasi ya 8 kati ya nchi 30 za Afrika zinazolima pamba. Tanzania inashika nafasi ya 22 duniani kati ya nchi 77 zinazolima pamba. Katika hali kama hiyo, Tanzania Afrika na duniani tunalima pamba. Pamoja na Tanzania kuwa nafasi nzuri sana katika kilimo cha pamba lakini kuna tunachokosea na hivyo hatupati faida kubwa kiuchumi kutokana na zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia muda wote nilio nao kuishauri Serikali kwamba tutumie zao hili la pamba kupata wawekezaji wa *textile industry* (viwanda vya nguo). Mheshimiwa Rais alipoteua Waziri wa Uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, lengo lake ni kwamba anataka kuboresha uwekezaji nchini. Mimi ni Mbunge mkongwe, namfahamu Mheshimiwa Waziri aliye na dhamana ya Uwekezaji, Mheshimiwa Angellah Kairuki, nimshauri afanye kila jitihada

kuhakikisha zao la pamba linapata wawekezaji wa *textile industry*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kidogo niongelee nchi ya Bangladesh. Nchi ya Bangladesh ipo katika Bara la Asia. Ni nchi ndogo, ina eneo la kilomita za mraba takribani 148,000. Pamoja na udogo huo, Bangladesh ina *population* ya watu wapatao milioni 165. Nalinganisha Bangladesh na nchi yangu Tanzania. Tanzania ukiilinganisha kieneo na Bangladesh ni kubwa ina eneo za kilomita za mraba 945,087 na kulingana na sensa ya mwaka 2017, *population* yake ni milioni 57.31. Nimependa kuilinganisha Bangladesh na Tanzania kutokana na jinsi ambavyo nchi hii ndogo ya Bangladesh....

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni yangu kwa maandishi kuhusu hoja ya Waziri Mkuu. Awamu hii ya Tano, hali ya kisiasa si shwari sana kama tunavyoaminishwa. Utamaduni ulioanza kujengeka wa kubana Vyama vya Upinzani visishiriki siasa kwa uhuru kwa kusingizia taarifa za kiintelejinsia ilhali Chama Tawala wanaandama, wanaitisha mikutano ya ndani bila shida yoyote. Nia hii ovu ya *double standard* inachochea uvunjifu wa amani na kujenga chuki kubwa baina ya Chama Tawala na Vyama vya Upinzani, kinyume kabisa na maono na kazi kubwa aliyofanya Baba wa Taifa kujenga mshikamano wa Kitaifa kwamba sisi wote ni ndugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamata Wapinzani na raia na kuwajaza mahabusu kwa uonevu na kuwanyima dhamana ni hatari kwa amani na usalama wa nchi. Wizara husika ihakikishe kesi za mahabusu zinasikilizwa na haki kutendeka kwa kuachiwa kwa dhamana au kuhukumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ushiriki wa sekta binafsi. Mimi nilikuwa Kiongozi aliyesimamia *reforms* Serikalini na katika *reforms* hizo ni dhana ya *Public Private Partnership (PPP)* kwa masikitiko makubwa nimeona jinsi dhana hii ya *PPP* ilivyoachwa kabisa. Miradi mingi ya ujenzi wa majengo ya Serikali wanapewa taasisi za Serikali, ni kama

kutoa fedha kutoka mfuko wa kulia na kuhamisha mfuko wa kushoto kwenye suruali hiyo hiyo. Matokeo yake sekta binafsi imesinyaa, Serikali inasahau kwamba sekta binafsi inaposhamiri ndiyo inatoa ajira kwa wingi kuliko Serikali. Serikali isishangae kuona vijana wengi wasio na ajira, hii Serikali ya Awamu ya Tano ndiyo inayosababisha. Serikali ya Awamu ya Tano irejee kwenye *Blueprint* ya Awamu zingine na kuziendeleza, vinginevyo tutakuwa tunarudi nyuma kila Serikali mpya inapoingia madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri Mkuu na Mawaziri walioko chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kazi nzuri zinazotekelezwa na Serikali yetu ya Awamu ya Tano. Naridhishwa sana namna miradi mingi ya kipaumbele kwa Taifa inavyotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya PIC, tumeweza kutembelea miradi mingi inayotekelezwa kwa kipindi hiki. Miradi hii ni pamoja na SGR ambao ni mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa. Kazi inaenda vizuri sana na ujenzi unaenda kwa kasi na naamini ifikapo Novemba, 2019 huduma ya usafiri itawezekana kuanza kupatikana kwani hadi Morogoro kazi ni nzuri kabisa (Dar – Morogoro). Nampongeza Rais wetu na watendaji wote wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni ujenzi wa Kituo cha Kufua Umeme cha Kinyerezi I and II. Tumeweza kuona vituo vyote na kuona kiasi cha umeme kinachopatikana katika maeneo yote mawili, ni kazi kubwa imefanyika. Tumepata maelezo kuwa kwa sasa MW 1,650 zinapatikana kiasi hiki kinatosheleza mahitaji ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna utaratibu wa ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Stigler's Gorge ambapo

tutaweza kupata MW 2,100. Kiasi hiki ni kikubwa kuliko hata kiasi cha umeme tulichoweza kufanikiwa kupata tangu tupate uhuru. Kazi hii nayo imeanza katika hatua ya awali, inatia moyo na inaonyesha Mheshimiwa Rais alivyo mtu wa kuthubutu na sina shaka tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni ununuzi wa ndege na ujenzi wa viwanja vya ndege nchini. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais adumu na Mungu ampe afya atimize malengo yake ambayo yamepokelewa vizuri sana na Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine ni miradi ya ujenzi wa vituo vya afya, hospitali za Wilaya na Mikoa. Hizi ni juhudi kubwa kabisa, naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada kusema hayo, naomba nichangie mambo ya jimboni kwangu. Naomba Serikali inipe Kituo cha Afya katika Kata za Ninde, Kijiji cha Ninde. Wananchi wamejenga kwa nguvu zao jengo la yumba 10, naomba tuwaunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba Kituo cha Afya katika Kata ya Kala. Kata hii iko umbali wa zaidi ya kilometa 150 toka Makao Makuu ya Wilaya. Ni muhimu sana wapatiwe kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Vijiji vya Kasapa King'ombe, Mlambo Ng'undwe na Mlalambo mgogoro wao wa mpaka na *Lwanfi Game Reserve* utatuliwe. Naomba utatuliwe ili wananchi waweze kuishi kwa amani na kuzalisha uchumi kwa manufaa yao na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro wa Shamba la Milundikwa JKT na vijiji vinavyozunguka vya Kasu, Milundikwa, Kisula na Malongwe. Nashauri wananchi waongezewe ardhi ya kulima ili wafanye kazi za kujiletea maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vijiji vya Katani, Malongwe, Sintali, Nkana Kasapa na Mkomanchindo viwe vya mwanzo mwanzo kupata umeme ili kuweka vizuri mazingira ya kisiasa na maendeleo jimboni. Naomba umeme uende katika vijiji hivyo kwa awamu hii ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Shule ya Sekondari ya Kala miundombinu yake ya nyumba za walimu itazamwe. Pia mabweni ya watoto wa kike hakuna na iko maeneo ya mwambao ambako mwamko wa elimu bado ni duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Namanyere - Ninde naomba ikamilishwe. Daraja la Kizumbi, Kata ya Kizumbi lijengwe kwani maombi yalishaletwa kwa maombi maalum lakini ni muda mrefu halipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kata ya Kala wapate kituo cha Afya. Wananchi wako tayari kutoa nguvu zao kushiriki katika ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Sintali pia hawana maji katika vijiji karibu vyote vinne. Naomba utafiti ufanyike kuona chanzo kizuri cha kusaidia wananchi hawa ambao vijiji vyao viko karibu karibu yaani Sintali, Nkana na Mkomanchindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashauri katika suala la kilimo Serikali ione namna ya kuendelea kutoa ruzuku kwa wakulima wa chini bila hivyo hali inaendelea kuwa mbaya sana katika uzalishaji na kumudu maisha kwa wakulima hawa. Pembejeo zitolewa hata kwa watu wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile masoko ya mazao ya wakulima hasa mahindi Mkoa wa Rukwa na mikoa yote inayolima zao hilo yatiliwe maanani vinginevyo wakulima watakata tamaa. Naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ilete mageuzi kwenye kilimo kama inavyofanya katika maeneo ya miundombinu mbalimbali kama ujenzi wa *SGR*, ujenzi wa barabara, viwanja vya ndege, afya na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kama Mheshimiwa Magufuli ni zawadi kwa Watanzania toka kwa Mungu. Ana maono na uthubutu na kweli anatatua yale yote yaliyoonekana kushindikana. Kama vile madawa ya kulevya; uzembe wa kazi Serikalini; wizi wa mali ya umma; urasimu na kuchelewesha maamuzi na uonezi hasa kwa watu wa chini. Mungu amzidishie aweze kufikia malengo yake kwa Watanzania.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mikakati gani kuanzisha Mfuko wa Wazee utakaowezesha wazee wasiokuwa kwenye ajira rasmi kujajiri kwenye shughuli za uzalishaji mali? Wapo wazee wenye nguvu na uwezo wa kuunda vikundi kwa ajili ya uzalishaji na shughuli za ujasiriamali tatizo kubwa hawana mtaji. Umri wa ujana unaishia miaka 45, wazee kuanzia miaka 46 kuendelea ambao hawana pensheni wanaishi kwa tabu sana vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetenga baadhi ya shule za msingi kwenye Halmashauri ya Wilaya na Miji kwa ajili ya kusajili watoto wenye mahitaji maalumu (walemavu). Nini mkakati wa Serikali kuwezesha miundombinu ya shule hizi kuwa rafiki kwa ajili ya watoto hawa walemavu wa aina mbalimbali? Nini mpango wa Serikali kupeleka walimu wenye ujuzi na taaluma ya kufundisha watoto hawa wenye mahitaji maalum ili waweze kunufaika na elimu kama wanafunzi wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la vijana kutokuwa na ajira linaendelea kila siku na kila mwaka vijana wanamaliza vyuo vikuu, vyuo vya kati katika fani mbalimbali. Ni vijana wachache sana wanapata ajira Serikalini na kwenye sekta binafsi. Nini mkakati wa Serikali kuwezesha vijana wengi kujajiri kwa kuwapatia mitaji na vifaa/mashine za kufanyia kazi za ujasiriamali kwenye viwanda vidogo vidogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kilimo ni sekta inayoajiri watu wengi ni maeneo yapi na wapi yametengwa

katika Mikoa mbalimbali ili kuwezesha vijana kujishughulisha na uzalishaji mashambani?

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wake wawili Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Kairuki pamoja na Naibu Mawaziri wawili katika ofisi hii kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba kuchangia eneo la sekta ya uwekezaji ambalo ni sehemu muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu. Kitengo cha Uwekezaji ni muda mrefu kimekuwa kikilalamikiwa sana kwa kuchelewesha uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje na kubwa zaidi ni urasimu kwa watendaji kutochukua maamuzi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo napenda kumsahuri Waziri mwenye dhamana kwenye Ofisi hii kwanza ni kwa watendaji kubadilika kifikra, wasifanye kazi kwa mazoea. Hili litawezekana kwa kutambua umuhimu wa ofisi kwamba ni nyeti na ikitekeleza majukumu yake ipasavyo nchini hii itasongo mbele katika kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu wa kutazama na kupitia kuona kama sheria za uwekezaji zilizopo kama zinachangia katika kurudisha nyuma uwekezaji. Kama hivyo ndivyo ni vema zikaletwa hapa Bungeni tuzifanyie mabadiliko lakini hili litawezekana kama tathmini itafanywa na Ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Waheshimiwa Wabunge wakichangia humu kwamba wawekezaji wengi wanakimbilia nchi jirani wakati fursa nyingi zipo hapa nchini. Naomba Waziri mwenye dhamana aliambie Bunge sababu hasa ni nini? Nashauri kiwepo kitengo katika Ofisi ya Waziri Mkuu cha kufanya tathmini na stadi ya mara kwa mara labda kila baada ya miezi sita ambayo itakuwa inatoa tathmini ya mafanikio, changamoto na wapi

uwekezaji umekua. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuleta ufanisi wa kitengo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kutoa mawazo yangu ni ajira hususani kwa vijana. Idadi ya vijana wasiokuwa na ajira inazidi kuongezeka. Kwa sasa tuna vyuo vingi na vinazalisha vijana wengi wa kada mbalimbali lakini pia wapo ambao hawajabahatika kuendelea na masuala ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri elimu ya ufundi hususani ya *VETA* ipewe kipaumbele, kila wilaya lazima iwe na chuo cha *VETA*. Hii itotoa fursa kwa vijana wetu kujifunza stadi mbalimbali na itapunguza changamoto ya ajira. Pia ni vema ofisi hii ikawa na utaratibu wa kuhakikisha vijana wanapata elimu ya ujasiriamali na iratibu na upatikanaji wa mikopo midogo midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 4 ambayo inatozwa na Halmashauri zetu kutokana na mapato ya ndani kamwe haiwezi kusaidia vijana kujiwezesha kuwa na miradi kwa sababu Halmashauri nyingi uwezo wa mapato umepungua na hata zile zenye uwezo huo watendaji wengi hawatimizi takwa hili la kisheria. Tusipokuwa makini kulitazama kundi hili muhimu la vijana kwa jicho la tatu hakika siku za usoni Serikali itakuwa katika wakati mgumu wa kutatua changamoto za vijana.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwani katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita imefanikiwa kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu hususan Jimbo la Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Serikali kupitia Wizara mpya ya Uwekezaji kuendelea kuhamasisha na kuvutia wawekezaji kutoka nje na ndani. Nchi yetu imejaliwa rasilimali mbalimbali yakiwemo madini. Katika Wilaya ya Mbeya kuna madini ya niobium ambayo ni adimu sana na mahitaji yake ni makubwa kwa viwanda vya vyuma,

mabomba ya mafuta, injini za ndege na hata vifaa vya kielektroniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza *TIC*, *EPZ* na Wizara ya Madini waweke mkakati wa kuvutia wawekezaji katika viwanda vya vyuma na niobium ambayo yanaweza kusaidia kupunguza gharama na hasa pesa za kigeni kwa kuagiza vyuma toka nje ya nchi. Kutokana na miradi mingi ya ujenzi wa madaraja, bomba la mafuta, *SGR* na vivuko, kiwanda cha niobium kitakuwa msaada mkubwa kupunguza gharama na pia kuwezesha nchi yetu kuuza madini yetu ambayo yameongezwa thamani na kwenda moja kwa moja kwa walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na azma yetu ya Tanzania ya viwanda, kuna mahitaji makubwa ya mafundi mchundo (*technicians*) na mafundi wasaidizi (*artisans*). Kwa vile Taasisi ya Maadilisho iliyopo Irambo, Mbeya DC ina miundombinu ambayo ni *under-utilized*, napendekeza Serikali (Wizara ya Afya) iruhusu shule hii ibadilishwe matumizi na kuwa chuo cha ufundi kwa Kanda nzima ya Mikoa ya Kusini Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mbeya ina changamoto kubwa za barabara na viongozi wa kitaifa walitoa ahadi za ujenzi wa barabara zifuatazo kwa kiwango cha lami, napendekeza ahadi hizo zitekelezwe. Barabara hizo ni Mbalizi – Shigamba – Isongole; barabara ya Mbalizi – Makongolosi na barabara ya Isyonje - Kikondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iimarisha usimamizi wa soko la zao la pareto. Pia nashauri liwe mojawapo ya mazao ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za kupeleka maji vijijini katika Jimbo la Mbeya bado upatikanaji wa maji ni changamoto kubwa hasa Kata ya Mjele na Mji Mdogo wa Mbalizi. Naomba Serikali itimize ahadi za kutatua kero hii kubwa ya maji katika Jimbo la Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa. Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba iliyosheheni taarifa muhimu za utekelezaji kwa vitendo lani ya Uchaguzi na pia kuandaa bajeti yenye dhamira ya dhati ya kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri wote, Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa taarifa ya bajeti hii. Wananchi wamejenga maboma mengi ya zahanati na wamefikia hatua mbalimbali na wamekuwa wakihitaji msaada kutoka Serikalini ili kukamilisha maboma hayo kwa ajili ya kupunguza mwendo kwenda kupata huduma za afya. Natoa rai katika bajeti hii Serikali iweke fedha kwa ajili ya kukamilisha baadhi ya zahanati. Aidha, nashauri uwepo mpango maalum wa Serikali na kujijwekea ratiba maalum ili kukamilisha maboma haya ya wananchi hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya visima vya maji imekwama kutokana na miundombinu. Visima vimechimbwa lakini baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Dodoma *pump* na mitambo hakuna. Ni budi Serikali ikayabaini maeneo yote nchini yenye kadhia hii na kuona jinsi ya kurekebisha ili wananchi waweze kufaidika na upatikanaji maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumepitisha sheria inayoitaka kila Halmashauri itoe asilimia 10 ya mapato kwa makundi ya wanawake, vijana na walemavu. Nashauri Serikali ifanye ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha kila Halmashauri inatekeleza pia urejeshwaji wa pesa hizo. Aidha, ifanyike tathmini mwishoni mwa mwaka wa fedha kuona wananchi waliofaidika wamebadilika vipi kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni budi uwekwe utaratibu wa utoaji taarifa kuhusiana na asilimia 10, ikiwezekana kila Halmashauri iwe inatoa taarifa ya maendeleo ya utoaji na

urejeshaji fedha kila baada ya miezi sita au jinsi Serikali itakavyoona inafaa. Hali kadhalika Maendeleo ya Jamii wapitie Halmashauri zote zisizofanya vizuri ili zichukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michezo kuanzia ukurasa wa 71-73 imezungumzia soka, je, timu za soka la wanawake hawakushiriki katika michezo? Michezo ya mpira wa pete na mingine inayochezwa na wanawake nayo ipewe kipaumbele ili kuonyesha pia wanawake wanashiriki soka na michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza uwepo wa ziada ya chakula ya tani milioni 3.32 za mazao yetu. Aidha, kipindi hiki mvua si nzuri na ukame umeathiri maeneo mengi, hivyo suala kilimo cha umwagiliaji bado inabidi Serikali ilisisitize kwani kutegemea mvua bado si salama kwa usalama wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri na watendaji wote kwa kuleta hotuba hii. Napenda kuchangia maeneo mawili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa Mfuko wa Kinga ya Bei za Mazao (*Price Stabilization Fund*). Eneo hili limechangiwa pia na Mheshimiwa Bashe. Nilitamani kumpa taarifa lakini nikaamua kuleta mchango kwa maandishi. Kati ya miaka ya 2012 – 2014, Wizara ya Kilimo ilianzisha mchakato wa kuanzisha *Price Stabilization Fund* kwa mazao ya korosho, kahawa, pamba na tumbaku kwa lengo la kukabiliana na madhara yanayotokea pindi bei ya mazao zinapoanguka hasa katika masoko ya dunia. Sijapata habari kwa nini mchakato huo haukuendelezwa au kama uliendelezwa ulifikia hatua gani. Nashauri Mheshimiwa Waziri alipeleze suala hili, inawezekana bado lina umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maafa yako ya aina mbalimbali kama vile njaa, ukame, moto, matetemeko, mafuriko na kadhalika. Leo napenda kuchangia suala la maafa yanayotokana na mafuriko. Mafuriko yanapotokea yanaathiri mazao, miundombinu kama ya biashara, reli, nyumba na kadhalika. Yako maeneo yenye mito ambayo mara kwa mara inaleta mafuriko yanayoharibu madaraja, barabara, reli, simu na kadhalika kama kule Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ijipange kujenga mabwawa makubwa ambayo yatakuwa na manufaa makubwa mawili. Kwanza kuepusha uharibifu wa miundombinu na pili yatumike kwa kilimo cha umwagiliaji wakati wa kiangazi. Suala hili linahitaji utayari wa kukabiliana na majanga, je, Serikali inao mkakati wa *disaster preparedness*? Hasara ambayo Serikali inapata kutokana na gharama za kurudishia miundombinu inayohabiriwa na mafuriko ni kubwa lakini pia uharibifu unapotokea unasababisha fedha na rasilimali nyingine kuelekezwa katika ukarabati wa miundombinu badala ya kuelekezwa kenye maeneo (miradi) mipya ya maendeleo.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi anazofanya kwa umahiri mkubwa. Namuomba Mungu azidi kumtia nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo ahadi za Mheshimiwa Rais katika Jimbo la Mbulu Vijijini ambayo ni barabara ya lami toka Mbulu – Haydom - Sibiti. Naomba itengwe fedha ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kutoka Haydom - Mbulu maana hatuna kabisa lami katika Jimbo la Mbulu Vijijini. Kwa kutekelezwa kwa ahadi hii ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli itakuwa imetatua kero kubwa ya wananchi ya kushindwa kufika katika Hospitali ya Haydom. Pili, kwa kufanya hivyo mtakuwa mmetekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa ujenzi wa Kituo cha Afya Dongobesh. Tunaomba tupewe fedha za kujenga Kituo cha Afya Maredadu maana wananchi wameshajenga katika hatua ya mwanzo ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la kutomalizika kwa miradi ya maji katika Jimbo la Mbulu Vijijini, mfano mradi wa Arri – Harsha na Tumati Mungasharq. Tunaomba msukumo wa Serikali katika miradi hii ya maji. Nashauri pawepo na Mamlaka za Maji za Mikoa ili ziweze kuisimamia miradi ya wilaya kwa ukaribu zaidi na *certificate* zilipwe kwa wakati.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waziri Mkuu akiwa Kiongozi Mkuu wa shughuli za Serikali Bungeni, hotuba yake imetoa mwelekeo mzuri kabisa wa vikao vyetu vyote vya bajeti za Wizara mbalimbali zitakazofuata. Serikali ya Awamu ya Tano imejenga msingi madhubuti wa kujenga Tanzania ya viwanda ikisadifu na kauli mbiu ya Chama cha Mapinduzi ya CCM mpya na Tanzania mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Magufuli akisaidiwa na Makamu wake wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa imedhamiria kwa dhati kujenga uchumi wa kisasa kwa kuja na mpango wa kuwa na miradi mikubwa ya kimkakati katika sekta mbalimbali ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa ya kiwango cha kimataifa (*Standard Gauge – SGR*), mradi mkubwa wa maji wa kufua umeme kutoka Mto Rufiji (*Stigler’s Gorge*) utakaosaidia kufua umeme wa MW 2,100, hii ikiwa ni katika kuhakikisha Tanzania ya viwanda inafikiwa kwani viwanda bila umeme haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya nishati kutokana na vyanzo mbalimbali kunasaidia sana utekelezaji wa miradi mbalimbali ya usambazaji wa huduma ya umeme kupitia Wakala wa Umeme Vijijini maarufu kama *REA*. Kwa hakika huduma hii imeleta mabadiliko makubwa katika shughuli za

maendeleo vijijini na hivyo kupunguza uhamaji wa watu kutoka vijijini kuhamia vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naipongeza Serikali kwa kuja na mpango kabambe wa kuimarisha huduma katika sekta ya afya kwa kujenga vituo vingi vya afya katika sehemu mbalimbali ikiwemo Wilayani Mbogwe ambapo vituo vya afya vya Iboya na Masumbwe ambavyo kwa pamoja vimepatiwa jumla ya shilingi milioni 800 na kwa hakika vituo hivi vimeboreshwa kwa kiwango kikubwa. Kwa hili, tunaipongeza sana Serikali, pia Serikali imetupangia shilingi milioni 500 tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya elimu, suala la elimu bila malipo limeleta changamoto kubwa sana na wananchi wengi wamejitokeza kupeleka watoto wao kuandikishwa darasa la kwanza. Katika hali hii Watanzania wengi wamepata fursa ya kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa reli kwa kiwango cha *Standard Gauge* kunategemewa kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya mawasiliano na uchukuzi, jambo ambalo litaokoa kwa kiwango kikubwa uharibifu wa barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imepiga hatua kubwa sana katika kupambana na biashara ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa viwanja vya ndege na ununuzi wa ndege mpya utachangia kwa kiwango kikubwa ukuaji wa uchumi kupitia sekta ya utalii kwa kuleta wageni toka ng'ambo na kuleta chachu ya upatikanaji wa pesa za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni sekta nyeti sana nchini kwani kinaajiri watu wengi sana karibu asilimia 75. Hivyo napenda kuishauri Serikali kuwekeza zaidi katika suala la utafiti wa ardhi, mbegu, magonjwa pamoja na visumbufu vya aina mbalimbali. Upatikanaji wa pembejeo zikiwemo mbolea na mbegu bora kutasaidia kuongeza tija katika uzalishaji wa

mazao ya chakula na ya biashara ili yaweze kuwa ni chachu ya kuifanya Tanzania ya viwanda iweze kutimia maana viwanda vyetu vitatumia malighafi kutokana na mazao ya kilimo. Naiomba Serikali izidi kuwekeza ama kukaribisha wawekezaji katika viwanda vya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana ambayo imeonesha mafanikio mengi sana ambayo yamefanyika nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutoa elimu bila malipo. Changamoto nyingi zimejitokeza kama upungufu wa vyumba vya madarasa, madawati, vyoo, nyumba za walimu, walimu na vitabu vya kujifunzia na kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuboresha afya za Watanzania nchini. Upande wa afya Jimboni kwangu kuna baadhi ya changamoto kama vile upungufu wa wahudumu katika vituo vya afya na zahanati zetu. Pia katika vituo vyetu vya afya hatuna mashine hata moja ya picha ya *X-ray* na baadhi ya vifaa muhimu vya uchunguzi wa afya ya binadamu. Pia kuna upungufu mkubwa wa vitambulisho kwa wazee kwa ajili ya matibabu bure kwa wazee. Ni wazee 100 tu kati ya 6,000 ambao wana vitambulisho nchini, sasa hawa wazee 5,000 watapatiwa vitambulisho hivyo lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuboresha baadhi ya kero kwa upande wa madini. Kwa upande wa Jimbo la Nyang'hwale bado kuna kero kubwa kwa wachimbaji wadogo kwa kutopimiwa maeneo yao na kupatiwa leseni za uchimbaji. Maeneo hayo ni Bululu, Ifugandi, Isonda, Isekeli, Lyulu, Nyamalapa, Kasubuya, Rubando, Iyenze, Shibaranga na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kupunguza kero ya maji vijijini na mijini. Kwa upande wa Jimbo langu la Nyang'hwale, kuna mradi mkubwa toka chanzo cha Ziwa Viktoria kutoka Nyamtukuza, Kakora, Kitongo, Ikangala, Kharumwa, Iyenze na Bukwimba. Mradi huu umeanza tangu 2014 hadi leo 2019 hata tone moja la maji halijatoka na kusuasua kwa wakandarasi wanadai Serikali haijwalipa fedha. Nataka kujua tatizo liko wapi, ni Serikali kutowapa malipo au wakandarasi ni matapeli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuboresha miundombinu ya barabara kwa viwango vya lami na changarawe. Kwenye Jimbo la Nyang'hwale kuna ahadi za viongozi wa nchi, kuna Rais wa Awamu ya Nne kuhusu ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami toka Kahama - Nyang'holongo – Bukwimba – Kharumwa – Nyijundu – Busorwa – Busisi. Pia Rais wa Awamu ya Tano naye aliahidi, je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja hii.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kusifia maendeleo mazuri ya demokrasia hapa nchini lakini ripoti iliyotolewa na Shirika Huru la *Freedom House* tarehe 10 Februari 2019 inaeleza kwamba Tanzania inashindana na maeneo yenye hatari kisiasa duniani. Hii ni kutokana na kukamata viongozi wa upinzani, kuzuia maandamano dhidi ya Serikali, kuzuia mikutano ya vyama vya upinzani na sheria ya kuimarisha chama tawala na kuminya vyama vya upinzani. Ripoti ya *Freedom House* inaendelea kueleza kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi 10 duniani ambazo zilipata maendeleo ambayo yameathiri mwelekeo wake wa kidemokrasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuridhika na hamasa za Watanzania katika uwekezaji wa ujenzi wa viwanda *page* 33, lakini ripoti ya taasisi ya *Quantum Global Research Lab* ya Machi 2018 juu ya uwekezaji Barani Afrika

inaeleza kwamba Tanzania huenda isifikie lengo lake la kujenga uchumi wa viwanda. Hii inatokana na mabadiliko ya sera za usimamizi wa fedha na rasilimali ambazo siyo rafiki kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti huu ulihusisha nchi 54 za Afrika ambapo Tanzania ilishika nafasi ya 13 mwaka 2018 kutoka nafasi ya nane mwaka 2017 kwa nchi zenye mazingira mazuri ya uwekezaji. Mabadiliko ya sera za fedha na mazingira magumu ya kuanzisha na kufanya biashara ambayo yanaathiriwa na ongezeko la kodi na upatikanaji wa leseni za biashara ni sababu za mkwamo wa ukuaji wa sekta binafsi na uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Benki ya Dunia (*WB*) urahisi wa kuanzisha biashara Tanzania uko chini ya wastani unaotakiwa na nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Naiomba Serikali kujitahidi kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji ili iweze kufikia malengo yake ya kufikia uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa Kitanzania wamekata tamaa kutokana na tatizo la ajira linalowakabili. Kati ya mwaka 2015 hadi Desemba 2018 jumla ya vijana 594,300 walimaliza vyuoni kati ya hao ni vijana 6,554 sawa na asilimia 1.1 ndiyo waliopata ajira. Hali hii inaonesha kushindwa kwa Serikali ya Awamu ya Tano katika kuwahudumia vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la vijana kukosa ajira baada ya kumaliza masomo yao kunaweza kusababisha madhara ya afya zao. Hivi karibuni Shirika la Afya Duniani (*WHO*) lilisema karibu vijana milioni 3.7 wanaugua ugonjwa wa sonona (*depression*) kutokana na ukosefu wa ajira. Niombe Serikali kuhakikisha vijana wanapomaliza masomo yao wanapatiwa ajira ili kuwaepusha na ugonjwa huo wa sonona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi zinapunguza kasi ya kuajiri na inapunguza wafanyakazi kutokana na

mazingira yasio rafiki kwao. Hivyo basi ni jukumu la Serikali kukabiliana na changamoto za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ya kusimamia utekelezaji wa Ilani yetu ya CCM ya 2015-2020, sambamba na Waheshimiwa Mawaziri Mheshimiwa Jenista na Manaibu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwanza kwenye hoja ya uwekezaji. Tunatambua Mheshimiwa Waziri Mkuu ameanzisha kampeni ya kufufua zao la michikichi katika Mkoa wa Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa Mbeya Wilaya ya Kyela. Zao hili la michikichi asili yake hapa Tanzania ni Mkoa wa Kigoma na sote tunatambua kuwa zao hili ndilo linalowapa kipato wananchi wa Kigoma likifuatiwa na zao la muhogo na maharage.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma nchi ya Malaysia walikuja kuchukua miche na kupeleka kwao, leo hii Malaysia ndiyo nchi inayoongoza duniani kwa uzalishaji wa *palm oil*. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa tamko la kuwa Chuo cha Kihinga kuwa kituo cha uzalishaji mbegu au miche, tunaomba bajeti itengwe kwa ajili ya uzalishaji na ununuzi wa miche ili basi Serikali iweze kuwapa wananchi wake ili dhamira ya kuwa na viwanda vya mafuta ya mawese iweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alikutana na wadau mbalimbali tarehe 28 Julai, 2018 akaja na Bank ya *TIB* na *TADB*, tuiombe Serikali masharti yawe mepesi ili wakulima wengi wa zao la michikichi wapewe mikopo kununua miche ya michikichi. Tumuombe pia Mheshimiwa Waziri Mkuu atuletee wawekezaji wa kununua mazao hayo na kuanzisha viwanda vya mafuta haya ya mawese ili kununua zao hili la michikichi. Nimezungumzia sana zao la michikichi kwa sababu ni zao

muhimu sana Tanzania na ulimwenguni kote wanatumia *palm oil*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie zao la muhogo. Tunatambua hivi karibuni Serikali ilipokea wawekezaji wanaotoka China wanaohitaji kununua mihogo tani kwa tani kupitia Wizara ya Kilimo. Tunacho Chuo cha Naliendelea kina mbegu nzuri sana za mihogo, swali langu wananchi wanaotoka kwenye mikoa inayolima zao hili wanapataje mbegu ili wawekezaji waweze kununua mihogo yenye tija?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, Wizara ya Uwekezaji isimamie uanzishwaji wa viwanda vya kutengeneza karatasi na mifuko ya karatasi ili tuondokane na uharibifu wa mifuko ya *plastic* inayotuchafulia mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie uwekezaji wa kwenye sekta ya uvuvi. Sekta hii tumeiacha sana lakini kama tutaiangalia vizuri inaweza kutuingizia pato kubwa katika taifa letu. Mfano tunaweza kununua meli za uvuvi katika maziwa yetu ya Victoria, Nyasa, Tanganyika na kadhalika. Kwenye bajeti ya 2018/2019, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alionyesha kuweka fedha za ununuzi wa meli za uvuvi, hata bajeti ya mwaka huu 2019/2020 kwenye mpango wa maendeleo tumeendelea kuonyesha kuwa Serikali imepanga kununua meli hizo za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma Mkoa wa Kigoma tuliwahi kupata mwekezaji toka Ugiriki alikuwa na meli ya uvuvi iliyoitwa YOROGWE. Meli hii ilikuwa inavua samaki wengi sana. Kigoma watu wengi wanajua tuna samaki aitwae mgebuka lakini tunao samaki aina nyingi kwa utafiti uliofanywa na Wachina wakagundua tunao aina za samaki 250. Kwa mfano, ninaowajua mimi na kuwala ni mgebuka, kohe, ngenge, sangara, monzi, singa, karongwe, mbaga, mneke, kabare, mbisu, mrombo ndubu na kadhalika. Natambua sekta ya uvuvi, mifugo na kilimo inachangia zaidi ya asilimia 40 ya pato la Taifa. Hivyo ni wakati muafaka sasa

Serikali yetu ikajikita kwenye sekta ya uvuvi, kilimo na mifugo ili pato letu la Taifa likue zaidi kwa sekta hizi tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo, naomba niendeleo kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayofanya kwenye Taifa hili. Sote tunamuona jinsi anavyofanya ziara mikoani na ndani ya wilaya zote kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya CCM ya 2015-2020 inatekelezwa ipasavyo. Nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Jenista, Waziri, Mheshimiwa Kairuki na Manaibu wote wawili kwa kufanya kazi nzuri ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MWENYEKITI: Sasa nahamia kwa wachangiaji wa Serikali kwenye hoja hii. Nitaanza na Mawaziri ambao tutawapa dakika tano tano tu, naanza kuwatambua wafuatao: Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako na Mheshimiwa Dkt. Kalemani, hawa wa kwanza. Mheshimiwa Jafo, haya naendelea Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako Waziri ni Waziri mkiniaandikia ni Waziri atachangia, siwezi kubadilisha. Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, dakika tano.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Ningependa kuanza kwanza kabisa kwa kusema naunga mkono hoja hii na napenda kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo wanafanya katika kuratibu shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia katika maeneo machache. Kwanza kuna suala la mafunzo ya ufundi stadi ambalo limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge wameonesha dhamira au nia ya kuona elimu ya mafunzo ya ufundi stadi inaendelea kuimarishwa katika maeneo yao. Niseme tu kuwa Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba inaongeza fursa na nafasi za mafunzo ya ufundi stadi

na kama ambavyo wiki iliyopita tulikuwa na Mheshimiwa Rais kule Namtumbo tunazindua Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Namtumbo. Pia kuna chuo vingine vya ufundi stadi ambavyo tunaendelea na ujenzi katika maeneo mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Ileje, Chato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaendelea na ujenzi wa VETA za Mikoa; Mkoa wa Kagera, Simiyu, Mkoa wa Njombe pamoja na Mkoa wa Geita. Pia Serikali imefanya ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) na mpaka sasa tumeshafikia vyuo 20 kati 34 na katika bajeti ya mwaka huu ambapo naamini Waheshimiwa Wabunge wataiunga mkono, tunategemea kufikia vyuo 34 vilivyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumziwa ni suala la udhibiti ubora wa shule. Ningependa kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali iko makini sana katika suala la udhibiti ubora kwa sababu tunaamini kwamba Wadhibiti Ubora wa Shule ndio jicho la Serikali katika kutuhakikishia kwamba tunafikia malengo yetu katika sekta ya elimu. Kwa hiyo Serikali inaendelea kuiangalia idara hiyo kwa makini zaidi na vile vile tumeendelea kuiimarisha katika kuhakikisha kwamba inapata vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita, Serikali ilitoa magari 45 kwa ajili ya ofisi mbalimbali za udhibiti ubora wa shule, lakini tumeendelea kuiimarisha katika vitendea kazi kama kompyuta. Pia tumeangalia namna Wadhibiti Ubora wanavyofanya kazi kwa sababu zamani Wadhibiti Ubora walikuwa wamekaa kipolisi polisi zaidi. Wanaenda kuwatisha Walimu badala ya kwenda kuwapa *support* yaani kwa maana kwamba kuwaonesha upungufu wao na kufanya kazi. Tumebadilisha mfumo na tumetengeneza kiuzi cha udhibiti ubora ambacho lengo ni kwenda kuboresha mifumo ambayo inajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile limezungumziwa suala la vifaa vya kufundisha hasa katika shule za sekondari. Serikali ya Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba maabara ambazo zilikuwa zimeanzishwa na

wananchi zinapata vifaa. Kwa hiyo jumla ya shule za sekondari 1,696 zimeweza kupata vifaa vya kufundishia masomo ya sayansi ambayo yapo kwenye muhtasari kuanzia kidato cha kwanza mpaka kidato cha sita, ni vifaa ambavyo vinajitosheleza. Niendeleo kuwahakikishia Wabunge kwamba kwenye sekta ya elimu na hasa kwenye masuala ya Mafunzo ya Ufundi stadi ambayo tunafanya na Ofisi ya Waziri Mkuu, tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ningependa kuzungumzia suala la elimu maalum ambalo pia nalo tunalifanya kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu. Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba wanafunzi wenye mahitaji maalum wanaendelea kupata elimu yao katika mazingira rafiki zaidi. Kwa hiyo, tuna progamu ya kusambaza vifaa na visaidizi kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum na tutaendelea kufanya hivyo kwa sababu tunaamini kwamba elimu ni haki ya kila mtoto na hata yule ambaye ana changamoto anastahili kupata elimu katika mazingira mazuri.

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa kwa ufafanuzi na mchango mzuri. Tunaendelea Waziri wa Madini, Mheshimiwa Doto Biteko dakika tano.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Nami kabla sijazungumza maeneno mengi naomba nioungue mkono hoja, lakini nimpongeze sana mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na wasaidizi wake Mawaziri; Mheshimiwa Jenista Mhangama pamoja na Mheshimiwa Angella Kairuki na Manaibu Waziri kwenye Wizara hii kwa kazi kubwa waliyoifanya na kwa namna kwa kweli ambavyo wamewasilisha hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwenye sekta ya madini yapo maeneo ambayo yamezunguzwa kwa urefu kidogo na Waheshimiwa Wabunge na moja ya jambo ambalo limeongelewa hapa ni habari ya kudhibiti utorohaji wa madini, kwamba Wizara ionge msukumo kwenye

utoroshaji wa madini. Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa *champion* mkubwa sana kwenye jambo hili, kama mtakumbuka aliitisha mkutano na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote nchini kwa ajili ya uanzishwaji wa msoko ya madini nchini. Tulikaa kwa siku mbili nzima na yeye mwenyewe alitoa msimamo mkubwa na hata wakati kwa kwenda kuzindua soko la madini kule Geita, yeye Mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu alichukua kazi hiyo ya kuzindua soko. Pia akatoa maelekezo kwa Waheshimiwa Wakuu Mikoa wote kwamba ifikapo Juni 30 mwaka huu, kila Mkoa kuwa na masoko ya madini mbalimbali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye mtoa hoja wetu leo kwa kweli amekuwa msimamizi mkubwa sana wa jambo hili. Hata hivyo, Wizara ya Madini tunafanya kazi ya kubwa ya kusimamia utoroshaji wa madini kama tulivyoeleza. Kwanza mambo yaliyokuwa yanasababisha utoroshaji wa madini ni kodi ambazo sio rafiki. Watu walikuwa wanaona nafuu kwenda kuuza kwenye masoko yasiyojulikana kwa sababu ya uwepo wa kodi nyingi ulikuwa unawafanya waogope kwenda kwenye masoko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi hizo ambazo zilikuwa kero kama ambavyo wao walisema Serikali imechukua hatua kubwa kabisa ya kuziondoa; *VAT withholding tax* zimeondolewa ili kuwaruhusu sasa wachimbaji wetu waweze kufanya biashara katika mazingira rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunaongeza sasa Vituo vya Ukaguzi wa Madini. Sasa hivi tunavyo vituo 87 kote nchini, tunataka tuviongeze mpaka vifike 166 na kazi tunaanza kuifanya mapema ili tuweze kusimamia vizuri madini haya ambayo yanasafirisha nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kapufi ameelezea habari ya wachimbaji wadogo wanapongia mikataba na wageni kwenye uchimbaji. Nataka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Kapufi na Waheshimiwa Wabunge na wachimbaji wote nchini, Serikali imewapa fursa Watanzania kutafua mbia au mtu wa kushirikiana naye kwenye kazi ya

uchimbaji kutoka mahali popote. Wajibu ambao anao huyu anayetafuata mbia, kwanza lazima huo mkataba wanaoingia waulete Serikalini ili Serikali iweze kuangalia kama unakinzana na sheria zetu za ndani, lakini kuangalia kama Mtanzania huyu hatanyonywa. Tunayo mifano mahali pengi Watanzania wamengia mikataba na wageni, ukienda kuangalia mwenye leseni ni Mtanzania, lakini kila anachopata Mtanzania ni asilimia tano hadi kumi. Hatuwezi tukakubali Watanzania wakanyonywa na Serikali yao ipo kwa ajili ya kuangalia maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwatoe wasiwasi na niwaombe wale wote wanaopata wawekezaji toka nje, wawalete na mikataba yao ofisi kwetu kwenye Wizara ya Madini, mikataba ile iweze kusajiliwa ili ipate nguvu za kisheria kwa ajili ya kusimamiwa, sisi tutawapa kila aina ya *support* watakayohitaji kutoka kwetu. Naomba vile vile niwatoe wasiwasi Watanzania kwamba kuna utaratibu wa watu wanaofanya kazi ya utafiti kutengeneza taarifa za kupika ili waweze kuziua kwa bei kubwa kwa watu kutoka nje. Jambo hilo kama Wizara linatufedhehesha sana, lakini zaidi sana linatuondolea imani kwa wawekezaji kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeamua Wizara ya Madini, tunataka tuanzishe mchakato wa kuanzisha Bodi itakayowasajili Wajiolojia wote hapa nchini ili kila mmoja anapofanya kazi ya utafiti na kutoa *geological report* aweze kubanwa na sharia, asiweze kupika matokeo kwa ajili ya kutafuta fedha.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa...

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri; Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama na Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki, Naibu Mawaziri pamoja na Watendaji wote wa Ofisi hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupongeza hotuba nzuri iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa ufafanuzi kwenye maeneo machache ambayo Waheshimiwa Wabunge waligusia katika sekta ya maliasili na utalii na kwa kuwa muda hautoshi naomba nijibu bila kuwatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni eneo la migogoro ya ardhi. Msimamo wa Serikali kwa sasa kwa migogoro yote ya mipaka, matumizi maeneo ya hifadhi ambayo yapo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii tupo katika Kamati ambapo Januari 15 mwaka huu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliunda Kamati ya Mawaziri kutokana Wizara nane ambao wamepita maeneo yenye migogoro, wamechambua taarifa mbalimbali na sasa tuko katika hatua za mwisho za kuandaa ushauri ambao tutaufikisha kwa Mheshimiwa Rais. Pindi atakapotoa maagizo yake tutarudi kinyumenyume kurekebisha mipaka *accordingly* ili kutatua migogoro hiyo na huo ndio mtazamo wetu. Kuna maeneo yamezungumziwa ya Kilombero, Serengeti, Grumet, kuna pembeni ya Mto Rubana, yote kwa ujumla wake jibu letu ni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni kukuza utalii wa fukwe. Limezungumziwa jambo hili kwa kiasi kikubwa; Mheshimiwa Mbaraka Dau na wengine, naomba niwahakikishie kwamba Serikali ya Awamu ya Tano kwa sasa imejipanga ipasavyo kukuza utalii wa fukwe na tutaanza kwa kuwekeza katika maeneo ya Ziwa Victoria, eneo la Chato, lakini pia fukwe za Bahari ya Hindi eneo la Saadan likihusianisha visiwa vilivyopo katikati ya Bahari ya Hindi, lakini pia kisiwa cha Mafia. Mafia

kuna vivutio vya pekee kuna *whale sharks* ambacho ni kivutio cha Kimataifa na watalii ambao ni *high end* wanapenda kuogelea pamoja na hao papa nyangumi ambao wanapatikana sehemu mbili tu duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapaangalia Mafia kwa jicho la kipekee na tunakusudia kuweka mkakati mahususi sambamba na kujenga maeneo ya vivutio vya fukwe, vivutio vya mikutano yaani kwa ajili ya kuendeleza *conventions tourism* lakini vivutio vya michezo kwa maana kuendeleza *sports tourism*. Michezo tunayoingalia kwa sana ni michezo kama ya gofu, *tennis*, michezo ya baiskeli ya kimataifa ambayo tunaamini kwa pamoja itakuza sana utalii wa fukwe ukilinganisha na utalii wa mikutano.

Sambamba na hilo tumetengeneza maeneo matatu ya kukuza utalii, hivyo kama nilivyosema eneo la Chato ambapo hifadhi za Taifa ambazo Bunge hili Tukufu katika Mkutano uliopita wa Bunge lilipandisha hadhi hifadhi za Burigi, Biharamulo na Kimisi pamoja na nyingine, eneo lile tunakushudia kuendeleza utalii wa fukwe pamoja na utalii wa mikutano. Eneo lingine ni hili la Saadan, pamoja na ufukwe wote Bagamoyo, Pangani mpaka Tanga na ukiunganisha na hivyo visiwa nilivyovitaja. Eneo lingine ni hili la Kilwa tukiunganisha Kilwa Kisiwani pamoja na ufukwe wote kuanzia Kilwa mpaka Mtwara. Kwa hivyo eneo la utalii wa fukwe kwenye bajeti yetu tutakayoisoma hapa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa mchango wako.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Ulega, dakika tano utafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile na Mheshimiwa Aweso ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO WA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kukushukuru wewe kwa fursa hii, lakini pili nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, mtoa hoja na timu nzima ya Wizara yake ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama na Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Angellah Kairuki na Naibu Mawaziri wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambapo wengi katika waliotoa hoja wamejielekeza katika kuona namna ambavyo sekta ya mifugo na sekta ya uvuvi zinaweza kuwa na mchango chanya katika pato la Taifa lakini vilevile katika kuinua maisha ya Mtanzania mmoja mmoja. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi imejipanga vyema sana katika kuhakikisha kuwa jambo hili la kuinua kipato cha Mtanzania mmoja mmoja linafanikiwa kupitia mifugo na uvuvi lakini vilevile kuwa mchango chanya katika pato kuu la Taifa. Mathalani, hivi sasa pato la Taifa katika upande wa mifugo ni asilimia 7 na upande wa uvuvi ni asilimia 3 na lengo letu ni kuinua na kuhakikisha kwamba asilimia hizi zinaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna gani tutafanya, ni mikakati mizuri tuliyojiwekea. Moja, ni kuhakikisha kwamba tunadhibiti vyema mnyonyoro wa thamani kuanzia katika kumuandaa ng'ombe mpaka kwenda kumchakata ambapo hivi sasa tumehakikisha kuwa kuna viwanda vipya vinavyokwenda kujengwa vya kuchakata nyama ya ng'ombe. Pale Pwani tuna Kiwanda kikubwa cha *Tanchoice* lakini hapo Morogoro tunacho Kiwanda kikubwa cha *Nguru Hills* lakini vilevile tupo katika maridhiano na Serikali ya Misri ambapo tutatengeneza kiwanda kikubwa sana pale Ruvi ambacho kitakuwa na uwezo wa kuhakikisha kuwa nyama nyingi inakuwa *processed* pale lakini vilevile ngozi na mazao mengine ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Dawati la Sekta Binafsi ambalo tumelianzisha sisi Wizarani kwetu, tumehakikisha vile viwanda ambavyo vilikuwa vinasuasua tumeviwezesha. Mathalani, katika upande wa nyama

Kiwanda cha Chobo pale Mwanza, tumesaidiana na wenzetu wa Benki ya Kilimo, katika kuhakikisha kuwa wanauchukua mkopo wao na kuwasaidia zaidi ili kuwajengea uwezo ambapo kiwanda kilikuwa kinaonekana kuwa kinasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ikini vilevile upande wa maziwa, tumefanya kazi kubwa ambapo hivi sasa kupitia agizo la Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli limewezesha Kiwanda cha *Tanga Fresh* kuwa na uwezo wa kutengeneza maziwa ya muda mrefu, tunaita *UHT* au *Long Life Milk*. Ndiyo kiwanda pekee katika Taifa hivi sasa kinachotengeneza maziwa lita zisizopungua 40,000 baada ya kuwezesha kupata mkopo wa shilingi 12 kutoka katika benki za kibiashara. Vilevile Wizara yetu tumewasaidia *Tanga Fresh* ambapo sasa wameweza kuchukuliwa mkopo wao huu na Benki yetu ya Kilimo (*TADB*) ambapo sasa watakuwa na uwezo zaidi hata wa kufikia lita 100,000 kuzi-*process* kwa siku moja. Hayo ni kwa ufupi katika upande wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa uvuvi, jambo kubwa tulilolifanya ni kuhakikisha kuwa tunafufua Shirika letu la *TAFICO*. Hadi sasa *TAFICO* inafanya vizuri, imeanza na tumeshapata pesa takribani shilingi bilioni 4.2 kutoka Serikali ya Japan ambazo zinaenda kusaidia katika kununua meli itakayoanza kufanya kazi ya kuvua samaki wetu lakini vilevile inaenda kufanya ushirikiano wa kuweza kupata meli zitakazokwenda kufanya uvuvi katika eneo la bahari kuu. Mchakato wa kupata eneo la bandari unaendelea ambapo tukishapata eneo hilo tukajenga bandari kazi ya uvuvi wa bahari kuu itakwenda kufanikiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi pia wamezungumzia juu ya sheria na kanuni zetu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ulega.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO WA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, atafuatiwa na Mheshimiwa Aweso na Mheshimiwa Nditiye ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo mawili ambayo yaligusiwa na wachangiaji katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni mabadiliko ya kisheria, kuna sheria mbili ambazo tunatarajia kuzileta Bungeni kwa mara ya kwanza. Tunatambua kumekuwa na changamoto katika ugharamiaji wa matibabu na hivyo kama Serikali tunakusudia kuleta Muswada wa Bima ya Afya kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tunatambua vilevile katika kufikia malengo ya 90-90-90 kwa maana ya asilimia 90 ya watu wote ambao wanaishi na Virusi vya UKIMWI tuweze kuwafikia na kuwapima, asilimia 90 ya wale ambao wamepimwa waweze kupata matibabu na asilimia 90 ya wale ambao watapata matibabu tuweze kufubaza kabisa Virusi vya UKIMWI, tumeona kwamba kumekuwa na changamoto hususani katika kundi la vijana na wanaume, hivyo tunataka kuja na mabadiliko ya sheria ili kuruhusu upimaji binafsi lakini vilevile kushusha umri wa upimaji kufikia miaka 15. Taratibu zote za mabadiliko haya ya sheria yako katika ngazi mbalimbali ndani ya Serikali na pindi taratibu hizi zitakapokamilika Miswada hii italetwa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo liligusiwa na wachangiaji ni kuhusiana na hali ya magonjwa nchini. Kwa muda mrefu tumekuwa tunapambana na magonjwa ya kuambukiza lakini sasa hivi tumeanza kuona ongezeko kubwa sana la magonjwa yasiyoambukizwa kwa maana ya kisukari, *pressure*, kiharusi na magonjwa ya figo. Sisi kama Serikali tumeona tunahitaji tuanze kujipanga upya, hivyo tunataka tuangalie mtiririko mzima wa huduma za afya kama

alivyokuwa ameongelea Mheshimiwa Mukasa kuangalia masuala ya elimu, kinga, tiba na huduma ya utengamao. Awali tulikuwa tumejikita sana katika masuala ya tiba tukaacha haya maeneo mengine. Ili sasa tuweze kupambana vizuri na magonjwa yasiyoambukiza tunahitaji tuhakikishe kwamba huu mtiririko mzima tunauzingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Afya tuko katika hatua za mwisho kuanzisha Mpango wa Taifa wa Magonjwa Yasiyoambukiza kama ilivyo kwa magonjwa ya UKIMWI, TB na Malaria. Tunataka tuje na Mpango wa Magonjwa Yasiyoambukiza ili tuweze kuwa na utaratibu mzuri wa kudhibiti magonjwa haya. Tutaweka utaratibu ambao utaanzia katika ngazi ya Taifa mpaka ngazi za kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ndugulile. Tunaendelea na Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri anayoifanya. Pia nitumie nafasi hii kuwapongeza wasaidizi wake, Mheshimiwa Jenista pamoja na Mheshimiwa Angellah Kairuki pamoja na Naibu Mawaziri wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa sisi katika Wizara yetu, tuna mambo mawili, moja ubadhirifu wa fedha za miradi ya maji vijijini. Tukiri kabisa kulikuwa kuna changamoto kubwa sana hasa katika maeneo ya vijijini kuona fedha zinalipwa lakini mradi haujakamilika na hata ukikamilika unatoa maji leo, kesho hautoi. Sisi hiyo kama changamoto tumeiona na baada ya kubadili muundo kwa maana Wahandisi wa Maji wengi walikuwa hawawajibiki kwetu na kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini, tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kupitisha Muswada ule na Mheshimiwa Rais amekwisha usaini,

tunaamini uanzishwaji wa Wakala wa Maji Vijijini tunaenda kuwa na muarobaini ambao utaenda kutatua tatizo la maji kabisa vijijini. Tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali kwa Wahandisi wa Maji pamoja na wakandarasi wababaishaji ambao wanatuchelewesha katika utekelezaji wa miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili ni kuhusu suala zima la ulipaji wa madeni ya wakandarasi. Utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha. Tulikuwa na madeni takribani zaidi ya shilingi bilioni 88 tunayodaiwa na wakandarasi, lakini nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Wizara ya Fedha kuliona hilo, wametupa takribani zaidi ya shilingi bilioni 44 ndani ya mwezi uliopita na wametupa *commitment* ndani ya mwezi huu watatupa tena shilingi bilioni 44. Kwa hiyo, tupo vizuri na tumejipanga katika kuhakikisha kwamba tunakamilisha miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Hussein, amezungumzia hoja ya mradi wake wa Nyang'wale, tumelipa zaidi ya Sh.1,705,000,000. Mwambie mkandarasi afanye kazi, hana uwezo, tutamuondoa katika kuhakikisha miradi ya maji inakamilika ili wananchi waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto, yapo mafanikio makubwa sana. Sisi kama Wizara ya Maji ambayo siyo Wizara ya Ukame, ukienda Arusha zaidi ya mradi wa shilingi bilioni 520; mradi wa Same Mwanga zaidi ya Dola milioni 300; ukienda Longido zaidi ya bilioni 16 wananchi wanapata maji; tunatoa maji Zwiwa Victoria na kuleta Tabora, Nzega na Igunga na hata Simiyu kwa Mheshimiwa Mbunge wa Bariadi kwako Mwenyekiti tunakupelekea maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumejipanga vizuri katika kuhakikisha kwamba hatutokuwa kikwazo sisi kama Wizara ya Maji kwa wananchi na Waheshimiwa Wabunge ili wananchi wetu waweze kupata maji safi salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Aweso. Tunaendelea na Mheshimiwa Eng. Nditiye, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Waitara ajiandae.

NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri pamoja na wasaidizi wake wote. Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mbalimbali iliyoelekezwa sana kwenye Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *SGR* liliongelewa sana, napenda tu kutoa taarifa kwamba mpaka sasa hivi kipande cha Dar es Salaam mpaka Morogoro tumekwishafikia asilimia 48. Kazi kubwa ya kujenga tuta kuanzia Dar es Salaam mpaka Morogoro imekamilika kwa asilimia 98. Imebakia kulaza reli na kuweka miundombinu ya umeme kusubiri uanzaji wa safari ambapo mwezi Novemba tuna hakika safari za kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro kwa njia ya *SGR* zitakuwa zimeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba *transfer of knowledge* tunaifanya kwa umakini wa hali ya juu sana. Kuna vijana wetu wengi sana ambao tumewa-*attach* kwenye mradi mzima lakini kuna wengine ambao tunawapeleka nje ya nchi kuwasomesha kwa awamu. Kwa hiyo, watakapoondoka hawa wakandarasi tutakuwa na timu nzuri kabisa ya kuweza kuendeleza mradi wetu kwa mapana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi waliongelea sana kuhusu meli kwenye Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Nitoe tu taarifa kwamba tayari tumekwishasaini mkataba wa kutengeneza meli moja Ziwa Victoria lakini tunakarabati meli ya MV Victoria na MV

Butiama kwenye Ziwa Victoria. Vilevile tumeshaingia mkataba wa kutengeneza meli moja mpya kwenye Ziwa Tanganyika pamoja na kukarabati MV Liemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi za dharti kwa Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi walizotupatia kwa uanzaji na kuimarisha Shirika letu la Ndege la ATCL. Michango yao mingi tumeipokea na tumeendelea kurekebisha hata ratiba ambapo sasa tunaweza ku-*move* sehemu mbalimbali kurahisisha usafiri wa Watanzania.

Sasa hivi kwa Dodoma siku nne tunasafiri asubuhi na jioni na tunaendelea kuimarisha na tutakwenda na ratiba nyingine mpya huku tukiendelea kukaribisha hata wawekezaji wengine kwa ajili ya kurahisisha usafiri wa anga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imeendelea kuimarisha viwanja vyetu vya ndege sehemu mbalimbali. Mpaka sasa kuna viwanja 11 ambavyo wakandarasi wako katika hatua mbalimbali ya kuvipanua kwa ajili ya kuweza kuhudumia ndege zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kuelezea masuala ya mawasiliano, Serikali yetu kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imeendelea kupeleka mawasiliano maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Mpaka sasa hivi nchi yetu tunawasiliana kwa asilimia 94 na hizo asilimia 6 zilizobakia tunaendelea kuzifanyia kazi kwa sababu nyingine ziko kwenye maeneo ambayo jiografia yake ni ngumu kidogo kupeleka mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, barabara za Mikoa zinaendelea kuunganishwa. Tunaamini hivi karibuni nchi yetu mikoa yote itakuwa imeshaunganishwa kwa lami, hasa kwa ile mikoa michache iliyobakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunasendelea na Mheshimiwa Subira dakika kumi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza nianze kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuisimamia Serikali ndani ya Bunge lakini pia na nje ya Bunge kwa kazi mbalimbali anazofanya mikoa mbalimbali. Niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri katika Wizara hii, Mheshimiwa Jenista na Mheshimiwa Angellah Kairuki pamoja na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanazofanya lakini pia kwa hotuba ambayo imewasilishwa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta yetu ya nishati ni nyeti na ndiyo maana kwenye mjadala wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wengi wamepata fursa ya kutoa uchauri, kuelezea wasiwasi wao na wengine pia wamepongeza. Kwa hiyo, kama Wizara tunashukuru kwa pongezi zote na tumepokea changamoto mbalimbali ambazo zimewasilishwa na tunaahidi tutaendelea kuzitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta yetu ya nishati ina mambo mengi; inasimamia suala zima la uzalishaji umeme, usafirishaji na usambazaji. Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia wamejielekeza pia kwenye jambo kubwa la muhimu la usambazaji wa umeme, hususani wamejielekeza kwenye mradi wa *REA* unaoendelea na wameonyesha changamoto ambazo zipo na wasiwasi pengine huu mradi unaweza usikamilike ndani ya wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwataarifu Waheshimiwa Wabunge, kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Tano, kupitia Wizara ya Nishati na Wakala wa Nishati Vijijini, inatekeleza miradi mbalimbali ya umeme vijijini. Pamoja na changamoto ambazo zimejitokeza, nataka niwape matumaini kwa kweli huu mradi unaendelea. Tangu tarehe

1 Julai, 2016 mpaka tarehe 30 Machi, 2019 takribani Vijiji 1,969 vimeshapelekewa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichanganya na vijiji ambavyo vilikuwa vimepelekewa miundombinu ya umeme mpaka tarehe 30 Juni, 2016 kama 4,396, tunapozungumza sasa tuna vijiji takribani 6,365 vyenye umeme kati ya vijiji 12,268 na hii ni asilimia 52 ya vijiji vyote kwa mujibu wa takwimu ambayo tumepata kupitia TAMISEMI. Nini maana yake? Maana yake ni kwamba pamoja na changamoto zinazoendelea lakini kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge tunavyoupima Mradi wa REA Awamu ya Tatu, ni kweli mikataba ilianza 2017, sote tulishiriki hapa lakini tarehe kabisa ya kuanza kazi tunaipima pale wakandarasi walipofunguliwa *Letter of Credit* ambayo ni Julai, 2018. Kwetu sisi mradi una miezi 24 na utakamilika tarehe 30 Juni, 2020. Itakapofika tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya vijiji 9,055 vitakuwa vyote vimepatiwa umeme na vitakavyosalia ni vijiji 3,213 ambavyo mpango wake na taratibu zake zimeanza katika Mradi wa REA Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikijibu maswali mengi na nashukuru pamoja na Waziri wangu mmekuwa mkitupa changamoto mbalimbali lakini kwetu sisi Wizara namna ambavyo tumeweka usimamizi ngazi ya Wizara, Kanda TANESCO na ndani ya REA na hivi karibuni tunaishukuru Seikali ilitupatia fedha tukaipa magari miko ya yote zaidi ya 26 kwa ajili ya usimamizi wa mradi huu na usimamizi ngazi ya wilaya na ma-*technician*.

Naomba niwatoe hofu hivi karibu tumetoa maelekezo kila wiki kuwasha vijiji vitatu na kila wakati tunapata taarifa. Tumetoa maelekezo ya kuwa kila wilaya kuwa na magenge zaidi ya matano. Kwa hiyo, naomba mtuamini kwamba sisi tunachopambana ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwamba vijiji vyote nchi nzima ifikapo 2021

vipatiwe umeme. Kwa hiyo, mtuamini kwamba uwezo tunao, nia tunayo na nguvu tunayo ya kulisimamia hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoendelea pia tutaliomba Bunge lako Tukufu litaidhinisha mradi, tunaanza *densification* Awamu ya Pili. Pamoja na kwamba hivi nilivyovitaja ni vijiji lakini ni wazi kwamba miradi kama hii mikubwa kwa Serikali inayofanya miradi mikubwa mingi; ujenzi wa Bwawa la *Stiegler's* na ujenzi wa miundombinu mbalimbali lazima kuwe na wigo. Kwa hiyo, baada ya kuona hivyo Serikali imetafakari tunakuja na mradi mwingine wa Ujazilizi Awamu wa Pili ambao utagusa vitongoji. Kwa hiyo, ikifika kwenye kijiji kama umefika kwenye vitongoji vitatu au vinne vimesalia vitongoji ujazilizi unakuja na zaidi ya shilingi bilioni 290 zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo pamoja na miradi ya *peri-urban* kwa Majiji makubwa zaidi ya shilingi bilioni 86 za kuanzia zimetengwa na Serikali yetu ya Awamu ya tano kupitia Wizara ya Nishati na taasisi zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imefanya uamuzi wa kisera, kupitia agizo la Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, baada ya kutafakari upelekaji wa miradi ya nishati vijijini na hoja ya kwamba ikipeleka *TANESCO* au na wadau wengine kuwe na bei tofauti au ikipelekwa na *REA* inakuwa na bei tofauti. Serikali imefanya maamuzi kuanzia sasa hivi miradi yote hiyo itapelekwa umeme wananchi wataunganishwa kwa bei ya Sh.27,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niseme wazi kabisa, Serikali itandelea kupambana na wale Vishoka ambao wanawaongezea wananchi bei lakini bei ya kuunganishia umeme ni Sh.27,000. Hii italeta matumaini hata kwa wananchi tunaowaambia wasubiri kwamba *TANESCO* watapeleka umeme vijijini kwa kupitia Sh.27,000, *REA* Sh.27,000 na sekta binafsi nayo Sh.27,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limezungumzwa ni suala la uzalishaji wa umeme. Serikali yetu imefanya mapinduzi kupitia Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli, imekuwa na maono ya kuzalisha umeme

mwingi ambao utashusha gharama ya umeme. Umeme mwingi utakaozalishwa ni kupitia vyanzo vya maji. Tunao mradi wa *Stiegler's Gorge* MW 2,115 tumeshamkabidhi mkandarasi *site* anaendelea vizuri; Mradi wa Rusumo MW 80 anaendelea vizuri; tumeanza mchakato wa Mradi wa Rumakali MW 358; na Mradi wa Ruhuji MW 222 unaendelea. Kwa hiyo, nataka niseme dhima au mpango huu wa Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha ifikapo 2025 tunazalisha MW10,000 kwa ajili ya kuhimili uchumi wa viwanda unaojengwa kwa kasi kubwa katika awamu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme dhima hii au mpango huu wa Serikali Awamu ya Tano ni kuhakikisha ifikapo 2025 tunazalisha Megawati 10,000 kwa ajili ya kuhimili uchumi wa viwanda unaojengwa kwa kasi kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine limezungumzwa hapa kwamba Serikali imeacha kutumia gesi, siyo kweli. Serikali inaendelea kutumia gesi kwenye masuala mbalimbali. Gesi katika kuzalisha umeme; na kwa sasa tuna mradi *Kinyerezi I Extension* Megawati 185; tumemaliza *Kinyerezi II* megawati 240; kuna mpango wa ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme Megawati 300 Mtwara pamoja na njia za kuzalisha umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukisema eti Serikali imehama kwenye uchumi wa gesi siyo sahihi na hata sasa tunasambaza gesi kwenye viwanda mbalimbali vikiwemo viwanda vya Jimbo la Mheshimiwa kaka yangu Ulega hapa Mkuranga. Tunaongeza viwanda vitano kuvisambazia gesi ili kupunguza gharama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mmesikia kiongozi wa Ujerumani ameipongeza Serikali na ameahidi kuleta kiwanda kikubwa cha mbolea na tumeshafikia makubaliano ya bei ya gesi kwenye viwanda vyote vya mbolea. Kwa hiyo, utaona gesi bado ina mchango mkubwa katika uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwamba hivi karibuni pia Mheshimiwa Rais ametuzindulia mradi wetu wa kusafirisha umeme wa Kilovoti 220, Makambako, Songea. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake kwa kazi nzuri anayoifanya na kwenye sekta yetu hatuna shida, hatuna tatizo la pesa. Tumekuwa tukiidhinihiwa na Wizara ya Fedha, nawashukuru sana. Hata ninaposema sasa, zaidi ya asilimia 16 tumeshapata pesa zake. Tunawaahidi tu utumishi uliotukuka na usimamizi wa miradi hii. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi/Vigelegele)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Waitara, dakika kumi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayofanya pamoja na Waziri Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Jenista Mhagama; Manaibu, ndugu yangu Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Stella Ikupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Rais, Mawaziri wote na Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kusaidia kusimamia utekelezaji mzuri na murua wa Ilani ya Uchaguzi wa mwaka 2015 - 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajibu yale maswali ya jumla sana kwa sababu ya muda, yako mengi lakini nitajitahidi. La kwanza, imezungumzwa hoja hapa ya *TARURA*. Tumefurahi sana kama Wizara kwamba kila Mbunge aliyesimama kuchangia humu alipongeza kazi kubwa na nzuri ambayo inafanywa na Wakala wa Barabara wa Mjini na Vijijini ya *TARURA*. Ila changamoto iliyokuwepo ni upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe tu taarifa kwamba tayari imeshaundwa timu ya Kitaifa ya kutambua barabara, itafanya kazi yake baada ya kuleta mrejesho wa kitaalamu. Sasa tutapitia upya kuangalia mgao ule wa asilimia 70 ya *TANROADS* na asilimia 30 ya *TARURA* ili hawa watu waweze kuongezewa fedha na waendeleo kuimarisha barabara zetu za mjini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo limezungumzwa ilikuwa ni hoja juu ya maboma ya afya. Kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 tulikamilisha maboma 207 na vituo 552 vimeendelea kuimarishwa. Kwenye bajeti hii ambayo imeletwa, nadhani kuanzia kesho, tumetenga fedha zaidi ya shilingi bilioni 10 kujenga Vituo vya Afya vingine vipya 52, lakini mbali na hizo hospitali 67 za mwanzo za mwaka huu ambazo tunamalizia, hapa pia tumetenga bajeti ya hospitali nyingine mpya 27. Kwa hiyo, kazi ile inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu leo swali la msingi hapa ni kwamba kuna maboma mengine ambayo wananchi wameendelea kujenga bado Serikali hii ya Awamu ya Tano ina nia njema kabisa kuendelea kusaidia kuyakamilisha ili huduma ya afya iendeleo kuimarika katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amejibu Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwamba kuna maboma ambayo yamekamilishwa lakini ile ni bajeti ya 2016/2017. 2018/2019 tunapeleka vifaa vya maabara kwenye Shule za Sekondari 1,250; lakini kama ambavyo inajulikana pia mwezi wa Kwanza Wizara ya TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia mradi wa *EPFR* tumeshapeleka fedha, shilingi bilioni 56 kwenye Elimu ya Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa Pili pia tumepeleka fedha shilingi bilioni 29.9 ili kukamilisha maboma. Hapa ninapozungumza tupo kwenye mchakato pia kupeleka fedha nyingine kumaliza maboma ya Shule za Msingi, Walimu

na watumishi wengine wa Serikali. Kazi kubwa inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya asilimia 10. Naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Kamati ya Utawala na TAMISEMI ya Bunge hili Tukufu. Katika bajeti hii ambayo imewasilishwa ya mafungu ya Wizara ya TAMISEMI kila Mkoa Wakurugenzi wote walilazimika kutoa maelezo ya ziada, kila mtu aeleze mpango aliyonao wa kukusanya asilimia 10 kwa vijana, akina mama na watu wenye elemavu, pia kuonyesha ameshafikisha asilimia ngapi na adhabu mbalimbali zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nilitaarifu Bunge kwamba katika kipindi hiki baada ya Bunge hili Tukufu kufanya mabadiliko makubwa ya sheria kifungu Na. 35, kwa kweli usimamizi umeimarika zaidi. Mwaka 2016/2017 fedha za mikopo zilizoenda kwenye makundi haya matatu maalum, tulipeleka shilingi 8,917,700,164/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017/2018 ile asilimia 10 ilipelekwa kwenye vikundi, shilingi 27,402,737.81. Kwenye vikundi 10,000 imeenda 72, lakini niseme tu, bahati nzuri sana naomba niwapongeze akina mama wa Taifa hili wamekuwa waaminifu sana na wamekopa sana kuliko vijana na watu wengine wote. Namba yao ilikuwa kubwa. Pia hata kwenye marejesho akina mama wamekuwa waaminifu, wamerejesha sehemu kubwa. Tunaomba waendeleo kuhimizwa, waelimishwe kwa weledi, wakope ili waweze kujikwamua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka mwezi Februari mwaka huu, 2019 tumeshakusanya fedha, zinapelekwa kwenye vikundi, shilingi 21,423,619,000/= zimeshaenda kwenye makundi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwamba sasa, baada ya maelekezo ya Kamati ya Utawala na Bunge hili Tukufu, kanuni za kazi hii zimeshaandaliwa, zipo kwenye hatua ya mwisho, lakini maelekezo yametoka kwamba sasa

kutakuwa na akaunti maalum ambayo fedha hizi zikikusanywa ni lazima ziingizwe pale. Kwa hiyo, kuna ujanja unafanyika wakipeleka fedha kwenye vikundi, fedha za marejesho wanajumlisha wanakwambia ni asilimia zaidi ya 100. Tukasema hapana, ili tutenganishe, kutakuwa na akaunti mahususi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazokusanywa ziingizwe kwenye akaunti hiyo, zikipelekwa kwenye vikundi zipelekwe hivyo na zikirejeshwa zionekane ili tuweze ku-*control*. Kwa hiyo, kazi inamalizika na watapewa maelekezo mahususi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja hapa ya posho ya Wenyeviti wa Mitaa na Madiwani. Naomba nijibu hoja hizo mbili kwa mkupuo. Juzi niliulizwa swali hapa, nirudie kwamba Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji na Wajumbe wao, kabla ya kufanya uamuzi wa kugombea ni lazima wakidhi sifa na vigezo vilivyo kwenye kanuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaelekezwa kwamba mgombea au Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji, Wajumbe wa Serikali za Mitaa na Wahumbe wa Halmashauri za Vijiji ni lazima wawe na kipato ambacho kinawawezesha kuishi. Kwa hiyo, ni lazima mtu apime uwezo wa kuhudumia. Kazi hii kimsingi ni kazi ya kujitolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunatarajia pamoja na hoja mbalimbali zilizopo kwamba waongezwe posho, cha kwanza ajue kwamba ni kazi ya kujitolea na apimwe kwa uwezo wake wa kusimamia ili pia kuepuka hata ubadhirifu mbalimbali ambao unaendelea kwenye maeneo yetu ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya posho ya Madiwani ni kweli. Posho ya Diwani kwa mwezi ni shilingi 350,000/= . Kwa Wenyeviti na Mameya ni mpaka Shilingi 400,000/= ukomo. Kila Halmashauri imejipangia utaratibu wa posho mbalimbali kwenye vikao vyao. Tumetoa maelekezo kwamba

imeonekana kwamba kuna Halmashauri nyingine wanalipa fedha kubwa sana, nyingine ndogo, kama ilivyo kwa Wabunge. Hata kama utaenda mahali gani, lakini ile *per-diem* unayolipwa na *sitting* inatambulika. Kwa hiyo, ikawekwa *flat rate*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maelekezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba kuwe na *flat rate* kwenye Halmashauri zetu. Kuna malalamiko, kuna barua tumepata, lakini ni kwamba ile posho ya kawaida Diwani atapewa; hizi posho za vikao na kulala, iwe *standard*. Kwa sababu kikao wanachokaa Dar es Salaam na sehemu nyingine ni ile ile, ukumbi ni ule ule. Kwa hiyo, kumekuwa na *double standard* ile. Kwa hiyo ndiyo maelekezo. Haki zao nyingine zile zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho za Wenyeviti wa Mitaa zinatofautiana. Kwa mfano, mimi ni Mbunge wa Ukonga, Ilala. Kule tulikuwa tunalipwa posho shilingi 40,000/=, lakini kwa sababu ya mapato ya Halmashauri ya Ilala tumepandisha mpaka shilingi 100,000/= . Kwa hiyo, kuwalipa Wenyeviti wa Mitaa inategemea na Halmashauri inapata kiasi gani? Hao hao inabidi wasaidie pia katika kukusanya kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengine wakitumwa kusimamia kodi hawasimamii, lakini ukweli ni kwamba Watanzania wote wanapaswa kulipa kodi ili miradi ya maendeleo iweze kukamilishwa. Hawa nao wasaidie kukusanya kodi, kuibua vyanzo, wakaangalie watu walinde miundombinu, fedha zitapatikana, watalipwa zaidi ya hiyo ambayo ipo katika eneo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imezungumzwa hapa, kulikuwa na hoja ya nyumba za wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Kwenye bajeti ya mwaka 2019/2020 tumetenga zaidi ya shilingi 4,626,000,000/= kwa ajili ya kujenga nyumba mpya na kukarabati. Kulikuwa na hoja hapa nadhani eneo la Liwale, wametengewa fedha zaidi ya shilingi milioni 330 kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna hoja ya magari ya Ma-DC, Wakurugenzi na Wakuu wa Miko. Naomba nitoe taarifa kwamba jambo hili tunalitambua na Serikali inaendelea kuhimiza, tutakuwa tunanunua magari kulingana na uwezo Serikali kadri muda unavyoenda. Vile vile viongozi hawa wamepewa dhamana kubwa katika maeneo yote ya Serikali za Mitaa, hawatakwama kufanya kazi zao. Tutafanya kila linalowezekana ili waweze kufanya kazi na waweze kufika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa ushauri, kuna Wilaya nyingine ni kubwa sana kulingana na jiografia yake na mazingira ya miundombinu ile. Kwa hiyo, tunatakiwa tuangalie vipaumbele kulingana na uwezo kadri ambavyo itakuwa inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo iliitokeza hapa walizungumzia ahadi za viongozi mbalimbali. Naomba tuwahakikishie kwa kasi hii ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali ya Awamu ya Tano na ushirikiano mzuri wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ahadi zote za viongozi na Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wote zitatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nilikuwa nataka nizungumzie hoja ambayo imejitokeza hapa. Kumekuwa na hoja kwamba nikiwa nazungumza wananiambia ongea kama Naibu Waziri, lakini nimeambiwa hapa kwamba inawezekana nafasi hizi tumehongwa. Nadhani nijibu hii hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nina uzoefu wa pande zote mbili; upande wa Upinzani na upande wa Chama cha Mapinduzi. Naomba niwapongeze Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa mnayofanya. Naomba niwaambie, kwa uzoefu ambao nimekaa miaka kumi upande huo, upinzani wa nchi hii bado sana. Bado sana kwa kweli wanapaswa kujipanga. Kwa kasi hii iliyoko sasa ya kuweka miradi kila mahali, hii kasi nadhani wanatakiwa kujipanga zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba ni kweli, kunaweza kuwa na hoja pinzani lakini wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani. Nani hamjui Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli? Nani anaweza kupambana naye? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira haya, sisi tuchape kazi.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Wabunge wa Viti Maalum wa Chama cha Mapinduzi. Nilikuwa nafuatilia *trend* ya Wabunge wa Upinzani hasa wa CHADEMA wale na Wabunge wa CCM, *big up* sana Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mbunge wa CCM akienda kwenye mkoa, mara amechangia *cement*, amepeleka mabati, amewezesha vikundi, ametoa elimu ya uraia, akisimama hapa anachangia vizuri. Kwa hiyo, hii ndiyo tofauti kubwa kati ya nyie akina mama wa hapa na Wabunge wa Viti Maalum kule. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, unajua wale watu wana msongo wa mawazo, siyo mikopo tu, hatima yao ya mwaka kesho. Hali ni mbaya! Kwa sababu kuna Wabunge hapa walishaanza kuaga kwenye Majimbo yao. Mbunge wa Tanga alizungumza juzi kwamba ni Mbunge wa kwanza wa Upinzani, akashindwa kumalizia kwamba Mbunge wa kwanza wa Upinzani na wa mwisho anaaga pale Tanga. Kwa sababu tunafanya *replacement*, wala siyo kunyang'anywa. Hawatanyang'anywa Ubunge, lakini watu wanaangalia, Watanzania wanaona kwa kazi ya Mheshimiwa Rais, miradi mikubwa inayofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nani anaweza akasimama akaponda ndege kweli? Nani anaweza akaponda? Unaponda ndege halafu unaenda unapiga *selfie* unaturushia tuangalie. Unaponda reli, Mbunge unatoka Morogoro pale, ikianza ile maana yake hata mabasi yale na nini havitakuwepo. Speed ndogo, unalala Morogoro, unafanya kazi Dar es Salaam. Ikianza Dodoma, unalala Dodoma unafanya kazi mahali popote pale. Haya ni mambo ambayo yanapaswa kuungwa mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwangu tu ni kumwambia Mheshimiwa Rais aendelee na kazi hii, Waheshimiwa Mawaziri na Waziri Mkuu, Makamu wa Rais, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, nyie ndio wenye dhamana ya nchi hii, Watanzania wamewaamini, wamewapa kura za kutosha. Kelele za chura hazimzui ng'ombe kunywa maji na kelele za mlango hazimzui mwenye mji kulala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri muwe na amani sana. Sisi tunazunguka, tumeenda. Leo wanasema ooh, sisi tunapishana kila mahali.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Tunafanya ziara kila mahali, lakini haya ni maelekezo, kama Rais halali, Waziri atalalaje? Mbunge wa CCM analalaje na watanzania wanataka maendeleo?

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Fedha zinakuja na zinasimamiwa. Watanzania nawaomba sana chonde chonde lipeni kodi. Fuata utaratibu, tii sheria bila shuruti, maandamano hayatakiwi. *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, maandamano kama unataka, chumbani kwako, hutaki utachakazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waitara. Niliona nikupe dakika nne zaidi ili uweze kuyasema yale ambayo unadhani yanapaswa kusemwa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Tunaendelea. Bado niko upande wa Serikali, ni wachangiaji hawa. Naanza na Mheshimiwa Stella Ikupa, dakika 20 na Mheshimiwa Mavunde dakika 20.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Awali ya yote, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha tena siku ya leo kuwa mbele ya Bunge lako Tukufu ikiwa ni mwaka 2018 nilipochangia bajeti ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitumie nafasi hii kuendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa miongozo na maelekezo ambayo ameendelea kunipatia katika nafasi hii ambayo ninahudumia kama Naibu Waziri ambaye nashughulikia masuala ya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa miongozo ambayo imeniwezesha na imeendelea kuwezesha kundi hili la watu

wenye ulemavu mahitaji yao kuweza kutekeleza vizuri. Pia naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge, Kazi Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, dada yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista ni mama, ni mlezi. Kwa kweli ninakushukuru sana Mheshimiwa Jenista kwa upendo wako, lakini pia kwa miongozo na maelekezo ambayo umeendelea kunipatia. Kwa kweli nashindwa nitumie lugha gani rahisi kuweza kumwelezea Mheshimiwa Jenista. Amekuwa ni rafiki wa karibu, amekuwa ni dada na mama, yaani amevaa nafasi zote kwa nafasi hii ninayoitumikia katika Ofisi hii ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Angellah Kairuki dada yangu, kwa muda mfupi ambao nimekuwa naye katika Ofisi ya Waziri Mkuu ameendelea kunielekeza na kunipatia maelekezo ambayo yanaendelea kunisaidia katika utendaji wangu. Pia naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu Mheshimiwa Antony Peter Mavunde kwa ushirikiano ambao ameendelea kunipatia. Ni ushirikiano mkubwa, sisi ni marafiki. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Antony Mavunde kwa ajinsi ambavyo ameendelea kunipatia ushirikiano mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Makatibu Wakuu wote watatu kwa majina yenu, kwa sababu ya muda naomba nisyataje kwa jinsi ambavyo mmendelea kunifanya niweze kutekeleza majukumu yangu katika Ofisi hii ya Waziri Mkuu. Vile vile nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu wakiwemo watumishi wa Kitengo cha Watu Wenye Ulemavu. Naomba niseme kwamba nawashukuru sana kwa jinsi ambavyo mnaniwezesha kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja kwa sababu ya muda, naomba niende kwenye ufafanuzi wa hoja ambazo

zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Kamati yetu ya kudumu ya masuala ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja kwamba Serikali iweze kuimarisha kitengo kinachohudumia masuala ya watu Wenye Ulemavu. Ushauri huu wa Kamati ni ushauri mzuri na ndani ya Serikali tayari tumeshaanza kuona ni jinsi gani tunaweza tukaongeza watumishi katika kitengo kinachohudumia na kuratibu masuala ya watu wenye ulemavu. Kuongezeka kwa watumishi hawa kutawezesha usimamizi na uratibu kuweza kufanyika kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika mwaka huu wa fedha kifungu cha Kitengo cha Watu Wenye Ulemavu kimeweza kuanzishwa ambacho ni Kifungu Na. 2034 na kupitia kifungu hiki, pia tunaona masuala mengi ya watu wenye ulemavu yataweza kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika kuendelea kuimarisha Kitengo hiki cha Watu Wenye Ulemavu, Serikali tunaona kwamba iko haja ya kuwajengea uwezo watumishi wa kitengo hiki kwa sababu masuala ya watu wenye ulemavu yako mengi, lakini pia yanaibuka kila kukicha. Kwa hiyo, uko umuhimu wa kuwajengea uwezo watumishi hawa na tumekuwa pia tukifanya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna suala la Baraza la Ushauri kwa Watu Wenye Ulemavu. Baraza hili, nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba litatangazwa hivi karibuni, muda siyo mrefu. Litakapokuwa limetangazwa baraza hili, basi tunaamini kwamba litatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria inavyoitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa kuna hoja ya Mfuko wa Taifa kwa Watu Wenye Ulemavu. Sheria yetu inatuongoza kwamba tunatakiwa kuwa na Mfuko huu wa Taifa kwa Watu Wenye Ulemavu. Maandalizi ya Mwongozo yanaendelea kukamilika na tayari kwa mwaka wa fedha ujao 2019/2020 tumetenga fedha zipatazo shilingi milioni 103 ambazo ni mbegu kwa mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nitoe rai kwa wadau mbalimbali kuweza kuchangia mfuko huu kwa sababu una matumizi mengi kwa kundi hili la watu wenye ulemavu. Ruzuku za Vyama vya Watu Wenye Ulemavu zinategemea mfuko huu na pia elimu na mafunzo vinategemea mfuko huu. Pia, tafiti mbalimbali ambazo zinahusiana na masuala ya watu wenye ulemavu yanategemea mfuko huu. Pia kuna masuala ya Utengemano kwa Watu Wenye Ulemavu yanategemea mfuko huu. Kwa hiyo, ni rai yangu kwamba Serikali tumeshaanza kwa kutenga hiyo fedha, basi na wadau mbalimbali waendeleo kujitokeza kuchangia mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia kuna hoja ya kwamba, Serikali ihakikishe kwamba inatua migogoro mbalimbali ambayo inajitokeza kwenye Vyama vya Watu Wenye Ulemavu. Serikali imekuwa ikifanya hivyo kwa kushirikiana na Msajili wa Vyama vya Kiraia lakini pia kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu. Ni kweli kuna migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mara kadhaa imeweza kuwaita wahusika wa vyama hivi na kuweza kutatua migogoro ambayo imekuwa ikiendelea. Sambamba na hilo, tumekuwa tukihakikisha kwamba chaguzi zinakuwa zinafanyika na mikutano inakuwa inafanyika kwa mujibu wa katiba na sheria ambavyo inataka ifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Watu Wenye Ulemavu sasa hivi kinaendelea kushughulikia kuhakikisha kwamba Mkutano Mkuu unaitishwa na Chama cha Watu wenye Ulemavu wa Viungo Tanzania (CHAWATA) na kuweza kufanya mkutano ambao imekuwa ni changamoto kubwa kwa chama hiki kwa muda mrefu. Kwa hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu inalishughulikia hili kwa kushirikiana na Chama cha Watu Wenye Ulemavu wa Viungo Tanzania kuona kwamba, mkutano unaitishwa na hatimaye uchaguzi ule unaweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya miundombinu ambayo inakuwa ni rafiki kwa watu wenye ulemavu. Serikali ihakikishe kwamba miundombinu inakuwa

ni rafiki kwa watu wenye ulemavu. Serikali yetu inazo sheria ambazo zinaelekeza kabisa kwamba, miundombinu inatakiwa iweje ili iweze kuwa jumuishi kwa watu wote. Niendeleo kutoa rai kwa mamlaka ambazo zinahusika na upitishaji wa michoro mbalimbali katika miji yetu, kuhakikisha kwamba inazingatia hii sheria, kwamba isipitishwe michoro ambayo inakuwa haijaonesha ni jinsi gani miundombinu itakuwa ni rafiki kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Serikali imeendelea kutoa elimu kwa mamlaka mbalimbali lakini pia hata kwa jamii zetu kuelekeza kwamba ni jinsi gani basi miundombinu inafaa kuwa rafiki kwa watu wenye ulemavu. Waheshimiwa Wabunge, hata nyumba ambazo tunakuwa tunajenga tuweze kuona kwamba ni jinsi gani zinakuwa ni rafiki kwa makundi yote. Mimi huwa nakuwaga na msemu kwamba; sipendi sana kusema kuwa kila mtu ni mlemavu mtarajiwa, lakini napenda kusema kila mtu ni mzee mtarajiwa. Kwani hata uzee hatuutaki, si kila mtu anapenda awe mzee, kwa hiyo kama unapenda kuwa mzee, kuna miundombinu ambayo itafika mahali haitakufaa utakapokuwa mzee. Kwa hiyo suala la miundombinu ni suala ambalo ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kwamba, miundombinu inakuwa ni rafiki kwa makundi yote. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa kuna hoja ya kwamba, Serikali iwasaidie watu wenye ulemavu wanapokuwa wanapatikanika ama wanapokuwa na kesi zao. Serikali imekuwa ikihakikisha kwamba, haki za watu wenye ulemavu zinafuatwa kwa kutumia Ofisi zetu za Ustawi wa Jamii, lakini pia niendeleo kutoa rai kwa asasi mbalimbali ambazo zinashughulika na masuala mbalimbali ya kisheria, kuona kwamba ziweze kuzingatia masuala mbalimbali yanayohusiana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wanasheria ambao wamekuwa wakijitolea katika eneo hili pia, niendeleo kuwapongeza na kuwashukuru na wamekuwa wakijitangaza kwamba wanaweza wakasaidi kundi hili la watu wenye ulemavu wanapokuwa wanapatikanika na kesi. Pia sisi kama

Serikali tumekuwa tukifanya hivyo mara kadhaa hata mimi mwenyewe nimeweza kuwaunganisha watu wenye ulemavu na Wizara ya Katiba na Sheria na wamekuwa wakisaidika. Kwa hiyo, ushauri huu mzuri tumeupokea na tutaendelea kuutekeleza kama ambavyo inatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya kusimamia na kudhibiti ile asilimia mbili ambayo inatolewa na halmashauri. Niseme kwamba, Serikali tumepokea ushauri huu mzuri, lakini pia tumeanza kuandaa kanuni kwa kushirikiana na Ofisi ya Mheshimiwa Rais, TAMISEMI kuandaa mwongozo na kanuni ambazo zitawezesha utolewaji na usimamizi wa hii asilimia mbili ambayo inatolewa na halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ama ushauri ambao ulitolewa kwamba Serikali ihakikishe inashughulikia ama kutatua changamoto mbalimbali ambazo zinahusiana na watu wenye ulemavu, kwa maana ya kwamba kuweka uratibu mzuri kwa masuala ya watu wenye ulemavu. Serikali imeendelea kufanya hivyo na kwa kuliona hilo tumeweza kuanzisha madawati katika Wizara zetu zote, pamoja na taasisi, madawati ambayo yanashughulikia masuala ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia tumeweza kufanya warsha mbalimbali kwa sababu tunatambua kwamba, ajira imekuwa ni changamoto kubwa kwa watu wenye ulemavu. Tumeweza kuandaa warsha mbalimbali ambazo Serikali kwa kushirikiana na *CCBRT*, tulifanya warsha ambayo iliwahusisha waajiri na kupitia hapo tukawaomba waajiri kwamba waweze kuendelea kuwaajiri watu wenye ulemavu. Kupitia warsha ile, kuna waajiri ambao pale pale waliweza kujitolea kwamba, wataajiri watu wenye ulemavu kadhaa, pale kadhaa, pale kadhaa.

Kwa hiyo, ilikuwa ni warsha nzuri ambayo iliendelea kuwa na mafanikio. Niendeleo kutoa rai kwa waajiri wote kuendelea kutenga nafasi katika ofisi zao kwa ajili ya kuajiri watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi ambayo yamefanywa na Serikali, lakini naona tayari nimeshagongewa kengele ya kwanza, pia sambamba na hilo tumeweza kufanya semina kwa wajasiriamali wenye ulemavu na hii ilikuwa ni kwa ajili ya kuwaonesha fursa ambazo zinapatikana ndani ya Serikali yetu sikivu ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Rais wetu, ambaye amejipambanua kwa vitendo kuendelea kulijali na kulipenda kundi hili la watu wenye ulemavu. Semina hii pia ilikuwa na mafanikio makubwa kwa sababu wajasiriamali wale wenye ulemavu waliweza kufahamu fursa mbalimbali ambazo wanaweza wakazitumia ndani ya Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye masuala yanayohusiana na UKIMWI, kulikuwa kuna hoja ya Kamati ambayo iliweza kusema kwamba, Serikali iweze kukamilisha mwongozo wa namna ya kamati zile ambazo zilikuwa zinatumika na masuala ya UKIMWI, basi ziweze kushughulikia masuala ya dawa za kulevya. Serikali yetu imepokea ushauri huo na tayari Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imekwishakasimu mamlaka ama shughuli za kupambana na dawa za kulevya kwa hizi Kamati za UKIMWI kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kulikuwa kuna hoja ya kwamba, Serikali iweze kuona umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani za maendeleo angalau asilimia 75, kwa ajili ya masuala ya UKIMWI kutekeleza hizi afua za UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ushauri huu mzuri pia umepokelewa na tayari Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na UKIMWI imeandaa mkakati wa jinsi gani itaweza kukusanya fedha na pia umeweza kuonesha ama kuainisha vyanzo vya mapato vya ukusanyaji wa fedha hizo. Tunaamini kwamba kupitia mkakati huu, tutaweza kuondokana na utegemezi wa kutegemea ufadhili kutoka nje na hasa tukizingatia kwamba, Mheshimiwa Rais wetu ni Rais ambaye anapenda sisi kama Taifa tuweze kujitegemea kwa mapato ama kwa fedha zetu ambazo tunazipata ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya Kamati kwamba Serikali iweze kuanzisha chanzo maalum ama mahususi ambacho kitawezesha kutunisha fedha ya Mfuko wa UKIMWI. Hii walipendekeza kwamba, iwe ni tozo labda kutoka kwenye maji na vitu kama hivyo. Ushauri huu pia ni mzuri sana na utawezesha kiukweli kwamba tutaweza kuendelea kujitegemea. Serikali imepokea ushauri huu na inaendelea kuufanyia kazi kuona ni jinsi gani tunaweza tukaanzisha tozo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia kuna hoja ya kwamba Serikali iweze kubuni uwekezaji katika kutekeleza afua za UKIMWI kwa kushirikiana na sekta binafsi. Hoja hii pia ni nzuri na imepokelewa, lakini pia niweze kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Bodi ya Mfuko wa Udhambi wa UKIMWI tayari ipo katika hatua za mwisho za kuajiri mtaalam ambaye atasaidia katika upatikanaji ama ni jinsi gani sasa fedha zipatikane. Sambamba na jukumu hilo, atafanya na jukumu hili la kuhakikisha kwamba basi, hizi sekta binafsi zinaweza kushirikishwa na hatimaye kuweza kufikia lengo ambalo limetarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa kuna hoja ya kwamba Serikali kwa ku... *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema haya, nami naomba niunge mkono hoja ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Stella Ikupa kwa mchango wako. Tunaendelea, Mheshimiwa Antony Mavunde, dakika ishirini.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami napenda nichukue fursa hii kwanza kabisa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa

heshima kubwa aliyonipa kuendelea kuhudumu katika eneo hili na imani kubwa aliyonionesha katika eneo hili ambalo mpaka hivi sasa nalihudumu kama Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru sana Makamu wa Rais, pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa miongozo yao, lakini kipekee kabisa niwashukuru sana Mawaziri, mama zangu wapendwa kabisa, mama Jenista Mhagama na dada Angella Kairuki kwa namna ambavyo wameendelea kunipa ushauri na kuniongoza na upendo wao wa dhati kwangu. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu Mheshimiwa Ikupa Stella Alex kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutimiza majukumu yangu kama Naibu Waziri. Tunafanya kazi kwa ushirikiano na upendo mkubwa sana, nakushukuru sana dada Ikupa. Niwashukuru vile vile Makatibu Wakuu wote, ambao siwezi kuwataja lakini nawashukuru wote chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, niwashukuru Watendaji wa Wizara, lakini mwisho niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini ambao walionionesha imani ya kuwa Mbunge wao, nawashukuru sana kwa upendo wao na naendelea kuwafanyia kazi ya kuwatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo sasa naomba nijielekeze katika kujibu na kufafanua hoja ambazo zimeletwa na Waheshimiwa Wabunge. Hoja ya kwanza ambayo nitaanza nayo, ni hoja ya ujumla juu ya miradi ya kukuza ujuzi ambayo inatekelezwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Waheshimiwa Wabunge wanaonesha namna ambavyo pia Serikali tuwashirikishe katika utekelezaji wa miradi hii ili wapate uelewa, lakini vilevile, wawe *wanai-own* wenyewe kwa maana ya nafasi zao za uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli; chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu tunatekeleza miradi ya ukuzaji ujuzi hasa kwa vijana na ambao katika mradi mmoja tulioanza nao hivi sasa mkubwa kabisa, ni mradi wa kitalunyumba ambao utakwenda kuwagusa vijana 18,800 nchi nzima. Mradi huu

wa ukuzaji ujuzi, ni mradi ambao utakwenda kuifikia kila halmashauri vijana 100, ambapo vijana 80 watafundishwa kulima kupitia kitalunyumba, na vijana 20 watafundishwa kutengeneza kitalunyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu ya kwanza tunafarijika kusema kwamba, wale vijana walioanza katika awamu ya kwanza hivi sasa wameshapata ujuzi wa kutengeneza vitalunyumba na wameanza kuaminiwa na kupata ajira katika baadhi ya makampuni hapa nchini. Katika utekelezaji wa mradi huu, kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema, utaratibu ni kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu iliandika mkoani na baadaye, mkoani walitoa taarifa katika wilaya, lakini kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao pia alielekeza kwa Waziri wetu, ambaye pia ameshusha kwetu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwamba hivi sasa miradi hii yote katika awamu ya pili ya utekelezaji tunaandaa utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba kila Mbunge katika eneo lake anafahamu mradi unavyotekelezwa na atapewa taarifa za awali. Tumeanza katika kutoa semina na kuelimisha Waheshimiwa Wabunge juu ya utekelezaji wa mradi huu, ambao naamini kabisa utakwenda kukidhi mahitaji katika kutatua changamoto za ukosefu wa ajira na ukosefu wa ujuzi kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ambayo ilizungumzwa hapa, ni hoja ya mkakati wa kusaidia ajira kwa vijana hasa vijijini. Ni hoja ambayo Wabunge wengi wameisema na wanataka kusikia mkakati wa Serikali. Mkakati wa kwanza wa Serikali katika kuhakikisha tunatua changamoto ya ajira hasa kwa vijana. Eneo la kwanza tunalolifanya ni katika kutoa elimu hasa katika kundi hili kubwa la vijana, kwanza kabisa kwenye tafsiri ya neno ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Ajira, ya mwaka 2008, ajira ni shughuli yoyote halali inayomuingizia mtu kipato. Kwa hiyo, tunaanzia hapo kwanza kuwafanya vijana wetu na wananchi wote kwa ujumla kuelewa nini maana ya ajira kwa sababu kumekuwapo na dhana

kwamba, ili mtu aonekane ameajiriwa lazima awepo ofisini tu. Kwa hiyo tumeanza na eneo hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, tunafahamu haiwezekani na katika hali ya kawaida watu wote kuweza kupata ajira katika mfumo rasmi. Kwa hiyo katika hili pia tunachokifanya ni kuelezea fursa zilizopo katika sekta isiyo rasmi ambayo pia itawezesha watu wengi zaidi waweze kupata ajira. Kwa hiyo, katika eneo hili, mkakati wetu ni kwamba hivi sasa kama Serikali kupitia azimio la mwaka 2014, ambalo lilikuwa ni chini ya aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, ilifanyikia Dodoma la Wakuu wa Mikoa wote kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali kwa ajili ya vijana. Mpaka ninavyozungumza hivi sasa, tayari yametengwa maeneo ya takribani ekari laki mbili kumi na saba elfu, mia nane na themanini na mbili nchi nzima kwa ajili ya shughuli za vijana za uzalishaji mali. Kwa hiyo lilikuwa ni eneo la kwanza katika mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni eneo la uwezeshaji, uwezeshaji wetu unafanyika kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Vijana ambao mpaka hivi sasa tayari tumeshavifikia vikundi takribani 755 na tayari billioni 4.5 zimetoka kwa ajili ya kuwawezesha vijana. Katika eneo hili fedha zinazotumika ni zile asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri ambazo pia zinatumika kama sehemu ya kuwawezesha vijana kwa ajili ya kupata mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo ipo zaidi ya 19 ambayo ukiunganisha kwa pamoja ina ukwasi wa kiasi cha shilingi trillioni 1.3 kwa pamoja yake, pamoja na benki ya kilimo ambayo ipo maalum kwa ajili ya kuwawezesha vijana na makundi mengine katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika eneo hilo la uwezeshaji pia, tunaendelea kuhakikisha kwamba vijana wengi zaidi wanapata fedha za mikopo ili wafanye shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetambua moja ya mkakati mwingine wa kusaidia na kutatua changamoto ya ukosefu wa ajiri ni kwenye eneo la ujuzi. Kwa mujibu wa tafiti ya mwaka 2014, ambayo inaitwa, *Integrated Labour Force Survey* inasema nchi yetu ya Tanzania ina takribani watu wenye uwezo wa kufanya kazi milioni 22.3. Changamoto kubwa iliyokuwepo ni katika eneo la ujuzi, ambapo watu wenye ujuzi wa juu kabisa ni asilimia 3.6, watu wenye ujuzi wa kati ni asilimia 16.5 na watu wenye ujuzi wa chini ni asilimia 79.9. Ili kwenda kuwa nchi ya kipato cha kati, ifikapo mwaka 2025 viko vigezo vimewekwa na moja ya kigezo kilichowekwa, ni katika eneo la nguvu kazi, lazima uwe una nguvu kazi yenye ujuzi wa juu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi yetu ya Tanzania hivi sasa, tunatekeleza mradi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambao lengo lake ni kuwajengea ujuzi vijana wetu wapate nafasi ya kuweza kujiajiri wenyewe kupitia ujuzi wao. Ninavyozungumza hivi sasa, tuna mradi ambao unaitwa ni Mradi wa Kurasimisha Ujuzi kwa Vijana, ambao wana ujuzi lakini hawajapitia mfumo rasmi wa mafunzo. Hivi sasa wataalam wetu na wakufunzi wa *VETA*, wanawapitia vijana hawa mtaani, ukienda leo mtaani, kuna kijana anajua kuchonga vitanda vizuri, anajua kupaka rangi vizuri, ni fundi mzuri wa magari, hajawahi kusoma *VETA*, hajawahi kusoma *Don Bosco*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachokifanya ni kurasimisha ujuzi wake, tunakwenda mtaani na wakufunzi wa *VETA* wanakaa nae, wana-*address* upungufu alionao *then* tunampatia cheti cha *VETA* cha ufundi pasipo yeye kwenda kusoma *VETA*. Mradi huo kwa mwaka huu utawafikia takribani vijana elfu kumi. Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yao wajiandae tutawafikia kwa ajili ya kuwawezesha vijana wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunao mradi wa mafunzo ya ufundi stadi ambao tunautekeleza chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ambapo Ofisi ya Waziri Mkuu inagharamikia mafunzo na fedha ya kujikimu kwa vijana hawa wa Kitanzania

ambao tunawafundisha ufundi mbalimbali; kujenga, umeme, ushonaji, masuala ya kompyuta na fani zinginezo. Katika eneo hili tumepiga hatua kubwa sana, tumeshawasomesha vijana zaidi ya 2,278 katika awamu ya kwanza na itaendelea, lakini asilimia kubwa tayari wameshapata kazi na wengine wamejajiri wenyewe. Kwa hiyo, ni dhahiri kuonesha kwamba program hizi za ukuzaji ujuzi zitasaidia sana katika kutatua changamoto katika eneo hili la vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ilisemwa hapa, ni kuhusu mikopo ya asilimia 10 ya Halmashauri lakini vile vile na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana namna ambavyo inachelewa kurejeshwa katika kundi hili kubwa la vijana.

Ni kweli kulikuwa kuna changamoto hiyo lakini Serikali hivi sasa kwa kushirikiana na halmashauri tumeendelea kufanya ufuatiliaji ili fedha hizi za mikopo katika makundi haya ya vijana, zirudishwe kwa maana ya Mfuko ule ambao ni *revolving* ili vijana wengine waweze kukopeshwa. Mpaka hivi sasa takribani shilingi milioni 356 zimerejeshwa kama sehemu ya marejesho ya mkopo ambapo vijana wengine pia watapata fursa ya kupata mkopo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imejitokeza hoja nyingine hapa kuhusu vibali vya kazi na imezungumzwa na Wabunge wengi sana. Mwaka 2015 Bunge hili tukufu lilitunga Sheria Na.1 ya Uratibu wa Ajira kwa wageni hapa nchini. Kwa mujibu wa sheria ile, kifungu 11 kinatamka bayana mtu mwenye mamlaka ya kutoa kibali cha kazi ni Kamishna wa Kazi ambapo mpaka atoe kibali lazima ajiridhishe kwamba kazi inayoombwa hatuna ujuzi wa namna hiyo ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ndivyo sheria inavyosema iliyotungwa na Bunge. Kamishna anachokifanya ni kusimamia sheria. Kamishna huyu tuliyenaye hivi sasa, Wakili Msomi Gabriel Malata anafanya kazi yake vizuri sana, ameonesha usimamizi uliotukuka na si kweli kwamba ni Mungu mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria hii, mtu akipeleka maombi ya kibali cha kazi inapaswa apewe ndani ya siku 14. Hivi sasa vibali vya kazi vinatoka ndani ya siku saba. Sisi tunaamini kabisa kwamba Tanzania siyo kisiwa, hatuwezi kuishi wenyewe. Tunapenda pia kupata wageni kwa ajili ya watu wetu kupata ujuzi lakini tunachokisema pamoja na hayo yote sheria yetu pia na yenyewe ichukue nafasi yake kwa maana ya vile vigezo vilivyowekwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili najua kumekuwa na kelele nyingi sana ya baadhi ya wadau ambao wengi pia hawasemi ukweli. Kamishna anachokifanya ni kuangalia vigezo mbalimbali katika utoaji wa vibali lakini hajiongozi mwenyewe kwa mapenzi yake na nafsi yake, ni sheria ndiyo inamtaka afanye hivyo. Kuna baadhi ya maeneo kuna udanganyifu kiasi kwamba Kamishna akiachia tu kila mtu aje afanye kazi hapa, vijana wetu pia na wenyewe watakosa fursa ya ajira kama ambavyo Ibara ya 173 ya Chama cha Mapinduzi imeeleza katika Ilani ya Uchaguzi, kinachofanyika hapa ni utekelezaji wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sisi Ofisi ya Waziri Mkuu siyo *robot* kwamba hatuwezi kuangalia mazingira ya dunia ya leo, tunahitaji na tunawapenda wawekezaji. Hivyo, nitoe rai kwa wawekezaji wote nchini, kumekuwepo na tatizo la wawekezaji hawa katika ufuatiliaji wa vibali kuwatumia watu wa kati ambao wamekuwa wakileta shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi yetu hivi sasa tumeunganishwa katika mfumo ambapo sasa tutatoa vibali vya *electronic* ambavyo vitapunguza urasimu. Mimi nataka mwekezaji mmoja aje anitolee mfano kwamba amewahi kuleta maombi yamekaa miezi sita hajawahi kujibiwa. Hivi sasa jambo hilo hakuna katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Mtu akileta maombi leo, kama yamekamilika ndani ya siku saba anapata kibali chake, *provided* awe amekidhi matakwa yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunakwenda katika mfumo mzuri zaidi, kibali kitatoka chini ya siku saba kama mtu akikamilisha nyaraka zake. Tunaunganisha sasa mfumo

wa vibali vya kazi na *residency permit*. Hivi sasa ndiyo tunakwenda katika utekelezaji wa programu hiyo, mtu akiomba kibali Kamishna wa Kazi atakiona na Uhamiaji wataona katika mfumo hapo hapo, Kamishna akimkubalia dakika hiyo hiyo Uhamiaji kule wataona wata-*issue residency permit*. Kwa hiyo, tunatoka kwenye mfumo wa siku saba mpaka siku moja ikiwezekana katika utoaji wa vibali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumekwenda mbali zaidi, kwenye eneo la rufaa, mimi ndiyo nashughulikia rufaa zote za vibali vya kazi. Hivi sasa rufaa zinazotoka *TIC* kwa mfumo tuliouweka hata nikikaa hapa ndani ya Bunge najibu rufaa zingine kupitia simu. Ni utaratibu ambao tumeuweka kwamba rufaa yoyote itakayoingia ili tusiwacheleweshe wawekezaji naiona moja kwa moja najijibia hapa hapa na kutoa maamuzi kama imekubaliwa au amekataliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwenye eneo hili. Eneo hili lina changamoto kubwa sana na maneno huwa yanakuwa mengi sana. Katika eneo hili nataka niwaambie ndugu zangu Watanzania na Waheshimiwa Wabunge ambao mko hapa, hatufanyi kazi kwa kumuonea mtu, hatufanyi kazi kuwafukuza wawekezaji, mimi nasimamia tena eneo la ajira nafahamu maana ya uwekezaji. Mwekezaji mmoja akija hapa akiwekeza tunapata fursa za ajira, vijana wengi zaidi watapata ajira. Nitakuwa mtu wa ajabu kuwa mtu wa kwanza kuwafukuza wawekezaji kupitia sharia. Nachokisema taratibu pia zifuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli Waheshimiwa Wabunge, atoke mtu Pakistan aje kuunga nyaya hapa na mimi nitoe kibali cha kazi? Tuwaache vijana wa *VETA, Don Bosco*, tumchukue mtu wa Pakistan aje kuunga nyaya Tanzania? Haiwezekani!

Kwa hiyo, tunachokifanya ni kusimamia sheria, naomba mtuunge mkono na mumpe moyo Kamishna huyu, anafanya kazi kubwa sana. Mkianza kumzonga na maneno hapa ndugu zangu mtamfifisha moyo, mpeni moyo, kazi yake ni kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mavunde kwa mchango wako. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) Mheshimiwa Kairuki.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nami nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Makamu wa Rais; Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na uongozi wao makini na mahiri na kwa namna ambavyo wanaliongoza Taifa letu ili liweze kwenda mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa ambayo bado anayo kwangu kwa kuiteua hivi karibuni kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya uwekezaji. Itakumbukwa kwamba Mheshimiwa Rais alipofanya mabadiliko haya ilimpendeza kuweka jukumu la kuratibu, kuhamasisha, kuvutia na kusimamia suala zima la maendeleo ya uwekezaji nchini chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kimsingi uamuzi ule ulikuwa na mambo ya msingi matatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kwa namna ambavyo yameonesha yeye mwenyewe na Serikali yake inavyotambua umuhimu na mchango mkubwa ambao uwekezaji unao katika ujenzi wa Taifa letu.

Pili, ni imani kubwa ambayo Mheshimiwa Rais yeye mwenyewe anayo kwa sekta binafsi nchini lakini kwa wawekezaji kwa ujumla wake. Tatu, ni usikivu wa Mheshimiwa Rais wetu juu ya kilio cha sekta binafsi na uwekezaji ambacho Mheshimiwa Rais kupitia uteuzi huu ameamua kukisikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uamuzi huo, Mheshimiwa Rais amethibitisha kwa vitendo kwamba anajali sekta binafsi na wawekezaji. Itoshe tu kusema kwamba utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Taasisi za Udhhibiti kupitia *Blueprint*; Mpango Jumuishi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara ya Uwekezaji nchini na tatu kuteua Waziri mahsusi wa Uwekezaji pamoja na kuhamishia jukumu hili la uratibu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni sehemu tu ya mambo mengi ambayo yanaonesha dhamira njema ya Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla kwa sekta binafsi na uwekezaji. Hakika mwenye macho haambiwi tazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee pia napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake mahiri kabisa ambayo imeweka msingi na mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo baadhi yake kama ambavyo mlisikiliza hotuba ile mwanana kabisa iligusa masuala ya uwekezaji. Pili, napenda sana kumpongeza pacha wangu na dada yangu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu), Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Ikupa; Makatibu wetu Wakuu, mama Tarishi, mama Mwaluko pamoja na Bwana Massawe na watumishi wote kwa ushirikiano mkubwa ambao wanatupatia katika ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, nichukue nafasi hii kuishukuru sana Kamati yetu ya Bunge ya Kudumu ya Sheria na Katiba kupitia kwa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mchengerwa, Mheshimiwa Najma pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa ushirikiano mkubwa walionipatia na kwa mchango na ushauri wao mkubwa ambao tunaamini utatuletea ufanisi katika majukumu yetu. Mwisho kabisa, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa umahiri wao katika kusimamia shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na si kwa umuhimu na nitakuwa sijatenda haki nisipowashukuru sekta binafsi kwa ujumla na wawekezaji wote kwa namna ambavyo wamewekeza mitaji yao katika kuhakikisha kwamba wanakuza uchumi wetu wa Taifa. Pia kuwapongeza sana *TNBC*, niwashukuru kipekee *TIC* ambayo iko chini ya Ofisi yangu, *EPZA*, *TPSF*, *TCCIA*, Balozi zetu za Tanzania nje ya nchi pamoja na *CEO Roundtable* lakini na Wakuu wa Mkoa wote, Wakuu wa Wilaya, Wenyeviti wetu wa Halmashauri na viongozi mbalimbali na wananchi ambao wameona na kutambua umuhimu wa uwekezaji katika uchumi wa Taifa letu. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, nitaendelea kukutana na wawekezaji na wafanyabiashara ili kuweza kusikiliza kero na changamoto zao mbalimbali kwa lengo la kuzitatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipeke kabisa nimshukuru sana mume wangu mpenzi Balozi Mbelwa Kairuki pamoja na watoto wangu. Zaidi pia viongozi wote na wanachama wa UWT Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Wajumbe wa Baraza Kuu la UWT Taifa kwa namna ambavyo wamekuwa wakinipa ushirikiano pia kunivumilia wakati ninapotekeleza majukumu yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kabla sijajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge nianze na maelezo ya jumla kwa kuelezea umuhimu wa uwekezaji ambao upo katika maendeleo ya Taifa lolote ulimwenguni. Kwa hakika wote tunatambua mchango mkubwa wa wawekezaji katika kuongeza ajira, uzalishaji na tija pia kwa namna ambavyo unashiriki katika kuongeza Pato la Taifa, kuleta teknolojia mbalimbali na kuwezesha wananchi na kupunguza umaskini. Ni kutokana na umuhimu huo ndiyo maana Serikali imejipanga kikamilifu kuhakikisha kwamba uwekezaji wa ndani na nje unakua kwa kasi sambamba na kuhakikisha kwamba wananchi wetu nao pia wanaweza kunufaika na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka 10 nikitolea tu takwimu za mwaka 2008 - 2018, *TIC* iliweza kusajili

miradi takriban 6,596. Napenda kusema kwamba hii si miradi yote ya uwekezaji, iko miradi mingi ya uwekezaji ambayo imeingia nchini na mitaji yake lakini unakuta mingine bado haijasajiliwa T/C. Ni miradi yenye thamani ya zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni 79.4 ambapo si kiwango kidogo na umeajiri zaidi ya wafanyakazi 788,547. Tutaendelea kuhakikisha kwamba tunaendelea kuongeza mitaji zaidi kutoka nje lakini zaidi pia kuhakikisha kwamba wawekezaji wetu wa ndani na wenyewe wanashiriki katika uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tutaendelea kuhakikisha kwamba tunasonga mbele katika tasnia ya uwekezaji kama ambavyo tumetambuliwa na ripoti mbalimbali za Kimataifa za uwekezaji tumepiga hatua, tunaongoza katika nchi za Afrika Mashariki lakini pia katika nchi ambazo zinapendekezwa kuwekeza Afrika Tanzania ni miongoni mwa nchi chache ambazo zimependekezwa katika uwekezaji. Jukumu letu kubwa ni kuhakikisha kwamba wote kwa pamoja tuongeze jitihada ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kuvutia wawekezaji zaidi kutoka nje ili waweze kuiona Tanzania kama kituo au nchi bora kwa ajili ya kuweka uwekezaji wao. Hili ni jukumu letu sote Waheshimiwa Wabunge ambao tuna wananchi nyuma yetu, mna Halmashauri ambazo ziko chini yenu mnazoziongoza, tuendeleo kuwa mfano na tutoe ushirikiano ili kuhakikisha kwamba wawekezaji wetu wanapokuja basi waweze kuwekeza mitaji yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhamasisha wawekezaji wa ndani, tunaendelea na mikakati yetu mbalimbali kama Serikali kuhakikisha kwamba tunafanya makongamano ya ndani na nje ya nchi. Pia tunatoa elimu ya uwekezaji kuwawezesha wawekezaji wetu wadogo wadogo nao waweze kupata mitaji ya kuwekeza kutoka katika taasisi za fedha ikiwemo katika Benki ya Kilimo kama ambavyo Waziri wa Mifugo ameeleza lakini pia tutaendelea na mikakati mingine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pia katika takwimu mbalimbali ukilinganisha na mwaka 2005 ambapo

wawekezaji wa ndani walikuwa ni takriban asilimia 25 tu lakini nafurahi kusema kwa sasa wawekezaji wa ndani ni zaidi ya asilimia 72. Tutaendelea kuhamasisha ili kiwango hiki kiweze kukua zaidi ili Watanzania nao waweze kuona manufaa ya uwekezaji na waweze kupata pato kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia malengo yetu kiuchumi kama Serikali, tumeweka vipaumbele au mipango katika kuvutia miradi ya uwekezaji katika sekta ambazo zina tija na zina mchango mkubwa kiuchumi na kwa wananchi. Lengo kubwa la kufanya hivyo ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha minyororo ya thamani katika mazao ya kilimo, mazao ya uvuvi pamoja na mifugo lakini pia katika masuala ya madawa ya binadamu, kemikali na bidhaa kwa ujumla ambazo zinatumiwa kwa wingi nchini lakini pia ambazo zinaajiri wananchi wengi na ambazo zinatumiwa malighafi zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaje vipaumbele vichache ni pamoja na uzalishaji wa mafuta ya kula kwa kutumia mbegu zinazozalishwa. Hili limeelezwa vizuri sana na Waheshimiwa Wabunge wengi sana na ukiangalia tuna upungufu wa zaidi ya tani 320,000. Kwa hiyo, napenda kuwatangazia Watanzania hii ni fursa kubwa ambayo naamini kila moja akijipanga kwa namna ya uwezo wake wa kimtaji tunaweza tukatumia soko hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, uzalishaji wa mbegu. Ukiangalia kwa sasa mbegu zinazozalishwa nchini ni tani 51,000 tu lakini mahitaji ambayo yanaagizwa kutoka nje ni tani zaidi ya 16,000 na mahitaji kwa ujumla wake ni tani zaidi ya 370,000. Kwa hiyo, hapa napo jamani ndugu zangu ni fursa, hebu tuwekeze katika uzalishaji wa mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni suala la sukari. Ukiangalia mahitaji ni zaidi ya tani 670,000 kwa sukari ya viwandani pamoja na ya majumbani na tumekuwa tukiagiza kwa kiasi kikubwa nje ya nchi ukilinganisha na kiwango ambacho kinazalishwa hapa. Hapa napo tunaweka mkazo

ili tuhakikishe kwamba tunajitosheleza kwa mujibu wa uwekezaji wetu uzalishaji wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni uzalishaji wa dawa za binadamu na nafurahi na kushukuru sana kwa namna ambavyo tumeshirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Afya katika kuhakikisha kwamba tunachochea, kuhamasisha na kuvutia wawekezaji katika sekta hii ya dawa. Tumeona pale Zegereni viko viwanda vingi ambavyo vimejengwa na wakati wowote vitaanza kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ni ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya uvuvi wa kisasa pamoja na kuchakata viwanda vya samaki. Vilevile tuna masuala ya vifungashio, ni fursa kubwa na katika korosho tuna tani zaidi ya 230,000 ambazo lazima ziweze kuongezewa thamani kwa kuchakatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau hoja ya Mheshimiwa mama Kilango, Mheshimiwa Njalu na Waheshimiwa wengi sana ambao walionyesha umuhimu wa kuwekeza katika viwanda vya nguo. Napenda kuwashukuru wote walioongelea suala hili ikiwemo na viwanda vya ngozi, viatu, maziwa, pembejeo pamoja na mbolea tunaiona hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa sasa ambacho Serikali imekifanya kupitia mazao sita ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali imeyatamka kama mazao ya kimkakati na pamba ikiwemo ni kuhakikisha kwamba tunaongeza uzalishaji ili wanapokuja wawekezaji katika sekta hii basi waweze kuwa na uzalishaji ambapo watakuwa na uhakika wa malighafi kwa siku 260. Kwa mujibu wa ufanisi wa viwanda unatakiwa uwe na malighafi mfululizo kwa siku takriban 260.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachokifanya hivi sasa kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Wizara zingine za kisekta ni kuhakikisha kwamba tunaongeza malighafi ili tuwe na malighafi ambazo zitaweza kujitosheleza.

Nawashukuru, tutaendelea kukaa na wadau kuhakikisha kwamba tunaweza kuzitambua kwa kina changamoto ambazo zinawakabili ili kuhakikisha kwamba watakuwa na viwanda ambavyo wamewekeza kwa tija na kuweza kupata faida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea, pamoja na changamoto zote hizo nilizoieleza, wako wengine ambao malighafi zinawatoshela lakini bado wana changamoto. Tutahakikisha tunaweka vivutio maalum kwa ajili ya wale watakaowekeza katika sekta hizi ambazo nimezieleza ni za vipaumbele ili kuhakikisha kwamba wanaweza kuendesha viwanda vyao kwa tija na kuweza kutupatia pato zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala kama zipu, vifungo na *materials* mbalimbali ambazo unakuta zinatumiwa katika viwanda vya nguo ambavyo kimsingi usipoviondolea kodi inakuwa ni ngumu wao kuzalisha kwa faida. Kama tulivyoieleza hapa yuko Mheshimiwa nadhani ni Salum Mbuzi mwenye kiwanda cha *Jambo Spinning* ambaye alitueleza changamoto zake na nimhakikishie kwamba ni maeneo ambayo tunayafanyia kazi ili tuweze kupata suluhu katika suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau hoja za uwekezaji katika hoteli, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla amezeleza vizuri. Tutaenda kuangalia masuala ya utalii katika *Selous Game Reserve*, Kilwa Kivinje, Mafia pamoja na sehemu zingine. Yako maeneo mengi kwa sasa niishie kwenye vipengele hivyo tu na mengi nitaeleza nitakapokuwa najibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo ya utangulizi, niungane na wote walionitangulia lakini zaidi kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika suala zima la uwekezaji. Nawashukuru sana kwani natambua nia yenu kama Waheshimiwa Wabunge ni kuona kwamba tunakuwa na mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji nchini lakini kuhakikisha kwamba

mazingira haya yanaboreshwa na kila siku kuhakikisha kwamba taasisi na Wizara zetu zinaweza kubadilika, kwenda na wakati ili kuhakikisha kwamba kodi, ajira na bidhaa zinaweza kupatikana kupitia uwekezaji tulionao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kujibu hoja hizi, nihitimishe kwa kutoa rai kwa mamlaka mbalimbali zihakikishe kwamba zinakuwa wabunifu na kuona namna gani wanaweka mikakati ya kufanikisha uwekezaji nchini kwa kuwa uwekezaji ni suala mtambuka. Ni muhimu wakaonesha kwa vitendo kila Afisa wa Serikali aone ni kwa namna gani anaweza kujenga taswira na mazingira mazuri ya uwekezaji nchini. Kwa kitendo kimoja tu inaweza ikatuondolea wawekezaji wengi sana ambao kuwarudisha itakuwa ni shida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho kabisa niwahakikishie katika suala zima la wepesi wa kufanya biashara. Ni suala ambalo kwa kweli nitajikita nalo sana kupitia viashiria vile 11. Niitakaa na Mawaziri wa sekta kwa sekta na menejimenti zao na kuhakikisha kwamba yale yote yaliyoelezwa katika viashiria vya Tathmini ya Benki ya Dunia ambapo kwa mwaka huu tumekuwa nafasi ya 144 kati ya nafasi 190, hii ni nafasi ambayo tulikuwa 2016, 2017 tulishapiga hatua nzuri tukawa 132, hatuwezi kurudi nyuma. Ukiangalia malengo yetu mwaka 2025 ni kufikia nafasi ya 95 katika wepesi wa kufanya biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana sekta zote mkae mkao mzuri, tutakuja kuketi. Bahati nzuri nimeshawapata wale wathamini wenyewe Benki ya Dunia wako Chile na nina mpango wa kufanya nao *video conference* wiki hii ambapo wamepanga kunipitisha katika kila kiashiria ni nini hasa wanakiangalia ili kuhakikisha kwamba tunapiga hatua katika wepesi wa kufanya biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho kinaturudisha nyuma, katika kujaribu kupitia ripoti za wepesi wa biashara wa nchi mbalimbali, unaangalia Rwanda, unaangalia Uganda, wanatupita katika *rank* hiyo. Kwenye

uwekezaji tunawashinda, iweje kwenye wepesi wa kufanya biashara hawa watushinde?

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo nimeligundua, ukiangalia katika *improvements za reforms* ambazo nchi nyingine wamehesabika wamefanya vizuri, moja au mbili tu, inaonekana yako mengi mazuri ambayo tumeyafanya lakini unajikuta wale wanaohojiwa hawayaelezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye hili naomba sana, wako Wanasheria wa Kampuni binafsi za kisheria na wako watoa huduma wengine mbalimbali ambao wanapata huduma pia kwenye taasisi zetu, yale mazuri yanayofanywa na Serikali, basi wasisite kueleza maboresho ambayo yamefanywa. Kwa sababu kwa kufanya hivyo, mwekezaji anaangalia pia *ranking* ambayo nchi inayo katika wepesi wa kufanya biashara, ndipo anaamua pia kwenda kuwekeza. Kwa hiyo, kwenye hili nitaomba sana ushirikiano na ni imani yangu kila mmoja ataweza kubadilika na kutoa ushirikiano kwenye hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nijibu sasa hoja ambazo zimeelezwa. La kwanza ambalo lilikuwa ni kubwa ni kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa ajili ya kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ili kuweza kuongeza fursa za ajira na biashara na hivyo kuongeza kipato kwa wananchi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba kama Serikali tunapokea ushauri huu na niendeleo kuwahakikishia kwamba, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha mazingira ya biashara ya uwekezaji, kama nilivyoeleza awali ili kurahisisha uanzishaji na zaidi ukuaji wa biashara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuongeza maeneo mbalimbali ya kiuchumi (*special economic zones*) na kuhakikisha kwamba upatikanaji wa ardhi na kuwa na miundombinu wezeshi ambayo itaweza kuwasaidia wawekezaji wetu kuweza kuwekeza. Pia tutaendelea

kufanya vikao vya mashauriano na wawekezaji wetu na wafanyabishara kupitia ngazi mbalimbali za kisékta mikoā na wilaya ili kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali ambazo wamekuwa wakizibainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya Msemaji wa Kambi Rasmi Bungeni, ambapo yeye alikuwa haamini kama Serikali au kupitia *TIC* tumeweza kuvutia zaidi ya miradi 145 mpaka sasa. Napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbowe, nimtajie tu chache, kuna *Alpha Pharmaceuticals* ya Dar es Salaam, ambayo watawekeza zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 20 na ajira zaidi ya 40. Tunayo *Bio-Sustain Limited* ya Singida ambao hawa watakuwa wakichakata mafuta ya alizeti na watawekeza zaidi ya Dola milioni 11 za Kimarekani; tunayo *GBRI Business Solution* ya Shinyanga; tunayo *Kilimanjaro Bio-Chemical Limited* ambao watakuwa wanazalisha *Ethanol*; tunayo *KOM Food* ya Shinyanga ambao nao wataweza kuchakata alizeti na watawekeza zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 20; tunayo pia *MW Rice Millers* ambao nao pia watawekeza zaidi ya dola milioni 17. Siyo maneno na akiitaka orodha hii kwa kina; na anaweza kwenda kuwatafuta wawekezaji hao ambao wamesajili miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbowe pia alitaka kujua mgawanyo wa hizi dola bilioni 1.18. Napenda kumwambia kwamba kwa wawekezaji wa ndani, tunatarajia kwamba watawekeza mitaji ya dola milioni 401.66, lakini kwa upande wa wawekezaji wa nje, watawekeza mitaji ya zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 127; na kwa upande wa miradi yenye ubia kati ya wawekezaji wa ndani na nje, watawekeza Dola za Kimarekani milioni 423.75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba sana wawe na imani. Tunachoki-*present* hapa ni takwimu na taarifa ambazo ni thabiti na zina ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kulikuwa kuna hoja nadhani ya Mheshimiwa Anna Kilango, kulikuwa na Mheshimiwa Mashimba na wengine wengi; ni kwa namna

gani tunaendelea kuwalinda wazalishaji wa ndani? Niendeleo kuwahakikishia tu kwamba, kupitia mfano wa hatua za kikodi, kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018, iliongezwa kodi kwa wale wanaoagiza mafuta mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. Kwa yale ambayo ni ghafi, kuna kodi ambayo ilianzishwa ya takriban asilimia 25 na kwa mafuta ambayo yamechakatwa ilianzishwa kodi ya zaidi ya asilimia 35.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeendelea kudhibiti uingiaji wa mafuta ya kula kutoka mipakani. Lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba tunalinda viwanda vyetu vya ndani na tutaendelea kufanya hivyo na kuhakikisha kwamba tunakuja na hatua nyingine za kikodi ili kulinda viwanda vyetu vya ndani pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja nyingine kuhusiana na mifugo, kuona ni kwa namna gani tunaweka vivutio vya kodi kama nilivyoeleza kule mwanzo. Kwenyewe pia kupitia Sheria ya Fedha, waliweza kupunguziwa kodi ya makampuni na hili lilifanyika kupitia viwanda vya ngozi, pamoja na viwanda vya madawa vipya. Badala ya kulipa *Corporate Tax* ya asilimia 30, wao kwa sasa wanalipa *Corporate Tax* ya asilimia 20 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye kodi ya ongezeko la thamani kwa upande wa mitambo na vifaa vya viwanda hivyo na kwenyewe pia kodi hizi ziliondolewa. Tunaweza kuona kwa kiasi kikubwa Serikali inaweza kuweka jitihada katika kuhakikisha kwamba viwanda vinalindwa, lakini kuweza kuwapa nafuu wawekezaji waliowekeza katika sekta hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya kuendelea kuhakikisha kwamba tunafanyia maboresho sera yetu pamoja na sheria. Niendeleo kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, tayari tumeshafanya tathmini ya mazingira ya uwekezaji na tumeshabainisha maeneo ambayo ni muhimu yanayohitaji kufanyiwa mapitio ili kuboresha mazingira haya ya uwekezaji. Kufuatia tathmini

hiyo, tutakuja sasa na Sera mpya ya Uwekezaji ambayo sasa hivi imeanza kufanyiwa mapitio, tayari tumeshaanza mchakato wa kupata timu ya watalamu ambao wataendesha zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sheria ya Uwekezaji na yenyewe kwa kiasi kikubwa tutaifanyia marekebisho ili kuhakikisha tunaondoa vikwazo vilivyopo, ikiwemo na kuwa na vivutio vipya katika sekta mbalimbali maalum kama nilivyozieleza huko awali. Pia kuona ni kwa namna gani suala zima la upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya wawekezaji, suala zima la miundombinu wezeshi kwa ajili ya wawekezaji na kuondoa changamoto mbalimbali za kitaasisi ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na mazingira ambayo ni shindani kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshafanya tathmini na kuandaa *blueprint* kama nilivyoeleza kule mwanzo na masuala yote muhimu ambayo yamekuwa yakikwamisha uwekezaji yalishabainishwa na hata wahusika ambao wanatakiwa kutatua changamoto hizo wanajulikana. Ni suala ambalo kupitia mpango kazi ule jumuishi ambao niliusema, pindi tu utakapokuwa tayari, basi hili nalo litaweza kuondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, pamoja na kwamba mpango kazi jumuishi unaandaliwa, lakini tayari yako maeneo ambayo yameshaanza kufanyiwa kazi. Kama ambavyo tumemsikia Mheshimiwa Mavunde ambavyo ameeleza, pia sasa hivi wanapita sheria ile namba moja ya mwaka 2015, kuweza kuona wanaweza kuleta ufanisi kiasi gani katika masuala mazima ya vibali vya ajira pamoja na taratibu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukiangalia katika masuala ya tozo, kwenye sekta tu pekee ya kilimo; nawapongeza sana Wizara ya Kilimo, kwa kuwa tayari, kuweza kuondoa zaidi ya tozo 114, siyo jambo dogo. Kwa hiyo, naomba tu Wizara nyingine, badala ya kuona wanataka maduhuli makubwa, hebu tuangalie kikapu kikubwa zaidi.

Tutakapochangia katika Mfuko Mkuu wa Hazina, naamini mengi yataweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kuwaomba Mawaziri wenzangu, kila mmoja aweze kupitia tozo ambazo zinaweza zikapunguwa; nampongeza Mheshimiwa Ummu naye pia anajiandaa kupunguza tozo mbalimbali kupitia *TFDA*. Nampongeza Mheshimiwa Jenista kupita *OSHA* zaidi ya tozo tano wameweza kufuta; lakini pia Wizara ya Madini, waliokuwa wenzangu tukiwa nao zaidi ya tozo tisa ziliweza kuondolewa katika uzalishaji wa chumvi. Naamini Serikali itaendelea kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa kumaliza hoja chache, napenda tu kusema kwamba kwa upande wa zao la chikichi, ukiangalia tumeweka kipaumbele pia katika zao hili. Tayari kupitia *TIC* zaidi ya hekta 13,000 zimetengwa katika Mkoa wa Kigoma kwa kutambua kwamba zao hili ni la muhimu na la kipaumbele na kuhakikisha kwamba tunakuwa na mafuta ya kupikia ya kutosha na hii ni malighafi muhimu sana kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya utangulizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja za Mheshimiwa Shangazi kuhusiana na namna ya kulinda mazao ya wakulima, hususan katika kuondoa *parking fees, landing fees* pamoja na kuondoa tozo mbalimbali katika *cold-rooms*. Ni hoja nzuri na ninaamini kwa kuwa tulitembelea Rungwe pamoja na Hai na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, naamini kupitia *Task Force* ile ni eneo ambalo atakuwa ameliangalia ili kuona ni kwa namna gani wanaweza kulinda mazao au bidhaa ambazo zinaweza kuharibika kama nyanya, matunda na mbogamboga kupitia *regime* ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza pamoja na maandishi. Niwahakikishie hoja zote, endapo kuna nyingine ambazo hatujazijibu, tumezipikea, tutazinakili na tutaweza kuwawasilishia majibu, kila mmoja ataweza kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi, kwa kuwa nina mwezi mmoja tu katika ofisi hii, niendeleo kuwaomba sana ushirikiano wa dhati kabisa na tutakuja katika maeneo yenu ili kuweza kutembelea uwekezaji katika sekta mbalimbali. Tunaomba mtupatie ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Nakusukuru sana kwa mchango wako mzuri sana, umeanza vizuri. Umepewa deski ambalo ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi hii. Kuna timu nzuri tu ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini pia katika *Sectoral Ministries* ambazo ni muhimu sana mkafanya nao kazi kwa karibu.

Waheshimiwa Wabunge hapo ndiyo tumefikia mwisho; siyo kwamba tumefikia mwisho wa hoja hii, hapana, lakini kwa mchana huu ndiyo mwisho. Tutakaporejea jioni saa 11.00, atanza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, naye asafishe njia ya mtoa hoja. Kwa hiyo, atakuwa na dakika zisizozidi 30 na baadaye mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Mkuu atahitimisha hoja yake tuliyoanza nayo siku ya Alhamis wiki jana. Atafanya hivyo kwa muda usiozidi saa moja. Baadaye Bunge litaingia kwenye Kamati ya Matumizi, kama mnavyofahamu Kanuni zetu.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana, tangu jana mmenisaidia sana na mpaka kipindi hiki; jioni atakuwepo Naibu Spika, ndiye ataongoza shughuli za Bunge mpaka kwenye Kamati ya Matumizi na baadaye Bunge kurejea.

Kwa hiyo, nawashukurui sana pamoja na meza, wamenisaidia sana kuweza kufika tulipofika hapa leo. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 6.50 mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Tunaendelea na majadiliano, sasa nimwite Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Ofisi ya Waziri Mkuu

(Majadiliano Yanaendelea)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia sisi Wabunge wote afya njema na kuweza kukutana jioni hii ya leo, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nikupongeze sana wewe mwenyewe binafsi kwa kweli unaongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa sana sana na ni mfano mzuri wa viongozi wanawake katika Taifa letu, hongera sana. Pia upeleke salamu zangu za shukrani kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mheshimiwa Spika kwa kazi nzuri anayoifanya kuliongoza Bunge letu akisaidiana na Wenyeviti wa Bunge, mnafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kuanza kuhitimisha hoja hii bila kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Rais huyu kwa kweli amejipambanua kuwa Rais shupavu anayeaminiwa na kutumainiwa na Watanzania wengi na hasa wanyonge. Kwa kweli nchi yetu imepata jembe, imepata Mheshimiwa Rais mahiri kabisa; na tumeshuhudia kwa muda mfupi maendeleo yamekuwa makubwa sana.

Kwa pamoja naye nimpongeze sana Makamu wa Rais mama yetu Samia Suluhu Hassan, lakini ninaomba kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wangu na watendaji wote ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tunamwona Mheshimiwa Waziri Mkuu kama kioo na kiongozi mahiri anayeweza kutuongoza vyema ndani ya Taasisi yetu. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba upokee shukrani zangu za dhati kwa uongozi wako ambao umetufanikisha, umenifanikisha mimi na wenzangu kufika katika hatua hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mwenye macho haambiwi tazama, hawa viongozi wetu wakubwa niliowataja hapo juu wameweza kulipatia Taifa hili maendeleo makubwa sana kwa kipindi kifupi cha takriban miaka mitatu. Tumeona maendeleo makubwa kwenye Sekta ya Ujenzi, barabara, madaraja, meli, reli, miundombinu ya maji, afya, elimu na mambo mengine mengi kadha wa kadha. Serikali ya Awamu ya Tano chini ya usimamizi wa viongozi hawa imefanya mabadiliko makubwa na jitihada hizi tuziunge mkono Watanzania wote pamoja na sisi Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi ya pekee kumkaribisha ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, dada yangu mpenzi Mheshimiwa Angella Jasmine Mbelwa Kairuki, Waziri mwenye dhamana ya Uwekezaji, nina imani naye kubwa, tutashirikiana sana, ni Waziri mchapakazi, mwanamke wa mfano, Mheshimiwa Angella karibu sana.

Vilevile naomba nichukue nafasi hii kuwatambua na kuwashukuru sana Manaibu wangu wawili; Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde na Mheshimiwa Stella Ikupa, vijana hawa wasomi, wenye weledi, wazalendo, waaminifu na wachapakazi, kwa kweli wamekuwa ni nguzo kubwa sana sana katika kazi zangu na ni mhimili mkubwa kwangu. Nawashukuru sana sana Makatibu Wakuu wote watatu ndani

ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na watendaji mbalimbali ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisahau kabla sijaenda mbele niwashukuru wapigakura wa Jimbo la Peramiho, Mwenyezi Mungu awape baraka kwa kuendelea kunijali na kunipa imani. Nawashukuru pia watoto wangu, vilevile niombe tu kuwaomba Ndugu zangu wana Peramiho, mwezi Novemba mwaka huu habari ni ileile, hakuna kulala na mwakani mwaka 2020 matokeo ni yaleyale hakuna kupunguza. Kwa hiyo nawashukuru sana wapigakura wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusingeweza kufika hatua hii sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu bila juhudi za Kamati ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti Ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Wajumbe wa Kamati wamefanya kazi kubwa; pia Kamati ya UKIMWI inayoongozwa na kaka yangu Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa na dada yangu Mheshimiwa Jasmine Tisekwa na Wajumbe wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Jimbo uko pia ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, hivyo basi, nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa George Simbachawene na Ndugu yangu Mashimba Mashauri Ndaki na Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa na miongozo na ushauri walionipatia. Kazi hii inafanyika kwa kutumia kanuni ya 99(2) ambacho kinaniruhusu sasa kukaa hapa mbele ya meza yako ili mwisho wa hotuba yangu lakini, mwisho wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuombe fedha za kutekeleza majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hivyo basi, nitaanza kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na zile ambazo tutashindwa kuzijibu kwa siku hii ya leo tutazijibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mambo mahususi ambayo pia ni mambo ya jumla, Waheshimiwa Wabunge wengi wameunga mkono na kupongeza sana bajeti yetu,

lakini wakimpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, hata hivyo, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wametilia shaka Ofisi ya Waziri Mkuu na utendaji kazi wake kama kweli umetekeleza majukumu yake sawasawa. Kwanza, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge uwepo wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 52 mpaka Ibara ya 57 ya mwaka 1977; Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiye mratibu na msimamizi mkuu wa utekelezaji wa shughuli na mipango yote ya Serikali, Wizara na Taasisi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwanza ni lazima tujue Mheshimiwa Waziri Mkuu hajajiweka mwenyewe, amewekwa kwa mujibu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, wote tumeshuhudia ni kwa kiasi gani Mheshimiwa Waziri Mkuu huyu amekuwa mchapakazi na ameteteleza majukumu yake kisawa sawa kweli kweli. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameweza kufanya ziara takriban katika mikoa yote nchi nzima ya Tanzania kwenye wilaya zote, kwenye halmashauri zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, suala la msingi hapa siyo idadi ya ziara zilizofanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ziwe ziara fupi ama ziara ndefu ama ziara zilizofanywa na viongozi wa kitaifa; suala la msingi hapa ni yale matokeo ya ziara hizo zilizofanywa na viongozi wakubwa wa kitaifa na Mawaziri na Viongozi wengine wote ndani ya Serikali ya Awamu ya Tano. Jambo la kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu ziara zake na viongozi wengine wa kitaifa zimeweza kurudisha nidhamu na uwajibikaji kwa watumishi wa umma katika nchi nzima ya Tanzania, lakini ziara hizo zimezaa matunda ya kuongezeka kwa kasi ya utekelezaji wa miradi ya huduma za jamii, ikiwemo, elimu, afya, maji, miundombinu ya barabara, umeme na kadhalika na sisi ni mashahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara hizi na Mheshimiwa Waziri Mkuu halali na ziara hizo, zimeweza kuongeza tija kwenye mazao ya kilimo na hasa mazao ya biashara ya kimkakati, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakupongeza sana. Ziara hizo zimeweza kuimarisha ukusanyaji wa mapato ndani ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Nitoe tu wito kwetu sisi

Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote tuanze kulipa kodi kwa hiari bila shuruti. Pia ziara hizi zimeimarisha hali ya usalama, amani na utulivu nchini na kuongeza mshikamano wa kitaifa na umoja wa kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa ushahidi mkubwa, juzi nilikuwa Mkoa wa Songwe kwenye shughuli za Mwenge wa Uhuru na shughuli za Mwenge wa Uhuru mwaka huu zilifanyika kwenye eneo la Mlooo ambalo pale Mheshimiwa Mbunge wake ni wa CHADEMA, lakini wananchi wote waliionesha ushirikiano bila kujali chama, bila kujali itikadi za vyama, dini zao wala makabila. Sasa unaona tu ni kwa namna gani nchi hii amani na utulivu viko sawasawa na wananchi wanaendelea kushikamana pamoja na kujenga umoja wa kitaifa. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuwe mawakala wa amani na utulivu katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako masuala yamezungumzwa hapa kuhusu Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge wengine wanatia shaka na wanalalamika kwamba Bunge hili limeshindwa kutekeleza majukumu yake sawasawa na yako maneno mengi ambayo yamekuwa yakitafsiri kazi na mwenendo mzima wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bunge hili la Kumi na Moja. Hata hivyo, nitaeleza mifano michache ya kuonesha ni kwa kiasi gani Bunge hili limefanya kazi ya kutukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo ninaposimama mbele yako Waheshimiwa Wabunge hawa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wameshaiuliza Serikali yao maswali yasiyopungua 2,653, lakini wameshauliza maswali ya nyongeza yasiyopungua 8,202, ni kazi nzuri imefanywa na Waheshimiwa Wabunge hawa. Maswali hayo yalikuwa yanataka kuwa na uhakika wa uwakilishi wa wananchi katika kufuatilia Mpango wa Taifa wa Maendeleo, bajeti za Serikali, ahadi za viongozi wetu na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka kusema kitu kidogo ukiangalia maswali hayo yote yasiyopungua 10,000 na kitu, ukijumlisha maswali ya nyongeza na maswali ya msingi, yanaonesha hawa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi wametumwa nini na wananchi wao kuja kuliuliza Bunge na kuiuliza Serikali. Maswali haya kipaumbele kiliwekwa kwenye Sekta ya Maji, Umeme, Afya, Elimu na Miundombinu. Imeletwa hoja ndani ya Bunge hili katika bajeti hii kwamba, kipaumbele cha wananchi wa Tanzania ni Katiba pendekezwa, Katiba iliyopendekezwa ambayo inatarajia kubadilisha Katiba tuliyonayo sasa, Waheshimiwa Wabunge wengi wamesisitiza kwamba hicho ndiyo kipaumbele cha wananchi kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuliarifu Bunge lako Tukufu maswali yaliyoulizwa humu ndani ambayo yanatokana na kero za Watanzania, yameletwa na wawakilishi wa Watanzania, Wabunge nimesema hapa yanafika kama maswali 10,000 na kitu, lakini katika maswali hayo 10,000 na kitu maswali yaliyoletwa na Waheshimiwa Wabunge hawa wakiwakilisha mahitaji ya Watanzania yaliyokuwa yanadai Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi ni maswali mawili tu kati ya maswali hayo 10,000 na kitu. Hapa nataka kusema nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu hapa, naendelea kusesitiza kama kweli sisi ni wawakilishi wa wananchi, maswali tunayoyaleta Bungeni yanaashiria mahitaji ya Watanzania, basi mahitaji ya Watanzania kwa sasa ni maji, umeme, afya, elimu, miundombinu, utawala bora, masuala ya wafanyakazi na mambo mengine yanayohusiana na maeneo niliyoyasema hapa. Hivyo basi, suala la Katiba mpya, suala la Katiba pendekezwa, suala la Tume ya Uchaguzi kwamba haitendi haki, kwa maswali yetu sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge, hayo siyo maeneo ya kipaumbele kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili limefanya kazi kubwa, limetunga Sheria mbalimbali, limeridhia mikataba, limetengeneza maazimio mbalimbali mpaka tunapofika siku

hii ya leo Bunge letu Tukufu limeshatunga Sheria mpya zisizopungua 44, lakini zimefanya mabadiliko ya Sheria mbalimbali takribani kama zizopungua 95. Nirudi pale pale, haitoshi kusema tumetunga, tumefanya mabadiliko ya Sheria hizo zote nyingi, tumetunga Sheria hizo zote mpya, hizo Sheria zinaakisi nini katika mahitaji ya Watanzania na nchi nzima ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitasema Sheria chache kama mfano tu wa kazi nzuri iliyofanywa na Bunge letu Tukufu. Moja kwa mfano tumefanya marekebisho ya Sheria ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya Na.5 ya mwaka 2015 (*The Drugs Control Enforcement Act*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uwepo wa Sheria hii; uingizaji na matumizi ya dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania kwa kazi nzuri iliyofanywa na Waheshimiwa Wabunge imekwenda mpaka asilimia 90, udhibiti na uingizaji wa dawa umedhibitiwa kwa asilimia 90 ndani ya Taifa letu. Nashangaa kama kazi hizi nzuri hatutazisema na kujisemea sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge na Bunge letu, basi kwa kweli hatujitendei haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili pia limetunga Sheria ya kutambua kwa mfano, Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi ya Tanzania, kitu ambacho kilikuwa kinaliliwa na Watanzania wengi. Vilevile tumefanya marekebisho ya Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura Na. 200 na Sheria hii imetusaidia sana kudhibiti ufisadi katika Taifa hili, kwa hiyo ni lazima tujipongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria nyingine nzuri ambayo lazima niiseme ni marekebisho ya Sheria ya ununuzi wa umma ambayo imesaidia sana kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa kufanya *procurement* (*The Tanzania National Electronic Procurement System*). Hiyo imepunguza ubadhirifu kwenye manunuzi ya umma, kwa hiyo tunajipongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili limetunga Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Na.9 ya

mwaka 2018 na Sheria hiyo imezaa nini? Inakwenda kuzaa mradi muhimu sana wa ujenzi wa reli, Mtwara - Mbamba Bay - Mchuchuma na Liganga. Sheria hii mpya ya PPP inakwenda kuzaa ujenzi wa reli ya Tanga Mwambani, Arusha, Musoma, ujenzi wa kipande cha barabara ya treni cha Tanga - Arusha, lakini na barabara nyingine kutoka Dar es Salam – Chalinze - Morogoro. Kwa hiyo unaona ni kwa kiasi gani hili Bunge ambalo wengine wanabeza kwamba haliwezi, halijafanya kazi nzuri limewezaji kufanya kazi nzuri kwa kiasi hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengine mazuri tu kwa mfano Azimio la Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe ambalo baadaye litatuletea kuwa na bwawa kubwa la maji la ubia ambalo litazalisha umeme, huduma za viwandani na mahitaji ya nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Bunge hili nimeridhia mkataba wa eGA mkataba kati ya Serikali ya Uganda na Tanzania kuhusu bomba la mafuta, ni Bunge hilihili. Mkataba huo tija yake unaenda kuzaa ajira zisizopungua 10,000 kwa vijana wa Tanzania wakati wa ujenzi, lakini baada ya hapo ajira takriban 1,000 zitapatikana katika kuendesha mradi huo. Mikoa nane, Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, Tanga itanufaika na mradi huo, Wilaya 24 na Vijiji 134 vyote vinanufaika na mradi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niseme kwa kweli Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ukiacha hapo Ofisi ya Waziri Mkuu imeridhia Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Na. 185 wa mwaka 2003 na imeridhia pia Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani (*Maritime Labour Convention*) ya mwaka 2016. Mikataba hii imeweza kuongeza fursa za ajira kwa Mabaharia wa Kitanzania kwenye meli za ndani na meli za nje ya nchi, imeweza kuleta mafunzo fursa za mafunzo ya kitaalam, lakini imeongoza viwango vya kazi za staha kwa Mabaharia wetu. Kwa hiyo, kazi hizo zote zimefanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu uratibu na usimamizi na zimetufikisha mahali pazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo lilizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, ni suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi. Jambo hili lilizungumzwa sana eneo la *local content* kwa maana ya ushiriki wa Watanzania katika kumiliki uchumi wa Taifa lao. Ofisi ya Waziri Mkuu imekamilisha kazi ya msingi sana ya kutengeneza Mwongozo na tunaamini Mwongozo huu utawezesha wadau kutambua wajibu na majukumu yao katika kushiriki kwenye suala zima la kuhakikisha Watanzania na wao wanapata ajira katika miradi yote inayozalishwa katika Taifa letu, lakini vilevile masuala ya ununuzi kama wa bidhaa, ununuzi wa huduma na mambo mengine watanzania pia wanaweza kushiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitisha Mwongozo huo, mwamko ni mkubwa kweli kweli, naomba nitoe mifano michache, wakati tulipomaliza kuandaa Mwongozo huu wa *local content* tumefanya utafiti na tumegundua yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwenye mradi mkubwa wa uwekezaji wa daraja ya Mfugale, daraja la Mfugale lilitoa ajira 616, Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya Mwongozo huo kati ya ajira 616 ajira 589 zilichukuliwa na Watanzania na ilikuwa ni asilimia 95 ya ajira zote. Hiyo haitoshi, lakini ununuzi wa bidhaa mbalimbali ambazo zilitumika katika ujenzi wa huo mradi ulitaka makampuni 28 ndiyo yaende yakafanye ununuzi wa hizo bidhaa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kati ya makampuni hayo 28, makampuni 24 yote yalikuwa ni makampuni ya Watanzania, makampuni ya wazawa na ilikuwa ni asilimia 85 ya makampuni yote. Makampuni matatu tu ndiyo yalikuja kutoka nje na kampuni moja ilikuwa ni ya ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hilo linaendelea kusimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, ni hivyo hivyo hata kwenye barabara za juu za Ubungo, mpaka sasa ajira ya Watanzania ni asilimia 89, kwenye mradi wa *SGR*, asilimia ya Watanzania kwenye ajira katika mradi huo ni asilimia 93, mradi huo wa *SGR* kuna *sub-project* ndani ya mradi huo na ndani

ya mradi hiyo *sub-project* imetoa ajira 1,129 za Watanzania na wageni ni 152 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni mifano michache, tunayo mifano mingi sana ambayo Ofisi ya Waziri Mkuu inafuatilia na tukipata muda tutaiweka hapa. Naomba niwaambie Ofisi ya Waziri Mkuu inafanya kazi kukuza ajira kwa kutumia miradi ya kimkakati ambayo inaendeshwa na Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli na msimamizi wake akiwa ni Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miradi hiyo ni pamoja na *Salender Bridge* na umeme Rufiji. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge hatutakiwi kubeza mambo haya yanayofanywa na Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilizungumzwa sana hapa na Wabunge wachache ilikuwa ni Ofisi ya Msajili wa Vyma vya Siasa. Kumekuwa na hali ya upotoshaji na ninaomba niseme ya upotoshaji kwamba hali ya kisiasa ni tete na ni mbaya na demokrasia inaminywa. Mimi naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba hali ya demokrasia katika nchi yetu ni shwari na ni tulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kabisa kufananisha hali ya siasa na demokrasia katika nchi yetu na mataifa yanayotuzunguka ambayo tumekuwa tukiona na kushuhudia hali jinsi ilivyo huko. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa kama mnaona kuna tatizo hebu tujaribu kusaidiana, kushauriana na kukaa kwenye meza moja kujadiliana na kutatua matatizo yetu kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Hapa tumeshuhudia viongozi wa vyama wakihama kutoka chama kimoja kwenda chama kingine. Kama hali ya kidemokrasia na siasa ingekuwa siyo nzuri, unapata wapi raha ya kuhama kutoka chama kimoja kwenda kingine? Hiyo ni dalili tosha kwamba hali yetu kisiasa hapa ni nzuri. Hiyo ni sababu tosha inamfanya mtu awe huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waitara aligombea mwaka 2015 kupitia CHADEMA leo Mbunge wa Chama cha Mapinduzi ni kwa sababu ya utulivu wa kisiasa na demokrasia. Mheshimiwa Nyalandu alishinda Chama cha Mapinduzi leo amehamia CHADEMA ndiyo mambo hayo hayo ya utulivu. Mheshimiwa Lowassa aligombea Urais kupitia CHADEMA leo amerudi CCM, utulivu huo wa demokrasia. Ndugu yetu Maalim Seif alikuwa CUF kindakindaki lakini leo yuko ACT-Wazalendo, huu ndiyo uhuru. Waheshimiwa Wabunge tuko shwari, anayetaka kuhama ahame, anayetaka kubaki abaki, safari ya siasa na demokrasia inaendelea, taratibu na sheria zifuatwe tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme kama ni masuala ya uchaguzi hakuna chama ambacho kilikataliwa kuweka mgombea na kushiriki kwenye uchaguzi. Hatukuwahi kusema hivyo na tumeendelea kusimamia kuona kwamba kila chama kinaendelea kupata haki. Nirudie kusema kama haki haipatikani vipo vyombo vya sheria vitatusaidia kupata haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mifano, wako watu ambao walihisi kwamba haki zao zimepotea. Nitatoa mifano miwili na mifano hiyo inatupelekea kuthibitisha kwamba ukiona kwenye demokrasia na hali ya siasa nchini haiko sawa nenda Mahakamani utapata haki tu. Mfano wa kwanza, tarehe 22 Februari, 2019 Mheshimiwa Ally Saleh alishinda kesi dhidi ya Bodi ya Wadhamini wa Chama cha CUF kwenye Mahakama Kuu, iliamuliwa na jopo la Majaji na alishida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 18 Machi, 2019, Mheshimiwa Lipumba alishinda na akatambulika yeye ni Mwenyekiti halali wa Chama cha Wananchi (CUF). Haki hii haikupatikana Bungeni wala mahali popote ilipatikana Mahakamani. Leo nimemsikia hapa Mheshimiwa Bwege nampongeza sana amesema sisi CUF sasa ni chama kimoja, wamoja, ni kitu kimoja hatutaki mgogoro lakini kama watu wasingekwenda Mahakamani mgogoro wa Chama cha

Wananchi CUF usingekwisha na mpaka leo ungeendelea kuwa ni mgogoro mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niviombe vyama vya siasa kuendelea kutii Sheria ya Vyama vya Siasa. Lengo la sheria yetu ni kufanya hivi vyama viwe ni taasisi. Kwa mfano, leo Maalim Seif alivyohama kama chama chake cha CUF kisingekuwa taasisi ingekuwa shida lakini kwa sababu ni taasisi ndiyo maana na leo Mheshimiwa Bwege amesema sisi ni CUF moja kwa sababu chama ni taasisi. Sheria hii inataka vyama viwe taasisi na visiwe vyama vya mtu mmoja kwamba mtu mmoja ndiye anakiendesha chama yeye peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunataka vyama hivi kupitia Sheria yetu ya Vyama vya Siasa tuendeleo kuondoa chuki, ubaguzi wa dini, vitendo vya vurugu, kulinda amani na utulivu na ustawi wa Taifa hili, sisi wote ni Watanzania. Niendeleo tu kutoa wito kwa wenzangu wote na viongozi wote wa vyama kutii sheria bila shuruti. Hilo ni jambo zuri na litaendeleo kudumisha umoja wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja Tume ya Taifa ya Uchaguzi siyo huru, watendaji wake siyo huru, muundo wake siyo huru, jambo hili limesemwa sana. Mimi hapa leo ni Yohana Mbatizaji tu naandaa mapito ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenye Wizara yake atakuja kusema zaidi hapa. Nataka niseme jambo moja, Tume ya Uchaguzi imewekwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 74(1) na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 na kifungu cha 4(1) kinaeleza sifa ya Wajumbe wa Tume ya Taifa ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa sifa za Wajumbe wawili tu kwanza kwenye Bunge hili kwa siku ya leo. Mjumbe wa kwanza ni Mwenyekiti wa Tume ya uchaguzi, sifa yake, anatakiwa awe Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa, tena amefanya kazi hiyo ya Ujaji kwa miaka isiyopoungua 15 na Makamu Mwenyekiti wa Tume hivyo hivyo. Wajumbe wa Tume sifa zao zinatokana na kifungu cha 4(1) kwenye Sheria, Sura 343.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijulize kidogo, kwa namna hiyo ya aina na sifa za Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi na hasa hao Viongozi Wakuu (Majaji) na jinsi wanavyopatikana na Majaji hawa nimetoa mfano hapo mbele ndiyo hao hao wamehusika kutoa haki hata kwa vyama ambavyo ni vya upinzani, leo hii tunasemaje kwamba Tume hii ya Uchaguzi siyo Tume halali, haitendi haki? Naomba kwa kweli hebu tujaribu kujiuliza zaidi na tuendeleo kulunga mkono Tume yetu ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko hoja hapa zimesemwa kwamba Wakurugenzi wa Halmashauri wanatuhumiwa wao ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi, walikuwa ni wagombea wa Ubunge kwenye Majimbo kupitia Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo Halmashauri 185 lakini humu ndani kuna Wabunge 392. Ukichukua Wabunge 392 ukasema hawa Wakurugenzi wote ndiyo waligombea ukagawa kwa hiyo 185 ina maana kila Halmashauri ina Wakurugenzi wawili na 1.18, sasa huo uhalali sijui unapatikana wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine kubwa, suala la uumini wa chama kwa kiongozi yoyote liko katika moyo wake na linatawaliwa na Sheria za Utumishi wa Umma. Naomba niseme kidogo, humu ndani ya Bunge letu wako Wabunge walikuwa ni wafanyakazi katika taasisi mbalimbali za Serikali lakini leo ni Wabunge kupitia vyama vya upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iko mifano tu wengine walikuwa mpaka Viongozi Waandamizi, Makatibu wakuu wa Wizara lakini wametoka na leo ni Wabunge wakiwakilisha vyama vingine. Tuna uhakika gani kwa tuhuma hii kwamba hawa Wakurugenzi wote niliowasema 185 eti ni waumini wakubwa wa Chama cha Mapinduzi? Naomba tukubali kwamba Tume ya Uchaguzi inaongozwa na Katiba, Ibara ya 74 na naomba muamini kwamba uchaguzi utakuwa huru na

wa haki kama tulivyoingia, tutaendelea kuingia na Tume itaendelea kutusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Uchaguzi imeshafanya kazi kubwa, imeshafanya uhakiki wa vituo vya kupiga kura 37,814, kati ya vituo hivyo 407 viko Zanzibar. Imeshafanya majaribio ya vifaa vya kuboresha daftari kwenye Wilaya mbili Kisarawe na Morogoro. Imeshafanya maandalizi ya kuhakikisha kwamba kanzidata ya Daftari la Kudumu la Wapiga kura iko tayari na mifumo mingine yote iko tayari. Serikali imeshatenga bajeti kwenye MFUKO MKUU wa Serikali kwa ajili ya kuboresha Daftari vilevile kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge tuko salama, maandalizi yako salama, uchaguzi utafanyika kwa amani, tusiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja moja ililetwa na Mheshimiwa Bulembo kuhusu suala la kibali cha ajira ya wageni kwa mwekezaji mmoja. Naomba hii hoja nisijibu kwa sababu mwaka jana hoja hii ilivyotolewa, eneo ambalo lilitakiwa lifanyiwe kazi na Ofisi ya Waziri Mkuu tumeshalikamilisha. Ombi la kibali cha mwekezaji huyu kuwa raia wa Tanzania limekwenda Uhamiaji, mwenye mamlaka ya kuzungumza jambo hili ni Waziri wa Mambo ya Ndani. Kwa hiyo, naomba niliache nisitolee ufafanuzi suala hili, Waziri wa Mmabo ya Ndani ndiye mwenye mamlaka ya kupitia sheria na kujua huyu mwekezaji kama atapewa uraia ama hawezi kupewa uraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kuhusu namna gani Serikali yetu imeshirikiana na taasisi nyingine kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia programu mbalimbali. Nikuhakikishie kwamba tumekuwa na miradi ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mfano, Mradi wa Miundombinu ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini (*MIVARF*) umefanyakzi nzuri sana Bara na Visiwani. Mradi huu umewafikia wakulima wadogo wakiwemo wafugaji, wavuvi, wafanyakazi na umetoa mikopo kwa watu mbalimabli, umewawezesha wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo

wadogo vijijini, asasi za kifedha, vyama vya msingi vya ushirika na asasi zinazojishughulisha na usindikaji wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo machache nitayasema hapa kama ni matunda ya mradi huu ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambao umeongeza nguvu kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kazi nyingine zilizofanywa na mradi huu ni pamoja na ukarabati wa barabara. Jumla ya kilomita 1,076.6 zimekarabatiwa pande zote mbili za Muungano na zimeweza kurahisisha sana usafirishaji wa mazao ya wakulima. Mradi huu umejenga na kukarabati maghala 35 ambayo yamekwishakukamilika na maghala sita yanaendelea kukarabatiwa. Vilevile wakulima wameweza kuunganishwa na huduma za fedha, zaidi ya shilingi milioni 300 zimekopeshwa kwa wakulima hao kupitia mpango wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili la ukarabati na ujenzi wa maghala, asilimia 40 ya wanawake katika maeneo hayo wameweza kunufaika na kuweka mazao yao katika maghala hayo. Mradi umejenga masoko 16 na matokeo yake programu hii ya ujenzi wa masoko imerahisisha wakulima kuwaunganisha na wafanyabiashara na kuuza mazao yao na Halmashauri zimeweza kuongeza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mradi huu umeweza kutoa ruzuku za mashine na mitambo ya usindikaji wa mazao ili kuongeza thamani ya mazao. Kazi hiyo imefanyika vizuri, mashine takribani 34 zimeweza kusimikwa kwenye maeneo mbalimbali ndani ya nchi yetu ya Tanzania Bara na Visiwani. Kwa hiyo, kazi hiyo pia imefanyika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi umeweza kuwajengea uwezo wazalishaji katika kuzalisha na kutafuta masoko na kuwaunganisha na masoko. Vilevile mradi umeweza kuongeza Mfuko wa Huduma za Fedha Vijijini kupitia asasi za kifedha. Pia mradi kabla haujafungwa umeanzisha Mfuko wa Dhamana yaani *Guarantee Fund* kwa ajili ya ubunifu kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya

Kilimo. Shughuli hii Mheshimiwa Waziri Mkuu ataizundua muda siyo mrefu. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge baada ya uzinduzi wa jambo hili tuungane pamoja ili kuhakikisha kwamba tunaitendea haki programu hii iweze kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba baadhi ya wanachama wa Chama cha *CUF* wamehamia ACT-Wazalendo na kuonekana kwamba Serikali inatumia nguvu kupitia Msajili wa Vyama vya Siasa ili kukikandamiza Chama cha ACT. Waheshimiwa Wabunge, naomba tu niwaambie, Msajili haangalii chama hiki kikubwa, kidogo, kikoje yeje anafuata sheria na utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo tu kusema Waheshimiwa Wabunge, nguvu ya chama pia inapimwa pia na idadi ya Wabunge ndani ya Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania. Sasa sisi wote tutajiliza kama ACT-Wazalendo inaweza ikamtikisa Msajili ama kuitikisa Serikali nzima kwa sababu kiongozi mmoja ama wanachama fulani wamejiunga na Chama cha ACT-Wazalendo. Sisi wote nadhani tunaweza tukatafakari na tukapata majibu labda nisiendeleo kusema zaidi ya hapo na jambo hili liko tu wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimetolewa hoja kuhusu utendaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Naomba kukubaliana na Waheshimiwa Wabunge liko eneo bado halijakaa vizuri kwenye mifuko hii. Naomba kuwahakikishia kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tutajitahidi, tunachotaka ni kuhakikisha michango inafika kwenye mifuko kwa wakati, wastaafu wanafanyiwa uhakiki, ulipaji wa mafao unafanyika kwa wakati, usumbufu kwa wastaafu unaondolewa haraka sana. Wakurugenzi mko hapa naomba mnisikilize vizuri na kwa kweli tutaendelea kuchukua hatua kama haya tunayoendelea kuyaagiza hayatekelezwi na sisi kama Serikali hatutakuwa tayari kubeba dhamana yenu na ninyi ndiyo wenye wajibu wa kuyasimamia haya yote na kuhakikisha kwamba wastaafu hawaendelei kupata shida, wanaendelea kupata maisha mazuri hata baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya Serikali kutumia nguvu nyingi kama Polisi wakati wa kusimamia uchaguzi. Najua iko sheria inasimamiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani atakapokuja Waziri atatoa maelezo. Naamini kabsia suala la msingi hapa ni kufuata sheria bila shuruti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hizi ni nyingi kwell kwell lakini kwa sababu muda unapingana nami, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge maswali yaliyobakia tutayajibu kwa maandishi, nawashukuru sana kwa michango yenu. Naomba kuunga mkono hoja, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi/Vigelegele)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutupa afya njema na kutujalia kukutana tena kwenye Kikao hiki cha Sita cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuhitimisha mjadala huu kuhusu hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziuri Mkuu, taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kutoa shukrani za dhati kwa makundi mbalimbali kama yalivyotamkwa na Mawaziri wote walionitangulia, nami sikusudii kurudia ila nitayapitia kwa makundi lakini wote waamini kuwa natambua mchango wao mkubwa katika kuwezesha Ofisi hii kutimiza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, natoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa michango yao mizuri kwenye hoja ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nawashukuru sana Mheshimiwa Spika, wewe Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kusimamia kwa umahiri mkubwa mwenendo mzima wa majadiliano ya hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, taasisi zake na Mfuko wa Bunge pia kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri waliochangia hoja pamoja na Naibu Mawaziri, Ofisi ya Waziri Mkuu; Makatibu Wakuu; Naibu Makatibu Wakuu; Wakuu wa Idara; Mashirika; Wakala na Taasisi zote za Serikali pamoja na watumishi wengine katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa waliyoifanya na ushrikiano walionipa katika kipindi chote cha mjadala wa bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa pongezi zenu kwa Serikali na kwa michango yenu yenye dhamira ya dhati kabisa, michango yenye hoja za kuboresha mipango na kazi zilizokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha mwaka 2019/2020. Mjadala huu umeendelea kuthibitisha uimara na umakini wa Bunge katika kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba na kuishauri na kuisimamia Serikali kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mjadala huu Waheshimiwa Wabunge 142 walichangia hoja Ofisi ya Waziri Mkuu. Kati ya hao, Waheshimiwa Wabunge 98 walichangia kwa kuzungumza moja kwa moja hapa Bungeni na Waheshimiwa 44 walichangia kwa maandishi. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya Waziri Mkuu. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa muda, naomba uridhie nisiwataje, aidha, majina yao yote yaingizwe katika *Hansard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejibu hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge kupitia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, halikadhalika hoja zilizosalia zitajibiwa kwa maandishi. Vilevile baadhi ya hoja zenu zitatolewa ufafanuzi wa kina na Waheshimiwa Mawaziri

ambao watajipanga vizuri kuzitolea ufafanuzi wa kutosha wakati wa kuwasilisha bajeti zao za kisekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua kuwa kuna msuala muhimu yameibuliwa wakati wa majadiliano haya. Kadhalika mtakubaliana nami kwamba mjadala ulikuwa wa kina na wa kiwango cha juu na umakini unaostahili. Ninakiri kuwa michango ya Waheshimiwa Wabunge na hoja zao zilizoibuliwa zina uhusiano wa moja kwa moja na utendaji wa kazi za Serikali. Aidha, masuala muhimu hususan usafiri wa anga, utalii, bandari, maji, makusanyo ya kodi na uwekezaji ndiyo ambayo kwa kiasi kikubwa yamekuwa ni kitovu cha mjadala mzima wa michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kabla ya kuingia moja kwa moja katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, naomba nitolee ufafanuzi baadhi ya masuala muhimu yaliyoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge kwenye hoja hii ya Waziri Mkuu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ilikuwa suala la bniashara na uwekezaji. Serikali imeendelea kujenga mazingira wezeshi na rahisi ya kufanya biashara na uwekezaji bila kuathiri ubora na viwango, sambasamba na kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Hata hivyo, licha ya azma hiyo nzuri ya Serikali, bado kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara na wawekezaji kama walivyoeleza Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ufafanuzi kwa yale masuala yaliyogusa vyombo vya udhibiti kama vile Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*), Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*), Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka nyingine za udhibiti pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA*, *OSHA*, *BRELA*, Taasisi ya Mionzi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wafanyabiashara kuhusu

Mamlaka hizi na namna ya utendaji kazi wake, miongoni mwa kero hizo ni mchakato wa muda mrefu wa kupata leseni za biashara, gharama za usajiri wa bidhaa zinazotowwa na *TFDA*, suala la viwango vya *TBS*, madai ya kuwepo kwa unyanyasaji unaofanywa na *TRA* kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi dhidi ya wafanyabiashara, umbali wa Makao Makuu wa Maabara za Taasisi za Mionzi na eneo wanalofanyia kazi kama vile bandari, viwanja vya ndege na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa ni hatua ya kuondoa kero hizo, katika nyakati tofauti Viongozi wetu wa Kitaifa wamekuwa wakichukua hatua za makusudi kuzungumza na wafanyabiashara pamoja na wawekezaji. Mazungumzo haya yamekuwa yakijielekeza zaidi katika kupokea kero na kuzitafutia ufumbuzi kero hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ameweza kukutana na wadau mbalimbali wa biashara na uwekezaji zikiwemo taasisi za Serikali, wafanyabiashara wakubwa na wadogo, wachimbaji wa madini na wakulima katika nyakati tofauti. Aidha, nami nimekutana na wawakilishi wa wafanyabiashara wadogo na wafanyabiashara wa kati tarehe 28 Februari, 2019 Jijini Dar es Salaam. Kadhalika tarehe 6 Machi, 2019 nilitembelea Shirika la Viwango vya Taifa Tanzania na Mamlaka ya Chakula na Dawa na kufanya mazungumzo na viongozi na watendaji wa taasisi hizo akiwemo Mkemia Mkuu wa Serikali na baadaye tarehe 16 Machi 2019 tulikutana tena kwa pamoja na *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazungumzo hayo, nilielekeza viongozi na watendaji wa mamlaka hizo za udhibiti kutekeleza majukumu yao kwa uaminifu, uadilifu na weledi wa hali juu huku wakijiepusha na vitendo vya rushwa, kuhamisha mafaili ya ofisi, ofisi za wafanyabiashara na kukusanya komputa na kuondoka nazo. Badala yake watumie nafasi hiyo kuwaelimisha wafanyabiashara ili kuwafahamisha nini kinabadilika? Nini kinatakiwa? Hasa katika kufuata utaratibu, kanuni na sheria na miongozo mbalimbali inayohusu biashara na uwekezaji na kuondoa

urasimu na mianya ya rushwa katika kutekeleza majukumu ya taasisi hizo kwa kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ambayo imeonekana kuwa kikwazo cha biashara na uwekezaji ni mwingiliano wa majukumu ya taasisi hizo. Kwa mfano, uwepo wa majukumu yenye kufanana kwa *TFDA* na *TBS* na Mkemia Mkuu, Bodi ya Maziwa, Bodi ya Nyama, Baraza la Mifugo, *EWURA*, *SUMATRA* na *TANROADS* ni kikwazo kikubwa katika kurahisisha mazingira ya kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari nimeshatoa maelekezo na yameanza kufanyiwa kazi kwa Waheshimiwa Mawaziri wa Sekta hizo zote chini ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera na Uratibu, kwamba wakae pamoja kupitia sheria na mganyo wa majukumu yao kwenye taasisi zao za udhibiti ili kuondoa mkanganyiko uliopo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Mapato na Taasisi zake, nawaelekeza tena Mawaziri husika kuhakikisha kuwa wakuu wa taasisi hizo wanaendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kuzingatia sheria bila kuwabughuzi wafanyabiashara na wawekezaji hapa nchini. Kwa upande wa wawekezaji, nao pia natoa rai wahakikishe kuwa wanazingatia sheria na kanuni ili pande zote ziweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuzisisitiza mamlaka hizi za udhibiti kupanua wigo wa shughuli zao hususan maeneo ya mipakani, kuimarisha matumizi ya kielektroniki ili kuondoa urasimu kukabiliana na mianya ya rushwa na hasa katika utoaji huduma zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo limezungumza upande wa Uhamiaji. Kama ambavyo nimeeleza kwenye hotuba yangu, Serikali pia imeendelea kuboresha taratibu za Idara ya Uhamiaji kwa kutekeleza awamu ya pili ya mradi wahamiaji wa mtandao. Mradi huo wenye kuhusisha utoaji

wa VISA na vibali vya ukazi vya kielektroniki utarahisisha zaidi shughuli za utalii, biashara na uwekezaji hapa nchini kwa kuondoa urasimu hususan muda mrefu unaotumika kufanya maombi hayo ili kupata vibali hivyo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hatua thabiti za kuvutia uwekezaji zinazochukuliwa na Serikali, haikunishangaza kwa Tanzania kuibuka kinara katika kuvutia uwekezaji miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki ambapo tulivutia mitaji yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.18. Hii ni kwa mujibu wa *report* ya mwaka 2018 ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya biashara na maendeleo. Tunaendelea kuvutia mitaji zaidi ya uwekezaji na ninaamini tutafikia malengo tunayokusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuwavutia wawekezaji kujenga viwanda nchini hususan vyenye kutumia nguvu kazi kubwa na malighafi zinazozalishwa hapa nchini kwa lengo la kutengeneza ajira, kuongeza tija kwenye uzalishaji wa bidhaa na huduma na kuipatia Serikali fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Sekta ya Utalii. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na kuipongeza Serikali kwa hatua za kuboresha Sekta ya Utalii hususan ununuzi wa ndege mpya, pia wametoa mapendekezo ya ndege hizo kufanya safari katika nchi za ukanda wa Maziwa Makuu na maeneo ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuwafamisha Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali itaendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Utalii. Uboreshaji wa usafiri wa anga unakwenda sambamba na utangazaji na utajiri mkubwa kwa vivutio vya utalii tulivyonavyo kama vile, uoto wa asili, wanyama, fukwe, malikale, tamaduni za makabila yetu yasiyopungua 120 na vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutoa msukumo kufungua kanda za Kusini katika maendeleo ya

utalii kwa kuviendeleza vivutio vya utalii vilivyopo kwenye ukanda huo ili vichangie kukamilisha ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi. *(Makofi)*

Aidha, Serikali inaendelea na mkakati wa kuunganisha na kufungua ukanda wa ziwa kwa kuendeleza Mapori ya Akiba maarufu kama BBK, yaani Biharamulo, Burigi na Kimisi pamoja na Ibanda na Rumanyika kuwa Hifadhi za Taifa. Mpaka sasa takribani shilingi bilioni nne zimeshatumika kuimarisha ulinzi, kuainisha mipaka, kujenga miundombinu ya utalii, kuweka mifumo ya kielektroniki ya utawala na ya kukusanya mapato pamoja na kuendeleza vivutio vya utalii vinavyopatikana kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, kuimarika kwa usafiri wa anga nako kumeendelea kuchangia vyema ukuaji wa Sekta ya Utalii nchini. Mathalan baada ya kuwasili kwa ndege zetu kubwa tatu zinazojumuisha *Boing 787 Dreamliner* na nyingine mbili aina ya *Air Bus A220-300*. Shirika la Ndege la Tanzania sasa limeanza safari za kwenda nchi jirani za Zambia na Zimbabwe. Halikadhalika, muda siyo mrefu shirika hilo litaanza safari za masafa ya mbali zitakazohusisha nchi za China, India na Thailand. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuipongeza Bodi ya Utalii nchini ambayo mwezi Novemba, 2018 iliingia makubaliano na kampuni ya *Touch Road International Holding Group* kwa ajili ya kutekeleza mradi huo uitwao *Tour Africa the New Horizon*. Mradi huo utasaidia kuongeza idadi ya watalii kutoka China ambapo kwa kuanzia tunatarajia kupokea watalii 10,000 kwa mwaka 2019. Aidha, mwezi Mei mwaka huu Tanzania inategemea kupokea watalii wasiopungua 300 kutoka nchini humo na tayari tumeshapokea watalii 336 kutoka nchi mbalimbali walioingia wiki iliyopita kwa njia ya meli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya *Touch Road* inayo nia pia ya kufanya uwekezaji mpya kwenye ujenzi wa hoteli, maeneo ya viwanda na kanda maalum ya uchumi wa makazi. Napenda kutoa wito kwa mamlaka na wadau

mbalimbali wanaojihusisha na sekta hii muhimu ya utalii, kuliangalia vyema suala la viwango vya gharama za malazi kwenye mahoteli ya kitalii pamoja na tozo mbalimbali za kuingia kwenye maeneo yenye vivutio vya utalii. Kumekuwepo na malalamiko kuwa gharama zetu kwenye maeneo hayo ziko juu na kwa hiyo, zinasababisha utalii wa ndani kupungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuisitiza pia kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wote kwa ujumla kuenzi utalii wa ndani. Aidha, Mamlaka za Utalii zote zitoe vivutio mbalimbali kwa watalii wa ndani ili nao wapate fursa kujionea utajiri wa maliasili tulizonazo hasa uoto wa asili, wanyama, fukwe, malikale na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumzia upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali nchini sambamba na kuipongeza Serikali, lakini pia walikosoa utekelezaji na ubora wa baadhi ya miradi ya maji na vilevile wameonesha kutorodhishwa sana kwa baadhi ya maeneo kwa sababu hayajafikiwa na miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na usambazaji wa maji licha ya changamoto hizi. Hata hivyo, Serikali inachukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa miradi yote ya maji inayotekelezwa inatoa matokeo yanayokusudiwa. Kwa kuanzia Mheshimiwa Rais aliunda Tume Maalum ili kupitia, kufanya tathmini na kutoa mapendekezo juu ya hatua za haraka zinazostahili kuchukuliwa. Hatua hizo zitalenga hasa kuhakikisha kuwa thamani ya fedha ya miradi hiyo inayosambazwa mikoani kote na Wilayani inapatikana na kuleta tija kwenye maeneo miradi hiyo inapotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa tumehakiki madai ya Wakandarasi waliotekeleza miradi hiyo na kulipa shilingi bilioni 138. Aidha, hivi karibuni tutapata fedha nyingine kiasi cha shilingi bilioni 44. Sasa naielekeza Wizara husika ihakikishe kuwa Wakandarasi na Watendaji wa Serikali kufuatilia ufanisi wao kuwa unakuwa wa kiwango cha kuridhisha wakati wote.

Waheshimiwa Wabunge endeleeni kutoa ushauri kwenye Sekta ya Maji. Malengo yetu ni kuhakikisha kwamba tunafikia mpaka ngazi ya vijiji ili wananchi wote waweze kunufaika kwa kupata maji safi na safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie maji na usafi wa mazingira. Changamoto nyingine katika eneo la maji ni uharibifu wa mazingira ambao umeshika kasi kubwa. Ni lazima hatua za haraka zichukuliwe ili kuiepusha nchi yetu na janga hili. Katika kuhakikisha kuwa tunaondokana na janga hili, Bunge lilipitisha Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019 yenye lengo la kuimarisha mfumo wa utoaji huduma za maji na usafi wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, sheria hiyo itaongeza uwajibikaji katika utoaji wa huduma ya maji, utaimarisha ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji. Kufuatia kuundwa kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*RUWASA*) na kuleta uendelevu kwa miradi ya maji vijijini, nawaagiza viongozi wote kuanzia ngazi ya vijiji kuchukua hatua za makusudi katika kusimamia utunzaji wa vyanzo vya maji na kudhibiti vitendo vya uharibifu wa mazingira. *(Makofi)*

Aidha, viongozi na watendaji watakaobainika kutosimamia ipasavyo sheria husika, hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono jitihada hizi za Serikali ili kuweza kudhibiti uhalibifu wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba mnamo tarehe 5 Mei, mwaka 2016 Serikali ilitoa kauli ndani ya Bunge lako Tukufu kuhusu dhamira ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki hapa nchini. Kuanzia wakati huo hadi sasa Serikali imekuwa ikifanya maandalizi ya kutimiza dhamira hiyo. Hivi karibuni nimemwagiza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, anayesimamia masuala ya Mazingira ikiwemo kuzungumza na wadau mbalimbali, ikiwemo wenye viwanda vya kutengeneza mifuko ya plastiki

kwa ajili ya kuhakikisha kwamba jambo hili linatekelezwa kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya plastiki nchini yameendelea kuleta madhara makubwa ikiwemo vifo vya mifugo kwa kula plastiki, kuziba kwa mifereji mingi nchini, uchafuzi wa mazingira na kushindikana kwa kuoza taka kwenye vituo vya kukusanya taka. Kuanzia tarehe 1 Juni, 2019 itakuwa ni marufuku kutengeneza, kuingiza, kuuza na kutumia mifuko ya plastiki kwa ajili ya kubebea bidhaa za aina yoyote. *(Makofi)*

(Hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu Alikohoa)

WAZIRI MKUU: Na washindwe! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie tena. Kuanzia tarehe 1 Juni, 2019 itakuwa ni marufuku kutengeneza, kuingiza, kuuza na kutumia mifuko ya plastiki kwa ajili ya kubebea bidhaa za aina yoyote. Aidha, ifikapo tarehe 31 mwezi Mei mwaka huu 2019 itakuwa ni mwisho wa kutumia mifuko ya plastiki kwa ajili ya kubebea bidhaa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia sasa tunatoa fursa ya viwanda kubadilisha teknolojia yao, wauzaji kuondoa mizigo yao au kumaliza kuiuza yote na kadhalika. Ofisi ya Waziri wa Nchi, Makamu wa Rais, itajiandaa kutumia kanuni chini ya Sheria ya Mazingira ili kulifanya katazo hili kuwa na nguvu ya kisheria. Tunachukua hatua hii ili kulinda afya ya jamii, wanyama, mazingira na miundombinu dhidi ya athari kubwa zinazotokana na taka za plastiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchukua hatua hizi, tumetambua kwamba kuna baadhi ya bidhaa lazima zifungwe kwenye vifungashio vya plastiki. Vifungashio kwa bidhaa hizo havitapigwa marufuku kwa sasa. Kwa msingi huo, katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais yatatolewa maelekezo ya kina kuhusu katazo la vifungashio

Ia aina hii hasa katika maeneo ya uzalishaji wa viwanda, Sekta ya Afya na Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yetu kuwa utaratibu huu pamoja na kutunza mazingira, utatoa fursa kutengeneza ajira nyingi, hususan za watu wa chini kupitia utengenezaji wa mifuko mbadala ya plastiki pamoja na kutumia kikamilifu fursa ya viwanda vya karatasi vilivyopo nchini kikiwemo kiwanda cha Mgololo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia makusanyo ya kodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Waheshimiwa Wabunge wameainisha maeneo kadhaa ambayo yanalenga kuboresha utendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Maeneo hayo ni pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuongeza wigo wa kulipa kodi na maeneo haya kuweka viwango himilivu ili kuchochea walipa kodi wengine wengi zaidi kulipa kwa hiyari na kujenga mazingira rafiki kwa walipa kodi. Serikali imepokea ushauri huo na itaufanyia kazi, ili kuondoa kero kwa walipa kodi nchini. Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli amefanya mabadiliko makubwa na kutoa maelekezo mahususi, hivyo nawaelekeza watendaji wote kuzingatia maelekezo wanayopewa na kuacha tabia ya kutoa visingizio vinavyokwamisha utekelezaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa nimetoa maelezo haya ya msingi, sasa nijielekeze kwenye baadhi ya hoja ambazo zimetolewa. Ziko hoja ambazo tayari zimeelezwa na Waheshimiwa Mawaziri na Waziri wa Nchi alipokuja hapa mbele, hivyo nitapitia kwa haraka kwenye maeneo yale ya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(13) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba nitumie nafasi hii kujibu na kufafanua baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza, Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kwamba, vipaumbele vyake vinalenga

kuboresha na kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa lengo la kuvutia wawekezaji wa hapa ndani na nje ya nchi. Hatua ambayo itatengeneza ajira kwa wananchi wengi na kuongeza fursa za biashara na mapato kwa wananchi na Taifa kwa ujumla wake. Serikali imepokea ushauri wa Kamati. Aidha, moja ya vipaumbele vya mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano ni kuimarisha mazingira ya biashara ya uwekezaji, ili kuwezesha uanzishaji na ukuaji wa biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza hilo Serikali itaendelea kuweka kipaumbele kwenye kuimarisha miundombinu wezeshi kama vile usafiri kwenye maeneo ya ujenzi wa reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari, lakini pia huduma za umeme na maji ili kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara na uwekezaji kwa wawekezaji kwa ujumla. Aidha, Serikali itaimarisha upatikanaji wa ardhi, kuendeleza maeneo maalum ya uwekezaji (*Special Economic Zones*) na kutekeleza *programs* za kuboresha mazingira ya uwekezaji, ikiwa ni pamoja na mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa mazingira ya biashara nchini (*Blue Print for Regulatory Reforms to Improve Business Environments*). Vilevile Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano na majadiliano na sekta binafsi kupitia Baraza la Biashara la Taifa pamoja na mikutano ya wadau wa sekta mbalimbali wa ngazi za Kitaifa, mikoa na wilaya ambapo changamoto zinazobainishwa kwenye vikao hivyo ziweze kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya pili ya Serikali ilete Bungeni haraka iwezekanavyo Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 na marekebisho yake ambapo kwa mambo mengine itawezesha, moja kuunda Tume Huru ya Uchaguzi (*Tanzania Independent Electoral Commission*) na yale yote ambayo pia yanaingia kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni Idara huru inayojitegemea na inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

ya mwaka 1977. Tume hiyo inatekeleza majukumu yake kwa uhuru bila kuingiliwa na mtu au chombo chochote kwa mujibu wa Ibara ya 74(7) na Ibara ya 74(11) ya Katiba. Aidha, ni vema ikafahamika kuwa uteuzi wa Wajumbe wa Tume hufanywa kwa kuzingatia matakwa ya Katiba. Hivyo, njia inayotumika kuwateua Wajumbe au Mkurugenzi wa Uchaguzi haiathiri uhuru wa tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hoja ambayo pia, imezungumzwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi alipokuja hapa, uchaguzi wa Serikali za mitaa kwamba, uchaguzi wa Serikali za Mitaa usisimamiwe na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na badala yake usimamiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Serikali ishughulikie jambo hili mapema ili kuepuka usumbufu unaoweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa imani kubwa mnayoonesha kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo ni huru juu ya utekelezaji wa majukumu yake na kuona umuhimu wa kuiongezea jukumu la kusimamia uchaguzi wa Serikali zamitaa.

Hata hivyo, majukumu ya tume yameainishwa katika Ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni pamoja na kusimamia uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivyo, jukumu la kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa si miongoni mwa majukumu ya tume kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya nne ambayo pia imezungumzwa kwa upana wake juu ya Sheria ya Vyama vya Siasa ambayo imeharamisha shughuli za siasa nchini na kuzifanya kuwa kosa la jinai. Hii inadhihirika kutokana na sheria hii kuwa na vifungu vingi vinavyotoa adhabu ya jamii, kifungo au vyote kwa pamoja kwa wanasiasa ili msajili na Serikali na vyombo vyake hakuna kifungu hata kimoja ambacho kinawagusa kama wakikiuka utekelezwaji wa sheria ya namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 3 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeruhusu uwepo wa vyama vingi vya siasa hapa nchini, hivyo hakuna sheria ya nchi inayoweza kufanya siasa kuwa kosa la jinai. Adhabu zilizopo katika Sheria ya Vyama vya Siasa zinaendana na aina ya kosa linalotolewa kwa mujibu wa sheria iliyopitishwa na Bunge. Aidha, Kifungu cha 20(2) cha Sheria ya Vyama vya Siasa kinamruhusu mtu yeyote ambaye anadhani Msajili wa Vyama vya Siasa amekiuka Sheria ya Vyama vya Siasa kwenda Mahakamani kupata haki yake. Serikali inavitaka vyama vya siasa na taasisi mbalimbali kuzingatia sheria pale zinapotekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tano ilikuwa ni kilimo cha zao la pamba nchini kwamba, bado hatujatumia zao la pamba vizuri katika kuongeza pato la Taifa na kuinua maisha ya Watanzania. Serikali ijizatiti kusimamia uwekezaji kwenye kilimo cha zao la pamba kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa mkakati wa viwanda vya nguo hapa nchini ili kufikia malengo na kuwa na Taifa lenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. Sekta ya pamba na mnyororo wake wote wa thamani ni sekta ya kipaumbele ambayo pamoja na kuwahakikishia soko wakulima na kuongeza kipato chao uwekezaji katika viwanda vya nguo unatengeneza ajira nyingi kwa vijana, hivyo kuinua kipato chao na kuboresha maisha ya watu walio wengi. Kwa kutumia mkakati wa kuzalisha nguo na mavazi mbalimbali (*cotton to clothing*) Serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa viwanda kwa kutumia teknolojia za kisasa na kutengeneza nguo kuanzia kuchakata pamba hadi nguo kwa kuhakikisha kuwa taratibu zote zinafanyika nchini na msisitizo uwe ni utengenezaji wa nyuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya sita, Serikali itumie fursa ya uwepo wa mifugo mingi nchini kwa kuwekeza katika viwanda vya kuchakata nyama ili rasilimali ya mifugo iweze kunufaisha Taifa badala ya nchi jirani kunufaika na mazao ya mifugo inayotoka hapa nchini kwetu. Serikali inaendelea

na jitihada za kuvutia uwekezaji katika mzao ya mifugo kwa ushirikiano na wawekezaji binafsi wa ndani na nje kwa ranchi za Taifa. Mfano ni uendelezaji wa ranchi ya Taifa ya Ruvu ambapo Serikali imeingia makubaliano ya awali ya kujenga machinjio makubwa ya kisasa, unenepeshaji wa mifugo na ufungashaji wa nyama. Aidha, kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018 Serikali imeweka vivutio vya kikodi kwa kupunguza kodi ya makampuni kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 20 kwa viwanda na bidhaa za ngozi, pamoja na kuondolewa kwa kodi ya ongezeko la thamani kwa mitambo na vifaa vya viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya saba, Serikali iangalie namna ya kuondokana na urasimu katika kuwezesha jitihada za wawekezaji, hasa kwa wageni wanaokuja na mitaji yao kuja kuwekeza hapa nchini. Ili kuondokana na urasimu, Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1977 iliunda kituo cha uwekezaji hapa Tanzania kitiwacho *TIC* ambapo huduma mbalimbali ikiwemo usajili, utoaji wa vibali mbalimbali na leseni na kwa ajili ya uwekezaji unafanyika katika eneo moja (*One Stop Facilitation Centre*) ambapo taasisi zilizokuwepo awali ni pamoja na *TRA*, *Ardhi*, *Brela*, *Uhamiaji* na *Kazi*, ndizo pekee zilikuwa zinapatikana kwenye kituo hicho. Kwa sasa Serikali imeongeza taasisi nyingine ikiwemo *OSHA*, *NEMC*, *TFDA*, *TBS*, *TANESCO* na *NIDA*, hivyo vyote vinafanya jumla ya taasisi 11 kutoa huduma katika eneo moja pale kwenye kituo chetu cha uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imeendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa njia ya mtandao ili kupunguza muda na gharama katika kupata huduma kwa wawekezaji wetu hapa nchini. Vilevile Serikali imeunda Kamati ya Taifa inayojumuisha wakuu wote wa taasisi zinazotoa huduma kwa wawekezaji kwa lengo la kujadili maeneo ya kuboresha na urahisishaji wa upatikanaji wa vibali na leseni. Serikali imeongeza huduma za uwekezaji kwa kuanzisha Ofisi za *TIC* katika kanda zote hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nane ilikuwa Serikali ifanye tathmini na kuangalia vikwazo vinavyokwamisha

harakati za uwekezaji nchini, ikiwa ni pamoja na kutunga sheria mpya, kurekebisha baadhi ya sheria, ili kuendana na mahitaji ya *Blue Print*. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi mwaka 2017 ilifanya tathmini ya kina na kuandaa *Blue Print* ambayo imebainisha masuala yote muhimu yanayokwamisha uwekezaji na kuainisha maeneo yote muhimu yanayohitaji kurekebishwa ikiwemo sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia uwekezaji hapa nchini na kwa kila taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hatua hiyo huduma zimeainishwa kwa kuanzisha mifumo ya kielektroniki ambapo wawekezaji sasa wataweza kufanya maombi ya vibali mbalimbali wakiwa popote bila kulazimika kufika kituoni kwetu. Mifumo hii itaondoa urasimu na kuhakikisha utoaji wa vyeti vya uwekezaji, leseni na vibali mbalimbali na hatua hizi zitapunguza gharama na muda wa mwekezaji kufuatilia vibali na leseni kupitia katika kila taasisi na badala yake anavipata kwenye eneo moja. Aidha, Kituo cha Uwekezaji Tanzania hivi sasa kina ofisi saba za kanda, Mwanza, Dodoma, Moshi, Kigoma, Mtwara, Mbeya na Dar-es-Salaam, lengo ni kuendelea kusogeza huduma karibu kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tisa, ni juu ya hali ya chakula kwa wananchi na wakulima wa Musoma kwamba, sio nzuri kutokana na mvua kutonyesha za kutosha na Serikali ijiandae kuwapelekea chakula na msaada wa njaa. Serikali inatambua uwepo wa mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha upungufu wa mvua katika maeneo mbalimbali nchini. Hali hii ilitabiriwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kipindi kilichoanza mwezi Novemba, 2018 hadi Juni mpaka mwaka 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia utabiri huo mamlaka za mikoa na wilaya husika zimeelekezwa kuchukua hatua za tahadhari, ikiwemo utunzani wa chakula, upandaji wa mazao ya muda mfupi na yanayostahamili ukame. Hivyo, nitoe wito kwa maeneo yanayopata mvua kwa sasa ni vyema kutumia vizuri mvua hizi zinazopatikana kwa kulima mazao yanayostahili, yasiyohitaji kiasi kikubwa cha mvua ili

kuyawezesha mazao hayo kuweza kuiva na hatimaye kujihakikishia kuwa tunakuwa na kiwango kizuri ha chakula hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa nimetoa hoja hizi, naomba kuhitimisha hoja yangu kwa kueleza kuwa nimesikiliza na kufuatilia kwa umakini sana mjadala kuhusu Hotuba ya Waziri Mkuu. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 mpaka Mwaka 2020 inatekelezeka vema chini ya jemadari Rais wetu mpendwa, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mwelekeo wetu ni mzuri, suala la msingi lililopo mbele yetu ni kuongeza umakini na kasi kwa malengo yote tuliyojiwekea ambayo dhamira ni kuwaletea maendeleo wananchi wote kwa Taifa na kwa ujumla yaweze kufikiwa na yaweze kuwafikia wananchi wote popote walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 7 Aprili, mwaka huu wa 2019 tuliadhimisha miaka 47 ya kumbukumbu ya kifo cha Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa kwanza wa Zanzibar na tarehe 12 mwezi huu, kwa maana ya keshokutwa tutaadhimisha miaka 35 ya kumbukumbu ya kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu, hayati Edward Moringe Sokoine. Watanzania tutaendelea kuwakumbuka viongozi hao kwa mchango wao mkubwa katika kuleta mabadiliko chanya hapa nchini, kutetea wanyonge na kudumisha misingi ya amani, mshikamano na umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na misingi imara iliyoachwa na viongozi tunaoendelea kuwakumbuka, Tanzania imeendelea kung'ara duniani katika eneo la amani na usalama. Kwa mfano, *report ya The Global Peace Index 2018*, inaonesha kuwa Tanzania imeendelea kuwa kinara wa amani kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na pia tunayapiku pia hata mataifa makubwa ambayo pia yenyewe yanasimamia amani kwa nchi changa. Amani tuliyonayo ni hazina kubwa tuliyoachiwa na viongozi wetu hawa. Wito wangu ni kuwa tuienzi na kuilinda amani ya nchi yetu ikiwa ni sehemu ya kuenzi jitihada za waasisi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawakumbusha Waheshimiwa Mawaziri, viongozi wateule wa Serikali na watendaji wote kuwa, wananchi wamejenga imani nasi baada ya Rais kutupa majukumu ya kumsaidia, hivyo kila mmoja wetu hana budi kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Tufanye kazi kwa bidii, tuache mazoea ya kiurasimu, tuchape kazi kwa maslahi ya Taifa na kwa maslahi ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa namalizia kufafanua hoja zangu napenda kuwakumbusha tena Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kuwa zimebaki siku tano tu kufikia tarehe 14 Aprili, mwaka 2019, siku ambayo Taifa letu litaweka historia kupitia timu yetu ya vijana, *Serengeti Boys*, itakayozindua mashindano ya mpira wa miguu, maarufu *AFCON Under 17*, dhidi ya timu ya Nigeria ikitafuta tiketi ya kucheza Fainali za Kombe la Dunia. Uzinduzi wa michezo hiyo utakaofanyika Uwanja wa Taifa tarehe 14 Aprili, siku ya Jumapili ni muhimu kwetu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwenda Uwanja wa Taifa kushuhudia na kuwashangilia vijana wetu ili waweze kushinda vizuri. Timu yetu imeandaliwa vizuri, tunahitaji kushinda michezo miwili tu ili tuweze kucheza Kombe la Dunia, sasa ni zamu yetu, Mungu ibariki *Serengeti Boys*, Mungu ibariki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme haya mawili yafuatayo: Wakristo duniani kote wanaendelea na kipindi cha toba ambacho ni muhimu katika imani kuelekea siku ya sikukuu ya pasaka. Niwasihi kuwa maisha mnayoishi katika kipindi hiki yalingane na maisha yetu ya kila siku. Kadhalika, kuelekea kumalizika kwa kipindi hicho niwatakie Watanzania wote heri na baraka ya Pasaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani nao unatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwezi Mei mwaka huu wa 2019. Napenda kutumia fursa hii pia, kuwatakia Waislam wote nchini mfungo mwema na wenye mafanikio, ili kila atakayefanya ibada hiyo aifanye kikamilifu na kama inavyoagizwa katika *Quran* Tukufu ili tuweze kufuata misingi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zilizo chini yake na Mfuko wa Bunge, kama nilivyowasilisha katika hoja yangu ya tarehe 4 mwezi huu wa Aprili, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Tunaendelea sasa na utaratibu wetu. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Tunaanza na Kitabu cha Pili.

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu

Kif. 1001 – *Administration and
HR Management*..... Sh.4,680,572,984/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Fungu 37, hili ndilo fungu lenye mshahara. Nimeletewa majina hapa kwa kadiri ya Kanuni zetu zinavyotaka ya Waheshimiwa Wabunge ambao wanataka kujadili kuhusu Fungu hili. Tutaanza na Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi lakini nimpongeze sana

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ya majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kupata ufafanuzi, kumekuwa na ukinzani kati ya Sheria ya Uwekezaji na Kodi. Serikali inatoa tamko gani hasa ukizingatia wako wawekezaji ambao wamepata vivutio kwa ajili ya miradi ya uwekezaji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji).

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Ritta Kabati kuhusiana na kukinzana kwa Sheria ya Uwekezaji na Sheria za Kodi, kwanza napenda kusema ni kweli na ukiangalia katika kifungu cha 20 ambacho kinaanzisha Kamati ya Uwekezaji wa Taifa (*NISC*) kimsingi vipo vivutio ambavyo wawekezaji mahiri na wawekezaji mahiri maalum wanapewa lakini kwenye sheria imetamka tu ile Kamati ya Uwekezaji lakini vivutio vyenyewe kimoja kimoja vile maalum havijaanishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo ipo na tumekuwa tukifanya mashauriano na Wizara ya Fedha ili kuona ni kwa namna gani kama mkakati wa muda mfupi tunaweza kutanzua vivutio hivyo ambavyo wawekezaji mahiri na wawekezaji mahiri maalum wamepewa. Kwa mkakati wa muda mrefu tutafanya marekebisho katika Sheria ya Uwekezaji ili kuhakikisha kwamba sasa vivutio badala ya kutolewa na ile Kamati ya Uwekezaji ya Taifa ya *NISC* basi vibainishwe moja kwa moja katika Sheria ya Uwekezaji lakini pia katika Sheria ya Kodi. Naamini kwa kufanya hivyo basi changamoto hii itaweza kutatuliwa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ritta Kabati naona ameridhika na maelezo, Mheshimiwa John John Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Ofisi hii ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Freeman

Mbowe alieleza kwa kirefu sana katika hotuba ile juu ya haja ya kuwa na Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi na sababu za kimsingi za kuwa na Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi. Alikwenda mbele zaidi katika hotuba yake kuambatanisha andiko refu lililoandikwa na Msomi wa Sheria Prof. Abdallah Safari ambalo limechambua miundo ya nchi mbalimbali ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kuhitimisha juu ya haja ya kuwa na Tume huru ya Uchaguzi na Tume gani inatakiwa ili ionekane kuwa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majumuisho Mheshimiwa Waziri wa Nchi na Mheshimiwa Waziri Mkuu wote wawili wametoa maelezo ambayo yamekataa hoja ya kuleta marekebisho ya Katiba na ya kisheria ili kuwe na Tume Huru ya Uchaguzi. Sijaridhika na majibu na nitaomba ufafanuzi wa nyongeza na iwapo ufafanuzi huo wa nyongeza hautaridhisha, nitaomba nipewe nafasi ya kutoa hoja ya kuondoa shilingi ili jambo hili lijadiliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba Tume iliyopo sio huru maana hoja ya Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi ni kwamba Tume ipo huru kwa sababu eti Ibara ya 74, 7, 10 na 14 zimeweka misingi ya Tume kuwa huru, jambo ambalo sio kweli. Wakati wa mchakato wa Katiba, Mwenyekiti wa iliyokuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati huo akiwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi alikwenda mbele ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba akatoa maoni akisema Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Tanzania siyo huru na naomba ninukuu maneno yake, Mheshimiwa Daniel Lubuva alisema, naomba ninukuu: "Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Jaji Damian Lubuva ametoa maoni mbele ya Tume ya Katiba akipendekeza kuwa Katiba mpya iunde Tume huru ya Uchaguzi na kwamba itambulike kwa jina la Tume Huru ya Uchaguzi. Jaji Lubuva aliyekuwa akitoa maoni hayo kwa niaba ya Tume ya Uchaguzi alisema kuwa, tuwe na Tume inayokubalika na wadau wote wa uchaguzi na wananchi kwa ujumla ambayo katika utekelezaji wa majukumu yake itafanya kazi bila kuingiliwa. Maneno yake sasa, uhuru wa Tume utaanzia tangu jina la Tume yenyewe." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwa nini wasikubaliane na hoja sio tu ya vyama vya upinzani...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, muda wako tayari. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ufafanuzi kwa hoja hii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimwambie Mheshimiwa Mnyika kwamba tunapozungumza suala la Tume ya Uchaguzi tunazungumzia Katiba na Katiba tuliyonayo sasa nimesema hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelezo vizuri sana, Ibara ya 74 ndiyo inaunda Tume ya Uchaguzi ambayo imekuwa ikifanya kazi zake kwa uhuru na kwa misingi yote ambayo inatakiwa kusimamia uchaguzi. Sisi wote tumekuwa ni mashahidi, Tume hii haijaanza kufanya kazi jana wala leo, hata sisi Wabunge wambao tupo ndani ya Bunge lako Tukufu tumesimamiwa uchaguzi na Tume hii hii ambayo leo inaambiwa siyo tume huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hivyo kwa sababu utaratibu wa kubadilisha Wajumbe wa Tume kwenye Tume hii ya Uchaguzi siyo utaratibu ambao unaondoa wajumbe wote wa Tume, ni utaratibu wa urithishaji. Kwa hiyo, utakuta kwamba wajumbe waliokuwa mwaka jana, huyu akimaliza mwaka huu kuna wengine wanaendelea na wengine wanabaki. Kwa hiyo, unapoisema Tume yenye uhuru, Tume iliyokuwa na uhuru wa kumleta Mnyika ndani ndiyo hiyo hiyo inaendelea kusimamia chaguzi zote ndani ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo maoni anayoyazungumza ya Jaji Lubuva yalikuwa ni maoni ya taasisi mbalimbali nchi nzima na ni mapendekezo tu ya jina, namna gani jina la Tume linaweza likaitwa pale mabadiliko yatakapofanyika. Msingi wa hoja hiyo utakuja kujadiliwa pale

ambapo Watanzania na Taifa tutakuwa tayari sasa kuhitimisha mjadala wa Katiba Mpya na hoja hii itakuja kuamuliwa. Kipindi hiki cha sasa, Katiba ambayo tunaendelea kuitumia ni Katiba hii na Tume ya Uchaguzi ni Tume hii ambayo inaelezwa kwa mujibu wa Katiba ndani ya Katiba tuliyonayo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kusema kwamba sijui ni kwa nini tu, Wabunge wa Upinzani wakati wanatoa hoja na tumekuwa tukiwasikia pia kwenye vyombo vya habari wanadai hata uchaguzi wa Serikali za Mitaa wangeamini kama ungesimamiwa na Tume ya Uchaguzi lakini sasa wanasema tena Tume hiyo ya Uchaguzi hawana imani nayo. Kwa hiyo, unaona tu hivi vitu ni *contradiction*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wabunge tuendeleo kuiamini Tume yetu ya Uchaguzi, tuendeleo kuitunza Katiba tuliyonayo sasa na muda wa Katiba ukifika mjadala wa Tume ya Uchaguzi utawekwa mezani na maamuzi yatafanywa na Watanzania wote na namna ya Tume itakayokuwa ina haki ya kusimamia uchaguzi utaratibu utapatikana. Wala sioni kama kuna sababu yoyote ya kutokuwa na imani na Tume ya Uchaguzi ambayo imeendelea kuweka viongozi wote mpaka sasa na sasa hivi Tume inaendelea kufanya kazi yake kwa misingi ya Katiba tuliyonayo sasa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na naomba kutoa maelezo ya kuondoa shilingi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika ili tuweze kutumia muda wetu vizuri kwa sababu ulishatoa maelezo marefu ya hoja yako, sasa toa hoja watu wakuunge mkono tuingie kwenye mjadala utapewa nafasi ya kuhitimisha hoja yako.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema tukafuata Kanuni kwa sababu Kanuni za Bunge

zinataka usiporidhika sasa utoe hoja. Kwa hiyo, naomba ufuata Kanuni.

MWENYEKITI: Kwani mwanzoni ulitumia ipi kuzungumza, ni Kanuni hiyo hiyo, toa hoja yako watu wakuunge mkono ili upate nafasi ya kuwasakiliza wenzako na wewe utahitimisha hoja. Kanuni ni hizo hizo tunazotumia. *(Makofi)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa umetoa maelekezo kinyume na Kanuni, naomba kutoa hoja jambo hili lijadiliwe.

MWENYEKITI: Futa kwanza hayo maneno ya kwamba nimetoa maelezo bila kufuata utaratibu kwa sababu kama unaufuata huo maana yake hata wewe upo nje ya Kanuni. Kwa hiyo, toa hoja yako kwa mujibu wa maelekezo ninayokupa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, okay, naomba kutoa hoja kwa mujibu wa maelekezo uliyonipa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika usipende kuvutana bila sababu, toa hoja, hayo maelezo unayatoa wapi? Toa hoja watu wakuunge mkono, kama huna hoja pia unaweza kukaa tuendelee na watu wengine. Toa hoja yako, usiongeze maneno ambayo siyo ya msingi, toa hoja. *(Makofi)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba suala hili lijadiliwe na Bunge.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kwa mujibu wa Kanuni zetu tutapata wachangiaji wachache kwa kadiri ya uwiano wetu ulivyo. Nawaona hapa Mheshimiwa Mollel, Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa

Kairuki na Mheshimiwa Maige. Tutaanza na Mheshimiwa Mollel.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naungana na Kambi ya Upinzani kuhusu hoja hii ya kwamba Serikali sasa ije na hoja au marekebisho ya kuunda Tume huru ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu Tume ya sasa haipo huru. Kwa nini nasema haiko huru? Tume ya sasa Mwenyekiti na wajumbe wake wanateuliwa na Mheshimiwa Rais. Hii Tume itakuwaje huru iache kusikiliza maelekezo ya Rais au kitu gani Mheshimiwa Rais anataka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haiwezekani kabisa hii Tume ikawa huru, haipo huru na tunahitaji Tume ambayo itaundwa kwa ... *(Makofi)*

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Tume ambayo itaundwa kwa Jopo ambalo litateua watu na hao watu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlinga na Waheshimiwa Wabunge, tuna mafungu mengi sana siku ya leo. Kwa hiyo, tutoe fursa watu wachangie hoja zao. Mheshimiwa Mollel.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Anazingua huyo.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii hoja kwamba tuwe na Tume huru ya Uchaguzi ni *valid* kabisa ili Mwenyekiti na wajumbe wake wateuliwe na Jopo na wapitishwe na Bunge lako Tukufu. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa na Tume huru yenye Mfuko wake wa pesa za uchaguzi ili kuweza kuendesha uchaguzi kwa uhuru na haki.

Tume ya sasa hivi kwa kweli haipo huru na hakuna haiwezi kufanya kitu kinyume na matakwa ya Rais. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika. Tume tuliyonayo sasa hivi haiko huru. Maeneo mengi ambayo Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba hata sisi wapinzani tumepita kwa kuwa tulitangazwa na Tume hiyo hiyo lakini tumepita kwa purukushani. Ni mpaka uende na vidumu vya petroli ama uhamasishe watu ndiyo utangazwe, vinginevyo huwezi kutangazwa. Sasa kwa nini katika Taifa kama hili ambalo tunapendana, kama mchezo upo halali tunatafuta refa ambaye wote tutaridhia, kwa nini hatukubaliani tupate refa mwamuzi kama mna ubavu huo au kama mnasema nyie mnapendwa na watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Jenista umezungumza kwamba tunataka Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tume isimamie, tunachozungumza tunataka Tume huru iundwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa naambiwa hoja ilikuwa ni moja, umezungumzia mbili hapo. Kwa hiyo, ile ya mwanzo imeshatosha, nimekumbushwa hapa. Sasa tunaelekea kwa Mheshimiwa Shangazi...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamaliza dakika zangu. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Alikuwa anazungumzia hoja ile ile.

MWENYEKITI: Hoja ni moja inayoruhusiwa kuzungumzwa kwa mujibu wa Kanuni, muombe Mheshimiwa Mnyika Kanuni uisome.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Hivyo mtatushinda kweli? *(Kicheko)*

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa mujibu wa Katiba tuliyoukuwa nayo na kwa mujibu wa Tumeya Uchaguzi sisi sote hapa tumeshinda kwa kutangazwa na Tume hiyo hiyo ambayo watu wanasema siyo huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii inafanya kazi nzuri sana na tumeshuhudia hata sisi Chama cha Mapinduzi hatujawahi kushinda Kiti cha Ubunge kule Pemba lakini kwa Tume hii hii na ndiyo inayotangaza matokeo lakini hatujawahi kulalamika popote kwamba Tume siyo huru. Kwa hiyo, Tume hii ni huru, anayeshinda kwa kishindo anatangazwa kuwa mshindi katika ngazi yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napingana na mtoa hoja, Tume hii ni huru kabisa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Almas Maige.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangaa sana upande ule wanasema Tume hii siyo huru, Tume hii kwa Katiba hii tuliyonayo ni huru. Wenzetu pia wameikubali muda wote, wameshiriki chaguzi zote na hata ikitangazwa leo uchaguzi Arumeru wanashiriki ila wao siyo uhuru kwa sababu sehemu nyingine wagombea wao hawakushiriki katika chaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwamba Tume hii ni huru kinyume na anachosema Mheshimiwa Mnyika. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nasema Tume ya Uchaguzi ni huru na nina ushahidi, niligombea nikiwa CHADEMA nikashinda, nimekuja CCM nimeshinda naendelea kuwa Mbunge na huo ni uhuru mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii ilisimamia uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi wa mwaka 1995, 2000, 2005, 2010 mpaka 2015 haikulalamikiwa ndiyo maana Wabunge wa Upinzani wapo ndani kwenye hili Bunge, ni Tume hii hii ilisimamia. Wanazungumza habari ya kuwa na Tume huru na kubadilisha Katiba; sasa hivi nchi hii tuna kero nyingi sana za wananchi za maji, madarasa, matundu ya vyoo na huduma za afya. Ukiona watu ambao hawana ajenda ni watu ambao wanashika hapa wanaacha, wanagusagusa na haya siyo maoni ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nasema habari ya kutumia fedha nyingi kubadilisha Katiba kwamba kuwe na Tume huru ambapo ni watu wachache wanataka hayo mambo, hatuna muda wa kupoteza.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kuzungumza kwamba wajumbe wa Tume hii ni Makada wa CCM ...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara kengele imegonga, Mheshimiwa Kairuki.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono maelezo ya Serikali. Kwanza kabisa, ukiangalia ni hisia tu ambazo hazina uthibitisho wowote lakini pili Tume hii ni huru kama ambavyo imeundwa kupitia Ibara ya 74(7) ya Katiba ambapo ukiisoma inaeleza wazi kabisa kwamba Tume ya Uchaguzi itakuwa ni idara huru inayojitegemea, sijui walitaka uhuru wa aina gani zaidi ya huo na itafanya maamuzi yake rasmi bila kuingiliwa na mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukienda katika Ibara ya 74(11) inasema kabisa katika kutekeleza madaraka yake, Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali au maoni ya chama chochote cha siasa, tunataka uhuru wa aina gani? Pia ukiangalia Ibara ya 36 ambayo imetoa madaraka ya Mheshimiwa Rais pia inaeleza kabisa na hata hii Ibara ya 74, itakapotokea Afisa wa Tume ya Uchaguzi kuna tabia/ mwenendo mbaa ambao umeufanya kwa mujibu wa kazi zake, Mheshimiwa Rais ana uwezo wa kuchukua hatua dhidi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda tu kusema kwamba hebu tuiamini Tume hii ya Uchaguzi, ni huru. Nadhani hapo mnachokitaka tu ni jina ambalo haliwezi kusaidia na wala kubadilisha chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, hitimisha hoja yako.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anasema Mheshimiwa Rais anaweza kuwachukulia hatua, maana yake ame-*contradict* hoja yake kwamba Rais anaweza kuingilia Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Rais huyu huyu, ili kuingilia Tume, leo kwa mfano amemteua mtu anaitwa Gimson Mhagama kuwa Mkurugenzi wa Nyasa, ambaye kisheria ndio atakwenda kusimamia uchaguzi, ambaye alikuwa Katibu wa CCM, alikwenda Singida huko, akaenda Iringa na mpaka anateuliwa ni Kiongozi wa CCM Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imetokea maeneo mengi ya nchi; na maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waitara kwamba Tume haijalalamikiwa nyuma ni ya uongo. Masuala ya kutaka Tume Huru yalianzia wakati wa Tume ya Nyalali mwaka 1991, Kamati ya Kisanga mwaka 1999 baada ya Uchaguzi wa 1995 ikasema bado kunahitajika Tume Huru; waangalizi wa uchaguzi wa ndani, wa nje miaka yote hii ya

uchaguzi wamekuwa wakitoa ripoti zao wakisema inatakiwa Tume Huru ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachokiona hapa ni kwamba hata upande wa CCM ninyi mlipobaki wenyewe kwenye Bunge Maalum la Katiba, ile Katiba inayopendekezwa bado mlipendekeza muundo tofauti wa uteuzi wa Tume ya Uchaguzi na uliopo sasa na mlikuwa wenyewe. Kama mnaamini Tume ilikuwa huru, kwa nini mlileta marekebisho hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waitara analeta hoja nyingine kwamba eti ukisema Tume Huru, moja kwa moja unataka Katiba Mpya. Kwa sababu Mheshimiwa Rais amekataa Katiba mpya akisema ni gharama, basi haihitajiki tena Tume Huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ninayoitoa tofauti na hoja ya Katiba mpya ni hoja ya kwamba kwa sababu Rais amekataa mchakato wa Katiba mpya, Bunge hili litumie lbara ya 98 ya Katiba hii hii... *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, muda wako umekwisha.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

(Hoja ya Mhe. John J. Mnyika ilikataliwa na Kamati ya Matumizi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na majina mengine ambayo tuko nayo hapa. Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majumuisho mazuri. Tumekuwa tukipata maafa kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kwa mfano, mwaka jana Korogwe tulipata mafuriko, kule Kagera kulikuwa na tetemeko na maeneo mengine. Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo yenye jukumu la kushughulika na maafa nchini na hasa uratibu wa maafa ikiwemo kuzuia au kuinga maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia bajeti sioni majibu ya namna gani bajeti inakwenda kutusaidia kupunguza au kuinga maafa kwenye maeneo mbalimbali ndani ya nchi yetu. Naomba nipate majibu ya Serikali, ni kwa nini bajeti ya maafa haiendani na mahitaji muhimu tuliyokuwa nayo kwenye nchi yetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Na. 7 ya mwaka 2015 ambayo inaweka uratibu wa maafa nchini, ukienda kwenye kifungu cha 7(1) kinaunda *Disaster Management Council*. Kazi mojawapo kubwa ya hii *Disaster Management Council* ni kuhakikisha kwamba inatengeneza mifumo ya kisera ya pamoja ya kitaasisi ili kuhakikisha kwamba tunaweka udhibiti ama tunachukua tahadhari ya viashiria vya maafa katika maeneo mengine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia kwenye fungu la Mheshimiwa Waziri Mkuu, bajeti inayotengwa kazi yake kubwa ni kuratibu mifumo yote ya kisekta ndani ya Serikali ambayo itakwenda kushughulikia hivyo viashiria vya maafa. Kwa mfano, tunapokwenda kujenga labda daraja la Mto Rufiji au daraja la Mkapa, linapojengwa na Wizara inayohusika na miundombinu, mpango wa ujenzi wa daraja hilo unaingiliana na viashiria vya maafa kwenye mafuriko kwenye mto huo, lakini kazi hiyo haitabajetiwa ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, itabajetiwa kwenye Wizara nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojenga viwanja vya ndege, ukiangalia faida ya viwanja vya ndege, tayari ile *Disaster Management Council* imependekeza kwamba viashiria vya maafa pia maafa yanaweza yakapatikana kama viwanja vya ndege havitakarabatiwa na kujengwa vizuri. Kwa hiyo, ukiangalia kimfumo na kiuratibu kwa ujumla wake ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, bajeti ya kukabiliana na maafa haiwekwi moja kwa moja kwenye ofisi yetu, lakini inabajetiwa kitaasisi kwa kuzingatia kwamba uratibu wa maafa ni suala la kitaasisi na siyo suala la idara ama ofisi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, zitakapokuja bajeti za Wizara nyingine, akiona kuna bajeti ya miundombinu, kuna bajeti ya maji, kuna bajeti ya kujenga hospitali, kuna bajeti ya Vituo vya Afya na huduma nyingine zote, hizo zote zina viashiria vya maafa na lengo lake pia kuna *element* ya kupunguza ama kuzuia maafa katika sekta zote za Serikali katika azma hii ya pamoja ya Sheria hiyo Na. 7 ya Maafa ya mwaka 2015. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Timotheo naona ameridhika na majibu.

Waheshimiwa Wajumbe, ninalo pia jina la Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa awali na mchango wangu wa maandishi nilijielekeza kwenye Sheria ya *Tanzania Investment Act*, kifungu Na. 24, naomba nikisome ili kuweka kumbukumbu sawasawa. Katika sheria hii kifungu Na. 24 kinasema, "*every business enterprises granted a certificate of incentives under this Act shall be entitled on initial automatic immigrant quarter of up to five persons during the start up period.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha sana, hii sheria tunaiuza kwa wawekezaji. Wawekezaji tunawaambia

kwamba mtakapokuja kuwekeza Tanzania mnapata watu watano ambao sheria haikutaja *expertise*, imetaja watu watano. Hakuna mahali popote. (*Makofi*)

MHeshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna sheria nyingine ya mwaka 2016, *The Non-citizen Employment Regulation Act, Cap. 436*, hii inampa mamlaka sasa Kamishna wa Kazi kutoa vibali vya kazi kutokana na anavyoona yeye inafaa. Shida iko hapa. Shida huku, hawa watu hawakutakiwa *expertise*, wakishafika sasa, wakishasajili kampuni katika mradi wa *TIC* anahitaji *expertise*. *Why* mnakuwa na *double standards*? Huku mnatoa kwa mkono wa kulia, huku mnachukua kwa mkono wa kushoto, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida, waliopitisha hii sheria akina Mheshimiwa Kapt. Mkuchika mwaka 1997, walikuwa na maana kubwa. Mtu hawezi kuleta Dola za Marekani milioni 300, 400 akawekeza halafu ukamwambia katika watu watano, *qualifications* hizi alizonazo Mtanzania, mtu wale watu wake watano katoka nao mbali katika kampuni. Haiwezekani! Hata wewe Mheshimiwa Jenista ukiunda kampuni yako, haiwezekani tena aje mtu akwambie kwamba kwa sheria hii basi wewe utachukua hawa watu wangu, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Kabudi anakuja na hoja anasema sasa, eti; tulia Mheshimiwa Prof. Kabudi, tulia.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijatoa hoja lakini.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Prof. Kabudi, tulia. (*Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Profesa Kabudi, nitakupa fursa ya kuongea. Nitakupa fursa Mheshimiwa Prof. Kabudi.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ngwali, muda wako umekwisha. Kwa hiyo, subiri ufafanuzi.

Mheshimiwa Ngwali umeeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe, naomba utulivu. Mheshimiwa, wewe umekaa Kiti cha *Chief Whip*, ukiwa unaongoza wewe vurugu unashangaza sana. Kwa hiyo, wewe kazi yako ni kutuliza watu wako badala ya wewe kuwa unafanya fujo.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.
(Kicheko)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja aliyowasilisha Mheshimiwa Mbunge, hakuna *contradiction* yoyote kati ya Sheria ya Uwekezaji na Sheria Na. 1 ya Uratibu wa Ajira kwa wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 19(1) cha Sheria ya Uratibu wa Ajira za Wageni kimesema bayana kwa kuazima maneno ya kifungu Na. 24 cha Sheria ya Uwekezaji, kwamba mgeni yeyote atakayekuja nchini kuanzisha au kufanya uwekezaji anayo *automatic immigrant quarter* ya watu watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwondolee wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba akienda leo *TIC* akaangalia orodha ya vibali vilivyotoka ambavyo ni vya

kampuni ambazo ziko *TIC registered*, ni zaidi ya 1,600. Siyo kweli kwamba mwekezaji huyu anazuiwa kuwa na watu wake watano. Sisi tunaielewa kwamba mwekezaji huyu analeta uwekezaji mkubwa ndani ya nchi na fedha zake pia, lazima awe na nafasi ya watu wa kulinda mtaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo kweli kwamba tunazuia watu haO watano wasipate vibali. Isipokuwa ambacho labda kinachanganywa hapa, sheria imesema vizuri kabisa nafasi tano; kutokea pale kwenda mbele ndiyo vigezo na masharti mengine yatazingatiwa. Hiyo ndiyo maana ya *incentive* kwamba lazima awe na watu wake watano na ndiyo *incentive* ambayo sheria imeitoa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ngwali.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja jambo hili lijadiliwe.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imeungwa mkono. Sasa tutafanya utaratibu wetu wa kuchukua majina ya Waheshimiwa Wabunge watakojadili hoja hii. Namwona Mheshimiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa Ole Nasha, Mheshimiwa Bashungwa, Mheshimiwa Dkt. Chegeni, Mheshimiwa Ally Saleh, Mheshimiwa Antony Komu na Mheshimiwa Sakaya.

Tutaanza na Mheshimiwa Cosato Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ahmed Ngwali tulivyokuwa kule Burundi tumecheza mpira mzuri sana, naye ni Mwalimu wetu. Sisi tunamwita Fabio Capello. Kwa hiyo, kwanza kabisa naamini atarejesha shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusema haya, nilikuwa najaribu kusema jambo moja la muhimu sana. Kuna nyakati lazima tusimame katika hali ambayo itatusaidia kama Taifa. Leo nilikuwa napitia *doing business* katika *East Africa* 2019; ukienda kuangalia, wenzetu Kenya wanashika nafasi ya 61 kutoka 80 mwaka 2018; Rwanda wanashika nafasi ya 29 kutoka 41 mwaka 2018; sisi tulikuwa namba 137 sasa hivi tuko 144. Maana yake ni kwamba kuna vikwazo na hili tumelisema katika michango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Ahmed Ngwali arejeshe shilingi kwa mantiki kwamba Serikali ikakae kuona kwamba kuna misigano ambayo inawafanya wawekezaji kwa namna moja au nyingine tunawakwaza. Hata leo Mheshimiwa Rais katika hotuba yake pale Njombe amelisema sana jambo hili. Kwa hiyo, kuna mambo tuyapokee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni tulivu, ni sikivu, inataka wawekezaji na mambo yatakwenda vizuri. Kwa hiyo mwalimu wangu, kocha wangu Fabio Capello, Mheshimiwa Ahmed Ngwali, rejesha shilingi tuchape kazi. (*Makofi*)

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tuondokane na hii kujisifu kila siku sisi tuko nafasi ya ngapi Afrika, duniani, tunataka hali halisi. Ili kuvutia *FDIs* ni lazima uwe *almost perfect* katika kutimiza sheria. Ni lazima uwe mzuri katika kuhakikisha kwamba mazingira yanakuwa mazuri ili kumvutia mwekezaji. Kitu kimoja tu kinaweza kuku-cost watu wakahama wakaenda nchi nyingine, tatizo hili ni tatizo la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichosema Mheshimiwa Ngwali, kuna mgongano hapa. Haina maana Mheshimiwa Mavunde kuinuka aka-*defend*. Ni kukubali kwamba kuna mgongano. Haiwezekani mtu aje awekeze mabilioni halafu usimpe ile *confidence* ya kuja na watu wake. Ni kuondoa hiyo kuhamisha; na tunasema tuna *One Stop Center*, kuhamisha hiyo kwamba mamlaka yale yawe upande

mmoja tu, sehemu ya kazi isihusike kabisa na mtu wa *start up*. Sehemu ya kazi ihusike na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu hapa alisema tufanye sasa, tukipe Kituo cha Uwekezaji mamlaka na kisiwe kituo. Haya yaondoke. Tumesema watu watano, kwa nini tunazunguka? Tumpe mtu watu watano, hao wengine wafuate taratibu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mhshimiwa Antony Komu.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni kubwa kweli kweli. Ukimsikiliza Mheshimiwa Rais huko aliko sasa hivi analalamika kuliko mtu yeyote, nasi tunaona vibaya sana Mheshimiwa Rais wetu kuwa analalamika na hatua hazichukuliwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu Mheshimiwa Angellah Kairuki amekiri hapa kwamba lipo tatizo na wanazungumza sasa na Waziri wa Fedha kujaribu ku-*sort out* na ndiyo maana kuna *blueprint* kwa ajili ya ku-*harmonize* hivi vitu. Sasa fursa ni hii hapa; tuchukue hatua leo. Nami nakubaliana na Mheshimiwa Ngwali kwamba tuache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoka kwenye ziara hapa za Kamati, Mheshimiwa Mgimwa, Mwenyekiti wetu, anajua. Hata hao watu watano; kuna kiwanda kule Mwanza cha mabondo; kupewa *permit* ya mtu mmoja imekuwa mbinde, haieleweki. Kwa hiyo, nafikiri hilo jambo ni kubwa kuliko ambavyo linavyofikiriwa. Kwa hiyo, naungana na Mheshimiwa Ngwali kwamba hili jambo limalizike sasa hivi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Ole Nasha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Ngwali, ambaye namheshimu sana, ni mtu makini sana, arudishe

shilingi ili tuendelee na kazi kwa sababu nafikiri mkanganyiko uliopo ni kati ya sheria na utekelezaji. Sheria kama sheria haina shida. Sheria ya Uwekezaji ikisema kwamba mwekezaji anakuwa na *right automatically* ya watu watano kama *incentive*, halafu bado sheria nyingine zikaweka taratibu za namna ya watu wao kuwa *vetted* na kuangalia kama wanafaa kuingia nchini, sheria haina shida wala haigongani, wala hakuna *contradiction*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ni pale utekelezaji wa sheria unapofanyika vibaya. Ninyi mlichoonesha, hata Mheshimiwa Komu alivyoonesha hapa ni kwamba kuna *incidences* ambazo mwekezaji amenyimwa kuwaingiza hao watu, lakini sasa huo ni upungufu wa utekelezaji wa sheria, siyo mgongano wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ni muhimu kuendelea kuwa na uwezo wa kuwanyima baadhi ya wawekezaji wasilete wafanyakazi bila kuwa *vetted*? Ni kwa sababu ya mambo mengi leo hii ukisema tu kwamba mwekezaji *automatically* ana haki ya kuwaleta wafanyakazi watano akikuletea majambazi, akikuletea *terrorist*, akikuletea watu ambao wana migongano na sheria katika nchi zao. Kwa hiyo, sheria siyo tatizo tu, kwa hiyo tunachosema tuendee kuhakikisha utekelezaji wa sheria unafanyika katika njia ambayo itaruhusu wawekezaji waweze kufanya kazi bila shida yoyote. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niseme kwamba, msema kweli ni mpenzi wa Mungu maadamu Mheshimiwa Rais amechukuwa jukumu hili kwanza la kuunda Wizara maalumu ya uwekezaji hii ni hatua moja wapo ya kwanza ya kuona kwamba ule upungufu uliopo wa kiutendaji na utekelezaji unatatuliwa. Leo asubuhi hapa Mheshimiwa Waziri nimemuuliza swali na akajibu akasema hivi, tuna mikakati mbalimbali pamoja na mambo mengine anayotaka kuyafanya ni ku-*harmonize*,

hayo anayosema Mheshimiwa Ngwali ni ya msingi kwa sababu kumekuwa na upungufu, lakini upungufu kama upo si unarekebishwa.

Naomba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri wanaohusika wakae chini tuone wapi ili tukafanye nchi yetu ikawa-*attract* wawekezaji kutoka nje. Tupunguze vikwazo ambavyo vinaleta matatizo. Namwomba Mheshimiwa Ngwali maadamu suala limeshajulikana arudishe shilingi yake tusonge mbele. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUGWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu wa upande wa huku kumwomba rafiki yangu Mheshimiwa Mohamed Ngwali arudishe shilingi kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Chegeni kitendo cha Serikali kuanzisha Wizara mahususi ya kushughulikia mambo ya uwekezaji ni *indication* kwamba Serikali ni sikivu na tayari jitihada za kuweka urafiki wa uwekezaji hapa nchini unafanyika. Pia hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelezea jinsi *TIC* ilivyotengeneza *One Stop Center* kwa ajili ya taasisi mbalimbali za Serikali kuhakikisha zinakuwa pale kwa ajili ya kuondoa *red tape*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Angella Kairuki amezungumzia mkakati wa *immediate strategy medium* na *long-term* na Serikali kwamba itaendelea kuangalia sheria na kanuni ambazo zinakuwa *unfriendly* na uwekezaji ili tuweze kuzidi kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji hapa nchini. Kwa hiyo, namwomba rafiki yangu Mheshimiwa Ngwali arudishe shilingi ili Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iweze kutimiza mambo mazuri ambayo jamesheheni kwenye bajeti yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Hoja ya msingi hapa ya Mheshimiwa Ngwali ni kuondoa vikwazo na kuondoa urasimu kwenye sekta ya uwekezaji ili Taifa letu liweze kuwa na wawekezaji wengi na tuweze kuhinua uchumi wetu. Ukijaribu kuangalia michango yote ya Waheshimiwa Wabunge wote waliosimama lengo letu ni moja kwamba lazima Serikali iangalie kwenye sekta ya uwekezaji kile ambacho kimefanya mgongano wa sheria, mgongano wa sera, chochote kile kiondoke ili tuweze kupata wawekezaji wengi wenye tija, tuweze kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwenye suala hili kikubwa ni *commitment* ya Serikali, inakwenda kufanya nini kwenye hii sekta kuhakikisha kwamba vitu ambavyo vimezungumzwa na Mheshimiwa Ngwali vinaondoka ili sekta hii iweze kuwa muhimu kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ngwali kwa lengo jema kabisa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikiliza hoja za Waheshimiwa Wabunge na naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba, Mheshimiwa Rais alipoamua kuunda Wizara hii ya Uwekezaji na akaiweka ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mujibu wa Katiba, nimesema hapa wakati nahitimisha hoja yangu, ndiyo ni Ofisi pekee ambayo inashughulikia uratibu wa shughuli zote na taasisi zote na sheria zote zinazotekelezwa ndani ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilipe taarifa Bunge lako Tukufu, nadhani walimwona Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea *TFDA*, *alitoa* maagizo makubwa, maagizo ambayo yanaonesha kwamba uwanda mzima wa suala la uwekezaji na *doing business* na masuala ya *Private Sector* ni

lazima taasisi zote za Serikali zirudi pamoja, zikakae pamoja na kutathmini sheria zote zilizopo na kutafuta njia muafaka ya kuondoa vikwazo na matatizo yanayoikabili *Private sector* na uwekezaji kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie kazi hiyo imeshaanza kufanyika ndani ya Serikali. Nimwombe Mheshimiwa Ngwali, sasa hivi tumejipanga kuhakikisha kwamba tunatatua vikwazo hivyo vyote, tunapitia sheria zinazogongana, tunapitia maeneo ya tozo mbalimbali zinazogongana, lengo letu ni kuhakikisha kwamba ufanyaji biashara uwekezaji na masuala mengine yote yanatakiwa yafanyiwe marekebisho yanafanyiwa marekebisho, ili kuhakikisha shughuli zote za uwekezaji na shughuli nyingine zote za uendeshaji wa Serikali zinakwenda sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Ngwali atuachie nafasi arudishie shilingi yangu, lakini arudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na tutakuja kuleta taarifa Bungeni kwa sababu ni lazima tukatafsiri *blue print*, tukaifanyie kazi na maeneo mengine mengine yote ya namna hiyo. Kwa kweli ni *commitment* yetu ndani ya Serikali kuhakikisha tunamsaidia Mheshimiwa Rais kuondoa vikwazo hivyo vyote chini ya uratibu wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ngwali.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, narudisha shilingi yao. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Kwa namna alivyotoa maelezo Mheshimiwa Waziri, nadhani tumemwelewa, lakini mwangalie namna ambavyo wawekezaji mmeshawapa ofisi, wakishaanza tena kurukaruka watoke ofisi ya uwekezaji, wanaelekea tena ofisi ya kazi, sijui na wapi? Hiyo ndiyo inayoleta shida na tafsiri pia inakuwa tofauti kidogo. Kwa hiyo muangalie hayo yote kwa pamoja kwa mujibu wa maelezo hayo ya Mheshimiwa Waziri.

Tutamalizia na Mhehimiwa Anna Lupembe.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nataka nipate ufafanuzi tu kwa sababu sisi watu wa pembezoni lazima tuulize na tuseme Serikali imeweka mkakati gani wa kuvutia uwekezaji katika maeneo ya pembezoni. Ukiangalia Mkoa wetu wa Katavi una fursa kubwa nyingi una maeneo makubwa, sasa Serikali imeweka mkakati gani ya kutuletea uwekezaji. Ahsante (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji ufafanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kujibu hoja ya Mheshimiwa Anna Lupembe, kwanza kabisa nipende kusema kwamba tunachotaka kuhakikisha miko ya yote inakuwa na uwiano sawa katika fursa za kiuwekezaji.

Pili kwa kutambua hilo ndiyo maana tumeweka ofisi zetu za Kanda saba kuhakikisha kwamba hata na maeneo ambayo ni ya pembezoni ambayo tuna baadhi ya Ofisi napo pia kunakuwa na ofisi zetu ili kuweza kutoa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kwa mujibu wa Sheria yetu ya Uwekezaji ambayo inatoa vivutio kwa uwekezaji mahiri, moja ya vigezo vitano ambavyo vimewekwa kwa ajili ya kuzingatiwa na Kamati yetu ile ya Kitaifa ya Uwekezaji ni pamoja na kuangalia wawekezaji ambao wanaenda katika *geographically disadvantage regions*, miko ya ambayo inachangamoto za kiuwekezaji, lakini kwa kutambua hilo ndiyo maana tutakuja na sharia, kuifanyia mapitio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapokuja na Sheria mpya, basi tutahakikisha tutakuwa na vivutio maalum kwa wawekezaji ambao wataenda katika maeneo mbalimbali ya pembezoni.

MWENYEKITI: Naona Mheshimiwa Anna Lupembe ameridhika na maelezo yaliyotolewa, Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji kuhusiana na kifungu namba 1001.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit.....	Sh. 1,162,637,662/=
Kif. 1003 - Policy and Planning Unit.....	Sh. 542,060,067/=
Kif. 1004 - Internal Audit Unit.....	Sh. 324,732,745/=
Kif. 1005 - Government Communication Unit.....	Sh. 195,394,766/=
Kif. 1006 - Procurement Management Unit..	Sh. 358,528,456/=
Kif. 1007 - Legal Services Unit.....	Sh. 160,658,540/=
Kif. 1008 - Management Information System.....	Sh. 247,328,460/=
Kif. 2001 - Civil Affairs and Contingencies..	Sh. 2,673,406,675/=
Kif. 2002 - National Festivals.....	Sh. 487,754,326/=
Kif. 3001 - Parliamentary and Political Affairs.....	Sh. 582,495,004/=
Kif. 4001 - Private Sector Development and Economic Empowerment.....	Sh. 2,860,309,996/=
Kif. 5001 - Coordination of Government Business.....	Sh. 657,575,267/=
Kif. 6001 - Investment Development Div.....	Sh. 1,721,957,001/=
Kif. 7001 - Government Printer.....	Sh. 2,454,241,051/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi

Kif. 1001 - Administration and Human Resources Management.....	Sh.1, 411,031,518/=
Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit.....	Sh. 72,865,203/=
Kif. 1003 - Planning, Monitoring and Evaluation Unit	Sh. 133,829,396/=

MWENYEKITI: Sawa, ili kumbukumbu zikae vizuri soma tena.

Kif. 1003 - <i>Planning, Monitoring and Evaluation Unit</i>	Sh. 133,829,396/=
Kif. 1004 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 103,695,262/=
Kif. 1005 - <i>Information, Communication and Technology Unit</i>	Sh. 185,975,394/=
Kif. 1006 - <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 120,956,351/=
Kif. 2001 - <i>Mediation</i>	Sh. 868,892,402/=
Kif. 2002 - <i>Arbitration</i>	Sh. 844,266,474/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 25 – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu

Kif. 1001 - *Administation and Human Resources Management*.....Sh. 7,980,744,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mosoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sina na ugomvi na Ofisi binafsi ya Waziri Mkuu, hoja yangu ni *subvote* 1001 kwenye *item* 22009 *Training – Foreign* ambayo mwaka uliopita kulikuwa kuna sabini milioni, mara hii kuna ziro na kwenye maelezo ukiangalia ya randama zao maelezo walivyoyatoa ya mambo ambayo yatafanyiwa kazi, lakini mara hii inaonekana hakuna lolote litakalofanyika. Naomba maelezo juu ya kifungu hiki cha 22009 - *Training Foreign* kwa nini kulikuwepo na milioni sabini, sasa je, mara hii ndiyo hakuna lolote la kufanya pamoja na maelezo ya kwenye randama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinahusu *Training* kwa wafanyakazi ambao wanasoma nje ya nchi, lakini wale wafanyakazi wote ambao walikuwa nje ya nchi, sasa hivi masomo yao

wameshayakamilisha, ndiyo maana huwezi kutenga, lakini kama watatokea wafanyakazi ambao watakwenda kwenye mafunzo kwa kipindi hiki cha katikati tunao uwezo wa kutumia *Vote 37* ambayo tumeshaipitisha ambayo ni ya uendeshaji wa ujumla wa shughuli nzima za Ofisi ya Waziri Mkuu. Ofisi ya Waziri Mkuu ina *Vote* mbili ina *private* Ofisi ambayo ni Waziri Mkuu na wafanyakazi hao hao ambao wako kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu inapotokea kuna suala linahitaji kuhudumiwa la dharura, kifungu kile cha 1001 cha *Vote 37* huwa pia kinaendelea kutumika.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu – 27 Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....Sh. 641,990,004/=

Kif. 1002 – *Finance and Account Unit*..... Sh. 239,478,000/=

Kif. 1003 – *Planning, Monitoring, Evaluation & Research Unit*.....Sh.130,202,000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijahoji niwakumbushe hasa upande wa Serikali kuitikia ili taarifa za Bunge zikae vizuri.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1004 – *Internal, Audit Unit*.....Sh.144,219,362/=

Kif. 1005 – *Procurement Management Unit*..Sh.134,760,000/=

Kif.1006 – *Information and Communication Technology Unit*.....Sh.126,802,000/=

Kif.1007 – *Communication and Civic Education Unit*.....Sh. 118,920,000/=

Kif.1008 – *Registration & Monitoring of Political Parties*Sh. 261,341,000/=

Kif.1009 – *Election Expenses and Grants Division*.....Sh. 21,691,908,634/=

Kif.1010 – *Monitoring of Political parties Unit*.....Sh. 0

Kif.1011 – Zanzibar Office.....Sh.181,840,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 42 – Mfuko wa Bunge

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka Mheshimiwa Spika ameshatoa maelekezo au uamuzi kuhusu Fungu hili. Hili ni Fungu 42 na linahusu Bunge na kwa sababu bajeti ya Bunge imepitia taratibu zile za vyombo vyetu vya uongozi hapa Bungeni, alivyotoa maamuzi hayo alisema kwamba ukihoji kifungu hiki ni kama unamhoji yeye Spika. Nadhani wale waliokuwepo watakuwa wanakumbuka alivyotoa maelezo hayo. Kwa hiyo, kifungu hiki hakiwezi kuhojiwa kwa maana ya kila fedha bali itatajwa fedha ile ya jumla halafu Bunge linahojiwa kwa namna hiyo.

WABUNGE FULANI: Hatujaelewa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ngoja nirudie tena, mafungu haya yalipokuwa yanahojiwa hapa Bungeni, Bunge la bajeti lililopita Mheshimiwa Spika aliagiza kwamba tunapohoji kwenye bajeti ya Bunge ni kama tunajihoji sisi wenyewe kwa maamuzi ambayo tumeshayafikia. Sasa kwa sababu huo siyo utaratibu, hatuwezi kuhoji bajeti ya Bunge. Kwa hiyo, inasomwa ile fedha ya jumla ili Waheshimiwa Wabunge wote waisikie na iingie kwenye rekodi kwamba ni fedha kiasi gani imetengwa kwa ajili ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, naamini mnawaamini wajumbe wenu mliowachagua humu Bungeni kwenda kuwawakilisha kwenye Tume na vyombo vingine vya maamuzi. Katibu tusomee ile jumla.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Jumla ya fedha inayoombwa katika Fungu hili ni shilingi 116,573,026,000.

Kif. 1001 – Administration and HR Management Div.....Sh.11,380,557,000/=

Kif. 1002 – <i>Library and Research Division</i>	Sh.327,526,000/=
Kif. 1003 – <i>Information and Communication Technology Unit</i>	Sh. 723,835,000/=
Kif. 2001 – <i>Budget Division</i>	Sh. 1,730,014,000/=
Kif. 2002 – <i>Table Office Division</i>	Sh. 83,710,783,000/=
Kif. 2003 – <i>Parliamentary Committees Division</i>	Sh. 10,740,297,000/=
Kif. 2004 – <i>Hansard Unit</i>	Sh. 741,957,000/=
Kif. 2005 - <i>Legal Services Division</i>	Sh. 1,016,311,000/=
Kif. 3001 – <i>Private Office of the Speaker</i>	Sh. 771,028,000
Kif. 3002 – <i>Private Office of the Deputy Speaker</i>	Sh. 346,814,000/=
Kif. 3003 – <i>Office of the Leader of Opposition</i>	Sh. 236,142,000/=
Kif. 3004 – <i>Private Office of the Clerk</i>	Sh. 672,655,000/=
Kif. 3005 – <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh. 453,354,000/=
Kif. 3006 – <i>Communication and International Relations Unit</i>	Sh. 2,598,440,000/=
Kif. 3007 – <i>Information, Education and Communication</i>	Sh. 0
Kif. 3008 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 255,792,000/=
Kif. 3009 – <i>Procurement Management Unit</i> ...Sh.	400,873,000/=
Kif. 3010 – <i>Defense and Security Unit</i>	Sh. 255,790,000/=
Kif. 3011 – <i>Estate Management</i>	Sh. 0
Kif. 3012 - <i>Zanzibar Office</i>	Sh. 210,858,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Kif. 1001- <i>Administration and Human Resources Management</i>	Sh. 1,993,474,000/=
Kif. 1002 – <i>Planning, Monitoring, Evaluation & Research Division</i>	Sh. 381,129,000/=
Kif. 1003 - <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh. 398,902,000/=
Kif. 1004 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 264,590,000/=
Kif. 1005 – <i>Legal Services Unit</i>	Sh. 284,082,000/=

Kif. 1006 - <i>Procurement Management and Logistics Unit</i>	Sh. 440,486,000/=
Kif. 1007 – <i>Zanzibar Office</i>	Sh. 89,480,000/=
Kif. 2001 - <i>Election Management Division</i> ...	Sh. 408,165,000/=
Kif. 2002 - <i>National Voters Registration and ICT Division</i>	Sh. 518,371,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2003 – <i>Voters Education and Public Information Division</i>	Sh. 455,615,000/=
---	-------------------

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo, kwenye *Voters Education, Subvote 2003, item 2010, Travel in country* imekuwa inashuka kila wakati. Mwaka 2017 shilingi milioni 37.4, mwaka 2018/2019 shilingi milioni 28.2, safari hii kuna shilingi milioni 8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la kutoa elimu kwa ujumla wake na safari za ndani za kikazi kwa shughuli hizi na ukiangalia kwenye randama na maelezo yenu inaonekana kuna tatizo hapa bado halijakaa vizuri. Naomba kupata maelezo inakuwaje wakati kuna shughuli za uchaguzi halafu mnapunguza pesa kwenye *voters education* au mnaandaa mazingira ya kushinda tu kwa njia nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ya kifungu hiki inatokana na mahitaji halisi lakini fedha ya ziada imetengwa kwenye *Subvote 1001*. Kwa hiyo, ile *Sub-vote 1001 Administration in General* ni fungu ambalo linatumika katika kuchukua tahadhari ya mafungu

hayo mengine yote. Kwa hiyo, hatuna shida utaratibu wote uko *under control*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye masuala ya elimu ya mpiga kura itakapoanza kutolewa mnakumbuka kwamba fungu ambalo huwa linatumika kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi na uendeshaji wa uchaguzi linatoka Mfuko Mkuu wa Serikali na linatengenezewa pia utaratibu wake wa kibajeti.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 65 - Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu

- Kif. 1001 - *Administration and HR Management*.....Sh. 3,508,251,422/=
- Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 262,885,000/=
- Kif. 1003 – *Policy and Planning Unit*Sh. 499,192,000/=
- Kif. 1004 – *Internal, Audit Unit*.....Sh.133,685,000/=
- Kif. 1005 – *Procurement Management Unit*...Sh.161,336,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mliletewa makaratasi kwenye meza yenu yaliyokuwa yanarekebisha baadhi ya mafungu ambayo ukurasa unaonekana umerudiwa kwa kuandika 402 na 402. Kwa hiyo, mliletewa karatasi kwa ajili ya kufanya marekebisha hayo. Katibu.

- Kif. 1006 – *Government Communication Unit*..Sh.81,320,000/=
- Kif. 1007 - *Information and Communication Technology Unit*.....Sh.106,479,000/=
- Kif.1008 – *Legal Service Unit*.....Sh. 34,500,000/=
- Kif. 2001- *Labour*Sh. 7,401,056,492/=
- Kif. 2002 - *Employment Division*..... Sh.431,902,086/=
- Kif. 2003 – *Registrar of Trade Unions* Sh.127,645,000/=
- Kif. 2004 – *Arusha Regional Labour Office*Sh.19,755,000/=

Kif. 2005 - Dodoma Regional Labour Office.....	Sh.19,005,000/=
Kif. 2006 – Geita Regional Labour Office.....	Sh.14,955,000/=
Kif. 2007 – Iringa Regional Labour Office.....	Sh.19,755,000/=
Kif. 2008 – Kagera Regional Labour Office.....	Sh.11,205,000/=
Kif. 2009 – Kigoma Regional Labour Office.....	Sh.9,455,000/=
Kif. 2010 – Kilimanjaro Regional Labour Office.....	Sh.10,805,000/=
Kif. 2011 – Lindi Regional Labour Office.....	Sh.9,855,000/=
Kif. 2012 – Manyara Regional Labour Office.....	Sh.7,455,000/=
Kif. 2013 – Mara Regional Labour Office.....	Sh.10,305,000/=
Kif. 2014 – Mbeya Regional Labour Office.....	Sh.15,505,000/=
Kif. 2015 – Morogoro Regional Labour Office.....	Sh.18,505,000/=
Kif. 2016 – Mtwara Regional Labour Office....	Sh.16,305,000/=
Kif. 2017 – Mwanza Regional Labour Office...Sh.	17,365,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naongeza nusu saa kwa mujibu wa Kanuni zetu.

Kif. 2018 – Njombe Regional Labour Office....	Sh.10,885,000/=
Kif. 2019 – Pwani Regional Labour Office.....	Sh.17,400,000/=
Kif. 2020 – Rukwa Regional Labour Office.....	Sh.10,505,000/=
Kif. 2022 – Ruvuma Regional Labour Office...Sh.	10,145,000/=
Kif. 2023 – Shinyanga Regional Labour Office.....	Sh.10,115,000/=
Kif. 2025 – Singida Regional Labour Office.....	Sh.10,502,500/=
Kif. 2026 – Tabora Regional Labour Office.....	Sh.11,082,500/=
Kif. 2027 – Tanga Regional Labour Office.....	Sh.16,570,000/=
Kif. 2028 – Temeke Regional Labour Office....	Sh.10,630,000/=
Kif. 2029 – Kinondoni Regional Labour Office.....	Sh.10,710,000/=
Kif. 2030 – Ilala Regional Labour Office.....	Sh.17,200,000/=
Kif. 2031 – Social Security Division	Sh.182,569,000/=

Kif. 2032 – *Youth Development*Sh. 912,278,000/=
Kif. 2033 – *Employment Services Unit*Sh. 828,342,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapa juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2034 – *Persons with Disability Unit*.....Sh.1,139,898,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza lazima nikiri kwamba nashukuru sana kuwekwa fungu hili. Fungu hili la *sub-vote* 2034 kwa wale wenzetu, maana kila mmoja ni mlemavu mtarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwenye *item 22008, Training - Domestic*. Kwa kuwa fungu hili ni jipya na Mheshimiwa Waziri, Jenista Mhagama anaeleza kwamba fedha hizi kama kuna upungufu tutaenda kwenye *Sub-vote 1001* kwenye *vote* yenyewe ya 65 au 37.

Kwa kuwa fedha zilizotengawa hapa ni kidogo sana na kwakuwa ni mara kwa kwanza kwenye historia Bunge kuwekwa *sub-vote 2034*, naomba kupata maelezo kwamba kuna mkakati gani wa ziada kwenye *Training - Domestic* kukidhi mahitaji ya uhalisia ya jambo hili kubwa, zaidi ya shilingi milioni nne ambazo zimewekwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Watu Wenye Ulemavu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki kimetengewa hii fedha kutokana na mahitaji halisi ya Kitengo hiki cha Watu wenye Ulemavu. Kwa hiyo, ni fedha ambayo inatosha kabisa kwa mafunzo ya ndani. Kama ambavyo nimechangia hotuba, nilisema tunategemea kwamba watumishi wetu wa kitengo hiki wanatarajia kupata mafunzo lakini pia tunategemea kuongeza idadi ya watumishi, lakini kwa watumishi waliopo, hii fedha inastahili kabisa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy

Kif. 1001 – *Administration & Human Resources Management*..... Sh. 7,592,818,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI

Kif. 1001 - *Policy, Planning and Research*.... Sh. 180,925,213/=

Kif. 1002 - *Finance, Administration & Resource Mobilization*.....Sh. 1,038,410,974/=

Kif. 1003 - *Monitoring and Evaluation*.....Sh. 210,840,713/=

Kif. 1004 - *Advacacy and Information Unit*.....Sh.192,132,588/=

Kif. 1005 - *Nationa Response*Sh. 609,433,338/=

Kif. 1006 - *Procurement Management Unit*Sh.108,772,000/=

Kif. 1007 - *Legal Services Unit*Sh.115,005,000/=

Kif. 1008 - *Management Information Systems Unit*.....Sh. 70,879,000/=

Kif. 1009 - *Interanal Audit Unit*.....Sh. 121,608,588/=

Kif. 1010 - *Social Programs Unit*.....Sh. 109,884,000/=

Kif. 1011 *Government Communion Unit*.....Sh. 54,667,586/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu

- Kif. 1001 – *Administration & Human Resources Management*..... Sh. 0
Kif. 2002 - *Civil Affairs and Contingencies*....Sh. 463,453,569/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Katika kifungu hiki cha 2001, *item* 5306 na 6575 vinahusiana na mabadiliko ya tabia nchi ya *Early Warning System* na Mfuko wa Maafa. Sasa ukiangalia fedha zilizotengwa mwaka huu unaoishia 2018/2019, chanzo cha fedha kwa maeneo haya ambayo ni muhimu sana, ni fedha za nje. Fedha hizo hizo zinazosomeka 2018/2019 na ndiyo hizo hizo zinazomeka 2019/2020 na chanzo chake ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *concern* ziko hapo kwamba fedha hizi zinafanana. Ina maana mwaka huu unaoisha hazikutoka, kwa hiyo, zinasomeka tena kwa mwaka huu; na *sources* siyo *local* ila tunategemea ufadhili au *grants* au kama ni *funds* au mikopo toka nje kwa vitu ambavyo kwa hali ya sasa hivi ya mabadiliko ya tabia nchi kuna mafuriko, kuna ukame kuna dhoruba ambazo hata wenzetu nchi za jirani zimewapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo sasa ya Mheshimiwa Waziri alivyokuwa anafafanua kutoka kwa Mheshimiwa Mjumbe, alikuwa anasema kwamba huu Mfuko wa Maafa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu uko *covered* kwenye sekta kama ni madaraja au *airport*. Nataka ufafanuzi kwamba suala hili liko *captured* katika sekta husika? Yaani kwamba madaraja yetu yanaweza kustahimili mafuriko, siyo maafa na *accommodate*; *airport* hizi na miundombinu nyingine zina- *accommodate* matetemeko ya ardhi; zina-

accommodate dhoruba za baharini ambazo zinakuja huku nchi kavu; zina-*accommodate* mvua hizi za mawe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji ufafanuzi kwenye jambo mahususi na la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi, nilikuwa nasikiliza Kiswahili sasa kuna maneno hapo sijaelewa vizuri, lakini naamini Mheshimiwa Waziri atakuwa ameelewa. Mimi nilikuwa nasikiliza Kiswahili. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa swali lako kwa Mheshimiwa Dkt. Sware. Unajua Mheshimiwa Dkt. Sware ameweka vitu vingi kwa pamoja lakini nimemwelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kitu kimoja. Wakati nilipoanza kujibu maswali hapa ndani, nilisema jambo la kwanza masuala ni ya maafa ni masuala mtambuka. Kwa mfano, hii miradi yote miwili; *Early Warning* anayoisema na mabadiliko ya tabianchi, Dkt. Sware, ulikuwa ni mradi maalum lakini ulikuwa haufanywi na Ofisi ya Waziri Mkuu peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mradi huu ulitengenezewa *package* yake na *package* hiyo ilikuwa *budgeted* kwa kazi zinayotakiwa kufanywa kwa gharama ya pesa ambayo imewekwa ili ku-*meet targets* ambazo zinatakiwa kufikiwa. Mradi huo ulikuwa unaenda hatua kwa hatua. Kwa mfano, tumeshaimarisha vituo 51 vya hali ya hewa katika mabonde ya mito (*automatic weather stations*) ambazo zimewekwa kwenye mabonde ya mito, lakini na nyingine zimewekwa kwenye vituo mbalimbali vya kupima mwendokasi wa upepo na hali ya hewa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa miradi hiyo imeanza katika maeneo tofauti, linapokamilika eneo la kwanza

inahamia kwenye eneo lingine. Miradi hii tunapoelekea sasa inaenda kwisha Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, siyo miradi ambayo inadumu. Sasa ukija kwenye swali lako kwamba ni kwa nini fedha hizi zinatengwa tu kutoka nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu kazi yetu sisi ilikuwa tunasimamia mradi huo tu. Mradi huo tuliokuwa tunausimamia, wadau hawakuwa Ofisi ya Waziri Mkuu peke yake. Kwa mfano, tulipokuwa tunashughulika na hizo *automatic wealth station*, tulikuwa tunafanya pia na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini tulikuwa tunafanya nao pamoja. Kwa hiyo, ukienda utakuta bajeti nyingine ziko kwenye sekta hizo husika na bajeti nyingine zinatengwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo *role* yetu ni *coordination* na *role* yetu ni kusimamia hiyo miradi na kuona kwamba kile kilichopangwa katika mradi kwa *phases* mbalimbali kinaweza kuwa kimefikiwa. Kwa hiyo, miradi hiyo yote sasa inaelekea mwisho na tunakaribia kuifunga. Fedha zilizopangwa ni mahitaji halisi ya hiyo miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha nyingine za ndani zinatengwa kwenye taasisi husika, kama ni mabonde, utakuta kwenye miradi ya maji wamo; kama ni masuala ya Mamlaka ya Hali ya Hewa utakuta hiyo miradi pia imo na wenyewe wataielezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo utaratibu ambao tumekuwa tukiutumia katika suala zima hili la ku-*manage* maafa kwa kuzingatia mfumo wa kitaasisi na wa kisekta ndani ya nchi yetu kwa ujumla wake.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 4001 - *Private sector Development and Economic Empowerment*.....Sh.0

Kif. 5001 - *Coordination of Government Business*.....Sh. 36,114,112,168/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 42 – Ofisi ya Bunge

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hii ni ya sehemu ya Bajeti ya Bunge. Kwa hiyo, Katibu atatusomea ile ya jumla.

NDG. RUTH MAKUNGU- KATIBU MEZANI: Jumla ya fedha zilizotengwa katika fungu hili ni shilingi 7,609,511,600/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Kif. 1001 – *Administration and Human Resource Management*.....Sh. 0

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - *National Voters Registration and ICT Division*Sh. 0

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niko kifungu cha 2002 - *National Voters Registration and ICT Division*, hiyo kasma ya 6583 - *Electoral Support Program* ambayo mwaka 2018 ilitegewa shilingi bilioni tano mwaka huu wa 2019 haijatengewa fedha. Mheshimiwa Waziri jana wakati anatoa taarifa kuna wakati alisema kwamba mwezi Mei mwaka huu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unaanza nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa nini fedha zimepunguzwa? Je, pesa za uboreshaji nchi nzima ziko wapi na ni kiasi gani? Kama unasema zipo kwenye Mfuko Mkuu

wa Serikali, basi *atleast* utupe *indication* tu kwamba kutakuwa na *figure* ya kiwango hiki, kwa hiyo, zoezi la uboreshaji litakuwa sawa sawa pamoja na hapa kuwa *zero*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka fedha uliopita Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilikuwa imeanza maandalizi ya awali ya kimifumo ndani ya Tume yenyewe. Kulikuwa na urekebishaji wa mifumo na vitu vingine ndani ya Tume yenyewe kama maandalizi ya awali, ndiyo maana ikatengwa fedha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ua Uchaguzi kama nilivyosema, Sheria Na. 343 ya Sheria ya Uchaguzi, fedha zote ambazo zinashughulika na suala zima la uchaguzi kwa ujumla, nilishasema kwamba zinatengwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa ukichukua hizi shilingi bilioni tano na nyingine zilizoongezeka, tumeshapokea tayari jumla ya shilingi bilioni 23, lakini tukiendelea kupokea awamu kwa awamu fedha zote ambazo zimetengwa kwa ajili ya shughuli hii kwa umoja wake. Ndiyo maana tunawaambia kwamba hizo shilingi bilioni 23 ni fedha za kuanzia, lakini gharama halisi inafika kama kwenye shilingi bilioni 144, kitu cha namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuboresha daftari imeshaanza kama nilivyosema na mifumo yote ya kitaasisi imeshawekwa tayari, mifumo yote ya uboreshaji wa daftari imeshawekwa tayari, ukaguzi wa vituo umeshafanyika, majaribio yameshafanyika, kanzidata imeshahuishwa. Kwa hiyo, kila kitu kipo tayari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa ukakika kabisa kama kila kitu kitakuwa kimekwenda sawa sawa mwezi Tano tunaweza kuanza uboreshaji wa daftari tayari kwa maandalizi ya uchaguzi wa mwaka 2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwahakikishe Waheshimiwa Wabunge, tumeshajipanga sawa sawa na suala hili halina matatizo kabisa, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi. Kama nilivyosema, kwa mujibu wa sheria, fedha hizi ninatengwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Hata fedha za uchanguzi tayari tumeshaanza kuweka makisio, nazo zitakuja kutolewa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea Waheshimiwa.

Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu

Kif. 1003 - *Policy and Planning Unit*.....Sh. 290,000,000/=
Kif. 2002 - *Employment Division*.....Sh.18,000,000/=
Kif. 2032 - *Youth Development*.....Sh.1,771,968,097/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI

Kif. 1001 - *Policy, Planning and Research*.....Sh. 362,065,416/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - *Finance, Administration & Resources Mobilization*.....Sh. 2,511,360,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Sub-vote* 1002, kwenye *item 5488-ATF*, huu ni mfuko wetu wenyewe wa kupambana na masuala ya UKIMWI. Utakuta kwamba mwaka uliopita 2018 kulikuwa na fedha zilizotengwa shilingi bilioni tatu; mara hii kuna shilingi bilioni mbili. Hata hoja ikija kwamba shilingi bilioni moja ilikwishatolewa, lakini kwa kuwa kuna punguzo la 23% la

wafadhili kwenye fedha za UKIMWI, wafadhili wenyewe (*Donors*) wameanza kuondoa fedha hizi; lakini kwenye fedha zetu za ndani tumeandaa mazingira ya kuzipunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni la kwetu sisi wenyewe. Naomba kupata maelezo, Mfuko wa Kupambana na Masula ya UKIMWI kutoka kwenye shilingi bilioni tatu mpaka shilingi bilioni mbili, huku wafadhili wameanza kuondoa fedha 23% ya fedha tunazopata sisi wenyewe. Tuambie ni kwa nini sasa? Serikali ina mkakati gani wa ziada kuhakikisha *ATF* inawekewa kiwango cha fedha kinachostahili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ufafanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya sheria Na. 6 ya mwaka 2015 yaliyofanywa na Bunge lako Tukufu, kifungu cha 12 (b) cha mabadiliko ya sheria hiyo kimeanzisha mfuko wa huu wa udhibiti wa UKIMWI na kifungu hicho pia kimeeleza vyanzo vya mapato ama vyanzo vya fedha kwa ajili ya mfuko huo. Sasa ukiangalia kwenye kifungu hicho, vyanzo vya fedha kwa ajili ya mfuko huo ni pamoja na fedha za ndani ambazo zitatafutwa kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaponzungumzia fedha ndani ambazo zinatafutwa kwa njia mbalimbali, ni pamoja na kufanya *fund raising*, pamoja na Bunge kutenga fedha kama tunavyotenga sasa hivi; ni pamoja na kutafuta chanzo chochote cha fedha kutokana na mapato mengine ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapotenga hii shilingi bilioni mbili, hilo ni eneo moja tu la fedha ambazo zinatengwa na Bunge. Mfuko huu kwa mujibu wa sheria una bodi yake na ile bodi nayo inatakiwa kuongeza tena

makusanyo ya fedha. Hayo makusanyo ya fedha yanatakiwa yawe kutoka humu ndani ya nchi. Kama mnavyojua kwamba tumeshaanza kutamka ile namba yetu ya 909090. Ile namba ya 909090 ni chanzo kingine kwa ajili ya mfuko huo nacho kikiingizwa hapa ni fedha hiyo hiyo ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ziko juhudi kubwa tu za namna mbalimbali. Hata hivyo, Serikali imeanza mazungumzo ndani ya Serikali ya kuona kama tunaweza kuwa na tozo ya namna yoyote ile. Mnafahamu Waheshimiwa Wabunge wakati wa majadiliano kati ya Serikali na Kamati ya Bajeti, tumeweka pia hoja ya kuwa na tozo ya kuendelea kuongeza chanzo hiki cha mapato. Mfuko umeendelea kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, umeshatoa shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya dawa za Septrin kwa Wizara ya Afya. Mfuko huo pia umeshatumia shilingi milioni 75 lakini umeweza ku-*fund raising* na kupata shilingi bilioni 12 kwa ajili ya kushughulikia afua mbalimbali kwenye mwambao wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge watupe tu muda, mfuko huu ni mchanga, sasa hivi una miaka miwili tu lakini unaona kwa kweli tumeanza vizuri na Serikali imeanza vizuri na sisi wenyewe kama Watanzania tunatakiwa kuongeza nguvu vya pamoja, kuongeza nguvu ya mfuko wetu ili kuwa na utegemezi wa ndani wa mapambano dhidi ya Ukimwi kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 - *Monitoring and Evaluation*.....Sh.1,318,543,857/=
Kif. 1004 - *Advocacy and information Unit*...Sh. 263,840,000/=
Kif. 1005 - *National Response*.....Sh. 899,328,000/=
Kif. 1007 - *Legal Service Unit*.....Sh. 244,235,474/=

Kif. 1008 - <i>Management Information Systems Unit</i>	Sh. 46,100,000/=
Kif. 1009 - <i>Internal audit Unit</i>	Sh. 99,800,000/=
Kif. 1010 - <i>Special Programs Unit</i>	Sh. 211,362,000/=
Kif. 1011 - <i>Government Communication Unit</i>	Sh. 0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge, Kanuni ya 104 (3) kifungu cha (a) na (b) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati Matumizi na limekamilisha kazi zake zote. Naomba sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2019/2020 – Ofisi ya Waziri Mkuu yaliidhinishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Nichukue fursa hii kuwatangazia kwamba sasa Bajeti ama Makadirio ya Mapato na Matumizi, Ofisi ya Waziri Mkuu mwaka 2019/2020, Bunge limeshayapitisha. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, nichukue fursa hii kuwatakia kila heri Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri ambao mpo nchi yake na Naibu Mawaziri kwa utekelezaji wa wale mliyotuahidi kwamba mnaenda kutekeleza na Bunge limeridhia fedha ambazo mmeziomba. Tunawatakia utekelezaji mwema na tunaamini mtayatilia maanani yale ambayo mmeshauriwa na Waheshimiwa Wabunge katika kuboresha utekelezaji wa hii bajeti ambayo imepitishwa leo. Kwa hiyo, tunawatakia kila heri ninyi pamoja na wataalamu waliopo chini ya ofisi yenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo hapa linatoka kwa Mheshimiwa John Kadutu ambaye ni Meneja wa *Bunge Sport Club*, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mazoezi rasmi yanaanza kesho katika Uwanja wa Jamhuri saa 12.00 asubuhi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa mwende huko. Hajasema Waheshimiwa Wabunge wanamichezo, kasema Wabunge wote. *(Makofi)*

Kwa hiyo, twende tukaboreshe afya kule ili siku Wizara ya Afya itakapoleta bajeti hapa, pengine tuipunguze kidogo, kwa sababu Wabunge wote watakuwa wako vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 2.07 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 10 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)